# PENTIKOSTARI

**CENTRE MISSION ORTHODOXE**
**KOLWEZI CONGO**
**2002**

# SIKU KUU YA UFUFUO WA BWANA YESU KRISTU
## SALA YA ASUBUI (ORTHROS).

**Elezo:** *Mu posho usiku karibu saa kumi na moja (11), mbele ya katikati ya usiku, mutumishi ya Kanisa atapika kengele. Waaminifu wataingia Kanisani na wataanza kuimba Kanuni ya lufu ya Bwana wetu Yesu Kristu.*

**PADRI**: Abarikiwe Mungu wetu daima, sasa. . . Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako. Mfalme wa mbinguni, Wewe Mfariji, roho. . .

**MSOMAJI**: TRISAGION: Mungu Mutakatifu. . .

**PADRI**: Kwa kuwa ufalme, uwezo. . .

**MSOMAJI**: Bwana hurumia *(mara kumi na mbili).* Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Njooni tumwinamie. . . ZABURI 50 (51).

*Kisha tunafuata KANUNI YA LUFU YA BWANA WETU YESU KRISTU*

**WIMBO YA KWANZA Sauti ya sita.**

**HIRMOS**: Zamani Bwana alizika mzulumu chini ya mawimbi ya bahari, wana wa taifa lililofukuziwa walizika Mwokozi wao udongoni. Lakini sisi, kama mabikira wa Israeli tunamwimbia Bwana: Kwani amevaa utukufu.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Ee Bwana, ni wimbo wa heri ninaimba pa Kaburi Yako; lakini Kaburi Yako imenifungulia milango ya uzima na lufu Yako ilikuwa mauti ya hadeze.

Utukufu kwa Baba. . .

Majeshi ya mbinguni na majeshi ya dunia yalipokuona pa kiti cha juu mbinguni na Kaburini hapa chini yakashituka kwa hii lufu. Hii jambo ilipita ufahamu wao: Hayakuweze kuvumilia pa kuona Muumba wa uzima wote amelala katika mauti.

Sasa na siku zote. . .

Kwa kujaza vyote na utukufu wako ulishuka chini ya udongo; hali yangu niliyoriti kwa Adamu haikuweza kukimbia machoni mwako, na kwa kupotea kwangu Kaburi yako imenifanya kuwa mpya, ee Mpenda-wanadamu,

**Katavasia:** Zamani Bwana alizika mzulumu. . .

**WIMBO YA TATU**

**HIRMOS:** Ee Wewe uliyetundika inchi juu ya maji, kiumbe kilipokuona umetundikwa kule Kalvario kikashikwa na woga kubwa na kikapaza sauti na kusema: Hakuna aliye Mtakatifu kuliko Wewe Bwana Mungu wetu.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Ulionyesha alama za maziko yako wakati ulipozidisha miujiza, lakini leo ni kwa wakaaji wa hadeze ulionyesha mafumbo Yako, ee Mungu-Mutu; na wanapaza sauti na kusema: Hakuna aliye Mtakatifu kuliko Wewe Bwana Mungu wetu.

Utukufu kwa Baba. . .

Ee Mwokozi, wakati ulipanua mikono Yako na ulifunikwa sanda Kaburini, uliunganisha wale waliotengana zamani. Ulikomboa wafungwa waliokulalamikia na kusema: Hakuna aliye Mtakatifu kuliko Wewe Bwana.

Sasa na siku zote. . .

Wewe ambaye hauwezi kuenea katika kitu hata kimoja, kwa kutaka kwako wanakufungia Kaburini. Matendo Yako yalifunua uwezo wako kwa wale wenyi kukuimbia na kusema: Hakuna aliye Mtakatifu kuliko Wewe Bwana Mpenda-Wanadamu.

**Katavasia:** Ee Wewe uliyetundika inchi pa maji, . . .

**PADRI**: Tena na tena kwa amani tumwombe Bwana. . . .

**KATHISMA** *Sauti ya kwanza*

Ee Mwokozi, maaskari waliolinda Kaburi Yako walianguka kama wafu, wakaangaziwa na mwangaza ilioangazia wanawake na ikawahubiri Ufufuo wako. Utukufu Kwako, Wewe mwenyi kuharibu mauti! Tunaangukia ku miguu yako, Wewe mfufuliwa Kaburini, ee Wewe peke Yako Mungu wetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . *(mara ingine hii wimbo).*

**WIMBO YA INE**

**HIRMOS:** Alipotambua kujishusha kwako kimungu Msalabani, Habakuki akapaza sauti mwenyi kujaa na woga: Ee Mwema kamili, uliangamiza nguvu ya watawala wakati uliungana na wakaaji wa Hadeze, wewe Mfalme wa vitu vyote.

Utukufu kwako, ee Bungu wetu, utukufu kwako.

Ee Mwokozi, leo unatakasa siku ya saba, hii zamani ulitakasa wakati ulipumzika kisha kuumba vyumbe vyako, kwa sababu unaumba ulimwengu na unautengenezea Sabato yako kwa mafundisho yako.

Utukufu kwa Baba. .

Ee Neno, ni kwa uwezo wako kamili ulishinda roho yako ilitengana na mwili, ukavunja pamoja milango ya mauti na ya Hadeze kwa nguvu Yako.

Sasa na siku zote. . .

Ee Neno kwa kuja Kwako Hadeze ilijazwa na uchungu wakati iliona mwanadamu amekuwa Mungu, Mutu mwenyi vidonda nyingi amejazwa na uwezo, hii ono ya woga ikamwacha bila kusema.

**Katavasia:** Alipotambua kujishusha Kwako kimungu. . .

**WIMBO YA TANO**

**HIRMOS:** Ee Kristu, wakati rehema yako kimungu ilionekana kwa sisi, Isaya akaona nuru yako ikainuka usiku na asubui akalalamikia: Wafu wataamuka, wakaaji wa Kaburi watasimama, na watu wote wa dunia watashangilia.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Ee Muumba, unawafanya wana wa dunia kuwa wapya, Wewe uliyewaumba na unachukua udongo wao. Kaburi na sanda yanafunua fumbo Yako, ee Neno: Kwa sababu mshauri mwema anaonyesha nia ya baba yako ambaye kwa ukarimu wake, ananifanya kuwa mpya katika Nafsi Yako.

Utukufu kwa Baba. . .

Unageuza mufu kwa lufu yako, na mwenyi kuharibika kwa Kaburi yako unawapa wafu hali isiyoharibika kwa sababu Wewe ni Mungu, unamufanya kuwa wa milele huyu ulichukua hali yake. Kwani mwili wako haikuona uharibifu, ee Bwana, na roho yako haikua katika Hadeze huko ulikuwa mgeni.

Sasa na siku zote. . .

Ulizaliwa kwa Msiyeolewa, ee Muumba wangu, na kwa ubavu wako wenye kuchomwa mkuki unaumba kiumbe mpya kwa ajili ya Adamu wa pili na Eva mpya. Ulilala usingizi wa ajabu, usingizi uliyo Chemchem ya uzima na iliamsha mzima, ewe Mwenyezi.

**Katavasia:** Ee Kristu, wakati rehema. . .

**WIMBO YA SITA**

**HIRMOS:** Yona alimezwa ndani ya tumbo ya Samaki lakini hakua mule, alitangulia kuonyesha Mateso yako na maziko yako. Alitoka mu tumbo ya nyama kama katika Chumba cha Arusi akiwaambia waaskari: Mulichunga paka majivuno na uwongo, lakini muliacha rehema.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Uliondolewa ku uzima, ee Neno, lakini haukutengana na mwili ulitwaa: Hata kama Hekalu yako ilibomolewa wakati wa Mateso yako, hata kama umungu wako na mwili wako ilikuwa kitu moja katika hii hali mbili, wewe peke yako ni Mwana wa Mungu, Mungu tena Mutu.

Utukufu kwa Baba. . .

Zamani ya Adamu ilikuwa ni lufu ya mwanadamu, lakini apana ya Mungu, kwa sababu kama hali ya uvumbi ya mwili wako iliteswa, hali yako ya umungu haikuteseka. Uliingiza uharibifu katika hali isiyoharibika na kwa Ufufuo wako ulifunua Chemchem ya uzima isiyoharibika.

Sasa na siku zote. . .

Hadeze inatawala wanadamu, lakini ufalme wake si wa milele. Ni Wewe, ee Mwenyezi, ulipolala Kaburini, kwa mkono wako wa ufalme ulivunja minyororo ya mauti. Uliwahubiri wale waliolala tangu zamani ukombozi wa kweli, ee Mwokozi, ukawa Mzaliwa wa kwanza katika wafu

**Katavasia:** Yona alimezwa katika tumbo. . .

**PADRI**: Ektenia kidogo.

**KONTAKION** *Sauti ya mbili*

Tunaona anakufa Huyu aliyefunga hadeze. Anafunikwa sanda na kupakaliwa manukato. Msiyekufa anawekwa kaburini kama mufu tena wanawake wanakuja kumupakaa manukato wakilia kwa uchungu na wakipaza sauti: Hii Sabato imebarikiwa katika yote, kwa sababu Kristu mwenyi kulala atafufuka siku ya tatu.

**IKOS**

Huyu aliye na vyote aliinuliwa Msalabani, tena viumbe vyote vinaomboleza kwa kumuona ametundikwa uchi juu ya muti. Jua linaficha nuru yake, nyota zinapoteza mwanagaza wao, kwa woga kubwa inchi inatetemeka, bahari inakimbia, na mawe yanapasuka. Makaburi yanafunguka, miili ya Watakatifu yanafufuka. Hadeze inalalamika, Wayuda wanafanya shauri sababu ya kuficha Ufufuo wa Kristu: Hii Sabato imetakaswa katika yote, kwa sababu Kristu aliyelala atafufuka siku ya tatu.

**SINAKSARI YA WATAKATIFU.**

*Na kisha tunasoma hii:*

Muposho Takatifu na Mkubwa tunashangilia Maziko ya Mwili wa Mungu wetu Bwana Yesu Kristu na Kushuka kwake kwa Hadeze, kwa ajili wao kizazi ya watu ilirudi kwa uzima ya milele. Amina.

**WIMBO YA SABA**

**HIRMOS:** Muujiza wa kweli! Huyu aliyeopoa vijana watakatifu ku tanuru ya moto anawekwa Kaburini. Ni kwa ajili ya wokovu wetu na tunamwimbia: Ee Mungu mkobozi, umehimidiwa.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Hadeze ilipigwa moyoni kwa kumupokea Huyu ambaye ubavu ulichomwa mkuki. Imelala yenye kuteketezwa kwa moto kimungu. Ni kwa ajili ya kutuokoa na tunamwimbia: Ee Mungu mkombozi, umehimidiwa.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Kaburi heshimiwa yenyi kupokea Muumba kama amelala. Ameonekana kama hazina kimungu ya uzima; ni kwa ajili ya wokovu wetu na tunamwimbia: Ee Mungu Mkombozi, umehimidiwa.

Utukufu kwa Baba. . .

Uzima wa ulimwengu anaitika kuwekwa Kaburini kama ilivyo sheria ya wanadamu. Lakini hii Kaburi inajifunua kuwa chemchem ya Uzima. Ni kwa ajili ya wokovu wetu na tunamwimbia: Ee Mungu Mkombozi, umehimidiwa.

Sasa na siku zote. . .

Katika Hadeze Kaburini, na katika Edeni mulikuwa Umungu moja na usiyotengana wa Kristu pamoja na Baba na Roho Mtakatifu. Ni kwa ajili yetu na tunamwimbia: Ee Mungu Mkombozi, umehimidiwa.

**Katavasia:** Muujiza wa kweli! Huyu aliyeopoa. . .

**WIMBO YA MNANE**

**HIRMOS:** Inama kwa woga, ee mbingu, na tetemekeni ninyi misingi ya inchi kwani tazama Mungu wa mbinguni amehesabiwa katika wafu. Amepokelewa kama mgeni Kaburini, enyi watoto, mtukuzeni; enyi makuhani, mwimbieni; enyi mataifa, msifuni milele.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Hekalu safi kamili limebomolewa na linasimamisha nyumba ya Daudi yenye kubomolewa. Huyu mwenye kukaa juu kabisa ya mbingu, Adamu wa pili, anashuka chini kabisa ya Hadeze sababu ya kumuamusha yule wa kwanza. Enyi watoto, mtukuzeni; enyi makuhani, mwimbieni; enyi mataifa, msifuni milele.

Tunahimidi Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, Bwana.

Nguvu ya Mitume inanguka, lakini kwa uhodari Yosefu wa Arimathea alipokuona uchi na umekufa, Wewe Mungu aliye juu kabisa, akaomba mwili wako na akaufunika sanda akipaza sauti: Enyi watoto, mtukuzeni; enyi makuhani, mwimbieni, enyi mataifa, msifuni milele.

Sasa na siku zote. . .

Ee Muujiza, ee rehema, ee uvumilivu wa kweli. Huyu mwenye kukaa juu kabisa ya mbingu anavumilia kufungwa katika jiwe lenyi kufungiwa, na Mungu anatendewa kama muogo. Enyi Watoto, mtukuzeni; enyi makuhani, mwimbieni; enyi mataifa msifuni milele.

**Katavasia:** Tunamusifu, tunamuhimidi na tunamusujudu Bwana.

Inama kwa woga, ee mbingu, na tetemekeni. . .

**SHEMASI**: Mzazi Mungu na Mama wa Nuru, tukimuheshimu kwa nyimbo, na kumutukuza.

## WIMBO YA TISA

**HIRMOS:** Usilie, ee Mama, wakati unapoona Kaburini Mwana wako uliyezaa bila mbegu. Nitafufuka, nitakutukuzwa kama Mungu nitashangilia katika utukufu wa milele wale wenyi kukusifu kwa imani na mapendo.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Ee Mama yangu, ni kwa kutaka kwangu odongo umeniifunika; walinzi wa Hadeze wanatetemeka pakuniona nimevaa mavazi ya kisasi yenyi damu, kwa sababu kwa Msalaba nimepiga maadui zangu, na kama Mungu nitafufuka na nitakukutukuza.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .

Viumbe vifurahi na wanadamu washangilie: Hadeze aliye adui imenyanganywa, wanawake wakuje na manukato kukutana nami, Mimi niliyekomboa Adamu na Eva na wazao wao wote, Mimi nitakayefufuka siku ya tatu.

**Katavasia:** Usilie, ee Mama, wakati unapoona. . .

**MSOMAJI**: TRISAGION: Mungu Mutakatifu. . .

## APOLITIKION

Wakati ulishuka ku mauti, uzima usiyo kufa, hapo uliregeza kuzimu, kwa unara wa umungu wako; na wakati ulifufua wafu waliyolala kuzimu, ezi zote za mbinguni zilipaza sauti; Mpaji wa uzima Kristu, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

**PADRI**: Utuhurumie, ee Mungu, kadiri ya huruma yako kubwa, tunakuomba utusikie na ukatuhurumie.

**MWIMBAJI**: Bwana hurumia *(mara tatu).*

**PADRI**: Tena tunakuuomba kwa ajili ya waorthodoksi wote.

**MWIMBAJI**: Bwana hurumia *(mara tatu).*

**PADRI**: Tena tunakuomba kwa ajili ya mwarkiepiskopu *(jina lake)* na kwa ajili ya ndugu zetu wote katika Kristu.

**MWIMBAJI**: Bwana hurumia *(mara tatu).*

**PADRI**: Tena tunakuomba kwa ajili ya ndugu zetu, mapadri, washemasi, watawa na wandugu wote katika Kristo.

**MWIMBAJI**: Bwana hurumia *(mara tatu).*

**PADRI**: Kwa kuwa wewe ndiwe Mungu wa huruma na mupenda wanadamu, na kwako tunautoa utukufu, kwa Baba, na Kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milel na milele.

**MWIMBAJI**: Amina.

**PADRI**: Aliyefufuka katika wafu Kristu Mungu wetu kweli, kwa maombezi ya Mzazi Mungu Bikira Takatifu Mama yake Maria. . .

*Kisha ndani ya Kanisa watazimisha mishumaa yote na Waimbaji wataingia ndani ya Fasi Takatifu (Ieron) na wataimba wote pamoja Eothinon ya Saba hii:*

Tazama giza na asubui, kwa nini Maria unasimama mbele ya Kaburi. Una giza mingi ndani ya akili yako, kwa ajili ya hii giza unatafuta Yesu amewekwa wapi. Lakini ona Wanafunzi wanakimbia mbio pamoja, namna gani walihakikisha ufufuo kwa sanda na kitambaa na walikumbuka Maandiko

juu ya hii mambo. Pamoja nao na kwa njia yao na sisi tukikusadiki tunakuimbia wewe Kristu muletaji-uzima.
*Kisha Padri atavaa manguo yake ya utukufu na atasimama mbele ya mlango mkubwa Takatifu na ataanza kuimba hivi:*
Kujeni mupokee nuru, toka Nuru isiyo mwisho na mumutukuze Kristu, aliyefufuka katika wafu.

*Hii wimbo Padri ataimba mara nyingi mupaka Waaminifu wote watawakisha mishumaa yao. Kisha waimbaji wataanza kutoka inje, Padri na Waaminifu wote wataimba hii wimbo:*

Ufufuo wako, ee Kristu Mwokozi wimbiwe kwa Malaika mbinguni na utustahilishe sisi wa dunia kukutukuze kwa mioyo safi.
*Wakati watafika inje ya kanisa pa fasi yenye kutayarishwa vizuri, Padri atasema:*
Na tumsihi Bwana Mungu wetu atustahilishe, kusikia Evangelio Takatifu.
**MWIMBAJI**: Bwana hurumia. *(mara tatu).*
**PADRI**: Hekima; inukeni tusikilize Evangelio Takatifu. Amani kwa wote.
**MWIMBAJI**: Na kwa roho yako
**PADRI**: Somo la Evangelio Takatifu ilioandikwa na Mwevangelisti Marko. Tusikilize. (16, 1-8)

Hata sabato ilipokwisha kupita Maria Magdalene na Maria mama ya Yakobo na Salome walinunua manukato, wapate kwenda kumupakaa. Hata asubui mapema sana, siku ya kwanza ya juma, wakakwenda kaburini, wakati jua lilipotoka. Wakasemezana: Nani atakayetufingirishia lile jiwe mbele ya mulango wa kaburi? Hata walipotazama, waliona ya kuwa jiwe limekwisha kufingirishwa, nalo lilikuwa kubwa sana. Wakaingia kaburini, wakaona kijana ameketi upande wa kuume, amevaa nguo nyeupe. Wakashangaa. Naye aliwaambia: Musishangae, munatafuta Yesu wa Nazareti aliyesulibiwa; amefufuka, hayuko hapa. Tazama pahali walipomuweka. Lakini kwendeni mukawaambie wanafunzi wake, na Petro, ya kwamba anawatangulia ninyi kwenda Galilaya. Mutamwona kule kama alivyowaambia ninyi. Wakatoka, wakakimbia toka kaburini; kwa maana walitetemeka na kustaajabu; wala hawakumwambia mutu neno, sababu waliogopa.
**MWIMBAJI**: Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.
*Kisha Padri anafukiza na chetezo mara tatu Evangelio na anasema:*

Kwa Utatu Mtakatifu, Wenye asili moja, Muumba wa uhai, usiotengana, utukufu uwe daima, sasa na siku zote, hata milele na milele.
**MWIMBAJI**: Amina.
**PADRI**: Kristu alifufuka katika wafu, kwa lufu alishinda mauti, kwa wale waliokuwa ndani ya Kaburi, aliwapatia uzima. *(mara tatu).*
*Kisha Padri atasema shairi moja-moja ya Zaburi 67( 68) na waimbaji wataimba:* Kristu alifufuka. . .
Mistari:
1. Mungu asimame, adui zake zote wasambazwe; wenye kumuchukia wakimbie vilevile mbele yake.
2. Kama moshi inavyopeperushwa, hivi uwapeperushe; kama taa inavyoyeyuka mbele ya moto.
3. Hivi waovu wapotee mbele ya Mungu, lakini wenye haki wafurahi.
4. Hii ndiyo siku aliyofanya Bwana, tushangilie na kufurahiwa nayo.

Utukufu kwa Baba. . . Kristu alifufuka. . .
Sasa na siku zote. . . Kristu alifufuka. . .
*Kisha Padri atapaza sauti:* Kristu alifufuka katika wafu, kwa lufu alishinda mauti, kwa wale waliokuwa ndani ya Kaburi.
**WAIMBAJI**: . . . aliwapatia uzima.
**PADRI**: Kwa amani tumwombe Bwana. . . *(Ektenia mkubwa)*

*Kisha tunafuata*

**KANUNI YA UFUFUO YA BWANA YESU KRISTU**

*Wimbo ya Mtakatifu Yoane Damaskinos*

**WIMBO YA KWANZA**

**HIRMOS:** Ufufuo ni leo mataifa tuangazwe Paska ya Bwana Paska. Kwani toka mauti kwa uzima na toka inchi kwa mbingu, Kristu Mungu ulitupitisha sisi tuliyoimba wimbo wa ushindi.

Utukufu kwa Ufufuo wako Takatifu, ee Bwana.

Tusafishe mahasa na tutaona kwa nuru ya Ufufuo isiyoweza kukaribia, Kristu mwenye kungaa kama umeme na tumusikilize wazi aseme furahini na tuimbe wimbo wa ushindi. (*mara ya mbili).*

Utukufu kwa Baba. . Sasa na siku zote. . .

Mbingu zifurahi kama inavyostahili na inchi ishangilie na dunia yote yenyi kuonekana na isiyonekana ifanye Karamu, kwani Kristu alisimama mwenye furaha ya milele.

**Katavasia:** Ufufuo ni leo. . .

Kristu alifufuka. . . *(mara tatu)* na kisha:

Yesu akifufuka Kaburini kama alivyosema, alitupatia sisi uzima wa milele na rehema kubwa.

**SHEMASI**: Ektenia kidogo: Tena na tena...

**PADRI**: Kwa kuwa ni Kwako uwezo na utawala na nguvu na utukufu ya Baba, na ya Mwana, na ya Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

## WIMBO WA TATU

**HIRMOS:** Kujeni kunywa kinywaji kipya chenye kufanyika kwa ajabu si toka mwamba isiyopandwa, lakini toka Kaburi pahali Kristu alitosha chemchem ya uzima usiyoharibika na juu yake tunasimamishwa.

Utukufu kwa Ufufuo wako Takatifu, ee Bwana.

Sasa vyote vilijazwa kwa nuru mbingu na inchi na vilindi, basi kiumbe chote kifanye Karamu ya Ufufuo wa Kristu juu yake kilisimamishwa.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .

Jana nilizikwa pamoja na wewe Kristu, leo ninasimama pamoja na wewe mufufuliwa. Nilisulibiwa pamoja na wewe jana, wewe mwenyewe unitukuze, ee Mwokozi katika Ufufuo wako.

**Katavasia:** Kujeni kunywa kinywaji kipya. . .

Kristu alifufuka *(mara tatu).* Yesu akifufuka Kaburini. . .

**SHEMASI**: Ektenia kidogo: Tena na tena..

**PADRI:** Kwa kuwa Wewe ni Mungu wetu, na Kwako tunakutolea utukufu kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata...

*Kisha Msomaji anasoma Ipakoi:*

## IPAKOI

Waliposadiki alfajiri, wakakuta jiwe limekwisha kusukumwa Kaburini, Maria na wenzake wakasikia Malaika akawauliza: Sababu gani munatafuta katika wafu Yeye aliye hai katika nuru ya milele. Tazameni sanda : Nendeni wepesi mukawaambie wote ya kwamba Bwana amefufuka, anashinda mauti. Uliwapa Mitume wako amani, ee wewe mwenye kutuokoa na kutujaza Ufufuo.

## WIMBO YA INE

**HIRMOS:** Katika zamu kimungu Habakuki aliyesema neno ya kimungu, asimame pamoja nasi na aonyeshe Malaika muletaji-nuru na mwenye kupaza sauti kubwa! Leo wokovu umekuja duniani na ya kama Kristu alifufuka sawa mwenyezi.

Utukufu kwa Ufufuo wako Takatifu, ee Bwana.

Kristu anaonekana mume sawa alifungua tumbo la Bikira, na anaitwa Mwana Kondoo sawa analiwa, huyu ni Paska yetu wasipo kilema sawa hakuonja zambi na anaitwa mukamilifu sawa Mungu wa kweli.

Utukufu kwa Baba. . .

Sawa Mwana Kondoo wa mwaka moja taji ya wema mwenye kubarikiwa kwetu ametolewa sadaka kwa kutaka kwake juu ya wokovu wa wote, Paska ya siri na tena toka Kaburi jua nzuri la haki aliangaa kwetu.

Sasa na siku zote. . .

Daudi babu wa Mungu alicheza na kuruka mbele ya Sanduku ya kivuli cha sheria, lakini taifa takatifu la Mungu linaona timizo ya mifano; tufurahi katika Mungu kwani Kristu alifufuka sawa mwenyezi.

**Katavasia:** Katika zamu kimungu Habakuki. . .

Kristu alifufuka *(mara tatu).* Yesu akifufuka Kaburini. . .

**SHEMASI**: Ektenia kidogo: Tena na tena...

**PADRI:** Kwa kuwa ewe Mungu Mwema na mpenda wanadamu na Kwako tunakutolea utukufu kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata...

**WIMBO YA TANO**

**HIRMOS:** Asubui mapema tuamuke, pahali pa manukato tutolee sifa kwa Rabi, na tutaona Kristu jua la haki lenyi kuleta uzima kwa wote *(mata ya mbili).*

Utukufu kwa Ufufuo wako Takatifu, ee Bwana.

Wafu waliokuwa wafungwa wa minyororo ya Hadeze walikukazia macho, kwa rehema yako isiyohesabiwa, ee Kristu; walijiharikisha kwa nuru wakatembea kwa shangwe na kupiga mwendo kwa kushangilia Paska ya milele. *(mara ya pili)*

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .

Tujongee na mishumaa mikononi kwa Kristu mwenye kutokea Kaburini kama Bwana Arusi, na tufanye Karamu pamoja na kundi lenye kupenda Karamu ya Paska ya Mungu inayoleta wokovu.

**Katavasia:** Asubui mapema tuamuke. . .

Kristu alifufuka *(mara tatu).* Yesu akifufuka Kaburini. . .

**SHEMASI**: Ektenia kidogo: Tena na tena...

**PADRI:** Kwa kuwa Jina lako liheshimiwa na tukufu kamili limetakaswa na kutukuzwa Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote...

**WIMBO YA SITA**

**HIRMOS:** Ulishuka katika vilindi vya udongo, na ulivunja mapigo ya milele iliyochunga wafungwa, ee Kristu, na kisha siku tatu kama Yona alitoka kwa samaki ulifufuka toka Kaburini. *(mara ya pili).*

Utukufu kwa Ufufuo wako Takatifu, ee Bwana.

Ulipochunga alama muzima, ee Kristu ulisimama kwa Kaburi, wewe usiyeharibu Bikira Mama yako kwa kuzaliwa kwako na ulitufungulia milango ya Paradizo. *(mara ya pili).*

Utukufu kwa Baba. . . sasa na siku zote. . .

Ee Mwokozi wangu mwenye kuishi na kutolewa sadaka bila kuchinjwa, sawa Mungu ulijitoa kwa Baba kwa kutaka kwako, ulifufua Adamu na uzao wake wote pamoja nawe wakati ulifufuka kaburini.

**Katavasia:** Ulishuka katika vilindi. . .

Kristu alifufuka *(mara tatu).* Yesu akifufuka Kaburini. . .

**SHEMASI:** Tena na tena...

**PADRI:** Kwa kuwa Wewe Mfalme wa amani tena Mwokozi wa roho zetu na Kwako tunautoa utukufu, kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hate...

**KONTAKION** *Sauti ya mnane*

Ulipolala Kaburini, ee Bwana msiyekufa, ulivunja nguvu ya Gehena na ulifufuka na ushindi, ee Kristu Mungu wetu, ukawaamuru wabebaji-manukato wafurahi; ukawatazama Mitume wako, ukawapa amani, wewe mwenye kutuokoa na kutupatia ufufuo.

**IKOS**

Wakati, ee Jua la mbele ya jua zamani ulishuka Kaburini, wanawake wabebaji manukato walikutafuta kama mchana, walijiharikisha asubui mapema, wakambiana mumoja kwa mwingine: Rafiki zangu wapenzi, tuendeni tupakae marasi, mwili wenye-kuleta uzima wa huyu alizikwa na mwenye kufufua Adamu aliyeanguka na kulala Kaburini; tuendeni, tujiharikishe, sawa Waakili, tumuabudu na tumutolee marasi sawa zawadi, yeye mwenye kufungwa si kwa sanda ya kitoto lakini kwa sanda ya maziko; tulie na kupaza sauti tukisema: Simama, ee Rabi, wewe mwenye kufufua wale wenye kuanguka.

**SINAKSARI YA WATAKATIFU WA LEO**

*Kisha tunasoma:*

Mu Juma Mukubwa na Tatakatifu ya Paska tunashangilia Ufufuo ubebaji-Uzima wa Bwana Yesu Kristu, Mungu na Mwokozi wetu.

*Kisha tunasoma hii:*

Tukikwisha kufikiri ufufuo wa Kristu, tumsujudu Mtakatifu wetu Bwana Yesu aliye peke yake bila zambi. Ee Kristu, tunasujudu Msalaba wako, tunaimbia na kutukuza Ufufuo wako takatifu, kwa

sababu wewe ni Mungu wetu, hatumjue tena mwengine ila wewe, jina lako tunalitaja, njooni Waaminifu wote tusujudie Ufufuo takatifu wa Kristu; na tazama, kwa Msalaba wake furaha inaonekana ulimwengu kote, bila ukomo tumutukuze Bwana na tuimbie Ufufuo wake, kwani alipoteswa Msalabani kwa ajili yetu amebadilisha kifo chake. *(mara tatu).*

Yesu alifufuka Kaburini kama alivyosema, alitupatia uzima wa milele na rehema kubwa. *(mara tatu).*

## WIMBO YA SABA

**HIRMOS:** Huyu aliponyesha watoto toka tanuru ya moto na kujifanya mutu anateswa kama mwenye kuweza kufa, na kwa mateso yake anavika mwili wa mauti uzuri na uzima usiyoharibika, huyu peke yake ni Mungu wa Mababu, mubarikiwa mwenye kutukuzwa kamili.

Utukufu kwa Ufufuo wako takatifu, ee Bwana.

Wanawake kwa mawazo kimungu walipoleta manukato wakaenda mbio nyuma yako, lakini walipokutafuta na machozi sawa mutu mwenye kuweza kufa, walikuabudu na furaha sawa Mungu aliye hai, walipasha habari njema ya Paska ya siri kwa Wanafunzi wako, ee Kristu.

Utukufu kwa Baba. . .

Tunafanya Karamu ya kufa kwa mauti na kushusha kwa Hadeze na malimbuko ya kuja kwa uzima ingine, uzima wa milele, na kwa furaha tunamusifu yeye mtengenezaji aliye peke yake Mungu wa mababu, mubarikiwa na mutukuzwa kamili.

Sasa na siku zote. . .

Kweli usiku yenye kuleta wokovu na nuru ni takatifu na ni Sikukuu, ilitangaza habari mbele ya siku yenye kuleta nuru ya Ufufuo, na katika hii usiku Nuru ya milele inaangaza mwili wote Kaburnii. *(mara ya pili).*

**Katavasia:** Huyu aliponyesha Watoto toka ya tanuru. . .

Kristu alifufuka *(mara tatu).* Yesu alifufuka kaburini. . .

**SHEMASI**: Ektenia kidogo: Tena na tena...

**PADRI:** Kwa kuwa uwezo na ufalme wako unabarikiwa na utukuzwa pamoja na Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu...

## WIMBO YA MUNANE

**HIRMOS:** Hii siku ya kusanyiko takatifu, siku ya kwanza ya juma, siku ya ufalme na utawala, Karamu ya makaramu na sikukuu ya sikukuu, katika hii siku tunatukuza Kristu milele.

Utukufu kwa Ufufuo wako Takatifu, ee Bwana. .

Kujeni tusharikie kuzaliwa kupya kwa muzabibu, kwa furaha kimungu, na ufalme wa Kristu katika siku kubwa ya Ufufuo, na tumusifu sawa Mungu milele.

Tunamuhimidi Baba, Mwana, na Roho Mutakatifu Bwana.

Ee Sayuni, nyanyua macho yako pande zote uone, kwani tazama wana wako wenye kwangaa kama nyota wanakuja kwako toka mangaribi na Kaskazini, toka Bahari na Mashariki, katika wewe wanamutukuza Kristu milele.

Sasa na siku zote. . .

Baba mwenyezi, Neno na Roho, hali moja katika nafsi tatu, ni Mungu mumoja, tumebatizwa katika jina na tunakutukuza milele .

Tunahimidi, tunatukuza na tunasujudu Bwana.

**Katavasia:** Hii siku ni kusanyiko takatifu, siku ya kwanza. . .

Kristu alifufuka *(mara tatu).* Yesu alifufuka toka kaburini. . .

**SHEMASI**: Ektenia kidogo: Tena na tena...

**PADRI:** Kwa kuwa Jina lako linabarikiwa na imetukuzwa Ufalme wako ya Baba, na ya Mwana, na ya Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata...

## WIMBO YA TISA

**SHEMASI**: Mzazi Mungu na Mama wa Nuru. . .

Shairi: Malaika aliita Mujaliwa neema Bikira Safi, Salamu na tena nitasema Salamu, Mwana wako alifufuka siku ya tatu Kaburini.

**HIRMOS:** Ungae, ungae Yesuralema mupya kwa sababu utukufu wa Bwana umepambazuka juu yako. Cheza sasa na shangilia, ee Sayuni, na wewe Muzazi Mungu Safi furahi, katika Ufufuo wa Mwana wako.

Shairi: Tukuza, ee nafsi yangu, yeye aliyefufuka, Kaburini siku ya tatu Kristu muletaji uzima.

Ah kimungu! ah mupendwa, ah nzuri sana ni sauti yako! Kwani uliahidi bila uwongo ya kama utakuwa pamoja nasi hata mwisho wa milele, ee Kristu sisi waaminifu wenye kuchunga hii ahadi ya matumaini tunakushangilia wewe.

Utukufu kwa Baba. . .

Tukuza, ee nafsi yangu utawala wa umungu usiyotengana ku nafsi tatu. Ah Paska kubwa na zabihu, ee Kristu! ah Akili na Neno na Nguvu ya Mungu, utupe sisi tushiriki pamoja nawe siku ya milele ya ufalme wako.

Sasa na siku zote. . .

Salamu Bikira, salamu, salamu Mubarikiwa, salamu Mutukuzwa kwani Mwana wako alifufuka siku ya tatu Kaburini. Ah kimungu! ah mupendwa, ah nzuri sana ni sauti yako!. . .

**Katavasia:** Malaika aliita Mujaliwa neema. . . Ungae, ungae. . .

Kristu alifufuka. . . *(mara tatu).* Yesu alifufuka Kaburini. . .

**SHEMASI**: *Ektenia kidogo:* Tena na tena...

**PADRI:** Kwa kuwa yasifiwe majeshi yote ya mbinguni na kuleta utukufu kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote hata...

**EKSAPOSTILARI.** *Sauti ya mbili*

Kwa mwili, ee Mufalme na Bwana ulipolala kama mutu mwenye kuweza kufa, ulifufuka siku ya tatu; ukasimamisha Adamu toka uharibifu na mauti, ewe Paska uzima usiyoharibika na Mwokozi wa dunia. *(mara tatu)*

## MASIFU. *Sauti ya kwanza.*

*Tunaimba sifa ine za Ufufuo na sifa ine za Paska. Toka Kitabu cha Paraklitiki kwa sauti ya Kwanza pa fasi ya Masifu tunaimba hii nyimbo ine :*

Kituo: 1. Musifuni kwa matendo yake makuu, musifuni kwa kadiri ya wingi wa ukuu wake.

Tunasifu, ee Kristu, mateso yako kwa ajili ya wokovu wetu, na tunatukuza Ufufuo wako.

Kituo: 2. Musifuni kwa mvumo wa baragumu, musifuni kwa kinanda na kiumbi.

Bwana, wewe uliyevumilia Msalaba, uliyeharibu mauti, na uliyefufuka katika wafu, tuliza uzima wetu, kwa kuwa Wewe ni mwenyezi peke yako.

Kituo: 3. Musifuni kwa ngoma na michezo, musifuni kwa nzenze na filimbi.

Ee Kristu, wewe uliyeteka Hadeze, na ulifufua mutu, kwa ufufuo wako, utustahilishe na moyo safi, tukusifu na kukutukuza.

Kituo: 4. Musifuni kwa matoazi yenye kuvuma; musifuni kwa matoazi yenye kuvuma sana. Kwa mwenye pumuzi na amsifu Bwana.

Tukitukuza mapendo yako yenye kumufaa Mungu, tunakusifu, ee Kristu; ulizaliwa kwa Bikira, na ulikuwa msiyetengana na Baba; uliteswa sawa mutu na ulivumilia Msalaba kama ulivyotaka; ulifufuka kaburini kama ulitoka katika nyumba ya arusi juu ya wokovu wa dunia, Ee Bwana, utukufu kwako.

**STIKHIRA YA PASKA** *Sauti ya tano*

Kituo: 1. Mungu asimame, adui zake zote wasambazwe; wenye kumuchukia wakimbie vilevile mbele ya uso wake.

Paska zabihu leo imeonekana kwetu. Paska mupya takatifu, Paska ya siri. Paska iheshimiwa kamili, Paska Kristu Mwokozi, Paska bila doa, Paska Kubwa, Paska ya waaminifu, Paska yenye kutufungulia milango ya Paradizo, Paska yenye kutakasa waaminifu wote.

Kituo: 2. Kama moshi inavyopeperushwa, hivi uwapeperushe; kama taa inavyoyeyuka mbele ya moto.

Kujeni Wanawake mulioona na kutangaza habari, ambieni Sayuni: pokea kwa sisi habari njema ya furaha ya Ufufuo wa Kristu. Furahi, cheza na shangilia, ee Yerusalema, kwa kumuona Mufalme Kristu mwenye kutokea Kaburini kama Bwana arusi.

Kituo: 3. Hivi waovu wapotee mbele ya uso wa Mungu na wenye haki wafurahi.

Wanawake wabebaji manukato asubui mapema walisimama mbele ya Kaburi ya Muletaji-uzima, walipata Malaika mwenye kukaa juu ya jiwe na huyu akawaambia akasema; kwa nini munatafuta Yeye aliye hai katika wafu, kwa nini munalilia Yeye asiyeharibika katika uharibifu; kwendeni mukawapashe Wanafunzi wake habari.

Kituo: 4. Hii ni siku aliyofanya Bwana, tufurahi na kushangilia ndani yake.

Paska ya furaha, Paska Bwana Paska, Paska iheshimiwa kamili ilizika kwetu. Paska kwa furaha tukumbatiane, ah Paska ukombozi wa sikitiko, kwani leo Kaburini Kristu alipoangaa kama Bwana arusi mwenye kutoka nyumbani mwake alijaza wana wake na furaha, na kusema muwapashe Mitume habari.

**DOKSASTIKON.** *Sauti ya tano.*

Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa roho Mutakatifu. Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Ufufuo ni leo, tuangazwe ku Karamu, tukumbatiane mumoja kwa mwingine. Tuseme wandugu, tuwasamehe wale wenyi kutuchukia, kwa sababu ya Ufufuo na tupaze sauti: Kristu alifufuka katika wafu, kwa lufu alishinda mauti, kwa wale waliokuwa ndani ya Kaburi, aliwapatia uzima.

*Na mara ingine*: Kristu alifufuka. . . *(mara tatu).*

*Elezo: Kutoka siku ya Paska kufika mu Juma ya Thomas, hii wakati tunaitaja Juma "Diakenisimos". Katika Juma Diakenisimos pahali pa Sala ya Apodipnon Kidogo, Saa ya Tisa na Saa ya kwanza, ya Tatu na ya Sita na Mesoniktikon tunasoma hii sala ya Ufufuo. Ni hivi:*

PADRI: Abarikiwe Mungu wetu daima, sasa na siku zote, hata milele na milele.

WAIMBAJI: Amin.

Kristu alifufuka katika wafu, kwa lufu alishinda mauti, kwa wale waliokuwa ndani ya kaburi, waliwapatia uzima. *(mara tatu).*

Tukipokwisha kufikiri ufufuo wa Kristu, tumsujudie Mtakatifu wetu Bwana Yesu aliye peke bila zambi, ee Kristu, tunasujudia msalaba wako, tunaimbia na kutukuza ufufuo wako takatifu, kwa sababu uko Mungu wetu, hatumjue tena mwengine ila wewe, jina lako tunalitaja, njooni waaminifu wote tusujudie Ufufuo takatifu wa Kristu; tazama, kwa msalaba wake furaha inangaa duniani kote, tumutukuze Bwana na tuimbie Ufufuo wake, kwani alipoteswa msalabani kwa ajili yetu ameharibu mauti kwa lufu yake, *(mara tatu).*

Walipokuja asubui mapema, wakakuta jiwe limekwisha kusumwa pembeni ya kaburini, Maria na wenzake wakasikia malaika akawauliza: Sababu gani munatafuta katika wafu Yeye aliye hai katika nuru ya milele? Tazameni sanda : Nendeni wepesi mukawaambie wote ya kwamba Bwana amefufuka, anashinda mauti, maana ni Mwana wa Mungu mwenye kuokoa wanadamu.

Ulipolala kaburini, ee Bwana Msiyekufa, ulivunja nguvu ya Hadeze na ulifufuka na ushindi, ee Kristu Mungu wetu, ukawaamuru wanawake wabebaji manukato wafurahi; ulipoonekana kwa Mitume wako ukawapa amani, *w*ewe mwenye kutuokoa na kufufua.

Kaburini na Mwili wako, Kuzimuni na roho yako kama Mungu, Paradizoni na Munyanganyi, unatawala pamoja na Baba na Roho Mtakatifu, ee Kristu uliye popote na kuujaza ulimwengu.

Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho mtakatifu.

Uliye na utukufu kupita Paradizo, kweli mwenyi kuangaa kupita makao ya mfalme, ee Kristu uliyeonekana kwetu, kaburi yako inaleta uzima : Ni chemchem ya ufufuo wetu.

Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amin.

Furahi, ee makao yenye kutakaswa, hema takatifu ya Aliye-Juu, ee Mzazi-Mungu, ni kwa ajili yako tumepewa furaha, kwa hii tunapaza sauti na kusema: Umebarikiwa katika wanawake, ee Malkia usiye na doa.

Bwana hurumia *(mara 40).* Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku. . . Uliye wa tamani kwashinda wakheruvi, uliye na utukufu kwa pita bila kiasi wa Serafi, uliye ukimuzaa Mungu Neno, umebaki bila kukuharibu, uliye Mzazi-Mungu kweli tunakutukuza wewe.
Kwa jina la Bwana, ee Padri, bariki.
PADRI: Kwa maombezi ya Wapateri watakatifu, ee Bwana Yesu Kristu Mungu wetu, utuhurumie.
WAIMBAJI: Amina.

PADRI: Ee Rabi Mwenyezi Mubarikiwa, wewe Uliyeangaza muchana na mwangaza wa jua na uliyeangaza usiku na mwangaza wa nyota, Wewe uliyetustahilisha kupita siku nzima na kukaribia usiku. Sikia maombi yetu na ya watu wote na kutuhurumia makosa ya kujuwa ao yasipo kujuwa. Pokea sala zetu za Mangaribi na rehema yako kubwa, na wema wako, kwa uriti wako. Malaika wako watakatifu watulinde. Utupe silaha yako ya haki, utuongoze na ukweli wako na nguvu yako. Utuokoe toka kila uovu na kila mutego wa shetani. Utupe kwa hii mangaribi na kwa hii usiku kamilifu, takatifu, amani isiyo na zambi, bila majaribu, bila mawazo mbaya, hata siku zote za maisha yetu, kwa maombezi ya Mzazi-Mungu na ya Watakatifu wote, waliokupendeza tangu milele. Amina.

Kristu alifufuka katika wafu, kwa lufu alishinda mauti, kwa wale waliokuwa ndani ya kaburi, aliwapatia uzima.

## LITURGIA TAKATIFU YA MTAKATIFU YOANE KRISOSTOMO

**PADRI**: Uhimidiwe Ufalme wa Baba. . .
**MWIMBAJI**: Amina.
**PADRI**: Kristu alifufuka. . . *(mara tatu)*
*Padr**i** atasema Mistari ya Zaburi 67( 68):*
Mungu asimame, adui zake zote wasambazwe, wenye kumuchukia wakimbie vilevile mbele ya uso yake.
**WAIMBAJI**: Kristu alifufuka...
**PADRI**: Kama moshi inavyopeperushwa, hivi uwapeperushe kama taa inavyoyeyuka mbele ya moto.
**WAIMBAJI**: Kristu alifufuka...
**PADRI**: Hivi waovu wapotee mbele ya Mungu na wenye haki wafurahi.
**WAIMBAJI**: Kristu alifufuka...
**PADRI**: Hii ni siku aliyofanya tufurahi na kushangilia ndani yake.
**WAIMBAJI**: Kristu alifufuka...
**PADRI**: Utukufu kwa Baba...
**WAIMBAJI**: Kristu alifufuka. . .
**PADRI**: Sasa na siku zote. . .
**WAIMBAJI**: Kristu alifufuka. . .
**PADRI**: Kristu alifufuka katika wafu, kwa lufu alishinda mauti, kwa awale waliokuwa ndani ya kaburi
**WAIMBAJI**: aliwapatia uzima.
**PADRI** ao **SHEMASI**:
Kwa amani tumwombe Bwana. . . *Ektenia ukubwa.*

## ANTIFONON YA KWANZA

Musomaji: Mushangilie Mungu, ee inchi yote.
**WAIMBAJI**: Kwa maombi ya Muzazi Mungu. . .
**MSOMAJI**: Mwimbe utukufu wa jina lake;tukuzeni sifa yake.
**WAIMBAJI**: Kwa maombi ya Mzazi Mungu. . .
**MSOMAJI**: Mwambieni Mungu: Kazi zako ni za hofu kabisa!
**WAIMBAJI**: Kwa maombi ya Mzazi- Mungu. . .
**MSOMAJI**: Inchi yote watakuabudu, na wataimba kwako.
**WAIMBAJI**: Kwa maombi ya Mzazi- Mungu. . .
Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .
Kwa maombi ya Mzazi- Mungu. . .

**SHEMASI**: Ektenia kidogo.

**ANTIFONON YA MBILI**

**MSOMAJI**: Mungu atuhurumie na atubariki.

**WAIMBAJI**: Utuokoe, ee wewe Mwana wa Mungu, uliyefufuka katika wafu. . .

**MSOMAJI**: Atuangazie uso wake na atuhurumie.

**WAIMBAJI**: Utuokoe, ee wewe Mwana wa Mungu, uliyefufuka katika wafu. . .

**MSOMAJI**: Njia yako ijulikane duniani, wokovu wako katika mataifa yote.

**WAIMBAJI**: Utuokoe. . .

**MSOMAJI**: Watu wakusifu, ee Mungu; watu wote wakusifu.

**WAIMBAJI**: Utuokoe. . .

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Uliye Mwana wa peke. . .

**ANTIFONON YA TATU**

**MSOMAJI**: Mungu asimame, adui zake zote wasambazwe; wenye kumuchukia wakimbie vilevile mbele yake.

**WAIMBAJI**: Kristu alifufuka katika wafu. . .

**MSOMAJI**: Kama moshi inavyopeperushwa, hivi uwapeperushe kama taa inavyoyeyuka mbele ya moto.

**WAIMBAJI**: Kristu alifufuka. . .

**MSOMAJI**: Hivi waovu wapotee mbele ya uso wa Mungu na wenye haki wafurahi.

**WAIMBAJI**: Kristu alifufuka. . .

**KUINGIA (ISODIKON)**

Katika Makusanyo yenu, mtukuzeni Mungu, mtukuzeni Bwana, enyi wazao wa Israeli. Utuokoe, ee Mwana wa Mungu, uliyefufuka katika wafu, tunaokuimbia. Alliluia.

*Kisha:* Kristu alifufuka *(mara tatu).*

**IPAKOI**

Walipokuja asubui mapema, wakakuta jiwe limekwisha kusumwa pembeni ya kaburini, Maria na wenzake wakasikia malaika akawauliza: Sababu gani munatafuta katika wafu Yeye aliye hai katika nuru ya milele? Tazameni sanda : Nendeni wepesi mukawaambie wote ya kwamba Bwana amefufuka, anashinda mauti, maana ni Mwana wa Mungu mwenye kuokoa wanadamu.

**KONTAKION**

Ulipolala kaburini, ee Bwana Msiyekufa, ulivunja nguvu ya Hadeze na ulifufuka na ushindi, ee Kristu Mungu wetu, ukawaamuru wanawake wabebaji manukato wafurahi; ulipoonekana kwa Mitume wako ukawapa amani, *w*ewe mwenye kutuokoa na kufufua.

**SHEMASI**: Tumwombe Bwana.

**PADRI**: Kwa kuwa Wewe ni Mtakatifu, ee Mungu wetu na kwako tunautoa. . .

**WAIMBAJI**: Ninyi wote muliobatizwa katika Kristu, mumevaa Kristu.

**MATENDO YA MITUME (APOSTOLOS) (1, 1-9)**

Katika kitabu cha kwanza, Teofilo, nilikuandikia mambo yote aliyoanza Yesu kufanya na kufundisha, hata siku ile alipochukuliwa juu nyuma ya kuagiza kwa Roho Mutakatifu mitume aliowachagua, na nyuma ya kuteswa kwake aliwatokea, akawaonyesha kwa alama nyingi ya kuwa yuko hai, akaonekana nao kwa muda wa siku makumi ine, na kusema nao maneno ya ufalme wa Mungu. Hata, akikutana nao, akawaagiza wasitoke Yerusalema, ila wangoje ahadi ya

Baba muliyosikia kwangu; kwani Yoane alibatiza kwa maji, lakini ninyi mutabatizwa katika Roho Mutakatifu nyuma ya siku si nyingi. Wakati walipokutanika wakamwuliza, wakisema: Bwana, utarudishia Waisraeli ufalme wao tena wakati huu? Akawaambia: Si maneno yenu kujua nyakati wala majira Baba aliyoweka katika mamlaka yake mwenyewe. Lakini mutapokea nguvu wakati Roho Mutakatifu anapokuja juu yenu, nanyi mutakuwa washuhuda wangu katika Yerusalema, na katika Yudea yote, na Samaria, hata mupaka wa dunia. Akikwisha kusema maneno haya, akanyanyuliwa nao wakitazama, wingi likamupokea toka macho yao.

**WAIMBAJI**: Alliluia *(mara tatu).*

**EVANGELIO YA YOANE (1, 1-17)**

Katika mwanzo alikuwa Neno, na Neno alikuwa pamoja na Mungu, na Neno alikuwa Mungu. Huyu kwa mwanzo alikuwa pamoja na Mungu. Vitu vyote vilifanyika kwa huyu; na pasipo yeye hakikufanyika hata kitu kimoja kilichofanyika. Ndani yake ulikuwa uzima, an uzima ulikuwa nuru ya watu. Na nuru ilingaa katika giza na giza halikuishinda. Palitokea mutu ametumwa kutoka kwa Mungu, jina lake Yoane. Huyu alikuja kwa ushuhuda, ili ashuhudie nuru, watu wote wapate kuamini kwa huyu. Huyu hakuwa nuru ile, lakini alikuja ashuhudie nuru ile. Ilikuwa nuru ya kweli inayotia nuru kila mutu anayekuja katika ulimwengu. Alikuwa ulimwenguni, na ulimwengu ulifanywa naye na ulimwengu haukumutambua. Alikuja kwake, nao walio wake hawakumupokea. Lakini wote waliomupokea aliwapa uwezo wa kuwa watoto wa Mungu, ndio wale walioamini jina lake. Waliozaliwa, si kwa damu, wala si kwa mapenzi ya mwili; wala si kwa mapenzi ya mutu, lakini kwa Mungu. Na Neno alifanyika ya mwili, akakaa kwetu, tukatazama utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee akitoka kwa Baba, amejaa neema na kweli. Yoane akamushuhudia, akapaza sauti yake, akisema: Huyu ndiye niliyemusema habari zake. Anayekuja nyuma yangu amekuwa mbele yangu, kwa maana alikuwa mbele yangu. Na katika utimilifu wake sisi sote tulipokea, na neema juu ya neema. Kwa kuwa torati ilitolewa kwa mukono wa Musa, neema na kweli zilikuja kwa mukono wa Yesu Kristo.

**WAIMBAJI**: Utukufu kwako, ee Bwana, utukufu kwako.

*Pahali pa wimbo*: Niwajibu kweli… *leo, tutaimba hii:*

*Sauti ya tano*

Malaika aliita Mujaliwa neema, Bikira Safi, salamu na tena nitasema salamu, Mwana wako alifufuka siku ya tatu Kaburini.

Ungae, ungae Yesusalema mupya, kwa sababu utukufu wa Bwana umepambazuka juu yako. Cheza sana na shangilia, ee Sayuni, na ewe Mzazi Mungu Safi furahi katika Ufufuo wa Mwana wako.

*Mbele ya hii sala ya mwisho Padri atasoma Mafundisho ya Mtakatifu Baba yetu Yoane Kristostomo. Kisha yake tunaimba Apolitikion yake:*

## Mafundisho ya Mtakatifu Baba yetu Yoano Kristostomo

Mtu wowote mwabudu tena rafiki wa Mungu afurahi juu ya hii mwangaza wa sikukuu nzuri. Mtumishi wowote mwema awe na furaha kubwa kwa ajili ya Bwana wake! Yule alijitoa katika mafungo apate kupokea sasa mushahara wake! Yule alitumika tangu saa ya kwanza apokee sasa mushahara wake wa kweli. Kama mumoja alikuja kisha saa ya tatu afurahie hii siku na kuishukuru! Kama mumoja alichelewa mpaka saa sita, asikuwe na shaka, kwa sababu hapoteze kitu! Kama kuna mmoja aliongojea mpaka saa tisa, ajongee bila shaka! Kama kuna mmoja alichelewa mpaka saa kumi na moja, asiwe na haya ya ukosefu wa juhudi yake, kwa sababu Rabi ni mwema, anapokea wa mwisho kama vile wa kwanza. Anapokea ku mapumziko yule wa saa ya kumi na moja sawa mtumishi wa saa ya kwanza. Anahurumia wa mwisho tena anatunza wa kwanza. Analeta kwa huyu, na anahurumia mwengine. Anapokea matendo tena anakubali mwoyo mwema kwa mapendo. Anaheshimia tendo tena anasifu nia nzuri. Kwa hivi, muwe wote na furaha ya Bwana wenu; wa kwanza kama wa mbili, mutapokea tunzo lake. Watajiri sawa wamaskini, wenyi kukataa na wavivu muungane wote juu ya kusifu hii siku. Kama mulifunga ao hamukufunge, leo mufurahi. Meza iko tayari, kuleni wote; mwana ngombe eko tayari, hata mmoja asirudi na njaa. Mukubali wote ku karamu ya imani, ku hazina ya wema. Hata mumoja asisikitike juu ya umaskini wake, kwa sababu Ufalme unaonekana kwa ajili ya wote. Hata mumoja asilielie juu ya makosa yake, kwa sababu huruma inatokea kaburini. Hata mumoja asiogope mauti, kwa sababu lufu ya Bwana ilitukomboa wote; alishinda mauti kisha kufa kwake. Yeye alishuka katika wafu, kwa lufu yake alishinda mauti. Alijaza mauti na uchungu wakati mwili wake ulishuka kuzimuni. Ni kwa hii Nabii Isaya alieleza ya kama: Mauti ilisirika wakati mulikutana chini ya udongo. Mauti ilizani ya kama ni mwili wa mwanadamu, lakini alikuwa Mungu mbele yake; ilizani ya kama ni mwanadamu, lakini ni mtawala wa mbingu; ilipokea ile iliona, ilianguka kwa sababu haikujue umungu wake.

Ee lufu, wapi ushindi wako?
Kaburi, wapi ushindi wako?

Kristu amefufuka, lakini wewe unanguka chini. *(Taifa anajibu: Amefufuka)*

Kristu amefufuka, mashetani wanaanguka.

Kristu amefufuka, malaika wanafurahi.

Kristu amefufuka, tazama uzima unatawala.

Kristu amefufuka, hakuna wafu kaburini. Kwa sababu Kristu amefufuka katika wafu waliotangulia kulala. Kwa kuwa Utukufu na Uwezo ni kwake milele na milele. Amina.

**APOLITIKION YA MTAKATIFU YOANE.** *Sauti ya mnane*

Kwa kinywa chako kama taa, neema imekuja duniani na ulimwengu uliangaziwa, umefunua hazina ya fazila, umetuonyesha ukubwa wa unyenyekevu. Utufundishe na kinywa chako, ewe Baba yetu Yoane Krisostome, utuombee kwa Mwana, Kristu Mungu, aokoe roho zetu.

*Waimbaji hawataimba:* Jina la Bwana lihimidiwe tangu sasa. . . *lakini wataimba mara tatu:* Kristu alifufuka…

*Ku mwisho ya Liturgia Padri atapaza sauti na msalaba pa mukono wake atasema mbele ya waaminifu wote:* Kristu alifufuka. *Waaminifu watajibu:* Kweli alifufuka. *(Vile watafanya mara tatu).*
*Kisha padri atasema:* Utukufu kwa Ufufuo wake Takatifu wa siku tatu.
*Waaminifu watamujibu:* Tunasujudu Ufufuo wake wa siku tatu.

*Na kisha watu wote wataimba*: Kristu alifufuka katika wafu kwa lufu alishinda mauti, kwa wale waliokuwa ndani ya Kaburi, aliwapatia uzima.

# SALA YA MANGARIBI YA MAPENDO KWA SIKU YA UFUFUO YA BWANA YESU KRISTU

**Elezo:** *Padri anavaa manguo yake takatifu yote, anakamata pa mukono ya kuhume chetezo na ku mukono ya kushoto mushumaa ya kuwaka, anaanza kufukiza Meza Takatifu na kusema hivi:*

**PADRI**: Utukufu kwa Utatu Mtakatifu, wenye asili moja, Muumba wa uzima, usiotengana, daima, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**WAIMBAJI**: Amina.

**PADRI**: Kristu alifufuka *(mara tatu).*

**Elezo***: Mwisho ya mwimbo: "Kristu alifukuka… hile ya tatu, wataimba waimbaji na padri atakuwa pa mulango Bora na atafukiza na chetezo ma picha Takatifu na kisha waaminifu pempeni.*

**WAIMBAJI**: Kristu alifukuza *(mara sita).*

Na mistari ya Zaburi 67 (68) sawa ku mwanzo ya Liturgia ya Ufufuo.

*Kisha **PADRI** Ektenia mkubwa .*

**WAIMBAJI**: Bwana nimekuita. . . *Sauti ya mbili.*

Kituo: Kama wewe Bwana, ukihesabu maovu, ee Bwana, nani atakayesimama? Lakini usamehe ni pamoja nawe, ili uogopwe.

Kujeni tumwabudu huyu alizaliwa kwa Baba mbele ya nyakati, Mungu Neno aliyechukuwa mwili kwa Bikira Maria; kwa sababu alivumilia Msalaba, alijitoa ku maziko kwa kutaka kwake, na alifufuka katika wafu, aliniokoa mimi mpotevu.

Kituo: Ninangojea Bwana, nafsi yangu inangoja, na ninatumainia neno lake.

Kristu Mwokozi wetu alizima maandiko mbaya ya ndani yetu kwa kuipigilia Msalabani, na aliharibu nguvu ya mauti. Tuabudu Ufufuo wake wa siku ya tatu.

Kituo: Nafsi yangu inangoja Bwana, kuliko walinzi wanaongoja asubui; ndiyo, walinzi wanaongoja asubui. Ee Israeli, utumainie Bwana.

Tuimbieni Ufufuo wa Kristu pamoja na Malaika wakuu; kwa maana huyu ni Mkombozi na Mwokozi wa roho zetu; ni maogopesho ya utukufu, na nguvu ya uwezo, eko nakuja tena kuhukumu dunia aliumba.

Kituo: Maana pamoja na Bwana ni rehema, na pamoja naye ukombozi mingi. Naye atakomboa Israeli na maovu yake yote.

Malaika alihubiri ya kuwa wewe ni Rabi, huyu alisulubiwa na kuzikwa; na aliwaambia wanawake : kujeni tazameni, pahali alipolala Bwana, kwani amefufuka kama alivyosema, kwa kuwa

yeye ni mwenyezi; ndiyo maana tunakuabudu, wewe peke yako msiyekufa. Ee Kristu Mletaji uzima, utuhurumie.
Kituo: Musifu Bwana, ninyi mataifa yote; mumutolee, ninyi watu wote.

Kwa Msalaba wako ulivunja laana ya muti; kwa maziko yako uliharibu nguvu ya mauti; na kwa Ufufuo wako uliangaza ukoo wa wanadamu; kwa hii, tunapaza sauti na kusema : Ee Kristu mwema na Mungu wetu, utukufu kwako.
Kituo: Maana rehema yake ni kubwa; na kweli ya Bwana inakaa milele. Musifu Bwana.

Mbele yako, Bwana, milango ya mauti ilifunguka na woga; wachungaji wa kaburi waliogopa kwa kukuona; kwa maana ulivunja milango ya shaba, na kuzuia makomeo ya chuma, na ulituondoa toka giza na kivuli cha mauti, na ulivunja minyororo ilitufunga.

Utukufu kwa Baba. . . *Sauti ya mbili.*

Tunapoimba wimbo wa wokovu, tunaimba : kujeni wote nyumbani mwa Bwana tusujudu na tuseme : Ewe uliyesulubiwa juu ya muti, na kufufuka katika wafu, na uliye katika kifua cha Baba, samehe zambi zetu.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION** *Sauti ya mbili*

Kivuli cha sheria kimefifia kwani neema imekuja; kama kichaka kilipowaka moto bila kuteketezwa, vivyo hivyo Bikira ulizaa na ulikaa Bikira; pahali pa nguzo ya moto, jua la haki lilipanda pa fasi ya Musa, ndiye Kristu aliye wokovu wa roho zetu.

**MWANGAZA UPOLE (ILARON). . . PROKIMENON**

Ni nani aliye Mungu Mukubwa kama Mungu wetu, Wewe ni Mungu peke yako aliyetenda matendo ya ajabu.
**MSOMAJI**: Ee Mungu, ulionyesha mataifa yako nguvu yako.
Ni nani aliye Mungu Mkubwa. . .
Kituo: Na nikasema: sasa nitanza; hii ni uwezo wa mukono wa kuume wa Mwenyezi
**WAIMBAJI**: Ni nani aliye Mungu Mkubwa. . .
**MSOMAJI**: Nilikumbuka matendo ya Bwana na nilifurahi.
**WAIMBAJI**: Ni nani aliye Mungu Mkubwa. . .
**PADRI:** Hekima; Inukeni tusikilize Evangelio Takatifu. Amani kwa wote.
**WAIMBAJI:** Na kwa roho yako.
**PADRI:** Somo ya Evangelio Takatifu ilioandikwa na Yoane Mwevangelizaji. Tusikilize.
**WAIMBAJI:** Utukufu kwako, ee Bwana. utukufu kwako.

**EVANGELIO katika Mwevangelizaji Yoane** (20, 19-25).

*Elezo: Hii Evangelio Kanisa yetu inaleta baraka kuisoma katika lugha mbalimbali.*

Basi mangaribi ya siku ile ile, ikiwa siku ya kwanza ya juma, wakati milango ilipofungwa pahali walipokuwa wanafunzi kwa sababu ya kuogopa Wayuda, Yesu akakuja, akasimama katikati, akasema nao: Amani kwenu. Naye akikwisha kusema maneno haya, akawaonyesha mikono yake na mbavu zake. Basi wanafunzi wakafurahi wakati walipoona Bwana.

Basi Yesu akasema nao mara ya pili: Amani kwenu; kama Baba alivyonituma mimi, ninawatuma ninyi vilevile. Naye wakati alipokwisha kusema maneno haya, akawapulizia, akawaambia: Mupokee Roho Mutakatifu. Wo wote mukiwasamehe zambi, zinasemehewa kwao, na wo wote mukiwafungia zambi, zinafungwa kwao.

Lakini Tomasi, mumoja wa wale kumi na wawili, anayeitwa Mupacha, hakuna pamoja nao wakati alipokuja Yesu. Basi wanafunzi wengine wakamwambia: Tumeona Bwana.
Lakini akawaambia: Nisipoona katika mikono yake alama za misumari, na kutia kidole changu katika alama za misumari, na kutia mukono wangu katika mbavu zake, sitaamini hata kidogo.
**WAIMBAJI:** Utukufu kwako, ee Bwana. utukufu kwako.
**SHEMASI:** Tuseme sisi wote, kwa moyo wetu na kwa roho yetu, tuseme.
**MSOMAJI** *atasema kisha kila ombi:* Bwana, hurumia.

**SHEMASI ao PADRI**: Bwana mwenyezi. Mungu wa mababu, tunakuomba, utusikie na ukatuhurumie.

**PADRI:** Utuhurumie, ee Mungu, katika huruma yako kubwa, tunakuomba utusikie na ukatuhurumie.

**PADRI:** Tena tunakuomba kwa ajili ya madini na wakristu waorthodoksi wote.

**PADRI:** Tena tunakuomba kwa ajili ya Mwarkiepiskopo wetu. . . . *(jina lake)*

**PADRI:** Tena tunakuomba kwa ajili ya ndugu zetu, mapadri, washemasi, watawa na wandugu wote katika Kristu.

**PADRI:** Tena tunakuomba kwa ajili ya kupata rehema, uzima, amani, afya, wokovu, ulinzi, usamehe na maondoleo ya zambi za watumishi wa Mungu, madini yote na wakristu waorthodoksi ambao wanakaamo na wanakutana katika muji huu *(ao nyumba ya watawa)*, wa parokia, na walaiki, na wasaidizi wa hii hekalu takatifu.

**PADRI:** Tena tunakuomba kwa ajili ya watulivu na wenye heri, wajengaji wa hii hekalu takatifu, kwa ajili ya baba na ndugu zetu waliofariki ambao wamelala kaburini na kwa ajili ya waorthodoksi wanaolala hapa na popote duniani.

**PADRI:** Tena tunakuomba kwa ajili ya wafazili wa hii hekalu takatifu na heshima, kwa ajili ya waletaji, kwa ajili ya wote wenye kutumikamo, na wenye kuimbiamo, na kwa ajili ya watu wote waliyo hapa ambao wanaongojea rehema yako kubwa.

**PADRI:** Kwa kuwa wewe ndiwe Mungu wa huruma na mpenda wanadamu na tunakutukuza. Baba. Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**WAIMBAJI:** Amina.

**MSOMAJI ao PADRI** mkubwa:

Ee Bwana, utujalie mangaribi hii kutulinda na zambi, umehimidiwa u, ee Mwana na Mungu wa Baba zetu, jina lako limehimidiwa na limetukuzwa milele. Amina. Ee Bwana, huruma yako iwe nasi tunavyokutumaini wewe, Ee Bwana umehimidiwa u, unifundishe zilizo haki zako. Ee Mtakatifu, umehimidiwa u, uniangaze kwa haki zako. Ee Bwana, huruma yako ni ya milele, usikose kutuangalia sisi viumbe vya mikono yako. Sifa na utukuufu ni wako, wa Baba, na wa Mwana na waRoho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

**SHEMASI:** Tumalize ombi letu la mangaribi kwa Bwana.

**WAIMBAJI:** Bwana, hurumia.

**SHEMASI:** Utulindie, utuokoe, utuhurumie, utuchunge, ee Mungu kwa neema yako.

**WAIMBAJI:** Bwana hurumia.

**SHEMASI:** Mangaribi hii kamili iwe timilifu, takatifu, tulivu, yasio zambi, tuombe kwa Bwana.

*Waimbaji wataimba kisha kila ombi:* Utupe, ee Bwana.

**SHEMASI:** Malaika wa amani, mlinzi wa roho na miili yetu, tuombe kwa Bwana.

**SHEMASI:** Usamehe na maondoleo ya zambi zetu na ya makosa yetu pia, tuombe kwa Bwana.

**SHEMASI:** Vilivyo vyema na vifaavyo kwa roho zetu, tena kuwe amani katika dunia, tuombe kwa Bwana.

**SHEMASI:** Kuyamaliza maisha yetu inabaki katika amani na toba, tuombe kwa Bwana. .

**SHEMASI:** Tuombe ili mwisho wa maisha yetu uwe kikristu, kwa amani, bila aibu, tena tuone mufano mzuri mbele ya kiti cha hukumu cha Kristu.

**SHEMASI:** Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili, asiye na doa, mbarikiwa kushinda Malkia wetu mtukufu. Mzazi-Mungu na Bikira daima, pamoja na watakatifu wote, ili sisi kila mmoja mwenyewe na wenzetu wote, hata maisha yetu pia, tujiweke mikononi mwa Kristu Mungu.

**WAIMBAJI:** Kwako, ee Bwana.

**PADRI:** Kwa kuwa u Mungu mwema na mpenda wanadamu, na kwako tunautoa utukufu kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

**PADRI:** Amani kwa wote.

**WAIMBAJI:** Na kwa roho yako.

**PADRI:** Tuinamishe vichwa vyetu kwa Bwana.

**WAIMBAJI:** Kwako, ee Bwana.

*Sala ya kuinamisha nayo kichwa, sauti ya chini:*

**PADRI:** Ee Bwana Mungu wetu uliyeinamisha mbingu na ukashuka kwa ajili ya wokovu wa wanadamu, tazama watumishi wako na uriti wako kwa sababu wewe ni Kuhani Mshindi na Mpenda-wanadamu usiyeongojea msaada wa wanadamu, maana wao wanaongojea huruma yako na kutumainia wokovu wako, uwalinde hii mangaribi na hii usiku hata na wakati wote kwa maadui na kwa matendo ya Shetani muovu na mwenye mawazo mbaya.

*Padri anapaza sauti.*

**PADRI:** Kwa kuwa uwezo wa ufalme wako uhimidiwe na utukuzwe Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

### APOSTIKHA *Sauti ya mbili*

Ufufuo wako, ee Kristu Mwokozi, uliangaza ulimwengu nzima, na uliita tena kiumbe chako; Bwana mwenyezi, utukufu kwako.

*Kisha tunaimba WIMBO YA PASKA (Angalia Masifu ya Orthros ya Paska: Sauti ya tano*

1. Paska zabihu leo imeonekana kwetu, Paska mupya Takatifu. . .
2. Kujeni Wanawake. . .
3. Wanawake Wabebaji manukato. . .
4. Paska ya furaha, Paska ya Bwana Paska. . .

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .

Ufufuo ni leo na tuangazwe kwa Karamu. . .

**KUAGA (APOLISIS)**

## MU KAZI MOJA ASUBUI YA JUMA DIAKENISIMOS

*Elezo: Padri atavaa manguo yake takatifu, atatayarisha chetezo, atakamata Msalaba na mushumaa ku mukono wake wa kushoto, na chetezo ku mukono wake wa kuume, atafukiza mara tatu Evangelio juu ya Meza takatifu na anasema :*

Utukufu uwe daima kwa Utatu Mtakatifu, wenye asili moja, Muumba wa uzima, usiotengana, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**MWIMBAJI**: Amina.

**PADRI**: Kristu alifufuka katika wafu, kwa lufu alishinda mauti, kwa wale waliokuwa ndani ya Kaburi, aliwapatia uzima. *(mara tatu).*

*Kisha Padri atasema shairi moja-moja ya Zaburi 67( 68) na waimbaji wataimba:* Kristu alifufuka. . .

Mistari:

1. Mungu asimame, adui zake zote wasambazwe; wenye kumuchukia wakimbie vilevile mbele yake. Kristu alifufuka. . .
2. Kama moshi inavyopeperushwa, hivi uwapeperushe; kama nta inavyoyeyuka mbele ya moto. Kristu alifufuka. . .
3. Hivi waovu wapotee mbele ya Mungu, lakini wenye haki wafurahi. Kristu alifufuka. . .
4. Hii ndiyo siku aliyofanya Bwana, tushangilie na kufurahiwa nayo. Kristu alifufuka. Utukufu kwa Baba. . . Kristu alifufuka. . .

Sasa na siku zote. . . Kristu alifufuka. . .

*Kisha Padri atapaza sauti na kusema :* Kristu alifufuka katika wafu, kwa lufu alishinda nauti, kwa wale waliokuwa ndani ya Kaburi.

**WAIMBAJI**: . . . aliwapatia uzima.

**PADRI ao SHEMASI** *atapaza sauti atasema hivi Irinika (maombi ya amani) :*

*Waimbaji watajibu kwa kila ombi:* Bwana hurumia.

**SHEMASI***:*

Kwa amani tumwombe Bwana.

PADRI: Kwa ajili ya amani kutoka juu, na ya wokovu wa roho zetu, tumwombe Bwana.

PADRI: Kwa ajili ya amani ya dunia yote, ya kusimama kuzuri kwa Ekklezia Takatifu ya Mungu na ya umoja wa wote, tumwombe Bwana.

PADRI: Kwa ajili ya nyumba hii Takatifu, na ya wanaoingiamo na imani, na heshima na kwa kumuogopoa Mungu, tumwombe Bwana.

PADRI: Kwa ajili ya Arkiepiskopo wetu. . .*(jina lake)*, ya Upresbiteri uheshimiwa, ya Ushemasi katika Kristu, ya Wateule wote na ya Watu wote, tumwombe Bwana.
PADRI: Kwa ajili ya mji huu na inchi hii, kila mji na inchi, na ya waaminifu wanaoishi humo, tumwombe Bwana.
PADRI: Kwa ajili ya kutupa hewa nzuri, udongo nzuri, na nyakati za amani, tumwombe Bwana.
PADRI: Kwa ajili ya wasafiri hewani, baharini na nchini, ya wagonjwa, ya wenye kuteswa, ya mateka, na kwa ajili ya wokovu wao, tumwombe Bwana.
PADRI: Kwa ajili ya kutuokoa toka kila sikitiko, hasira, hatari na uhitaji, tumwombe Bwana.
PADRI: Utulinde, utuokoe, utuhurumie, utufazilie, ee Mungu kwa neema yako.
PADRI: Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili, Asiye na doa, Mbarikiwa kushinda, Bibi wetu Mtukufu, Mzazi-Mungu na Bikira daima, pamoja na watakatifu wote, ili sisi kila mmoja mwenyewe, na wenzetu wote, hata maisha yetu pia, tujiwekeye mikononi mwa Kristu Mungu.
MSOMAJI: Kwako, ee Bwana.
PADRI: Kwa kuwa utukufu wote, na heshima na usujudu ni haki yako, ya Baba, na ya Mwana na ya Roho Mtakatifu. Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

*Kisha tunafwata **KANUNI YA UFUFUO WA BWANA YESU KRISTU***
*Wimbo wa Mtakatifu Yoane Damaskinos*
*Elezo: Ku mwimbo wa Kanuni ya Yoane Damaskinos tutaimba Eksapostilarion ya Ufufuo (mara tatu). Na kisha mara moja tutaimba Masifu.*

## MASIFU. *Sauti ya mbili :*

*Tutaimba Masifu ya Ufufuo ya Siku ya Mungu katika kitabu cha Paraklitiki.*

Kila mwenye pumuzi na kila kiumbe kinakusifu, ee Bwana, kwa sababu kwa Musalaba wako uliharibu mauti, sababu ya kuwaonyesha wanadamu ufufuo wako katika wafu, kwa mapendo yako kwa Mpenda-wanadamu.

Wayuda walisema nini, namna gani waaskari waliyochunga Mfalme walimupoteza? Sababu gani jiwe halikuchunge mwamba wa uzima? Ao walete huyu alizikwa, ao wamwabudu Bwana alifufuka, wakisema pamoja na sisi: Ee Mwokozi mwenye kutujaza rehema yako, utukufu kwako.

Mataifa, furahini na shangilieni! Malaika aliyekaa juu ya jiwe la Kaburi alitutangazia habari njema akasema : Kristu, Mwokozi wa dunia alifufuka katika wafu, na alijaza ulimwengu na harufu yake nzuri. Mataifa, furahini na shangilieni.

Bwana, siku ya wewe kupata mwili, Malaika mumoja alimwambia Mjaliwa neema : Salamu! Siku ya Ufufuo wako, Malaika mumoja alikuja kusukuma jiwe la mulango wa kaburi yako tukufu : pahali pa sikitiko na mauti, mumoja alileta furaha, mwingine alimutangaza Bwana Chemchem ya uzima; ndio maana tunakutukuza tukisema : Ewe Mfazili wa dunia, utukufu kwako.

*Elezo: Kisha tutaimba WIMBO WA PASKA (Angalia Masifu ya Orthros ya Paska) : Sauti ya tano.*
1. Paska zabihu leo imeonekana kwetu, Paska mupya Takatifu. . .
2. Kujeni Wanawake. . .
3. Wanawake Wabebaji manukato. . .
4. Paska ya furaha, Paska ya Bwana Paska. . .

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .
Ufufuo ni leo na tuangazwe kwa Karamu. . .
**PADRI:** Tumalize ombi letu ...Kuaga.
*ELEZO: Mu ibada ya Liturgia tutafwata desturi sawa vile jana Siku ya Ufufuo wa Kristu.*

# MU KAZI MOJA MANGARIBI YA JUMA DIAKENISIMOS

*Elezo: Tutaimba sawa jana. Waimbaji wataanza kuimba:* «Bwana nimekuita...». *Watasimama pa shairi ya sita na wataimba Wimbo wa Ufufuo ya Kristu ya Paraklitiki.*

*Sauti ya Tatu.*

Nguvu ya mauti ilivunjwa kwa Msalaba wako, ee Kristu Mwokozi, na udanganyifu wa Shetani uliharibiwa, basi wanadamu wenye kuokolewa kwa imani wanakutolea daima nyimbo zao.

Ulimwengu iliangazwa kwa Ufufuo wako, ee Bwana, Paradizo ilifunguliwa tena; na kwa kukusifu viumbe vyote, vinakutolea daima nyimbo zao.

Ninatukuza nguvu ya Baba, na ya Mwana, naimbia uwezo wa Roho Mtakatifu, umungu usiyogawanyika na usiyoumbwa, Utatu wa asili moja, wenye kutawala milele na milele.

Ee Kristu, tunaabudu Msalaba wako heshimiwa, tunaimbia na kutukuza Ufufuo wako; kwa ajili ya alama ya vidonda vyako, sisi wote tumepona.

Tunamwimbia Mwokozi aliyepata mwili kwa Bikira; Aliyesulubiwa kwa ajili yetu, na aliyefufuka siku ya tatu sababu ya kutupa sisi rehema yake kubwa.

Wakati alishuka kuzimuni, Kristu alitangaza habari njema akisema : Muwe na moyo, nimeshinda; mimi ni Ufufuo; nitawafufua ninyi kwa kuvunja milango ya mauti.

Utukufu kwa Baba...

Tunasimama bila kustahili katika makao yako takatifu, tunakutolea wimbo wetu wa mangaribi, na ndani yetu tunapaza sauti na kusema : Ee Kristu Mungu uliyeangaza ulimwengu kwa ufufuo wako siku ya tatu, opoa watu wako ku mukono wa adui yako, ewe Mpenda-wanadamu.

Sasa na siku zote...**THEOTOKION**.

Ewe Mtukufu kamili,namna gani hatutashangaa kuzaliwa kwa Mungu-mtu? Maana bila kujua mume, ee Bikira usiye na doa, ulizaa Mwana katika mwili bila baba, Huyu aliyezaliwa kwa Baba mbele ya wakati pasipo mama, bila kugeuka, bila kuchanganyika ao kugawanyika, lakini mwenye kulinda hali zake zote mbili. Kwa hii, ee Mama Bikira bibi malkia, umuombe kwa ajili ya wokovu wa roho za wale wenye kukuamini na kukutambua kama Mzazi-Mungu.

**KUINGIA.** Kisha: Mwangaza upole (ilaron)...

**PROKIMENON.** *Sauti ya saba.*

Mungu wako eko mbinguni na duniani, aliumba vitu vyote kwa kutaka kwake.

Shairi: Wakati wana wa Israeli walitoka katika inchi ya Misri na nyumba ya Yakobo ilipokuwa katikati ya watu wabaya, Yudasi akawa patakatifu pa Bwana.

Mungu wako eko mbinguni na duniani, aliumba vitu vyote kwa kutaka kwake.

Shairi: Bahari ilipoona hivi ikakimbia, Yordani ikarudi nyuma.

Mungu wako eko mbinguni na duniani, aliumba vitu vyote kwa kutaka kwake.

Ewe Bahari kwa nini unakimbia? Yordani kwa nini unarudi nyuma?

Mungu wako eko mbinguni na duniani, aliumba vitu vyote kwa kutaka kwake.

SHEMASI: Tuseme sisi wote, kwa moyo wetu na kwa roho yetu, tuseme.
*Shemasi ataendelea sawa yulu mu Juma Mangaribi, siku ya Ufufuo wa Kristu.*
MSOMAJI *atasema kisha kila ombi:* Bwana, hurumia.

## APOSTIKHA *Sauti ya tatu.*

Kwa mateso yako, ee Kristu, ulileta giza ku jua, kwa nuru ya Ufufuo wako, ulifurahisha ulimwengu, pokea wimbo wetu wa mangaribi, ewe Mpenda-wanadamu.

Elezo: Kisha tutaimba WIMBO WA PASKA (Angalia Masifu ya Orthros ya Paska): *Sauti ya tano*

1. Paska zabihu leo imeonekana kwetu, Paska mupya takatifu. . .

2. Kujeni Wanawake. . .
3. Wanawake Wabebaji manukato. . .
4. Paska ya furaha, Paska ya Bwana Paska. . .
Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .
Ufufuo ni leo na tuangazwe kwa Karamu. . .
**PADRI:** Tumalize ombi letu ...

**Kuaga**

**Elez**o*: Mu ibada ya Liturgia tunafwata desturi sawa vile jana, Siku Ya Ufufuo wa Kristu.*

# MU KAZI MBILI ASUBUI YA DIAKENISIMOS

*Tangazo: Na leo na kila siku ya hii Juma Ibada ya asubui inafanyika katika desturi ya siku ya Ufufuo ya Kristu asubui.*

## MASIFU

*Tunaimba na shairi ine wimbo wa Ufufuo katika Kitabu cha Paraklitiki.*

Kujeni, mataifa yote, mujue nguvu ya fumbo ya ajabu; kwani Kristu Mwokozi wetu, Neno aliyekuwa katika mwanzo, alisulibiwa kwa ajili yetu, alizikwa kwa kutaka kwake, na alifufuka katika wafu kusudi aokoe ulimwengu. Tumwabudu yeye.

Ee Bwana, walinzi walieleza maajabu yako yote; lakini baraza ya ubatili, walijaza mukono wao wa kuume na zawadi, waliwaza ya kama wataficha Ufufuo wako, uliyotukuzwa kwa wanadamu. Utuhurumie.

Dunia yote ilijazwa na furaha wakati ilipata maarifa ya ufufuo; kwani Maria Magdalena alikuja kaburini, alikuta Malaika mwenyi kuvaa mavazi ya kuangaa amekaa juu ya jiwe, na akasema: sababu gani munatafuta yeye aliye hai katika wafu; Hayuko hapa, lakini alifufuka kama alivyosema, anawatangulia kwenda Galilaya.

Katika mwangaza yako, ee Rabi Mpenda-wanadamu, tutaona mwangaza; kwa sababu ulifufuka katika wafu, uliwapa wanadamu wokovu kusudi viumbe vyote vikutukuze, wewe peke yako usiye na zambi. Utuhurumie.

*Elezo*:Kisha tutaimba WIMBO WA PASKA (angalia Masifu ya Orthros ya Paska): *Sauti ya tano*
1. Paska zabihu leo imeonekana kwetu, Paska mupya Takatifu. . .
2. Kujeni Wanawake. . .
3. Wanawake Wabebaji manukato. . .
4. Paska ya furaha, Paska ya Bwana Paska. . .
Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .
Ufufuo ni leo na tuangazwe kwa Karamu. . .
Kristu alifufuka. *(mara tatu).*
**PADRI:** Tumalize ombi letu ... **Kuaga.**
*ELEZO: Mu Ibada ya Liturgia tunafata Desturi sawa vile jana, Siku Ya Ufufuo ya Kristu.*

# MU KAZI MBILI MANGARIBI YA DIAKENISIMOS

*Elezo: Tutaimba sawa jana. Waimbaji wataanza kuimba: «Bwana nimekuita...». Watasimama pa shairi sita na wataimba Wimbo wa Ufufuo wa Kristu katika kitabu cha Paraklitiki.*

*Sauti ya ine*

Ee Kristu Mungu, tunapoabudu daima Msalaba wako wenye kuleta uzima, tunatukuza ufufuo wako wa siku ya tatu; katika hii ulifanya mupya hali ya wanadamu iliyoharibika, ee Mwenyezi, na ulituonyesha njia ya kupanda mbinguni, kwa kuwa wewe peke yako ni Mwema na Mpenda-wanadamu.

Ee Mwokozi, kwa kuondoa mateso iliyoletwa na zambi juu ya muti iliyokataziwa, ulisulubiwa juu ya muti wa msalaba; na kwa kushuka kwako kuzimuni ulivunja milango ya mauti, ee Mungu mwenyezi; ndio maana tunaabudu Ufufuo wako katika wafu, na kwa shangwe tunakutukuza tukisema: Ee Bwana mwenyezi, utukufu kwako.

Ulivunja milango ya Hadeze, ee Bwana, na kwa lufu yako, uliharibu ufalme wa mauti; na uliopoa ukoo wa watu toka uharibifu, mukuleta ku dunia uzima na usiyoweza kuharibika na rehema kubwa.

Kujeni, mataifa, tuimbie ufufuo wa Mwokozi wa siku ya tatu; kwa ajili ya hii tulikombolewa toka minyororo isiyofunguliwa ya Hadeze, na wote tulipata uzima usiyoharibika; tunapaza sauti na kusema : Ewe uliyesulibiwa, uliyezikwa na uliyefufuka, utuokoe kwa ufufuo wako, wewe peke yako Mpenda-wanadamu.

Ee Mwokozi, Malaika na wanadamu wanatukuza ufufuo wako wa siku ya tatu; kwa ajili ya hii mipaka za dunia ziliangazwa, na wote tulikombolewa toka utumwa wa adui, tukipaza sauti: Ewe mwenyezi Mwokozi muletaji-uzima, utuokoe kwa ufufuo wako, wewe peke Mpenda-wanadamu.

Ulivunja milango ya shaba, na kukata mapingo ya chuma, ee Kristu Mungu, na ulifufua uzao wa watu wenye kuanguka; kwa hii tunapaza kwa sauti moja: Ewe Bwana, uliyefufuka katika wafu, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba...

Ee Bwana, kuzaliwa kwako kwa Baba ni kwa mbele ya wakati na ya milele; kupata kwako mwili kwa Bikira ni kwasiyofasiriwa na kufafanuliwa kwa watu; na kushuka kwako Hadezeni ni kwa woga kwa Shetani na malaika wake; kwani ukishinda mauti, ulifufuka katika siku tatu, ukiwapa watu uzima usiyoharibika na rehema kubwa.

Sasa na siku zote...**THEOTOKION**.

Nabii Daudi alitekuwa Babu-Mungu kwa ajili yako, alikutabiri katika zaburi kwa yule aliyekufanyia maajabu: Malkia anasimama ku mukono wako wa kuume. Kwa sababu Mungu alikuonyesha wewe mama muletaji uzima, yeye aliyetwa mwili toka wewe kwa mapenzi yake bila baba, kusudi aumbe mara ingine mufano yake, iliyoharibika kwa tamaa, na kupata kondoo aliyepotea mulimani, kumubeba ku mabega yake, na kumutoa kwa Baba, kwa kuiunganisha pamoja na Ezi za mbinguni kwa kutaka kwake, na kuokoa dunia, ee Mzazi-Mungu; yeye ni Kristu, mwenye juwa na rehema kubwa zaidi.

**KUINGIA**. *Kisha:* Mwangaza upole (ilaron)...

**PROKIMENON.** Sauti ya mnane.

Nitapazia Mungu sauti yangu; Hata Mungu sauti yangu, na ye atanisikia.
Shairi: Kwa siku ya taabu yangu nilitafuta Bwana.
Nitapazia Mungu sauti....
Shairi: Ninanungunika, na roho yangu inashindwa,
Nitapazia Mungu sauti....
SHEMASI: Tuseme sisi wote, kwa moyo wetu na kwa roho yetu, tuseme.
MSOMAJI *atasema kisha kila ombi:* Bwana, hurumia.

## APOSTIKHA *Wimbo ya Paraklitiki. Sauti ya Ine***.**

Ee Bwana, ulipopanda juu ya Msalaba, ulizimisha mafingo yetu yakutoka kwa mababu zetu; na uliposhuka ndani ya hadeze, uliopoa wafungwa tangu zamani, ukaleta uzima usiyoharibika ku uzao wa watu; kwa hii tukiimba tunasifu ufufuo wako, uletao uzima na wokovu.

Tangazo:Kisha tunaimba WIMBO YA PASKA (Angalia Masifu ya Orthros ya Paska: *Sauti ya tano*
1. Paska zabihu leo imeonekana kwetu, Paska mupya Takatifu. . .
2. Kujeni Wanawake. . .
3. Wanawake Wabebaji manukato. . .
4. Paska ya furaha, Paska ya Bwana Paska. . .
Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .
Ufufuo ni leo na tuangazwe kwa Karamu. . .
**PADRI:** Tumalize ombi letu ... **Kuaga.**
*TANGAZO: Mu Ibada ya Liturgia tunafata Desturi sawa vile jana, Siku Ya Ufufuo ya Kristu.*

# MU KAZI TATU ASUBUI YA DIAKENISIMOS

*Tangazo: Na leo na kila siku ya hii Juma Ibada ya asubui inafanyika katika desturi ya siku ya Ufufuo wa Kristu Asubui.*

## MASIFU

*Tunaimba na shairi wa ine wimbo ya Ufufuo ya Kitabu Paraklitiki. Sauti ya Ine.*

Ewe uliyevumilia, Msalaba na lufu, na ulifufuka katika wafu, Bwana Mwenyezi, tunasifu Ufufuo wako.

Pa Msalaba wako, ee Kristu, ulituopoa toka fingo ya Kale, na kwa lufu yako uliharibifu Shetani, mwenye jeuri kwa hali yetu, na kwa ufufuo wako ulijaza vyote kwa furaha; kwa hii tunapaza sauti kwako: Ewe Bwana, uliyefufuka katika wafu, utukufu kwako.

Pa Msalaba wako, ee Kristu Mwokozi, utuongoze kwa ukweli wako, na utuokoa toka mitego ya adui; Ewe uliyefufuka katika wafu, utufufue sisi tuliyoanguka katika zambi, myolosha mukono wako, ee Bwana Mpenda-wanadamu, kwa upatanisho ya watakatifu wako.

Pasipo kujitenga toka kifua cha Baba yako, ee Mwana wa pekee Neno la Mungu, ulikuja duniani kwa kupenda-wanadamu, ukijifanya mtu bila ugeuzo, na ulivumilia katika mwili Msalaba na lufu, ee Msiyeteswa katika umungu; ukifufuka katika wafu, ulipatia uzima usiyokufa kwa uzao wa watu, sawa yako Mwenyezi.

*Tangazo:Kisha tunaimba WIMBO WA PASKA (Angalia Masifu ya Orthros ya Paska): Sauti ya tano:*

1. Paska zabihu leo imeonekana kwetu, Paska mupya Takatifu. . .
2. Kujeni Wanawake. . .
3. Wanawake Wabebaji manukato. . .
4. Paska ya furaha, Paska ya Bwana Paska. . .

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .
Ufufuo ni leo na tuangazwe kwa Karamu. . .
Kristu alifufuka. (mara tatu).
**PADRI:** Tumalize ombi letu ... **Kuaga.**
*TANGAZO: Mu Ibada ya Liturgia tunafata Desturi sawa vile jana, Siku Ya Ufufuo ya Kristu.*

# MU KAZI TATU MANGARIBI YA DIAKENISIMOS

*Tangazo: Tunaimba sawa jana. Waimbaji wataanza kuimba: «Bwana nimekuita...». Watasimama pa shairi sita na wataimba Wimbo ya Ufufuo ya Kristu ya Paraklitiki.Sauti ya Tano*

Kwa Msalaba wako muheshimiwa, ee Kristu, ulipatiya Shetani haya, na kwa ufufuo wako ulifanya uchungu wa zambi kuwa bure, na ulituokoa toka milango ya mauti; tunakutukuza, ee Mwana wa pekee.

Huyu anayeleta ufufuo ku ukoo wa watu, alipelekwa kama kondoo kuchinjwa; wafalme wa hadeze wakatetemeka mbele yake, na milango ya maumivu iliyanyuliwa; kwani Kristu, Mfalme wa ututuku, aliingia, akiwaambia wafungwa: Tokeni, na wale walio katika giza, mujionyeshe.

Ajabu kubwa! Muumba wa wasioonekana, akiteswa kwa mwili kwa ajili ya kupenda wanadamu, akafufuka sawasawa na musiyekufa. Kujeni wazao wa mataifa, tumuabudu huyu; kwani kwa wema wake tukiondoshwa toka udanganyifu, tumefundishwa kuimba Mungu mmoja, katika aine tatu.

Tunautoa kwako uabudu wa mangaribi, ewe Nuru isiyomwisho uliyeangaza dunia kama katika kioo kwa mwili katika mwisho ya milele, na ulishuka mupaka Hadeze, na kule ulizambalisha giza, ukaonyesha nuru ya ufufuo kwa mataifa; Bwana muletaji-nuru, utukufu kwako.

Tumusifu Kristu, mkubwa wa wokovu wetu; kwani wakati huyu alipofufuka katika wafu, dunia imeokolewa katika udanganyifu, kundi la Malaika wanafurahi, udanganyifu wa mashetani unatoka; Adamu aliyeanguka amefufuka, na Shetani ameharibiwa.

Askari walinzi waliambiwa kwa wavunja-sheria: Mufichw ufufuo wa Kristu, na mukamate feza, na museme: waakti tulipolala mufu aliimbwa toka kaburi. Nani aliona, nani alisikia siku moja watu wanaimba mufu? Na tena mwenye kupakaliwa na manukato na uchi, mwenye kuacha manguo yake ya maziko ndani ya kaburi? Musidanganyiwe, Wayuda; mufundishwe maneno ya manabii, na mujue ya kama kweli huyu ni Mwokombozi wa dunia na mwenyezi.

Utukufu kwa Baba...

Bwana, uliyenyanganya Hadeze, na ulishinda mauti, Mwokozi wetu, uliyeangaza dunia, kwa Msalaba wako muheshimiwa, utuhurumie.

Sasa na siku zote...**THEOTOKION**.

Katika Bahari Nyekundu, wakati moja mufano wa Bibi-arusi musiyeolewa ulijionyesha. Kule Musa alikuwa mugawanyi wa maji, hapa Gabrieli alikuwa mutumishi wa ajabu. Wakati ule Israeli alipita vilindini bila kulowanishwa, sasa Bikira alizaa Kristu bila mbegu; Bahari kisha kupita kwa Israeli ilibaki isiyowezekana kupita; Musiyeolewa kisha kuchukua Emmanueli, alibaki bila kuharibiwa. Mungu ndiwe uliye na uliyekuwako, na uliyefunuliwa sawasawa na mutu, utuhurumie.

**KUINGIA.** *Kisha*: Mwangaza upole (ilaron)...

**PROKIMENON** *Sauti ya mnane.*

Usikilize maombi yangu, ee Mungu, wala usijifiche kwa kusihi kwangu.
Shairi: Unisikilize na kunijibu.
Usikilize maombi yangu...
Shairi: Na hofu za mauti zimeniangukia.
Usikilize maombi yangu...
Shairi: Lakini mimi, nitaita Mungu.
Usikilize maombi yangu...
SHEMASI: Tuseme sisi wote, kwa moyo wetu na kwa roho yetu, tuseme.
MSOMAJI *atasema kisha kila ombi:* Bwana, hurumia.

### APOSTIKHA *Sauti ya Ine***.**

Tunakutukuza kwa sauti ya nyimbo, ee Kristu Mwokozi, mwenye kutwaa mwili bila kugawanyika toka mbingu; kwani ulikubali Msalaba na lufu, kwa ajili ya ukoo wetu, kwa kuwa wewe ni Bwana mpenda-wanadamu; ukinyanganya milango ya Hadeze, ulifufuka katika siku tatu kwa kuokoa nafsi yetu.

*Tangazo:Kisha tunaimba WIMBO WA PASKA (Angalia Masifu ya Orthros ya Paska):*

*Sauti ya tano*

1. Paska zabihu leo imeonekana kwetu, Paska mupya Takatifu. . .
2. Kujeni Wanawake. . .
3. Wanawake Wabebaji manukato. . .
4. Paska ya furaha, Paska ya Bwana Paska. . .

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .
Ufufuo ni leo na tuangazwe kwa Karamu. . .
**PADRI:** Tumalize ombi letu ... **Kuaga.**

*TANGAZO: Mu Ibada ya Liturgia tunafwata Desturi sawa vile jana, Siku Ya Ufufuo wa Kristu.*

## MU KAZI INE ASUBUI YA DIAKENISIMOS

*Tangazo: Na leo na kila siku ya hii Juma Ibada ya asubui inafanyika katika desturi ya siku ya Ufufuo ya Kristu Asubui.*

**MASIFU** *Sauti ya tano*

Ee Bwana, wakati Kaburi ilipotiliwa muhuri kwa wavinja-sheria, ulitoka katika Kaburi, sawa vile ulizaliwa kwa Mazai-Mungu; Malaika wako wasiyo-mwili hawakujua namna gani ulitwaa mwili;

askri waliokuchunga, hawa kusikia wakati gani alifufuka; kwa sababu hii mambo mbili ya ajabu ilifichwa kwa wenye kutafuta; lakini miujiza hii zimeonekanana kwa wenye kuabudu siri kwa imani na wanaoimba: Uturudishie shangwe na rehema kubwa.

Ee Bwana, ukivunja mapingo ya milele, ukikata minyororo, ulifufuka toka Kaburi, ukiacha sanda, kusudi ya kuishuhudia kweli maziko yako ya siku tatu; na ulitangulia kwa Galilaya, mwenye kulindwa katika pango. Rehema yako ni kubwa, ee Mwokozi msiyesikilikwa, utuhurumie.

Ee Bwana, wanawake walienda kw aharaka Kaburini, kusudi wakuone, ewe Kristu, uliyeteswa kwa ajili yetu; na wakifika, walikutanisha Malaika mwenye kukaa juu ya jiwe, lenye kufingirishwa kwa sababu ya woga, na aliwapazia sauti, akisema: Bwana alifufuka; museme kwa Wanafunzi ya kama alifufuka katika wafu, mwenye kuokoa nafsi yetu.

Bwana, kama vile ulitoka ijapokwa kaburi imefungwa, vinyo hivyo uliingia wakati milango ilipofungwa, na ulionekana mbele ya Wanafunzi wako, kwa kuwaonyesha mateso ya mwili wako, uliyokubali, ee Mwokozi muvumilivu; sawa sawa na mtu, muzaliwa wa ukoo wa Daudi, ulivumilia mapigo; laikini sawasawa na Mwana wa Mungu, uliopoa dunia. Rehema yako ni kubwa, ee Mwokozi msiyesikilikwa, utuhurumie.

*Tangazo:Kisha tunaimba WIMBO YA PASKA (Angalia Masifu ya Orthros ya Paska): Sauti ya tano*
1. Paska zabihu leo imeonekana kwetu, Paska mupya Takatifu. . .
2. Kujeni Wanawake. . .
3. Wanawake Wabebaji manukato. . .
4. Paska ya furaha, Paska ya Bwana Paska. . .
Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .
Ufufuo ni leo na tuangazwe kwa Karamu. . .
Kristu alifufuka. *(mara tatu).*
**PADRI:** Tumalize ombi letu ... **Kuaga.**
*TANGAZO: Mu Ibada ya Liturgia tunafata Desturi sawa vile jana, Siku Ya Ufufuo ya Kristu.*

## MU KAZI INE MANGARIBI YA DIAKENISIMOS

*Tangazo: Tunaimba sawa jana. Waimbaji wataanza kuimba: «Bwana nimekuita...». Watasimama pa shairi Kumi na wataimba Wimbo ya Ufufuo ya Kristu ya Paraklitiki na kisha Wimbo ya Mzazi-Mungu kwa Siku Kuu yake Chemchem ya Mpataji-Uzima.*

*Sauti ya Sita.*

Ee Kristu, ikiweza kushinda juu ya Hadeza, ulipanda juu ya Msalaba, kusudi ufufue pamoja nawe,wao waliokaa katika giza ya mauti, wewe uliye na uhuru katikati ya wafu. Wewe uliyechirizika uzima toka nuru yako, ee Mwenyezi na Mwokozi, utuhurumie.

Leo Kristu aliposhinda mauti, alifufuka, kama alivyosema na akaleta shangwe ku ulimwengu, kusudi wote tupaze sauti, na tuimbe hivi: Ee Chemchem ya uzima, Nuru isiyoweza kukaribiwa, Mwenyezi na Mwokozi, utuhurumie.

Ewe Bwana, uliye katika viumbe vyote, tutakimbilia wapi sisi wenye zambi? Juu ya mbinguni? Wewe unakaa. katika Hadeze? Ulishinda mauti. Katika chini ya bahari? Kule ni mukono wako, ee Rabi. Tunakimbilia kwako, tukikusujudu tunakusihi: Ewe Uliyefufuka katika wafu, utuhurumie.

Kwa Msalaba wako, ee Kristu, tunajisifu, tunaimba na tunasifu ufufuo wako; kwa kuwa wewe ni Mungu wetu, hatumujui mwengine ila wewe peke yako.

Tukimuhimidi Bwana daima, tunasifu ufufuo wake; kwa sababu akivumilia Msalaba, aliangamiza lufu kwa lufu yake.

Ututukufu kwa uwezo wako, ee Bwana, kwani uliharibu huyu aliyekuwa na nguvu za lufu, na ulitufanya mupya kwa Msalaba wako, ukitupatia uzima na usiyoweza kuharibika.

*Sasa tunaimba Wimbo wa Mzazi-Mungu Chemchem ya Mletaji-Uzima*

*Olin apothemeni. Sauti ya sita*

Ewe Malkia Mtakatifu kamili, ku mwanzo Rabi wa mbinguni alitimiza kwako tendo la ajabu, kwani toka juu mbinguni chemchem ya uzima alishuka tumboni mwako sawa mvua sababu ya kuleta wema wake duniani, maponyesho na fazila kwa watu wote na kwa wale wenye kuhitaji nguvu ya roho na afya ya mwili katika maji ya neema yako.

Ewe Malkia Bikira, ninaita kweli chemchem yako takatifu kuwa mkate wa mbinguni na wa Paradizo kwa sababu ulimwengu inajaa sawa mutoni na neema ya chemchem yako kwa kutimiza kila mara miujiza ya ajabu kwa wale wenye kutamainia kunywa hii maji, sisi wakristu tunakukimbilia daima na furaha na imani yenye kutakaswa.

Ewe Bibi-Arusi wa Mungu na Bikira, kwa wale wenye kukukimbilia na imani daima unawamwangia maji ya maponyesho toka chemchem yako. Kweli, unagawanya bure neema mingi, maponyesho kwa wagonjwa, nuru kwa vipofu, na unabariki wenye kukukimbilia. Unasimamisha vipofu, wenye kupooza unawapa nguvu, tena ule alikufa ulimufufua kwa kumumwangia maji mara tatu, na uliponyesha wagonjwa wote na kuwaondolea zambi zao.

Utukufu kwa Baba...

Ewe chemchem, nani ataeleza utukufu wako? Kwani unajaa na miujiza mingi na unatimiza maponyesho ya ajabu, unaonyesha watu wote matendo ya heri, apana paka ulifukuza magonjwa mbaya kwa wale walikuja kwako na imani, lakini tena unasafisha zambi rohoni mwao, wewe safi kamili, na unawapa wote neema kubwa.

Sasa na siku zote... **THEOTOKION**. *Sauti ya sita*

Nani hatakuita wewe Mwenye heri, Bikira Mtakatifu kamili? Nani hataimba kuzaliwa kwa Mwana wako bila mume? Kwani Mwana wa pekee aliyeangaa mbele ya wakati kwa Baba, yeye vilevile alitokea kwa wewe uliyesafi, akitwaa mwili usiyosemwa; yeye ni Mungu sawasawa na hali yake, na akajifanya mtu kwa kadiri ya hali ya watu kwa ajili yetu; yeye hagawanyike kwa uso mbili, lakini anajulikana kwetu katika hali mbili bila muchanganyo. Umusihi, ee Bikira mutaratibu na heriu daima, kwa murehemu nafsi yetu.

**KUINGIA** *Kisha:* Mwangaza upole (ilaron)...

**PROKIMENON.** *Sauti ya saba.*

Ninakupenda ee Bwana, nguvu yangu. Bwana ni mwamba wangu na boma langu na mwokozi wangu.
Shairi: Mungu wangu, mwamba wangu, ninayemukimbilia. Ninakupenda ee Bwana....
Shairi: Nitaita Bwana, anayestahili kusifiwa. Ninakupenda ee Bwana....
Shairi: Alisikia sauti yangu toka hekalu lake. Ninakupenda ee Bwana....
SHEMASI: Tuseme sisi wote, kwa moyo wetu na kwa roho yetu, tuseme.
MSOMAJI *atasema kisha kila ombi:* Bwana, hurumia.

## APOSTIKHA *Wimbo ya Paraklitiki. Sauti ya Sita.*

Ufufuo wako, ee Kristu Mwokozi, unaimbiwa kwa malaika mbinguni; na utustahilishe sisi wa dunia, tunakutukuza kwa mioyo safi.

*Tangazo: Kisha tunaimba WIMBO YA PASKA (Angalia Masifu ya Orthros ya Paska). Ao, kama Padri mkubwa anataka waimbaji wataweza kuimba Wimbo ya Apostikha ya Mzazi-Mungu.*

*Sauti ya tano*

1. Paska zabihu leo imeonekana kwetu, Paska mupya Takatifu. . .
2. Kujeni Wanawake. . .
3. Wanawake Wabebaji manukato. . .
4. Paska ya furaha, Paska ya Bwana Paska. . .

**APOSTIKHA YA MZAZI-MUNGU.** *Kheris askitikon...Sauti ya tano.*

Salamu, wewe chemchem mletaji-uzima, unaeneza miujiza katika ulimwengu wote; bahari takatifu kupita maji ya mtoni Nilo, wewe mwenye kumwanga neema; Siloamu ingine ya mbili, mwenye kushota maji ya ajabu katika mwamba, ulipata neema ya Yordani, wewe ni mkate wa wokovu kwa wale wenye kukuomba msaada wako, mikate mingi isiyomalizika; Wewe binti Mama wa Kristu unaleta neema kubwa duniani.

Enyi waaminifu wote, kwa wimbo wa ajabu tunatukuza wimbi ya mbinguni kwani alishusha bila mbegu duniani tone la mbinguni, ndiye Yesu Kristu. Huyu ni maji ya uzima naanawapa wale weko na kiu neema ya wokovu wao, na wenye kuikunywa na imani wanajaa wote na neema mingi juu ya wokovu wao.

Salamu, ewe chemchem mletaji-uzima, mwenye kumwanga daima zawadi, chemchem yenye kuponyesha magonjwa yote kwa uwezo wako; wewe ni nuru ya vipofu na utakaso wa wenye ukoma, unaponyesha wale wenye kukimbilia na imani ku Hekalu yako, uko kweli nyumba ya maponyesho bila malipo lakini tayari kwa wote; wewe mama wa Neno Kristu mwenye kuleta neema kubwa duniani.

Utukufu kwa Baba. . . *Sauti ya tano*

Sisi wenye kupenda sikukuu tuimbe na baragumu na tushangilie kwa hii maji, tucheze na furaha sababu ya matendo yote yanatoka daima ku chemchem mletaji-uzima. Wafalme na watawala kwendeni wepesi mupokee neema kwa chemchem, kwa sababu aliokoa wafalme na wagonjwa kitandani, kwa kugusa maji walisimama, Wachungaji na waalimu, hii mawimbi ibebaji-maji ya wokovu kujeni tukusanyike na tuishote; Wagonjwa wataponyeshwa, walio katika hatari watapata nguvu; walio na kiu watatulizwa; vipofu wataona nuru; viziwi watasikia; wagonjwa watapona; walio karibu kufa watapata uzima; waaminifu wote na fasi yote kujeni munywe hii maji ya wokovu na kupaza sauti mukisema: Ewe Bikira Malkia, kwani unagawanya zawadi siku zote, usiache daima kuombea watumishi wako.

Sasa na siku zote. . . *Sauti ya tano.*

Ufufuo ni leo na tuangazwe kwa Karamu. . .

**PADRI:** Tumalize ombi letu ... **Kuaga.**

*TANGAZO: Mu Ibada ya Liturgia tunafata Desturi sawa vile jana, Siku ya Ufufuo ya Kristu.*

# MU KAZI TANO ASUBUI YA DIAKENISIMOS

*Tangazo: Na leo na kila siku ya hii Juma Ibada ya asubui inafanyika katika desturi ya siku ya Ufufuo ya Kristu Asubui.*

*Kanuni ya Paska na kisha tunaimba Kanuni ya Siku Kuu ya Mzazi-Mungu, Chemchem ya muletaji-Uzima.*

**KANUNI YA MZAZI MUNGU CHEMCHEM YA MLETAJI-UZIMA**

**WIMBO YA KWANZA** *Sauti ya kwanza. Ufufuo ni leo.*

Ewe Bikira Mzazi-Mungu, wewe uliye chemchem, sasa unanipa neema ya neno sababu ya kutukuza Chemchem yako yenye kutuletea uzima na neema kwa waaminifu kwani wewe ulileta Neno.

Ewe Binti mpole, Hekalu yako inaonekana kwa wote kuwa nyumba ya maponyesho kwa sababu inafufua kweli toka mauti wale wenye kukukimbilia na imani na inaleta kwa wote furaha mingi.

Toka mbinguni wewe peke yako unatumwangia daima zawadi za kweli kama ulivyomurudishia Kipofu nuru juu ya yeye kuona na kumuondoa yule Leoni toka zimu ya uchafu kwa namna ya ajabu.

Salamu, ewe Maria mpole, wanadamu wote wanakutukuza kwa sababu Muumba wa vitu vyote alishuka kwako kama tone na alikuonyesha wewe Bibi-Arusi wa Mungu chemchem isiyokauka.

**WIMBO YA TATU** *Sauti ya kwanza*

Ewe Binti wa Rabi wa wote, ninakutambua kuwa Hekalu takatifu ya nuru na Chemchem isiyoharibika mahali inatoka maji ya Kristu tunayokunywa.

Ewe Malkia Chemchem, ulimuponyesha mfalme magonjwa yake ya mafigo iliyomuteswa tangu miaka mingi kama jiwe, kwa maji yako takatifu uliyaondoa.

Ewe Bikira Mzazi-Mungu mwenye kuleta neema mingi, vilema wanashangilia kwa ajili yako, wenye ukoma wanasafishwa, na mashetani wanakimbia.

Ewe Chemchem, unagawanya maponyesho kwa waaminifu wote, wafalme, watawala, maskini, watajiri na waongozi kwa sababu hii maji inatoka kwako ni dawa ya kweli.

**KONTAKION YA UFUFUO YA KRISTU**

**Kathisma. S***auti ya mnane***.** *Tin sofian ke Logon.*

Kujeni tuiimbie wote pamoja hii Chemchem takatifu yenye kutupatia uzima na neema sisi wenye kuiomba; kila siku inatoa maponyesho mbalimbali kama mutoni ya maji. Kwa hivi, sisi tunaokuja na mapendo na imani kuomba toka hii chemchem nguvu ya kweli isiyokufa na utulivu wa roho za waaminifu, tupaze sauti kwa midomo yetu tukisema : " Wewe ni utulivu wa waaminifu.

Utukufu kwa Baba…Sasa na siku zote*…(mara ingine)*

**KONDAKION YA MLETAJI-UZIMA** *Sauti ya mnane.*

Ewe Mjaliwa-neema ya Mungu, kwa chemchem yako isiyokauka daima unanipa maponyesho na zawadi ya neema ya ajabu; kwa sababu ulizaa Neno kwa namuna ya ajabu, ninakuomba unifurahishe katika neema yako ili nikupazie sauti nikisema: Salamu, ewe maji ya wokovu.

**IKOS (NYUMBA)**

Ewe Mzazi-Mungu usiyeharibika, ulizaa kwa ajabu Neno wa Baba asiye na mwanzo, ewe mupole, unifungue kinywa changu ili nikutukuze na kumupazia Chemchem sauti nikisema: Salamu, chemchem ya furaha isiyo na mwisho; salamu, mufereji wa uzuri imara; salamu, uharibifu wa magonjwa yote; salamu, utakaso wa desturi mbalimbali; salamu, maji safi yenye kuleta afya kwa waaminifu; salamu, maji ya wagonjwa yenyi kujaliwa neema; salamu, fundisho ya hekima yenyi kuondoa giza ya akili; salamu, zahabu ya roho yenyi kuleta furaha; salamu, mlima wa mktate wa mbinguni wenye kuleta uzima; salamu, kiziwa na maji tamu yenye kutoka kwa Mungu; salamu, wewe mwenye kuonyesha namna ya kuponyesha magonjwa; salamu, wewe mwenye kuzima moto ya magonjwa; salamu, ewe maji ya wokovu.

**SINAKSARI**

Mu kazi tano ya hii Juma ya Diakenisimos (Juma mupya) tunashangilia kufungua kwa Hekalu ya Mtakatifu kamili Malkia Mzazi-Mungu, Chemchem mletaji-uzima; tena tunakumbuka miujiza yote ya ajabu yalifanyika kwa msaada wa Mzazi-Mungu.

Shairi : Ewe Binti, kila mutu anaona safi mkate wa mbinguni, kiziwa cha Siloamu, baraza ya Solomoni na Chemchem yako.

Kwa maombezi ya Mama yako, ewe Kristu Mungu, utuhurumie.

**EKSAPOSTILARI YA PASKA**

**EKSAPOSTALARI YA MZAZI-MUNGU** *Sauti ya mbili. Sarki Ipnosas.*

Ee Malkia uliyezaa Kristu,, uko kweli chemchem ya maji ya uzima; kwa sababu unasafisha magonjwa ya roho na ya mwili kwa kugusa maji ya wokovu.

**MASIFU** *Sauti ya sita.*

Msalaba wako, ee Bwana, ni uzima na ufufuo kwa watu wako; na tunapoitumainia, tunakuimbia wewe, Mungu wetu, uliyefufuka, utuhurumie.

Maziko yako, ee Rabi, ilifungua Paradizo kwa uzao wa watu; na tukikombolewa katika uharibifu, tunakuimbia wewe, Mungu wetu, uliyefufuka. Utuhurumie.

Pamoja na Baba na Roho, tumwimbie Kristu, aliyefufuka katika watu, na tupaze sauti kwa yeye: Ewe ni uzima na ufufuo wetu. Utuhurumie.

Katika siku tatu ulifufuka, ewe Kristu, toka kaburi, kama ilivyoandikwa, ukiamusha pamoja nawe Baba yetu; kwa hii uzao wa watu tunakutukuza na tunaimba ufufuo wako.

*Wimbo ingine ya Mzazi-Mungu, chemchem ya Mletaji-Uzima. Sauti ya mbili.Ikos tu Efratha.*

Kwa wagonjwa wote maji ya chemchem ni wokovu wao, kujeni basi wepesi na imani mupokee neema.

Ee Kisima cha uzima, Chemchem isiyokufa inawapa wale wenye kuikimbilia hazina ya maponyesho mengi yasipo kuisha.

Maji ya Bikira inaleta nguvu rohoni mwa wanadamu, kwa hivi, sisi wenye zambi tunakimbilia kwa Binti kusudi tutakaswe.

Ee Bikira takatifu mwenye kutosha mukate wa mbinguni, Chemchem yako inaonekana daima kwa wale wanakuomba, kwa hivi, sisi wote tuende kushota msaada wako.

# MU KAZI TANO MANGARIBI YA DIAKENISIMOS

*Tangazo: Tunaimba sawa jana. Waimbaji wataanza kuimba: «Bwana nimekuita...». Watasimama pa shairi sita na wataimba Wimbo wa Ufufuo wa Kristu mu Paraklitiki.*

*Sauti ya mnane.*

Tunakutolea, ee Kristu, wimbo wa mangaribi, na ibada yenye maana; kwani ulipendezwa kutuhurumia kwa ufufuo.

Ee, Bwana, Bwana, usitutupe mbali ya uso wakol; lakini upendezwe kutuhurumia, kwa ufufuo.

Furahi, ee Sayuni takaitfu, Mama wa Makanisa, nyumba ya Mungu; kwani wewe ulipokea kwanza usamehe wa zambi, kwa ufufuo.

Neno aliyezaliwa toka Mungu Baba, mbele ya milelena yeye mwenyewe aliyetwaa mwili kwa Bikira asiyeolewa, katika miaka ya mwisho, alivumilia usulubisho wa lufu kutaka kwake, na aliokoa mutu aliyekufa tangu zamani, kwa ufufuo wake.

Tunatukuza, ee Kristu, ufufuo wako katika wafu; kwa hii uliopoa uzao wa Adamu, toka uzulumu wa Hadeze; sawa na Mungu ulileta duniani, uzima wa milele na rehema kubwa.

Utukufu kwako, ee Kristu Mwokozi, Mwana wa pekee wa Mungu, uliyepigiliwa Msalabani, na uliyefufuka toka kaburi siku ya tatu.

Utukufu kwa Baba...

Tunakutukza, ee Bwana, uliyevumilia Msalaba kwa kutaka kwako kwa ajili yetu na tunakuabudu, ee Mwokozi na mwenyezi; usitutupe mbali ya uso wako, lakini utusikie na utuokoe, ewe Mpenda-wanadamu, kwa ufufuo wako.

Sasa na siku zote... **THEOTOKION**. *Sauti ya mnane*

Mufalme wa mbinguni, kwa kupenda-wanadamu, alionekana juu ya inchi akazoea kati ya watu; kwani alipotwaa mwili kwa Bikira safi, na alipotokea kwa huyu, pamoja na hali ya umutu, huyu ni Mwana moja, kwa hali mbili, lakini hana uso mbili; kwa hii tukihubiri ya kama huyu kweli ni Mungu mkamilifu na Mtu mkamilifu, tunaungama Kristu Mungu wetu; umusihi ewe Mama usiyeolewa, kwa huruma wa nafsi yetu.

**KUINGIA.** *Kisha:* Mwangaza upole (ilaron)...

**PROKIMENON.** *Sauti ya mnane.*

Maana, wewe, ee Mungu, umesikia naziri zangu: Umenipa uriti wao wanaoogopa jina lako.

Shairi: Toka mwisho wa dunia nitakuita.Maana, wewe, ee Mungu......

Shairi: Nitakimbilia maficho ya mabawa yako.Maana, wewe, ee Mungu......

Shairi: Hivi nitaimbia jina lako sifa kwa milele.Maana, wewe, ee Mungu......

SHEMASI: Tuseme sisi wote, kwa moyo wetu na kwa roho yetu, tuseme.

MSOMAJI *atasema kisha kila ombi:* Bwana, hurumia.

**APOSTIKHA** *Sauti ya mnane.*

Ulipanda juu ya Msalaba. ee Yesu, uliyeshuka toka mbingu; ulikuja kwa lufu, ee Uzima usiyokufa. Wewe ni Nuru ya kweli kwa wale waliokaa gizani, ni ufufuo wa wote kwa wale walioanguka. Angazo na Mwokozi wetu, utukufu kwako.

*Tangazo:Kisha tunaimba WIMBO YA PASKA (Angalia Masifu ya Orthros ya Paska): Sauti ya tano*

1. Paska zabihu leo imeonekana kwetu, Paska mupya Takatifu. . .
2. Kujeni Wanawake. . .
3. Wanawake Wabebaji manukato. . .
4. Paska ya furaha, Paska ya Bwana Paska. . .

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .
Ufufuo ni leo na tuangazwe kwa Karamu. . .
**PADRI:** Tumalize ombi letu **...** **Kuaga.**
*TANGAZO: Mu Ibada ya Liturgia tunafata Desturi sawa vile jana, Siku ya Ufufuo ya Kristu.*

# MUPOSHO ASUBUI YA DIAKENISIMOS

*Tangazo: Na leo na kila siku ya hii Juma Ibada ya asubui inafanyika katika desturi ya siku ya Ufufuo ya Kristu Asubui.*

**MASIFU.** *Sauti ya mnane.*

Ee Bwana, japo ulisimama mbele ya baraza ya hukumu, ukihukumiwa kwa Pilato, lakini haukuache kiti cha ufalme pahali unapokaa pamoja na Baba; na ukifufuka katika wafu, uliopoa dunia toka utumwa wa adui, kama Mwema na Mpenda-wanadamu.

Ee Bwana, japo Wayuda walikuweka Kaburini kama mwenye kufa, lakini askari walikuchunga sawa Mfalme anayelala, na walikufunga kwa mhuri kama hazina ya uzima; lakini ulifufuka na ulileta uzima usiyoharibika kwa nafsi yetu.

Ee Bwana, ulitupatia Msalaba wako, kama silaha juu ya shetani; kwani yeye anaitetemekea na anaifazaikia kwa woga, bila kuweza kuona nguvu Yake; kwa kuwa Msalaba unafufua wafu, na uliharibu mauti; kwa hii tunaabudu, maziko na ufufuo wako.

Ee Bwana, malaika wako, aliyehubiri ufufuko, aliogopesha wachungaji; tena aliita kwa wanawake, akiwaambia: Kwa nini munatafuta yeye aliye hai katika wafu? Alifufuka, kwa kuwa Yeye ni Mungu na alileta uzima kwa ulimwengu.

*Tangazo:Kisha tunaimba WIMBO YA PASKA : Sauti ya tano*

1. Paska zabihu leo imeonekana kwetu, Paska mupya Takatifu. . .
2. Kujeni Wanawake. . .
3. Wanawake Wabebaji manukato. . .
4. Paska ya furaha, Paska ya Bwana Paska. . .

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .
Ufufuo ni leo na tuangazwe kwa Karamu. . .
Kristu alifufuka. *(mara tatu).*
**PADRI:** Tumalize ombi letu ... **Kuaga.**
*TANGAZO: Mu Ibada ya Liturgia tunafata Desturi sawa vile jana, Siku ya Ufufuo wa Kristu.*

# MU JUMA YA ANTIPASKA AO YA UPAPASO WA MT. MTUME THOMAS

## MU POSHO MANGARIBI YA MTUME THOMAS

*Elezo: Kisha: «Bwana nimekuita...» tunaimba wimbo kumi ya mt. Thomas..*

***Wimbo ya Siku Kuu:***

*Sauti ya kwanza*

Ee Yesu Mungu wetu Mwenyezi, milango ilipokuwa imefungwa na Wafwasi walipokuwa wamekusanyika, uliingia mara moja, na uliposimama katikati yao ukawapa amani na ukawaja na Roho Mtakatifu, ukawaambia wakae katika Yerusalema wasiende mbali mpaka wajazwe na nguvu ya juu mbinguni; ndio maana tunakulalamikia: Bwana, Ufufuo wetu, nuru yetu na amani yetu, utukufu kwako. *(mara mbili)*

Ee Bwana, siku munane kisha Ufufuo wako, ulionekana kwa Wafwasi wako mahali walikusanyika na ukawaambia: Amani kwenu! Kwa mfwasi mwenyi moyo mgumu ulimwonyesha mikono yako na ubavu wako, na kwa imani akakulalamiki: Bwana wangu na Mungu wangu, utukufu kwako. *(mara mbili).*

Ee Kristu, Thoma, anayeitwa Mupasa, hakuwa pamoja nao wakati uliingia milango yote yenyi kufunga; ndio maana hakusadiki maneno waliyomwambia, sababu ya kusabitisha ku imani njia ya wasiyoamini; lakini kwa wema wako hakukataa kumuonyesha ubavu wako takatifu na vidonda vya mikono yako na vya miguu yako: akaipapasa na wakati alikuona, akatambua ndani yako umutu na umungu wako, na akapaza sauti na kusema: Bwana wangu na Mungu wangu, utukufu kwako.*(mara mbili).*

Wafwasi walikuwa na shaka, lakini siku ya munane Mwokozi alionekana katikati yao mahali walikusanyika, na alipowapa amani, akamwita Thoma na akamwambia: Mtume kuja upapase mikono yangu iliyotobolewa na misumari. Ilifai Thoma awe na shaka sababu ya kuongoza roho za waaminifu kwa kumujua Mungu; na kwa woga akapaza sauti na kusema: Bwana wangu na Mungu wangu, utukufu kwako. *(mara mbili)*

*Sauti ya pili*

Ee Bwana, kisha Ufufuo wako, Wafwasi walipokusanyika na milango ilipokuwa imefungwa, ukasimama katikati yao, ukawapa amani, na Thoma alipohakikishwa kwa kuona mikono yako na ubavu wako, akakukiri kama Bwana na kama Mungu;Wewe mwenyi kuokoa wenye kukutumainia wewe, Mpenda-wanadamu, utukufu kwako.

Milango yote ilipokuwa imefungwa, Yesu akawatokea Wafwasi wake, akasimama katikati yao, akawaondolea woga na akawapa amani; kisha akamwita Thoma, akamwambia: Sababu gani hausadiki ya kama nimefufuka katika wafu? Leta mkono wako na uuweke katika ubavu wangu, tazama mikono yangu na miguu yangu, na sababu ya kutokusadiki kwako watu wote watajua Mateso yangu na Ufufuo wangu katika wafu sababu ya kupaza sauti pamoja nawe: Bwana wangu na Mungu wangu, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba… Sasa na siku zote… *Sauti ya sita*

Ee Kristu, milango yote ilipokuwa imefungwa, ulionekana kwa Wafwasi wako Thoma hakuwa pamoja nao, lakini ilikuwa ni maongozi ya Mungu, kwa sababu alisema : “ Sitasadiki kama nisipomuona Bwana, kama nisipoona ubavu wake humo mulitoka damu na maji, ni ubatizo; kama nisipoona kidonda kilichoponyesha vidonda nyingi vya wanadamu; paka nikiona ya kama si muzimu lakini ni mutu eko na mifupa na mwili. Wewe uliyeshinda mauti na kumusadikisha Thoma, Bwana, utukufu kwako.

### L I TI A *Sauti ya ine*

Ee Bwana, ulipoonyesha nuru ya umungu wako, milango ilipokuwa imefungwa, katikati ya Wafwasi wako ulionyesha waziwazi ubavu wako, ukawaonyesha vidonda vya mikono yako na vya miguu yako, ukawaokoa ku sikitiko iliwashika na ukawaambia waziwazi ukasema: Nina mwili,

munaiona, rafiki zangu, mimi si muzimu. Halafu ulimwambia Mfwasi alikuwa na shaka apapase vidonda vyako, ukasema: Tazama vidonda vyangu, usiwe tena na mashaka.
Na mkono wake alipohakikisha umutu wako na umungu wako, alipojaa na woga akapaza sauti na imani akasema: Bwana wangu na Mungu wangu, utukufu kwako.

*Sauti ya mnane*

Kristu alisema: Thoma, leta mkono wako uuweke katika ubavu wangu, tazama alama ya misumari, usiwe tena na mashaka, lakini sadiki. Alipopapasa Bwana na kidole, Thoma akapaza sauti na kusema: Wewe ni Bwana wangu na Mungu wangu, utukufu kwako.

Utukufu … Sasa…*Sauti ya mnane*

Milango yote ilipokuwa imefungwa na Wafwasi walipokusanyika, Mwokozi akaonekana mahali pale, na aliposimama katikati yao, akamwita Thoma akamwambia: Kuja upapase vidonda vyangu, na tazama alama ya misumari, usiwe tena na mashaka, lakini tangu sasa tangaza na imani Ufufuo wangu katika wafu.

**APOSTIKHA.** *Sauti ya ine*

Ni ajabu! Kukosa imani kunasabitisha imani; kwani Thoma alisema: Sitasadiki bila kuona. Lakini alipapasa ubavu wako, akatambua kuwa Mwana wa Mungu Bwana aliyejifanya mutu aliyesulubiwa katika mwili; akatangaza Ufufuo wako katika wafu na akapaza sauti mbele ya wote kwa sauti kubwa akasema: Bwana wangu na Mungu wangu, utukufu kwako.

*Shairi:* Tukuza Bwana, ee Yerusalema, Shangilia Mungu wako, ee Sayuni.

Ni ajabu! Nyasi haiteketezwe kwa moto ilipapasa : Kwani Thoma hakuteketezwa wakati aliweka mkono wake katika ubavu wa moto wa Yesu Kristu Mungu wetu, lakini aligeuza mashaka yake kuwa imani ya furaha, na rohoni mwake akapaza sauti na kusema: Ee Rabi uliyefufuka katika wafu, uko tena Mungu wangu, utukufu kwako.

Shairi: Maana alisimika miti ya milango yako, alitukuza wana wako katikati yako.

Ni ajabu! Ni Yoane aliegamia katika kifua cha Neno, na Thoma alistahiliwa kupapasa ubavu wake; wa kwanza alichunguzia siri ya ndani ya Mungu, mwingine alistahilishwa kutufundisha nia yake ya wokovu, kwa sababu alishuhudia waziwazi Ufufuo wake akisema: Bwana wangu na Mungu wangu, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba… Sasa na siku zote… S*auti ya tano*

Ee Mpenda-wanadamu, rehema yako ni kubwa sana, ulivumilia kupigwa na Wayuda, kupapaswa na Mtume, kupelelezwa na makafiri. Namna gani ulitwaa mwili, namna gani uliteswa msalabani Wewe peke yako usiye na zambi? Utufundishe kukulalamikia kama Thoma tukisema: Utukufu kwako, Bwana wangu na Mungu wangu.

**APOLITIKION** *Sauti ya saba*

Japo kaburi ilifungwa, sawa Uzima ulifufuka toka kaburi, ee Kristu Mungu wetu, na japo milango ilifungwa ulionekana kwa Wafwasi wako, Wewe uliye Ufufuo wa milele, na ulifanya mara ingine mioyoni mwetu Roho wa ukweli kwa rehema yako kubwa.*(mara tatu).*

## MU JUMA ASUBUI YA MTUME MTAKATIFU THOMA

**KATHISMA YA KWANZA.** *Tu lithu sfragisthentos Sauti ya kwanza*

Kwa kuwaogopa Wayuda Wafwasi walifichama na walikusanyika katika Sayuni; ulikuja katikati yao, ee Bwana wa wema, ukaonekana kwao milango ilipokuwa imefungwa, ukawajaza na furaha; uliwaonyesha mikono yako na kidonda cha ubavu wako, ukamwambia mfwasi asiyesadiki: Weka mkono wako katika ubavu wangu, unisadiki, ni mimi niliteswa kwa ajili yako.

Utukufu kwa Baba…Sasa na siku zote…*(mara ingine)*

**KATHISMA YA MBILI.** *Ton tafon su Sotir. Sauti ya* kwanza

Ee Kristu, japo milango ilikuwa imefungwa, ulionekana kwa Wafwasi wako kama Uzima; uliwaonyesha mikono yako, miguu yako na ubavu wako sababu ya kusabitisha imani yao kwa Ufufuo wako toka kaburini; lakini Thoma hakuwa pamoja nao, na kisha akasema : “ Nisipomwona mimi mwenyewe, sitasadiki neno hata moja.

Utukufu kwa Baba…Sasa na siku zote…*(mara ingine)*

*Kisha Polieleos tunaimba hii Kathisma ya tatu:*

**KATHISMA YA TATU.** *Ton tafon su Sotir. Sauti ya kwanza*

Bwana alipotoka kaburini na kuonekana kwa Mitume wake kwa namna ya ajabu, alimwambia Thoma akisema: Unaona ubavu wangu na alama ya misumari, sababu gani unakuwa na mashaka juu ya Ufufuo wangu wa kweli? Thoma, anayeitwa Mupasa akamujibu Muumba : " Uko kweli Bwana wangu na Mungu wangu.

Utukufu kwa Baba…Sasa na siku zote…*(mara ingine)*

*Sasa tunaimba Antifonon ya kwanza mu sauti ya ine. Kisha:* **PROKIMENON.** *Sauti ya ine*

Tukuza Bwana, ee Yerusalema, shangilia Mungu wako, ee Sayuni.*(mara tatu).*

*Shairi:* Kwani alisimika miti ya milango yako, alitukuza wana wako katikati yako.

*Kisha inafwata Evangelion Eothinon ya Kwanza, katika Matayo. Kisha waimbaji wanasoma: Tukiona Ufufuo wa Kristu... kisha wanaimba Zaburi 50 (51). Na kisha:* Utukufu…Kwa maombezi ya Mitume...Sasa...Kwa maombezi ya Mzazi-Mungu....Shairi: Unirehemu...Yesu alifufuka kaburini…

**WIMBO YA KWANZA.** *Sauti ya kwanza.*

**IRMOS:** Huyu aliokoa Israeli toka mateso ya utumwa wa Farao na kumuvukisha pakavu katika bahari nyekundu, tumwimbie wimbo wa ushindi, kwani amevaa utukufu.

Leo ni wakati mpya wa roho, kwa sababu Kristu alisimama toka kaburini Siku ya tatu kama jua, alifukuza baridi ya giza ya makosa yetu: tumwimbie kwani amevaa utukufu.

Saa yote tazama malkia alisindikiza Mfalme wa mchana : anafurahisha taifa la Kanisa na nuru yake, huyu mteule mpya mwenye kumwimbia daima Kristu aliyefufuka.

Ee Kristu, milango ya mauti ao ya kaburi ao makomeo haikuweza kukushinda, lakini ulipofufuka ulionekana kwa marafiki zako, ukawapa amani yenyi kupita wazo lolote.

**Katavasia ya kwanza**

Ni siku ya Ufufuo! Mataifa, twangazwe na furaha: Ni Paska, Paska ya Bwana! Kristu Mungu wetu anatuongoza toka mauti mpaka uzima, toka dunia mpaka mbinguni: Tuimbie ushindi wa Bwana.

**WIMBO YA TATU**

**IRMOS:** Ee Kristu, unisabitishe juu ya mwamba imara wa amri zako; uniangaze na nuru ya sura yako, maana hakuna Mtakatifu mwingine ila Wewe, Bwana.

Ee Kristu, kwa msalaba wako unatufanya kuwa wapya toka watu wa zamani, toka mauti ulituongoza katika uzima wa milele, ulituamuru kuishi na uzima mpya ndani yako.

Ee Kristu, ulipofungwa kaburini mwilini, wewe ambaye kitu hata kimoja hakiwezi kukuzuia, ulifufuka, na milango ilipokuwa imefungwa ulionekana katikati ya Wafwasi wako, ee Bwana Mwenyezi.

Ee Kristu, vidonda ulijeruhiwa kwa kutaka kwako kwa ajili yetu ulivionyesha kwa Wafwasi wako sababu ya kushuhudia Ufufuo wako tukufu.

**Katavasia ya tatu:** Kujeni, tunywe wote maji mapya ya chemchem ya uzima wa milele yenyi kutoka namna ya ajabu apana toka mwamba katika jangwa, lakini toka kaburi ya Kristu aliye nguvu yetu na furaha yetu.

**IPAKOI.** *Sauti ya sita*

Kama ulivyoonekana katikati ya Wafwasi wako ukawapa amani, kuja tena katikati yetu, ee Mungu Mwokozi, utuokoe.

**KONDAKION** *Sauti ya munane*

Ee Kristu Mungu wetu, na mkono wake Mtume Thoma alitafuta na kupapasa ubavu wako wenyi kuleta uzima, na wakati milango ilipokuwa imefungwa na ulipokuja katikati ya Wafwasi wako, akakulalamika akasema: Uko kweli Bwana wangu na Mungu wangu.

**IKOS** *Sauti ya mnane*

Namna gani mkono wa Mfwasi haukuyeyuka wakati ilipapasa ubavu wa moto wa Bwana? Nani alimupa nguvu ya kuupapasa! Kama asingelileta nguvu kwa hii mkono maskini, namna gani iliweza kupapasa vidonda vilivyotetemesha mbingu na dunia? Thoma alipokea neema ya kumupapasa Kristu na kumulalamikia: Uko kweli Bwana wangu na Mungu wangu.

**SYNAKSARI**

Leo, Juma ya pili ya Paska, tunashangilia Wakati mpya ya Ufufuo wa Kristu na upapaso wa Mtume Mtakatifu Thoma.

Tumbo la Bikira na kaburi haikukuzuia : Namna gani kitasa kitazuia kuja kwako?
Kwa maombezi ya Mtume wako Thoma, ee Kristu Mungu wetu, utuhurumie. Amin.

**WIMBO YA TISA**

**IRMOS:** Wewe uliye taa la nuru na Mama wa Mungu wetu, utukufu wa Bwana na uliye juu kabisa kuliko kazi zote za Muumba Mtakatifu, tunakutukuza kwa nyimbo zetu.

Ee Kristu, tazama siku ya nuru, yenyi kuangaa kupita nuru yote, yenyi kujaa na neema na mwanga ambayo ulipoangaa na uzuri ulionekana kwa Wafwasi wako, tunakutukuza kwa nyimbo zetu.

Wewe ambaye mkono maskini wa mwanadamu ilipapasa ubavu wako wenyi kuleta uzima na uliizuia isiteketezwe katika moto ya umungu wako, tunakutukuza kwa nyimbo zetu.

Bila kuona na macho yetu namna gani ulitoka kaburini sababu ya kufufuka kama Mungu, Ee Kristu, tunaisadiki na nguvu ya roho yetu na tunakutukuza kwa nyimbo zetu.

Angaa na nuru, ee Yerusalema mupya, maana utukufu wa Bwana iliangaa juu yako. Shangilia, cheza na furaha, ewe binti wa Sayuni; salamu tena, ee Mtakatifu Mzazi-Mungu hii siku ya leo anafufuka Mwana wako.

Bwana Mungu wetu ni ee Mtakatifu. *(mara tatu).*

**EKSAPOSTILARI** *Sauti ya tatu. O uranon tis astris.*

Tazama na mkono wako vidonda vya mikono na miguu yangu; Thoma hakatae kunisadiki mimi niliyejeruhiwa kwa ajili yako; unganisha sauti yako ku kundi la Mitume sababu ya kutangaza Mungu aliye hai. *(mara mbili).*

Leo wakati mupya inatoa harufu yake ya manukato ya maua yenyi kuchanuka, na viumbe vipya vinashangilia; leo Bwana anadidimisha milango yenye kufunga na anavunja makomeo ya mashaka kwa ushirika wake; Thoma Mtume wa Kristo kwa imani anamukiri akisema: Uko kweli Bwana wangu na Mungu wangu. *(mara moja).*

**MASIFU.** *Sauti ya kwanza. Panefimi Martires***.**

Kisha Ufufuo wako wa ajabu, ee Bwana chemchem ya uzima, sawa haukuvunja vifungo vya kaburi, ulionekana vilevile kwa Mitume wako watukufu milango yote yenyi kufunga ambao ulijaza furaha, ukawapa Roho wa ukweli kwa wema wako kubwa.*(mara mbili).*

Ee Bwana, Thoma, anayeitwa Mupasa, hakuwa pamoja nao wakati uliwatokea Wafwasi wako; ndio maana hakusadiki Ufufuo wako na akawaambia wale walikuona ya kwamba: Nisipoweka kidole changu katika ubavu wake ne katika alama ya misumari, sitasadiki ya kama amefufuka.

Kristu alisema: Thoma, unipapase, kwa sababu unaitaka, leta mkono wako na ujue ya kama niko na mifupa na mwili, mwili wa mutu; usiwe tena na mashaka, lakini sadiki! Thoma akamujibu akisema: Uko Bwana wangu na Mungu wangu, utukufu kwa Ufufuo wako takatifu.

Utukufu kwa Baba … Sasa na siku zote… *Sauti ya sita*

Siku munane kisha Ufufuo wako, ee Mwana wa pekee na Neno wa Mungu, ulionekana kwa Wafwasi wako milango yoteyenyi kufunga na ukawapa amani; kwa mfwasi asiyesadiki ulimuonyesha alama ya misumari na ulimwambia: Kuja upapase mikono na miguu yangu, na kidonda cha ubavu wangu. Mfwasi akahakikishwa na akapaza sauti na kusema: Utukufu kwako, Bwana wangu na Mungu wangu.

**DOKSOLOGIA KUBWA NA KUAGA**

# MU JUMA MANGARIBI YA SIKU KUU YA MT. THOMAS

**Elezo:** *Kisha: „Bwana nimekuita..." tunasimama pa ma shahiri sita na tunaimba wimbo ya Masifu ku asubui. (Tafuta mu Ibada ya asubui leo).*

*Kisha tunaimba wimbo ya Mineon tatu.*

Utukufu kwa Baba…Sasa na siku zote…*Sauti ya kwanza*

Ee Yesu Mungu wetu Mwenyezi, milango ilipokuwa imefungwa na Wafwasi walipokuwa wamekusanyika, uliingia mara moja, na uliposimama katikati yao ukawapa amani na ukawaja na Roho Mtakatifu, ukawaambia wakae katika Yerusalema wasiende mbali mpaka wajazwe na nguvu ya juu mbinguni; ndio maana tunakulalamikia: Bwana, Ufufuo wetu, nuru yetu na amani yetu, utukufu kwako.

**KUINGIA.** Mwangaza upole... **PROKIMENON.** *Sauti ya saba.*

Ni nani aliye Mungu Mukubwa, kama Mungu wetu, Wewe ni Mungu wa pekee, aliyetenda matendo wa ajabu.

Shairi: Ee Mungu, ulionyesha mataifa yako nguvu yako.

Ni nani aliye Mungu Mkubwa. . .

Shairi: Na nikasema: Sasa mitaanza; Hii ni mageuzo ya Mukono wa Kuume wa Mwenyezi

Ni nani aliye Mungu Mkubwa. . .

Shairi: Nilikumbuka matendo ya Bwana na nilifurahi.

Ni nani aliye Mungu Mkubwa. . .

SHEMASI: Tuseme sisi wote, kwa moyo wetu na kwa roho yetu, tuseme.

MSOMAJI *atasema kisha kila ombi:* Bwana, hurumia.

**APOSTIKHA.** *Sauti ya kwanza* **.**

Pokea, ee Bwana Mtakatifu, maombi zetu za mangaribi, na utupatie maondoleo ya zambi zetu; kwa maana ni wewe peke uliyeonyesha ku ulimwengu ufufuo.

Bahari ya makosa yangu ni kubwa, ee Mungu Mwokozi; nazama katika shimo la zambi: Kama utupe amani na utuhurumie.Ee Mungu wa mapendo, kwa maombezi ya watakatifu wote na ya Mzazi-Mungu, utuhurumie na utuokoe.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*Sauti ya kwanza.*

Siku munane kisha Ufufuo wako, ee Mwana wa pekee na Neno wa Mungu, ulionekana kwa Wafwasi wako milango yote yenyi kufunga na ukawapa amani; kwa mfwasi asiyesadiki ulimuonyesha alama ya misumari na ulimwambia. Kuja upapase mikono na miguu yangu, na kidonda cha ubavu wangu. Mfwasi akahakikishwa na akapaza sauti na kusema. Utukufu kwako, Bwana wangu na Mungu wangu.

**Apolitikion ya Siku Kuu**

Japo kaburi ilifungwa, sawa Uzima ulifufuka toka kaburi, ee Kristu Mungu wetu, na japo milango ilifungwa ulionekana kwa Wafwasi wako, Wewe uliye Ufufuo wa milele, na ulifanya mara ingine mioyoni mwetu Roho wa ukweli kwa rehema yako kubwa.

# MU KAZI MOJA ASUBUI KISHA JUMA YA MT. THOMAS

*Elezo: Padri atasema: Hahimidiwe Mungu wetu...Kisha ataimba Kristu alifufuka mara moja na waimbaji wataimba mara wa wili. Kisha Utukufu...Sasa...Utatu Mtakatifu...Bwana hurumia (mara tatu), Utukufu...sasa...Baba yetu...Wimbo tatu na Eksapsalmos, Bwana ndiwe...Apolitikion ya Mt. Thomas na kisha:*

**KATHISMA YA KWANZA** *Sauti ya kwanza. Ton tafon su Sotir.*

Ewe Mwokozi, maaskari waliyolinda Kaburi yako wakaangushwa chini kwa uugaro wa malaika aliyoonekana sababu ya kuwatangazia wanawake Ufufuo wako Takatifu; nawe mwenyewe kutuokoa ku mauti, tunakutukuza na tunasujudu mbele yako, Mfufuliwa kaburini na Mungu wetu mmoja.

Mama yangu alinichukua mimba katika zambi, na kama mpotevu sisubutu kutazama juu mbinguni, lakini mapendo yako inaniotumainia, na napaza sauti kwako: Ewe Mungu, unisamehe na uniokoe.

Utukufu kwa Baba...

Ee Bwana, utukufu wa mashindano na taji la Washindaji, ndiwe uzuri wa Mashahidi Watukufu. Kwa imara yao katika majaribu wakawakimbiza makafiri na wakapokea ushindi mbinguni kwa uwezo wa Mungu; ee Bwana, kwa maombezi yao uniokoe kwa Adui msiyeonekana na uniokoe.

Sasa na siku zote...**THEOTOKION**.

Muujiza wa ajabu, ee Mjaliwa neema, kiumbe kilishangilia na furaha pakukuona, bila mbegu ukapata mimba na ukamzaa namna isiyokadirika huyu ambaye Malaika mwenyewe hawawezi kutazama, ee Bikira Mzazi-Mungu, umuombe kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

**KATHISMA YA MBILI.** *Sauti ya kwanza. Ton tafon su Sotir.*

Alipogusa na mkono wake kidonda cha ubavu, Thoma hakuteketezwa, lakini akatazama na bidii vidonda na akamwambia huyu alichomwa mkuki kwa ajili yetu: Japo mateso ya Mateso yako uko kweli Bwana wangu na Mungu wangu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote…*(mara ingine)*

*Kisha tunasoma: Tukiona Ufufuo wa Kristu...Kanuni ya Siku Kuu na Mineon. Kontakion na Eksapostilarion ya Siku Kuu.*

## MASIFU. *Sauti ya kwanza.*

Tunasifu, ee Kristu, mateso yako kwa wokovu wetu, na tunatukuza Ufufuo wako.

Ulimwengu ingine umekuongojea, ee roho yangu na Mwamuzi atatangaza siri zako na zambi zako; usidumu katika uovu, lakini ujiharikishe kupaza sauti: Ewe Mwamuzi wangu na Mungu wangu, unisamehe na uniokoe.

Njooni, enyi mataifa yote, tuimbe mashairi na nyimbo za kiroho kwa kuwatukuza Mashahidi watukufu wa kristu, Watangazaji wa imani tena taa za ulimwengu, Chemchem isiyokauka ambako kunatiririka maponyesho; kwa maombezi yao, ee Kristu Mungu wetu, leta amani ku dunia na neema ya wokovu ku roho zetu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote... *Sauti ya kwanza.*

Ee Kristu, Thoma, anayeitwa Mupasa, hakuwa pamoja nao wakati uliingia milango yote yenyi kufunga; ndio maana hakusadiki maneno waliyomwambia, sababu ya kusabitisha ku imani njia ya wasiyoamini; lakini kwa wema wako hakukataa kumuonyesha ubavu wako takatifu na vidonda vya mikono yako na vya miguu yako: akaipapasa na wakati alikuona, akatambua ndani yako umutu na umungu wako, na akapaza sauti na kusema: Bwana wangu na Mungu wangu, utukufu kwako.

**APOSTIKHA YA SIKU KUU.** *Sauti ya pili.*

Takaseni midomo yenu, enyi wanadamu, sababu ya kumwimbia pamoja na Malaika za mbinguni huyu alifufuka kaburini siku ya tatu na kufufua wanadamu pamoja naye.

Shairi: Tukuza Bwana, ee Yerusalema, shangilia Mungu wako, ee Sayuni.

Ee Mwokozi, ulionekana kwa Mitume wako milango yote yenyi kufunga, na katika wao ulifanya mioyoni mwetu Roho wako Mtakatifu.

Shairi: Maana alisimika miti ya milango yako,Alitukuza wana wako katikati yako.

Ee Mfalme wa ulimwengu, tunapokuona sasa apana na macho yetu ya mwili lakini na mapendo ya roho yetu, tunasadiki ya kama uko Mungu na kwa nyimbo zetu tunakutukuza.

Utukufu kwa Baba…Sasa na siku zote…*Sauti ya kwanza*

Wafwasi walikuwa na shaka, lakini siku ya munane Mwokozi alionekana katikati yao mahali walikusanyika, na alipowapa amani, akamwita Thoma na akamwambia: Mtume kuja upapase mikono yangu iliyotobolewa na misumari. Ilifai Thoma awe na shaka sababu ya kuongoza roho za waaminifu kwa kumujua Mungu; na kwa woga akapaza sauti na kusema: Bwana wangu na Mungu wangu, utukufu kwako.

**Apolitikion ya mt. Thomas na Kuaga**

# MU KAZI MOJA MANGARIBI YA JUMA YA MT. THOMAS

*Elezo: Kisha: «Bwana nimekuita...» tunaimba wimbo sita; Tatu ya Siku Kuu ya mt. Thomas na tatu ya Mineon.*

***Wimbo ya Siku Kuu:***

*Sauti ya ine. Os geneon en martisin.*

Ee Bwana Mwenyezi, ulipofufuka toka kaburini, ulionekana kwa marafiki zako milango yote yenyi kufunga; ulimuonyesha Thoma alama ya misumari na ubavu wako uliyochomwa mukuki, ukamusabitisha katika imani, ee Neno wa Mungu, na akasadiki ya kama uko kweli huyu kwa kutaka kwake aliteswa na mateso yenyi kutuokoa.

Bwana anasema: Alipoona mapendo yangu ya milele na kujishusha kwangu, Thoma hakuwa na shaka, lakini aliamini ya kwamba mimi kweli ni huyu aliteswa na kufufuka siku ya tatu na aliyefungua vifungo vya Hadeze na kufufua wale walikufa tangu milele.

Ee Bwana Mwenyezi, aliposhangaa kwa ono, Thoma alipaza sauti na kusema wakati alikuona: Uko kweli Bwana wangu na Mungu wangu huyu aliteswa kwa ajili ya wanadamu na kuponyesha mateso ya roho zetu; nasujudu mbele ya uwezo wako, ee Bwana, na nitatangaza duniani kote nguvu na nuru ya Ufufuo wako takatifu.

***Wimbo tatu ya Mineon.***

Utukufu kwa Baba… Sasa na siku zote.. *Sauti ya kwanza.*

Wafwasi walikwa na shaka, lakini siku ya munane Mwokozi aliwatokea mahali walikusanyika, akawapa amani na akamwita Thoma akamwambia: Mtume, kuja upapase mikono yangu iliyotobolewa na misumari. Ilifai awe na mashaka sababu ya kuongoza roho za waaminifu kwa kumujuwa Mungu; na kwa woga Thoma akapaza sauti na kusema: Bwana wangu na Mungu wangu, utukufu kwako.

**APOSTIKHA.** *Sauti ya kwanza.*

Mataifa, tembeyeni pembeni ya sayuni na mumuzunguke, na mumutukuze ndani yake Yeye aliyefufuka katika wafu; kwa maana huyu ni Mungu wetu, aliyetukomboa ku maovu yetu.

Ee Mwokozi, tazama nahukumiwa kwa mawazo yangu na matendo yangu ya ukafiri; unipe nia za toba ili nikuombe, ee Mungu wangu: Uniokoe katika wema wake na unihurumie.

Enyi Mashahidi kustahili sifa yote, apana dunia iliyowaficha, ni mbingu iliyowapokea; milango ya Paradizo imefunguliwa kwa ajili yenu, na huko munakuwa na mti wa uzima; muombeni Kristu alete amani na neema ya wokovu ku roho zetu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya mbili*

Ee Bwana, kisha Ufufuo wako, Wafwasi walipokusanyika na milango ilipokuwa imefungwa, ukasimama katikati yao, ukawapa amani, na Thoma alipohakikishwa kwa kuona mikono yako na ubavu wako, akakukiri kama Bwana na kama Mungu;Wewe mwenyi kuokoa wenye kukutumainia wewe, Mpenda-wanadamu, utukufu kwako.

# MU KAZI MBILI ASUBUI YA JUMA YA MT. THOMAS

*Elezo: Padri atasema: Hahimidiwe Mungu wetu...Kisha ataimba Kristu alifufuka mara moja na waimbaji wataimba mara wa wili. Kisha Utukufu...Sasa...Utatu Mtakatifu...Bwana hurumia (mara*

*tatu), Utukufu...sasa...Baba yetu...Wimbo tatu na Eksapsalmos, Bwana ndiwe...Apolitikion ya Mt. Thomas na kisha:*

**KATHISMA YA KWANZA.** *Sauti ya kwanza. Tu lithu sfragisthentos.*

Wanawake walikuja asubui mapema Kaburini, malaika akawatokea na wakashikwa na woga; uzima ukangaa kaburini, muumija uliyowaogopesha na wakaenda kuwatangazia Wafwasi ufufuo wa Bwana: Katika uwezo wake kubwa, Kristu amenyaganya Hadeze na kufufua wafu wote toka uvumbi wa kaburi; akafukuza woga wa hukumu kwa uwezo wa Msalaba.

Kama mwenye haki anaokoa, wapi nitajionyesha mimi mwenye zambi? Sikuchukua wala uzito wala joto ya mchana, lakini unihesabie pamoja na wale wa saa ya kumi na moja, ee Mungu wangu, na uniokoe.

Kama maaskari wema, na shauri moja katika imani, bila woga na bila lauma mbele ya vitisho vya wazuluma, Wahodari, mulienda mbele ya Kristu, mkichukua msalaba wake wa samani. Ku mwisho wa Safari na wa mashindano mukapokea ushindi wa Juu-mbinguni. Utukufu kwa huyu ambaye nguvu yake ikawa tegemeo yenu, utukufu kwa huyu aliyemivika taji, utukufu kwa huyu anayetenda ndani yenu kwa kutuponyesha.

**THEOTOKION**

Kujeni, enyi Waaminifu wote, tumutukuze Mtakatifu Mzazi-Mungu, na tusujudu mbele yake: Ni boma letu imara; anaweza kutusemea kwa Mwana wake aliyezaa; kwa maombezi yake anaweza kutuokoa toka mauti na toka azabu zenyi kushambulia roho zetu.

**KATHISMA YA MBILI.** *Sauti ya tano. Ton Sinanarkhon Logon*

Kujeni, waaminifu wote, kwa nyimbo zetu tutukuze makumbusho ya Mtume na Mfwasi wa Kristu ambaye alipopapasa alama ya misumari aliandika mioyoni mwetu imani ya kweli alitafuta sababu ya kuisabitisha ulimwenguni; sasa anamuomba Mwokozi kusudi alete neema ya wokovu rohoni mwetu.

Utukufu kwa Baba…Sasa na siku zote…*(mara ingine)*

*Kisha tunasoma: Tukiona Ufufuo wa Kristu...Kanuni ya Siku Kuu na Mineon. Kontakion na Eksapostilarion ya Siku Kuu.*

## MASIFU. *Sauti ya kwanza.*

Bwana wewe uliyevumilia Msalaba uliharibu mauti, na uliyefufuka katika wafu, tuliza uzima wetu, kwa kuwa wewe ni mwenyezi peke yako. *(mara mbili).*

Ewe Mwokozi, usimzarau mtumishi wako mfungwa wa uzaifu na zambi, lakini amsha moyo wangu ku toba, unifanye kuwa mtumishi wa shamba lako la ms\zabibu, ee Bwana, ukinipa mshahara wa saa ya kumi na moja na neema ya wokovu.

Tazama waaskari wa mfalme mkuu: Walishindana na amri za wazulumu na walizarau mateso, kwa usharifu, wakakanyanga na kuvunja kosa lote; walipopokea taji walilostahili wanatupokelea amani kwa Mwokozi na neema ya wokovu kwa ajili ya roho zetu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya mbili*

Ee Kristu, milango yote ilipokuwa imefungwa, ulionekana kwa Wafwasi wako Thoma hakuwa pamoja nao, lakini ilikuwa ni maongozi ya Mungu, kwa sababu alisema: Sitasadiki kama nisipomuona Bwana, kama nisipoona ubavu wake humo mulitoka damu na maji, ni ubatizo; kama nisipoona kidonda kilichoponyesha vidonda nyingi vya wanadamu; paka nikiona ya kama si muzimu lakini ni mutu eko na mifupa na mwili. Wewe uliyeshinda mauti na kumusadikisha Thoma, Bwana, utukufu kwako.

## APOSTIKHA. *Sauti ya mbili. Ikos tu Efratha.*

Enyi waaminifu, pamoja na Malaika tuimbie daima Kristu aliyefufuka kaburini siku ya tatu na aliyefufua watu wote pamoja naye.

Shairi: Habari yao ilisikilika duniani kote, neno lao mpaka ku mwisho wa dunia.

Ee Mungu wa mapendo, Thoma alipopapasa ubavu wako imani yake ikaongezeka; na kwa ajili yake tangu sasa tunakutambua ya kama wewe ni Mungu.

Shairi: Mbingu zinahadisia utukufu wa Mungu, anga inatangaza tendo la mikono yake.

Ee Mwokozi, uliwapa watu wako amani wakati ulifufuka kaburini, eeMungu Mwenyezi, na toka Hadeze uliamusha dunia pamoja nawe.

Utukufu kwa Baba… Sasa na siku zote… *Sauti ya sita.*

Thoma, Bwana, Ee Kristu, milango yote ilipokuwa imefungwa, ulionekana kwa Wafwasi wako Thoma hakuwa pamoja nao, lakini ilikuwa ni maongozi ya Mungu, kwa sababu alisema: Sitasadiki kama nisipomuona Bwana, kama nisipoona ubavu wake humo mulitoka damu na maji, ni ubatizo; kama nisipoona kidonda kilichoponyesha vidonda nyingi vya wanadamu; paka nikiona ya kama si muzimu lakini ni mutu eko na mifupa na mwili. Wewe uliyeshinda mauti na kumusadikisha utukufu kwako.

# MU KAZI MBILI MANGARIBI YA JUMA YA MT. THOMAS

*Elezo: Kisha: «Bwana nimekuita...» tunaimba wimbo sita; Tatu ya Siku Kuu ya mt. Thomas na tatu ya Mineon.*

Wimbo ya Siku Kuu: *Sauti ya kwanza*

Mpenda-wanadamu aliyefufuka siku ya tatu alisema: Thoma, unipapase, tazama mikono yangu, vidonda vya miguu yangu na ubavu wangu; ujuwe ya kama umungu wangu haubadilike lakini ndani yangu nimechukua hali ya ubinadamu, ni kwa hii ninateswa mwilini.

Thoma alishituka wakati aliona alama ya misumari juu ya miguu na juu ya mikono, hii ono ya ajabu ikamushangaza: Alipopapasa na kuona na mkono wake ubavu wa Bwana, akashuhudia waziwazi mataifa Ufufuo wake kaburini siku ya tatu.

Nasikia furaha kubwa, ee Mwokozi, wakati naona Ufufuo wako umehakikishwa kwa nguvu ya Thoma : Sababu yake tunaweza kuhakikisha umoja wa umungu wako na wa ubinadamu wako katika hali mbili na nguvu yenyi kuungana ndani yako.

***Wimbo ya Mineon tatu.***

Utukufu kwa Baba… Sasa… *Sauti ya ine.*

Ee Bwana, kwa kuonyesha nuru ya umungu wako, ulionekana katikati ya Wafwasi wako milango yote yenye kufunga, uliwaonyesha vidonda vya mikono yako na vya miguu yako, ukawaokoa toka sikitiko iliyowaregeza na uliwaambia waziwazi: Nina mwili kama munavyoiona; rafiki zangu, mimi si muzimu. Lakini kwa Mfwasi alikuwa na shaka ulimuomba apapase vidonda vyako, ulimwambia ukisema: Tazama vidonda vyangu, usiwe tena na mashaka. Na Mfwasi alipohakikishwa na mkono wake ubinadamu wako na umungu wako, kwa woga akapaza sauti na imani akasema: Bwana wangu na Mungu wangu, utukufu kwako.

## APOSTIKHA *Sauti ya kwanza.*

Msalaba ulisimikwa kule Kalvario, ukatutirikizia uzima wa milele wa hii Chemchem isiyokauka: Ubavu wa Mwokozi.

Kujeni, Mataifa, tumusifu na tumwabudu Kristu, tutukuze Ufufuo wake katika wafu; kwa maana huyu ni Mungu wetu aliyekomboa dunia toka udanganyifu wa adui.

Enyi Mashahidi watakatifu, neema gani kwa ushujaa wenu! Mulitoa damu yenu na munapokea uriti wa mbinguni; sababu ya majaribu ya muda kidogo furaha yenu inadumu milele; kweli ni mabadiliko ya ajabu : kwa sababu muliacha vitu vyenyi kuharibika sababu ya kupokea mema ya milele; munashangilia pamoja na Malaika na munatukuza daima Utatu Mtakatifu wenye asili moja.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya mnane.*

Kristu alisema: Thoma, leta mkono wako uuweke katika ubavu wangu, tazama alama ya misumari, usiwe tena na mashaka, lakini sadiki. Alipopapasa Bwana na kidole, Thoma akapaza sauti na kusema: Wewe ni Bwana wangu na Mungu wangu, utukufu kwako.

# MU KAZI TATU ASUBUI YA JUMA YA MT. THOMAS

*Elezo: Padri atasema: Hahimidiwe Mungu wetu...Kisha ataimba Kristu alifufuka mara moja na waimbaji wataimba mara wa wili. KishaWaimbaji: Utukufu...Sasa...Utatu Mtakatifu...Bwana hurumia (mara tatu), Utukufu...sasa...Baba yetu...Wimbo tatu na Eksapsalmos, Bwana ndiwe...Apolitikion ya Mt. Thomas na kisha*

**KATHISMA YA KWANZA** *Sauti ya kwanza.*

Ewe Kristu, ulipopanda msalabani, uliharibu uzulumu na nguvu ya adui; apana ao Malaika ao mwanadamu aliyetuokoa, lakini ni Mungu yeye mwenyewe: Ee Bwana, utukufu kwako.

Isaki alitolewa sadaka juu ya mulima, Yona alishuka chini ya zimu; wote wawili walitangulia kuonyesha mateso yako, ee Mungu Mwokozi: wa kwanza kamba na sadaka, wa pili maziko, uzima, na Ufufuo wako takatifu Bwana, utukufu kwako.

Kwa mateso waliyoteswa Watakatifu kwa ajili yako, tunakuomba ukubali, ewe Mungu wetu, kuponya mateso yetu yote, ee Bwana Mpenda-wanadamu.

**STAVROTHEOTOKION.**

Ee Bikira, tunasabitishwa na ulinzi wako, na kwa maombezi yako tunaokolewa ku hatari yote na kulindwa kila wakati na Msalaba wa Mwana wako, sisi waaminifu wako, tunakutukuza.

**KATHISMA YA PILI.** *Sauti ya kwanza. Ton tafon su Sotir.*

Alipogusa na mkono wake kidonda cha ubavu, Thoma hakuteketezwa, lakini akatazama na bidii vidonda na akamwambia huyu alichomwa mkuki kwa ajili yetu: Japo mateso ya Mateso yako uko kweli Bwana wangu na Mungu wangu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*(mara mbili).*

*Kisha tunasoma: Tukiona Ufufuo wa Kristu...Kanuni ya Siku Kuu na Mineon. Kontakion na Eksapostilarion ya Siku Kuu.*

## MASIFU. *Sauti ya kwanza.*

Wewe uliyesulubiwa Msalabani kwa kutupatia uzima, tunakuimbia daima kama Rabi na Mwokozi wetu.*(mara mbili).*

Ee Kristu, wewe uliyeshinda Hadeze, ulitufufua sisi wote kwa Ufufuo wako takatifu, utupe moyo safi ili tukuimbie na tukutukuze kama inavyostahili.

Mashahidi Watakatifu wenye kustahili sifa yote, hapana wala jaribu, wala huzuni, wala njaa, wala uzulumu, wala hatari, wala hasira ya wanyama kali, wala upanga, wala moto ambazo kwa vitisho vyao viliweza kuwatenga ninyi mbali na Mungu; lakini ni kwa mapendo kwa ajili yake mulisahau ulimwengu mukiwa wageni ku mwili wenu na mukishindana kwa kuzarau mauti; na tena mukapokea tuzo la kweli la kazi yenu, mukawa warisi wa ufalme wa mbingu: Ombeni kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya mnane.*

Milango yote ilipokuwa imefungwa na Wafwasi walipokusanyika, Mwokozi akaonekana mahali pale, na aliposimama katikati yao, akamwita Thoma akamwambia: Kuja upapase vidonda vyangu, na tazama alama ya misumari, usiwe tena na mashaka, lakini tangu sasa tangaza na imani Ufufuo wangu katika wafu.

## APOSTIKHA

Ni jambo la ajabu! Ni muujiza wa ajabu! Namna gani mkono wa Mtume haikuteketezwe kama nyasi haikuungua katika moto ya Mungu?

Shairi: Habari yao ilisikilika duniani kote, neno lao mpaka ku mwisho wa dunia.

Enyi waaminifu, tujikaze kutakasa mikono yetu kwa kukataa tamaa kusudi na sisi vilevile tupapase ubavu wa Mwokozi.

Shairi: Mbingu zinahadisia utukufu wa Mungu, anga inatangaza tendo la mikono yake.

Ee roho yangu, tengeneza nia zako kwa kuonekana kwa Mungu : Ni hivi Kristu anataka itimizike wakati mupya.

Utukufu kwa Baba… Sasa na siku…*Sauti umoja.*

Tazama katika roho mageuzo ya hapa chini na tayarisha ndani na mapambo ya fazila sababu ya kuangaa na uzuri.

# MU KAZI TATU MANGARIBI YA JUMA YA MT. THOMAS.

*Elezo: Kisha: «Bwana nimekuita...» tunaimba wimbo sita; Tatu ya Siku Kuu ya mt. Thomas na tatu ya Mineon.*

***Wimbo ya Siku Kuu:***

*Sauti ya mbili. Ote ek tu ksilu.*

Ee Kristu, bila kwacha kifua cha Baba, kwa rehema yako ya milele ulionekana duniani mwenyi kuchukua mwili wetu; ulipoteswa na kufa msalabani, ulifufuka siku ya tatu, na milango yote ilipokuwa imefungwa uliingia kama Mungu Mwenyezi; Thoma alipopapasa na furaha ubavu wako wenyi kuleta uzima akakutukuza kama Bwana na kama Mungu.

Ulipopigiliwa misumari msalabani, askari alikuchoma mukuki; ee Kristu, ulionja nyongo na kuteswa mpaka kufa; ulizikwa kaburini na ulivunja vifungo vya Hadeze, ulifufua pamoja nawe wale walikufa tangu milele; na bila kuvunja milango ulionekana kwa Wafwasi wako sababu ya kusabitisha imani yao kwa Ufufuo wako.

Paska ni sikukuu ya hii wakati, Paska ya siri, Paska ya Mungu, Paska ya wokovu; Paska huko Kristo anatuongoza toka mauti mpaka uzima wa milele, Paska yenyi kufukuza mateso yote mioyoni mwetu; Paska yenyi kuwapa Wafwasi furaha, Paska yenyi kumwambia Thoma aseme: Wewe uliyenyanganya ufalme wa Hadeze, uko kweli Bwana wangu na Mungu wangu.

***Wimbo ya Mineon tatu***

Utukufu kwa Baba… Sasa na siku zote… *Sauti ya ine*

Ni jambo la ajabu: Kutokuamini kunasabitisha imani; kwani Thoma alisema: Sitasadiki bila kuona, lakini alipopapasa ubavu wako, akatambua kuwa Mwana wa Mungu Bwana aliyejifanya mutu na aliyeteswa mwilini mwake; akatangaza Ufufuo wake katika wafu na akapaza sauti mbele ya wote kwa sauti kubwa akasema: Bwana wangu na Mungu wangu, utukufu kwako.

**APOSTIKHA** *Sauti ya kwanza. Wimbo ya ufufuo.*

Kwa mateso yako, ee Kristu, ulituopoa ku tamaa mbaya, kwa Ufufuo wako unatukomboa ku uharibifu, utukufu kwako, ee Bwana.

Shairi: Habari yao ilisikilika duniani kote, neno lao mpaka ku mwisho wa dunia.

Kinubi cha sauti nzuri cha Mitume cha umoja anachotetemesha Roho Mtakatifu kilifukuza mafumbo yenyi kuongozwa na mashetani na kinatangaza Bwana peke yake, ikiopoa watu ku uwongo wa miungu ya uwongo na ikiwafundisha kwa kusujudu mbele ya Utatu wa asili moja.

Shairi: Mungu ni wa ajabu katika Watakatifu wake, Mumgu wa Israeli.

Enyi Mashahidi wenye kustahili sifa yote, apana dunia iliwaficha ninyi, ni mbingu iliwapokea ninyi; milango ya Paradi zo imefunguliwa kwa ajili yenu; na kule munapata mti wa uzima; mumuombe Kristu alete amani na neema ya wokovu rohoni mwetu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*Sauti ya ine*

Ni jambo la ajabu! Nyasi haiteketezwe kwa moto ilipapasa; kwa maana Thoma hakuteketezwa wakati aliweka mukono wake katika ubavu wa moto wa Yesu Kristu Mungu wetu, lakini aligeuza kutosadiki kwake kuwa imani ya furaha, na moyoni mwake akasema: Ee Rabi uliyefufuka katika wafu, uko tena Mungu wangu, utukufu kwako.

# MU KAZI INE ASUBUI YA JUMA YA MT. THOMAS

*Elezo: Padri atasema: Hahimidiwe Mungu wetu...Kisha ataimba Kristu alifufuka mara moja na waimbaji wataimba mara wa wili. Kisha Utukufu...Sasa...Utatu Mtakatifu...Bwana hurumia (mara tatu), Utukufu...sasa...Baba yetu...Wimbo tatu na Eksapsalmos, Bwana ndiwe...Apolitikion ya Mt. Thomas na kisha*

**KATHISMA YA KWANZA.** *Sauti ya kwanza. Tu lithu sfragisthentos.*

Ewe Bwana msiyekufa, Uzima wa wote, ulipopigiliwa msalabani na kuhesabiwa kati ya wafu, ulifufuka sikutatu, ewe Mwokozi, sababu ya kumfufua Adamu ku uvumbi wa kaburi, na Majeshi ya mbinguni, yanapaza kwako sauti, ewe chemchem ya uzima: Utukufu ku Mateso yako kimungu, ee Kristu, utukufu ku Ufufuo wako, utukufu ku mapenzi yako, ewe peke yako mpenda-wanadamu.

Enyi Mitume wenyi hekima muliyovua ulimwengu wote na kupokea kwa Mungu mapendo yake mtuombee sisi tunaoimba sasa: Ee Bwana, kwa maombezi ya Mitume wako, okoa watu wako wa Kristu ukilinda roho zetu ku hatari yote.

Wote, tuwasihi Mashahidi wa Kristu wenye kutuombea wokovu wetu, na wote tuendeni kukutana nao katika imani kwa kusamehewa na kuponyeshwa kwa walinzi hawa wa imani wenye kuwafukuza mashetani.

**THEOTOKION**

Ee Bikira safi kamili, Wafwasi na Mitume Watakatifukwa mafundisho yao yenyi kuongozwa wakawatangazia wote uzazi wako wa ajabu, wakitufundisha kusujudu mbele yako, ewe Mzazi-Mungu; tunakuomba uombe pamoja nao kwa ajili ya wokovu wa watumishi wako waamini.

**KATHISMA YA MBILI.** *Sauti ya kwanza. Ton tafon su Sotir*.

Neno alimwambia Thoma: Kisha kuona kidonda cha ubavu wangu, tangu sasa usiwe tena na mashaka sababu ya kutosadiki kwako;leta kidole chako, weka mkono wako katika vidonda vyangu, na tazama alama ya misumari; utatangaza duniani Ufufuo wangu toka kaburini wenyi kuleta uzima.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku...*(mara ingine)*

*Kisha tunasoma: Tukiona Ufufuo wa Kristu...Kanuni ya Siku Kuu na Mineon. Kontakion na Eksapostilarion ya Siku Kuu.*

## MASIFU. *Sauti ya kwanza.*

Tukitukuza ukubali kwako unaofaa kwa Mungu, tunakusifu, ee Kristu; ulizaliwa kwa Bikira, na ulikuwa usiyotengwa na Baba; uliteswa sawasawa na mutu, na ulivumilia Msalaba, kama ulivyotaka; wokovu wa dunia, ee Bwana, utukufu kwako.

Tushangilia kwa wimbo moja Mitume Petro na Paulo, Luka, Matayo, marko na Yoane, Andrea, Tomasi, Bartholomeo Yakobo, Filippo na Simoni: Kwa jamaa lote la Wafwasi tunatolea sifa na nyimbo zetu.

Enyi Mashahidi Watakatifu, furahini katika Bwana, kwani mumeshindana Wazulumu; wala upanga, wala vema sana; mumeshindana na wafalme na mumewashinda wazulumu; wala upanga, wala moto haukuwaogopesha ninyi, wala wanyama kali waliyorarua mwili wenu, lakini pamoja na Malaika mukamwimbia Kristu na mukapokea taji la mbinguni: Ombeni ili tupewe neema ya wokovu.

Utukufu kwa Baba....Sasa na siku zote...*Sauti ya inne.*

Ni jambo la ajabu! Ni Yoane aliegamia juu ya kifua cha cha Neno, na Thoma alistahiliwa kupapasa ubavu wake; wa kwanza alitezamia fumbo ya ndani ya Mungu, mwingine alistahiliwa

kutufundisha njia yake ya wokovu, kwani alionyesha waziwazi alama za Ufufuo wake akisema: Bwana wangu na Mungu wangu, utukufu kwako.

**APOSTIKHA.** *Sauti ya mbili. Ikos tu Efratha.*

Tufukuze mbali haya ya tamaa na mutikisiko wa mawazo kusudi tuone ikichanuka wakati mupya wa imani.

Shairi: Habari yao ilisikilika duniani kote,neno lao mpaka ku mwisho wa dunia.

Ee Mwokozi, ulionekana kwa Mitume wako watakatifu milango ilipokuwa imefungwa, katika wao ulifanya mioyoni mwetu Roho wako Mtakatifu.

Shairi: Mbingu zinahadisia utukufu wa Mungu, anga inatangaza tendo la mikono yake.

Ee Mfalme wa ulimwengu, tunapokuona sasa apana na macho yetu ya mwili lakini katika mapendo ya roho zetu, tunasadiki ya kama uko Mungu na kwa nyimbo zetu tunakutukuza.

Utukufu kwa Baba… Sasa na siku zote… *Sauti ya sita.*

Ee Mwana wa pekee tena Neno wa Mungu, siku munane kisha Ufufuo wako, ulionekana kwa Wafwasi wako milango yote ilipokuwa yenyi kufunga na kuwapa amani; kwa mfwasi aiyesadiki ulimuonyesha alama ya misumari na ukamwambia ukisema: Kuja upapase mikono yangu, miguu yangu na kidonda cha ubavu wangu. Mfwasi alihakikishwa na akapaza sauti na kusema. Utukufu kwako, ee Bwana wangu na Mungu wangu.

# MU KAZI INE MANGARIBI YA JUMA YA MT. THOMAS

*Elezo: Kisha: «Bwana nimekuita...» tunaimba wimbo sita; Tatu ya Siku Kuu ya mt. Thomas na tatu ya Mineon.*

***Wimbo ya Siku Kuu***

*Sauti ya kwanza. Ton uranion tagmaton.*

Tunapovaa nuru yenyi kuangaa kupita theluji, kwa hii ibada ya Paska tufurahie makumbusho ya hii siku ambayo Kristu aliye jua la haki aliposimama na kufufuka katika wafu, anatufurahisha na nuru yake ya milele.

Malkia wa karamu, malkia wa sikukuu ni hii siku ya leo, hii siku aliyofanya Bwana kweli; mataifa yote yafurahi katika Yeye kama anavyoimba Daudi, kwani Bwana aliwatokea Wafwasi wake milango yote ilipokuwa imefungwa sababu ya kuwapa amani.

Kutosadiki kwa Thoma kunahakikisha Ufufuo wa wokovu ambao Neno, aliye Mungu-Mutu, alishinda mapango ya Hadeze; na kwa ajabu na mkono wake akatambua alama ya misumari katika mikono na miguu sababu ya kusabitisha imani ya ulimwengu.

Utukufu kwa Baba… Sasa… *Sauti ya mbili.*

Milango yote ilipokuwa imefungwa, Yesu alionekana katikati ya Wafwasi wake, akawaondolea woga wao na akawapa amani; kisha akamwita Thoma akamwambia: Sababu gani hausadiki ya kama nimefufuka katika wafu? Weka mkono wako katika ubavu wangu, tazama mikono yangu na miguu yangu, na sababu ya kutosadiki kwako watu wote watajua mateso yangu na Ufufuo wangu katika wafu kusudi wapazwe sauti pamoja nawe wakisema: Bwana wangu na Mungu wangu, utukufu kwako.

**APOSTIKHA.** *Sauti ya kwanza.*

Msalaba bora wa Mwokozi ni boma kabisa ya kweli kwa sisi; tulipoutumainia, wote tumeokoka.

Shairi: Nitanyanyula macho yangu kwako, ee mwenye kuikala mbinguni, tazama...

Pokea, ee Bwana Mtakatifu, maombi yetu ya mangaribi, na utupe maondoleo ya zambi zetu; kwa maana ni wewe peke uliyeonyesha ku ulimwengu ufufuo.

Shairi: Utuhurumie, ee Bwana, utuhurumie, kwani tunayala na kuzarauliwa.

Ewe Mungu wa mapendo, kwa maombi ya Watakatifu wote na ya Mzazi-Mungu utupe amani na utuhurumie.

Utukufu kwa Baba....Sasa na siku zote...*Sauti ya mnane.*

Kristu alisema: Thoma, papasa ubavu wangu na mkono, tazama alama ya misumari, usiwe tena na mashaka lakini sadiki. Thoma alipopapasa Bwana na kidole chake akapaza sauti na kusema: Uko kweli Bwana wangu na Mungu wangu, utukufu kwako.

# MU KAZI TANO ASUBUI YA JUMA YA MT. THOMAS

*Elezo: Padri atasema: Hahimidiwe Mungu wetu...Kisha ataimba Kristu alifufuka mara moja na waimbaji wataimba mara wa wili. Kisha Utukufu...Sasa...Utatu Mtakatifu...Bwana hurumia (mara tatu), Utukufu...sasa...Baba yetu...Wimbo tatu na Eksapsalmos, Bwana ndiwe...Apolitikion ya Mt. Thomas na kisha*

**KATHISMA YA KWANZA .** *Sauti ya kwanza. Tu lithu sfragisthentos.*

E we Mpenda-wanadamu, tunasujudu mbele ya mti wa Msalaba wako ambayo ulipigiliwa misumari, wewe Uzima wa ulimwengu; kwa Munyanganyi aliyekuamini, ee Mwokozi, ukamfungulia Paradizo na ukamupa heri ya milele yeye aliyekuamini, ee Bwana, wakati alikupazia sauti na kusema: Unikumbuke, ee Bwana; kama yeye, utupokee na sisi tunaokulalamikia: Wote tumetenda zambi, usituzarau katika wema wako.

Ewe Mwokozi, waaskari waliyolinda Kaburi yako wakaangushwa chini kwa ugaro wa malaika aliyeonekana sababu ya kuwatangazia wanawake Ufufuo wako Takatifu; na wewe mwenye kutuokoa toka mauti, tunakutukuza na tunasujudu mbele yako, ewe Mfufuliwa kaburini na Mungu wetu moja.

Utukufu kwa Baba....

Ee Bwana, utukufu wa mashindano na taji ya Washindaji, ndiwe uzuri wa Mashahidi Watukufu: Kwa imara yao katika majaribu walifukuza makafiri na wakapokea ushindi mbinguni kwa uwezo wa Mungu; ee Bwana, kwa maombezi yao utupe sisi neema ya wokovu.

**STAVROTHEOTOKION** Sasa na siku zote..

Mwana-kondoo jike Safi alipoona Mwana-Kondoo na Mchungaji ametundikwa bila uzima juu ya mti, akalia na kulalamika akisema: Ee Mwanangu, namna gani nitateswa juu ya mapendo yako isiyokadirika na Mateso yako ya kutaka, ewe Bwana wa wema wote.

**KATHISMA YA MBILI.** *Sauti ya kwanza. Ton tafon su Sotir.*

Heri wewe uliyepapasa vidonda vya Mwokozi na ubavu wake wa ajabu iliponyesha kidonda kubwa cha Adamu na kuwapa waaminifu wote kwa maneno ya Mitune watakatifu heri isiyoharibika ya Ufufuo wake takatifu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*(mara ingine)*

*Kisha tunasoma: Tukiona Ufufuo wa Kristu...Kanuni ya Siku Kuu na Mineon. Kontakion na Eksapostilarion ya Siku Kuu.*

## MASIFU. *Sauti ya kwanza.*

Kwa Msalaba wako, ee Kristu, malaika na wanadamu wakafanya Eklezya moja, kundi moja la Kondoo; mbingu na dunia zinafuraha: Ee Bwana, utukufu kwako.*(mara mbili).*

Ee Kristu, tunasifu mateso yenye kutuokoa na tunatukuza Ufufuo wako takatifu.

Kujeni, enyi mataifa yote, tuimbe mashairi na nyimbo za kiroho kwa kuwatukuza Mashahidi watukufu wa Kristu, Watangazaji wa imani tena taa za ulimwengu, Chemchem isiyokauka ambako kunatiririka maponyesho; kwa maombezi yao, ee Kristu Mungu wetu, leta amani duniani na neema ya wokovu rohoni mwetu.

Utukufu kwa Baba....Sasa na siku zote...*Sauti ya mnane.*

Milango yote ilipokuwa imefungwa na Wafwasi walipokusanyika, Mwokozi akaonekana mahali pale, na aliposimama katikati yao, akamwita Thoma akamwambia: Kuja upapase vidonda vyangu, na tazama alama ya misumari, usiwe tena na mashaka, lakini tangu sasa tangaza na imani Ufufuo wangu katika wafu.

**APOSTIKHA.** *Os geneon en Martisin. Sauti ya ine*

Kwa Msalaba wako ulifungulia wanadamu Paradizo, uliamusha wafu, ewe Uzima wetu; ufufuka, ukaharibu nguvu ya mauti; kweli uliunganisha mbingu na dunia, uliwajaza Mitume na furaha kubwa, ee Neno wa Mungu,, ukawapa amani na neema ya Roho Mtakatifu.

Shairi:Habari yao ilisikilika duniani kote,neno lao mpaka ku mwisho wa dunia.

Mauti imeondolewa, uzima wa milele imechanuka, kisha miaka mingi minyororo ya Hadeze imevunjwa; inchi na mbingu zinashangilia pamoja na wazima, kwa sababu Kristu Amefufuka, mauti imenyanganywa mateka yake; wakati wa furaha imefika, na alionekana milango yote ilipokuwa imefungwa, Bwana mwenye kutupatia uzima.

Shairi: Mbingu zinaeleza utukufu wake, anga inatangaza tendo la mikono yake.

Leo siku Bwana aliyofanya tushangilie na furaha: Kristu ametokea kama Chemchem ya uzima, Hadeze imeondolewa, Mitume wanatangaza furaha, Thoma mwenyi mashaka anapapasa vidonda vya Bwana, na kwa hii anatangaza hali mbili za Kristu.

Utukufu kwa Baba… Sasa na siku zote… *Sauti ya mnane.*

Kristu alisema: Thoma, papasa ubavu wangu na mkono, tazama alama ya misumari, usiwe tena na mashaka lakini sadiki. Thoma alipopapasa Bwana na kidole chake akapaza sauti na kusema: Uko kweli Bwana wangu na Mungu wangu, utukufu kwako.

## MU KAZI TANO MANGARIBI YA JUMA YA MT. THOMAS

*Elezo: Kisha: «Bwana nimekuita...» tunaimba wimbo sita; Tatu ya Siku Kuu ya mt. Thomas na tatu ya Mineon.*

***Wimbo ya Siku Kuu:***

Ee Yesu Mungu wetu Mwenyezi, milango ilipokuwa imefungwa na Wafwasi walipokuwa wamekusanyika, uliingia mara moja, na uliposimama katikati yao ukawapa amani na ukawaja na Roho Mtakatifu, ukawaambia wakae katika Yerusalema wasiende mbali mpaka wajazwe na nguvu ya juu mbinguni; ndio maana tunakulalamikia: Bwana, Ufufuo wetu, nuru yetu na amani yetu, utukufu kwako.

Ee Bwana, siku munane kisha Ufufuo wako, ulionekana kwa Wafwasi wako mahali walikusanyika na ukawaambia: Amani kwenu! Kwa mfwasi mwenyi moyo mgumu ulimwonyesha mikono yako na ubavu wako, na kwa imani akakulalamikia: Bwana wangu na Mungu wangu, utukufu kwako.

Ee Kristu, Thoma, anayeitwa Mupasa, hakuwa pamoja nao wakati uliingia milango yote yenyi kufunga; ndio maana hakusadiki maneno waliyomwambia, sababu ya kusabitisha ku imani njia ya wasiyoamini; lakini kwa wema wako hakukataa kumuonyesha ubavu wako takatifu na vidonda vya mikono yako na vya miguu yako: akaipapasa na wakati alikuona, akatambua ndani yako umutu na umungu wako, na akapaza sauti na kusema: Bwana wangu na Mungu wangu, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba… Sasa na siku zote… *Sauti ya sita*

Ee Kristu, milango yote ilipokuwa imefungwa, ulionekana kwa Wafwasi wako Thoma hakuwa pamoja nao, lakini ilikuwa ni maongozi ya Mungu, kwa sababu alisema: Sitasadiki kama nisipomuona Bwana, kama nisipoona ubavu wake humo mulitoka damu na maji, ni ubatizo; kama nisipoona kidonda kilichoponyesha vidonda nyingi vya wanadamu; paka nikiona ya kama si muzimu lakini ni mutu eko na mifupa na mwili. Wewe uliyeshinda mauti na kumusadikisha Thoma, Bwana, utukufu kwako.

Sasa na siku zote...**THEOTOKION**

Utukufu wa ulimwengu, uliyopandwa kwa watu, na ulizaa Bwana, mlango wa mbinguni, tumusifu Bikira Maria, wimbo wa wasiyo mwili, na pambo ya waaminifu; kwa sababu yeye alikuwa mbingu, na Hekalu la umungu; yeye alipomoa ukuta ya adui, alibadilisha kwa amani, na alifungua

ufalme. Basi pakuwa na hii, nanga ya imani, tuiko na mlinzi, Bwana hivi aliyezaliwa Kwake. Kwa hivi kuwa na moyo, kuwa na moyo taifa la Mungu; kwa sababu yeye anagombanisha adui sawa mwenyezi.

## APOSTIKHA

Pokea, ee Bwana Mtakatifu, maombi zetu za mangaribi, na utupatie maondoleo ya zambi zetu; kwa maana ni wewe peke uliyeonyesha ku ulimwengu ufufuo.

*Shairi:* Bwana anatawala, amevikwa utukufu. Bwana anavaa uwezo na unamuzunguka.

Mataifa, tembeyeni pembeni ya sayuni na mumuzunguka, na mumutukuze ndani yake Yeye aliyefufuka katika wafu; kwa maana huyu ni Mungu wetu, aliyetukomboa ku maovu yetu.

*Shairi:* Kwa sababu ulikaza ulimwengu, ambao hautatikisika.

Kujeni Mataifa tumusifu, na tumwabudu Kristu, tutukuze Ufufuo wake katika wafu; kwa maana huyu ni Mungu wetu, aliyekomboa dunia katika udanganyifu wa adui.

*Shairi*: Ku makao yao kunafaa utakatifu, Bwana, juu ya urefu wa masiku.

Kwa mateso yako, ee Kristu, ulituopoa ku tamaa mbaya, kwa Ufufuo wako unatukomboa ku uharibifu, utukufu kwako, ee Bwana.

Utukufu kwa Baba....Sasa na siku zote...*Sauti ya tano.*

Ee Mpenda-wanadamu, rehema yako ni kubwa sana, ulivumilia kupigwa na Wayuda, kupapaswa na Mtume, kupelelezwa na makafiri. Namna gani ulitwaa mwili, namna gani uliteswa msalabani Wewe peke yako usiye na zambi? Utufundishe kukulalamikia kama Thoma tukisema: Utukufu kwako, Bwana wangu na Mungu wangu.

**Apolitikion** *(mara tatu).*

# MU POSHO ASUBUI YA JUMA YA MT. THOMAS

*Elezo: Padri atasema: Hahimidiwe Mungu wetu...Kisha ataimba Kristu alifufuka mara moja na waimbaji wataimba mara wa wili. Kisha Utukufu...Sasa...Utatu Mtakatifu...Bwana hurumia (mara tatu), Utukufu...sasa...Baba yetu...Wimbo tatu na Eksapsalmos, Bwana ndiwe...Apolitikion ya Mt. Thomas na kisha*

**KATHISMA YA KWANZA.** *Sauti ya kwanza.*

Ewe Mwokozi, maaskari waliyolinda Kaburi yako wakaangushwa chini kwa uugaro wa malaika aliyoonekana sababu ya kuwatangazia wanawake Ufufuo wako Takatifu; nawe mwenyewe kutuokoa ku mauti, tunakutukuza na tunasujudu mbele yako, Mfufuliwa kaburini na Mungu wetu mmoja.

Utukufu kwa Baba...*Tu lithu sfragisthentos*

Wanawake walikuja asubui mapema Kaburini, malaika akawatokea na wakashikwa na woga; uzima ukangaa kaburini, muumija uliyowaogopesha na wakaenda kuwatangazia Wafwasi ufufuo wa Bwana: Katika uwezo wake kubwa, Kristu amenyaganya Hadeze na kufufua wafu wote toka uvumbi wa kaburi; akafukuza woga wa hukumu kwa uwezo wa Msalaba.

Sasa na siku zote. **THEOTOKION.**

Wakati Gabrieli alisema kwako Bikira, salamu, kwa sauti; Rabi wa wote alichukua mwili, ndani yako safina takatifu, sawa mwenye haki Daudi alivyosema. Ulionekana kuwa munene sana kuliko mbingu, kwa sababu ulichukuwa Muumbaji wako. Utukufu kwa yule alikaa ndani yako; utukufu kwa yule alitoka kwako; utukufu kwa yule alitupatia uhuru, juu ya uzazi wako.

**KATHISMA YA MBILI.** *Sauti ya kwanza. Tu lithu sfragisthentos.*

Ee Bwana wa wema, kwa kuwaogopa Wayuda Wafwasi walijificha na walikusanyika katika Sayuni, ukawatokea milango ilipokuwa imefungwa, ukawajaza na furaha; uliwaonyesha mikono yako na kidonda cha ubavu wako, ukamwambia mfwasi asiyesadiki: weka mkono wako katika ubavu wangu, unisaidiki, ni mimi niliyeteswa kwa ajili yako.

Utukufu kwa Baba… Sasa na siku zote…*(mara mbili)*

*Kisha tunasoma: Tukiona Ufufuo wa Kristu...Kanuni ya Siku Kuu na Mineon. Kontakion na Eksapostilarion ya Siku Kuu.*

**MASIFU.** *Sauti ya kwanza.*

Ee Kristu,tunasifu mateso yako yenye kutuokoa na tunatukuza Ufufuo wako takatifu.

Wewe uliyesulubiwa Msalabani sababu ya kuangusha mauti na uliyefufuka katika wafu weka uzima wetu katika amani, ee Bwana mwenyezi.

Ee Kristu, wewe uliyeshinda Hadeze, ulitufufua sisi wote kwa Ufufuo wako takatifu : utupe roho safi ili tukuimbie na kukutukuza kama inavyostahili.

Tukitukuza mapendo yako ya umungu, tunakusifu, ee Kristu; bila kutengana na Baba ulizaliwa kwa Bikira, na kwa umutu wako uliteswa msalabani kwa kutaka kwako; ulitoka kaburini kama katika nyumba ya arusi sababu ya kuokoa dunia: ee Bwana, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba....Sasa na siku zote. *Sauti ya sita*

Ee Mwana wa pekee tena Neno wa Mungu, siku munane kisha Ufufuo wako, ulionekana kwa Wafwasi wako milango yote ilipokuwa yenyi kufunga na kuwapa amani; kwa mfwasi aiyesadiki ulimuonyesha alama ya misumari na ukamwambia ukisema: Kuja upapase mikono yangu, miguu yangu na kidonda cha ubavu wangu. Mfwasi alihakikishwa na akapaza sauti na kusema: Utukufu kwako, ee Bwana wangu na Mungu wangu.

**APOSTIKHA.** *Sauti ya kwanza. Panefimi martires.*

Kisha Ufufuo wako wa ajabu, ee Bwana Chemchem ya uzima, kama haukuvunja milango ya kaburi, uliingia vivyo hivyo kwa Mitume wako watukufu milango yote ilipokuwa imefungwa na ukawajaza na furaha, ukawapa Roho wa ukweli kwa wema wako kubwa.

Shairi: Tukuza Bwana, ee Yerusalema, shangilia Mungu wako, ee Sayuni.

Ee Bwana, Thoma, anayeitwa Mupasa, hakuwa pamoja nao wakati uliwatokea Wafwasi wako; ndio maana hakusadiki Ufufuo wako na akawaambia wale walikuona ya kwamba: Nisipoweka kidole changu katika ubavu wake ne katika alama ya misumari, sitasadiki ya kama amefufuka.

Shairi: Kwani alisimika miti ya milango yako, alitukuza wana wako katikati yako.

Kristu alisema: Thoma, unipapase, kwa sababu unaitaka, leta mkono wako na ujue ya kama niko na mifupa na mwili, mwili wa mutu; usiwe tena na mashaka, lakini sadiki! Thoma akamujibu akisema: Uko Bwana wangu na Mungu wangu, utukufu kwa Ufufuo wako takatifu.

Utukufu kwa Baba…Sasa na siku zote…*Sauti ya kwanza.*

Wafwasi walikuwa na shaka, lakini siku ya munane Mwokozi alionekana katikati yao mahali walikusanyika, na alipowapa amani, akamwita Thoma na akamwambia: Mtume kuja upapase mikono yangu iliyotobolewa na misumari. Ilifai Thoma awe na shaka sababu ya kuongoza roho za waaminifu kwa kumujua Mungu; na kwa woga akapaza sauti na kusema: Bwana wangu na Mungu wangu, utukufu kwako.

# MU JUMA YA WANAWAKE WABEBAJI-MANUKATO NA MT. YOSEFU WA HAKI

*Elezo: Padri atasema:* Ahimidiwe Mungu wetu...*na ataimba mara moja:* Kristu alifufuka. *kisha waimbaji wataimba mara mbili hii wimbo na kisha mara moja watasoma Zaburi Proimiakos. Kisha:* «Bwana nimekuita...» *na wimbo kumi; saba ya ufufuo, sauti ya mbili na tatu ya Wabebaji-manukato.*

***Wimbo ya Ufufuo****. Sauti ya mbili.*

Kujeni tumwabudu huyu aliyezaliwa na Baba mbele ya milele, Mungu neno aliyechukuwa mwili, kwa Bikira Maria; kwa sababu alivumiliya Msalaba, alijitoa ku maziko, kama alivyotaka, na alifufuka katika wafu, aliniokoa mimi mtu mpotevu.

Kristu Mwokozi wetu, alizimisha maandiko mabaya ya ndani zetu, kwa kuipigilia Msalabani, na aliharibu nguvu ya mauti. Tuabudu Ufufuo wake wa siku tatu.

Tuimbeni Ufufuo wa Kristu pamoja na malaika wakuu; kwa maana huyu ni Mkombozi, na Mwokozi wa roho zetu; na maogopesho ya utukufu, na nguvu ya uwezo, eko nakuja tena, kuhukumu dunia aliyeumba.

Malaika alihubiri ya kuwa wewe ni Rabi, mwenye aliyesulubiwa na aliyezikwa, na aliwaambia wanawake; kujeni tazameni, pahali alipolala Bwana, kwani amefufuka, kama alivyosema, kwa kuwa yeye ni mwenyezi; ndiyo maana tunabudu, wewe peke msiye kufa. Kristu Mpaji wa uzima, utuhurumie.

Kwa Msalaba wako ulivunja, apizo la muti; kwa maziko yako uliharibu, nguvu ya mauti; na kwa Ufufuo wako, uliangaza ukoo wa wanadamu; kwa hii, tunalalamika, ee Kristu mwema, na Mungu wetu Utukufu kwako.

Mbele yako Bwana, milango ya mauti ilifunguka na woga; wachungaji wa kuzimu pakukuona walipata woga; kwa maana ulivunja milango ya shaba, na kuzuia makomeo ya chuma, na ulituondoa ku giza, na kivuli cha mauti, na kupasua mafungo yaliyotufunga.

Pakuimba wimbo wa wokovu, tunaimba ku kinywa kujeni wote mu nyumba ya Bwana, tusujudu na tuseme; ee Wewe uliyesulubiwa pa muti, na uliyefufuka katika wafu, na uliye mu kifua cha baba, hurumia zambi zetu.

***Wimbo ya wanawake Wabebaji-manukato***

Asubui mapema, Wanawake walipekeleka manukato ku kaburi ya Bwana, hawakupata ile walitafuta, wakasikitika sababu ya hii mabadiliko, na mbele ya jiwe lililosukumwa wakaulizana mumoja kwa mwingine: Wapi mlango wa kaburi? Wapi walinzi Pilato alituma sababu ya kulinda kaburi? Lakini sikitiko yao ikaondolewa wakati walimuona Malaika mwenyi kuangaa aliyewaambia: Sababu gani munamutafuta mukilia huyu aliye hai na mwenyi kuwapa wanadamu uzima? Amefufuka katika wafu, Kristo Mungu wetu Mwenyezi mwenye kutupa sisi wote uzima wa milele, nuru na neema ya wokovu.

Sababu gani munachanganya machozi yenu na manukato munabeba? Jiwe limesukumwa, kaburi ni wazi; tazameni namna gani uzima imeshinda mauti, tazameni jiwe limekuwa ushuhuda wa nuru, tazameni usingizi gani walilala walinzi makafiri; ile ilikuwa zamani chini ya utumwa wa mauti imeokolewa kwa mwili wa Mungu wetu, Hadeze inalia na uchungu; lakini kwendeni upesi mukawaambie Mitume ya kwamba: Kristu mshindi wa mauti na Mzaliwa wa kwanza katika wafu anawatangulia kwenda Galilea.

Asubui mapema wanawake wabebaji manukato wakaenda kwa haraka ku kaburi yako kukutafuta, ee Kristu, sababu ya kupakaa manukato mwili wako takatifu; lakini kisha maneno Malaika aliyowaambia wakaenda wepesi kwa Mitume kuwapasha habari ya furaha wakasema: Amefufuka, Mfalme wa wokovu wetu; Mshindi wa mauti ameleta duniani uzima wa milele na neema ya wokovu.

Utukufu kwa Baba… *Sauti ya sita*

Wanawake Wabebaji-manukato walipofika kaburini na walipoona kaburi wazi na hawakupata mwili wako takatifu japo kuja kwao wepesi, wakalia na kusema: Nani alituiba matumaini yetu? Nani alibeba mwili tupu wenyi kupakaa manukato ambaye kwa Mama yake alikuwa kitulizo? Ole wetu! Namna gani aliuawa huyu mwenyi kuwapa watu uzima? Namna gani Mshindi wa Hadeze aliwekwa

kaburini? Lakini kwa uwezo wako, ee Mwokozi, fufuka siku ya tatu kama ulivyosema sababu ya kuleta neema ya wokovu rohoni mwetu.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION** *Sauti ya mbil*

Kivuli cha Sheria kinafifia mbele ya neema, sawa kichaka kiliwaka moto bila kuteketezwa, hivyo ulizaa Bikira, na ulibaki Bikira;jua la haki alisimama pahali pa nguzo ya moto, tazama Kristu anasimama pahali pa Musa, Yeye aliye Mwokozi wa roho zetu.

**MWANGAZA UPOLE (ILARON). . . PROKIMENON:**

Bwana anatawala, amevikwa utukufu *(mara tatu).*

**L I T I A** *Sauti ya kwanza*

Malaika mwenyi kuangaa alisema: Enyi wanawake wabebaji-manukato, nini munakuja kufanya kaburini? Sababu gani munamutafuta katika wafu Yeye aliye hai? Muwe na moyo: Bwana amefufuka!

Wanawake walikuja na woga ku kaburi yako sababu ya kupakaa mwili wako manukato, lakini wasipoipata wakaulizana mumoja kwa mwingine kwa kutokujuwa Ufufuo, Malaika mumoja aliwatokea na kuwaambia: Kristu amefufuka, ametupatia neema ya wokovu.

Maria Magdalena na Maria mwingine walikwenda kaburini kumutafuta Bwana, wakamuona Malaika mumoja mwenyi kuangaa kama umeme amekaa pembeni ya jiwe na akawaambia: Sababu gani munamutafuta katika wafu Yeye aliye hai? Hayuko hapa, amefufuka kama alivyosema, anawatangulia kwenda Galilea. Tunaposujudu mbele yake, tunaimba: Ee Mfufuliwa katika wafu, Bwana, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba… *Sauti ya sita*

Yosefu alikwenda kwa Pilato kumwomba mwili wa Yesu, akauweka ndani ya kaburi mupya; kwa sababi ilifai Kristu atoke kaburini kama katika nyumba ya arusi. Wewe uliyeharibu nguvu ya mauti sababu ya kuwafungulia wanadamu milango ya Paradizo, Bwana, utukufu kwako.

Sasa na siku zote...**THEOTOKION.** *Sauti umoja.*

Muumba na Mukombozi wangu, Bwana Yesu Kristu, alipotoka tumboni mwako ewe Bikira safi kamili, alivaa mwili wangu sababu ya kuokoa Adamu toka laana ya zamani; ndio maana, ee Bikira Mzazi-Mungu tunakutolea daima salamu ya Malaika tukisema: Salamu, Bibi Malkia mwenyi kutulinda na kutuchunga sababu ya wokovu wa roho zetu.

## APOSTIKHA

Ufufuo wako, ee Kristu Mwokozi, unangaza ulimwengu wote, na kwa neema yako unaita tena kiumbe chako; Bwana mwenyezi, utukufu kwako.

Kisha tunaimba WIMBO WA PASKA (Angalia Masifu ya Orthros ya Paska): *Sauti ya tano*

1. Paska zabihu leo imeonekana kwetu, Paska mupya Takatifu. . .
2. Kujeni Wanawake. . .
3. Wanawake Wabebaji manukato. . .
4. Paska ya furaha, Paska ya Bwana Paska. . .

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . *Sauti ya tano.*

Wewe mwenye kuvaa nuru kama nguo, Yosefu na Nikodemu walikushusha pa mti wa Msalaba na mbele ya mwili wako, bila kaburi, wakaomboleza kwa uchungu na wakasema wakilia: Ole, ee Yesu mpole kamili! Jua lililokuona Msalabani limepata giza na inchi imetikisika kwa woga; pazia la Hekalu likapasuka na nimekuona ukivumilia kwa ajili yangu kifo cha kutaka. Namna gani nitakuzika, ee Mungu wangu? Sanda gani nitakufunika? Na mikono gani nitagusa Mwili wako Takatifu? Wimbo gani nitaimbia kifo chako? Ewe mwenye rehema kamili, natukuza mateso yako! Naimbia maziko yako na Ufufuo wako nikilalamika: Ee Bwana, utukufu kwako!

Sasa na siku zote. . .

Ufufuo ni leo na tuangazwe kwa Karamu. . .

**APOLITIKION**

Wakati ulishuka ku mauti, Uzima usiyo kufa, hapo uliregeza kuzimu, kwa unara wa umungu wako; na wakati ulifufua wafu waliyolala kuzimu, ezi zote za mbinguni zilipaza sauti; mpaji wa uzima Kristu, ee Mungu wetu utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba...

Wakati msharifu Yosefu aliposhusha mwili wako takatifu Msalabani, akaufunika na sanda mweupe na akaupakaa mafuta ya samani na akauweka mu kaburi mpya; lakini ukafufuka siku wa tatu, ee Bwana, ukaleta ku dunia neema kubwa.

Sasa na siku zote...

Karibu ya Kaburi malaika wa bwana akawatokea Miroforo na akawaambia: Kwa wafu kunastahili manemane na manukato; mwili wa Kristu umeondolewa ku uharibifu; tafazeli muimbe: Bwana amefufuka, akileta ku dunia neema kubwa.

## IBADA YA ASUBUI

### KATHISMA YA KWANZA

Wewe usiyekataza jiwe lisifunge kaburini, katika Ufufuo wako, ukatupatia jiwe la imani, ee Bwana, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba. . .

Kundi ya Wafwasi, ewe Mzazi-Mungu, Mtukufu kuliko wote, lufu imevunjwa kwa lufu, na Hadeze imeshindwa kwa Msalaba wa mwana wako; alitufufua ku lufu, akatupatia uzima, wa milele; paradizo inapewa mara ingine kwa sisi, sababu ya kufurahiwamo kama zamani; tena tunatukuza na shukrani mapendo na uwezo wa Kristu Mungu wetu.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**

Mafumbo yako yanapita ufahamu wote, na yote ni tukufu, ee Mzazi-Mungu: ulikaa bila kosa Bikira na Mtakatifu, na ulikuwa kweli mama Mzazi wakati ulizaa Mungu wa kweli. Umuombe ili aokoe roho zetu.

**KATHISMA YA MBILI** *Sauti ya mbili*

Wanawake wabebaji-manukato walipokuja asubui mapema na walipokuta kaburi wazi, wakaenda wepesi kuwaambia Mitume wakisema: Mwenyezi ameharibu nguvu ya mauti, na wale walikuwa wafungwa wa Hadeze aliwaokoa wote; tangazeni na matumaini ya kwamba kweli amefufuka, Kristu Mungu wetu mwenyi kutupatia neema ya wokovu.

Utukufu kwa Baba…

Asubui mapema Wanawake walikuja kwa siri kaburini sababu ya kukupakaa manukato, waliogopa majivuno ya Wayuda na waaskari waliolinda kaburi; hali yao ya kike ilishinda nguvu ya kiume kwa sababu mapendo ilipata neema ya Mungu; ndio maana walipaza sauti na kusema: Fufuka, ee Bwana, utulinde na utuokoe sababu ya kupenda jina lako.

Sasa na siku zote... **THEOTOKION**

Umetukuzwa kuwapita wote, tunakuimbia, ee Mzazi-Mungu; mauti imeuawa, na Hadeze imevunjwa kwa Msalaba wa Mwana wako; ametufufua ku lufu, ametupatia uzima wa milele; tumepewa Paradizo mara ingine sababu ya kufurahiwamo kama zamani; tena kwa shukrani tunatukuza mapendo na uwezo wa Kristu Mungu wetu.

*Kisha tunaimba Mahimidi ya Ufufuo na tunasoma wimboυ ya Ipakoi :*

**IPAKOI.** *Sauti ya mbili.*

Ee Kristu Mungu, Wanawake walienda Kaburini kisha mateso yako kwa kuupakaa mwili wako manukato: Wakaona malaika ndani ya Kaburi na wakashikwa na woga, kwani wakasema: Bwana amefufuka sababu ya kuleta duniani neema ya wokovu.

*Kisha tunaimba Anavathmi ya sauti ya mbili. Tafuta mu Kitabu ya Paraklitiki.*

*Kisha tunaimba Kanuni ya Ufufuo ya siku ya Paska na Kanuni ya Wabebaji-Manukato.*

**Kanuni ya Wabebaji Manukato**

**WIMBO YA KWANZA** *Sauti ya mbili*

Ee roho yangu, imba wimbo wa Musa: Bwana ni msaada wangu, ulinzi wangu, ni yeye aliniokoa, ni Mungu wangu na nataka kumutukuza.

Ee Mungu usiyeteseka, uliteswa mwilini, ubavu wako ulichomwa mukuki, ukafungulia dunia damu na maji: Uko Mungu wetu, tunakutukuza wewe.

Natukuza Kusulubiwa kwako, Natukuza Kuzikwa kwako kaburini, naimbia na kuabudu Ufufuo wako, na nakulalamikia, ee Bwana wa wema: Uko Mungu wetu, tunakutukuza wewe.

Ulikunywa nyongo, ewe Bwana ambaye ndani yako Kanisa inapata utamu; kwa ubavu wako ulichomwa mukuki unaleta uzima wetu wa milele: Uko Mungu wetu, tunakutuza wewe.

Ee Mwokozi uliyefufua wafu, ulihesabiwa katika wafu; na ulionja mauti bila mwili wako kuharibika na uvumbi wa kaburi; Uko Mungu wetu, tunakutukuza wewe.

Sayuni ifurahi na mbingu ishangilie kama sisi : Kristu amefufuka, amefufua wafu wenye kuimba sasa : Uko Mungu wetu, tunakutukuza.

Ee Kristu, Yosefu alifunga sanda mwili wako takatifu na akakuweka ndani ya kaburi mupya, ee Mwokozi, wewe mwenye kufufua wafu.

Asubui mapema Wanawake watakatifu wabebaji-manukato walimuona Kristu; wakawaambia Wafwasi: Kweli Kristu alifufuka, muje mumutukuze pamoja na sisi.

Utukufu kwa Baba…

Utatu Mtakatifu kamili, Mungu mumoja wasipo mwanzo na mwisho, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, leta wokovu duniani : Uko Mungu wetu, tunakutukuza wewe.

Sasa na siku zote…

Ee Bikira Mtakatifu kamili, tumboni mwako ulimalizisha laana ya kale na ulichanusha baraka yetu kwa kumuzaa Mwana wako duniani : Eko Mungu wetu, hata kama anachukua mwili wetu.

**WIMBO YA TATU.** *Sauti ya mbili* :

Ee Bwana, roho yangu yenyi kukauka uistawishe izae matunda, wewe mwenye kustawisha mema yote kwa wema wako kubwa.

Ee Yesu,Mwokozi wangu, msalabani ulipanua mikono yako yenyi kutobolewa na

misumari sababu ya kukusanya watu wote wenye kupotea na kuwarudisha kwa kumujua Mungu.

Watu walimuomba Pilato: Utufungulie Baraba muovu, huyu mwenye haki umuinue, umusulubishe Bwana asiye na zambi.

Ee Kristu, wakati ulisulubiwa msalabani inchi ilitetemeka, nuru ilipata giza, wafu wengi walitoka kaburini, wakatukuza uwezo wako, ee Bwana.

Ee Bwana Yesu, aliposimama karibu ya msalaba wako, Mama Kondoo jike akakulalamikia akilia: Ole wangu,wapi anaenda Mwana-Kondoo aliyetolewa sadaka kwa ajili ya wokovu wa wote?

Ninaposujudu mbele ya Msalaba wako na Kaburi yako, natukuza Mateso yako, misumari ya mikono yako na mukuki ilichoma ubavu wako, na nabudu Ufufuo wako takatifu.

Ulipofufuka, ulinyanganya Adui yetu, kwa Ufufuo wako takatifu Adamu na Eva walifunguliwa wote wawili toka minyororo ya mauti.

Ee Kristu, wakati ulifufuka, makomeo na milango ya Hadeze yalipasuka, minyororo ya mauti yalivunjika, yakaogopa kwa uwezo wako, ee Bwana.

Yosefu akuje na asimame katikati yetu aseme: Amefufuka, Mungu niliyebeba mikononi, Yesu Mukombozi aliyefufua Adamu kwa tendo la mapendo yake.

Wale kumi na wawili wafurahi kama sisi, pamoja na wanawake wabebaji-manukato,na Yosefu, na Wafwasi wa Kristu, na wanawake watakatifu waliyomufwata Yesu.

Utukufu kwa Baba…

Pamoja na Baba natukuza Mwana, natukuza tena Roho wa ukweli, nabudu hali moja katika watu tatu mbalimbali wenye asili moja.

Sasa na siku zote…

Mwenye heri! Ee Bikira Mtakatifu, toka shina la Yese ulitokeza kwa ajili yetu katika mwili hii tawi yenyi kuchanuka, ndiye Kristu.

**KATHISMA** *Sauti ya mbili. Ta ano ziton.*

Mwokozi, Wanawake watakatifu walileta manukato kaburini na juhudi, na roho yenyi kufurahishwa na Malaika mwenye kuangaa walikutangaza kama Mungu wa ulimwengu, wakawaambia Wafwasi na furaha : Amefufuka, Bwana aliye Uzima wetu.

Utukufu kwa Baba..Sasa na siku zote...

Kundi ya Wafwasi, ewe Mzazi-Mungu, Mtukufu kuliko wote, lufu imevunjwa kwa lufu, na Hadeze imeshindwa kwa Msalaba wa Mwana wako; alitufufua ku lufu, akatupatia uzima, wa milele; paradizo inapewa mara ingine kwa sisi, sababu ya kufurahiwamo kama zamani; tena tunatukuza na shukrani mapendo na uwezo wa Kristu Mungu wetu.

**KONTAKION** *Sauti ya mbili*

Ee Kristu Mungu wetu, ulipowaamuru Wanawake wabebaji-manukato wafurahi, kwa Ufufuo wako uliondoa machozi ya Eva mama wa kwanza; uliwapa Mitume amri ya kutangaza: Mwokozi ametoka kaburini!

**IKOS**

Ee Mwokozi, walipokuja kwa kaburi yako, Wanawake wabebaji-manukato walikuwa na shaka, waliulizana mumoja kwa mwingine wakisema: Ni nani atakayetuondolea lile jiwe kutoka mulango wa kaburi? Lakini walipotazama, wakaona ya kuwa lile jiwe lilikuwa limekwisha kusukumwa pembeni; walipoogopa kwa kuangaa kwa Malaika, walishikwa na woga na wakawaza kukimbia; lakini kijana mwanaume akawaambia: Amefufuka, huyu munatafuta! Kujeni, tazameni mahali walipoweka mwili wa Yesu, mwende sasa mukawapashe wafwasi wake hii habari : “ Mwokozi ametoka kaburini!

**SINAKSARI**

Leo, Juma ya tatu kisha Paska, tunashangilia sikukuu ya Wanawake watakatifu wabebaji-manukato; tunakumbuka tena Yosefu wa Arimatea, mfwasi wa siri wa Bwana; na tunakumbuka vilevile Nikodemu aliyekuja usiku kumusikiliza Yesu.

Wanawake watakatifu wabebaji-manukato Walimutolea Kristu manukato : kwa kuwakumbuka

Mimi natoa pia wimbo sawa manukato.

Kwa maombezi ya Wanawake watakatifu wabebaji-manukato, ee Kristu Mungu wetu, utuhurumie. Amin.

**EKSAPOSTILARION YA PASKA**

**YA WABEBAJI-MANUKATO** *Sauti ya mbili. Ginekes akutisthite*

Wanawake wabebaji-manukato, sikilizeni habari yenyi kuleta furaha : Nafukuza Hadeze, huyu muzulumu mbaya, naondoa dunia toka chini ya kaburi; kwendeni wepesi kwa marafiki zangu, Wafwasi, kuwapasha sasa habari njema; kwa sababu ni hivi nilitaka viumbe vyangu vyangae na furaha, kwani katika wao zamani mateso iliingia duniani.

**MASIFU.** *Sauti ya mbili*.

Kila mwenye pumuzi na kila Kiumbe, kinakusifu, ee Bwana, kwa sababu kwa Musalaba uliharibu mauti, sababu ya kuonyesha kwa mataifa, ufufuo wako katika wafu, kwa maana ni wewe peke Mpenda-wanadamu.

Wayuda namna gani wakati askari walipochunga Mfalme walimupotesha? Sababu gani jiwe halikuchunge mwamba wa uzima? Ao watupatiye huyu aliyezikwa, ao wamwabudu huyu aliyefufuka, wakisema pamoja na sisi: Utukufu kwa wingi wa rehema Yako, ee Mwokozi wetu, utukufu kwako.

Furahini, mataifa na mushangilie; malaika alikaa juu ya jiwe la Kaburi; huyu akatuletea sisi habari njema, akatwambia: Kristu Mwokozi wa watu, alifufuka katika wafu, na akajaza ulimwengu kwa marasi. Furahini, mataifa na mushangilie.

Malaika alileta salamu kwa Mujaliwa na neema, mbele ya kuchukuwa miimba yako, ee Bwana; tena Malaika alisukuma jiwe la Kaburi yako tukufu, katika ufufuko wako. Malaika wa kwanza pahali pa sikitiko, akapasha habari ya alama ya furaha; Malaika mwengine pahali pa mauti, alitutangazia ya kama Rabi na Muletaji-uzima kwa sisi; kwa hii tunakupazia sauti: Ewe Bwana, Mufazili wa wote, utukufu kwako.

Wanawake walimimia manukato na machozi, juu ya kaburi yako, na vinywa vyao vilijazwa na furaha, wakati waliposema: Bwana amefufuka.

Mataifa na watu, wasifu Kristu, Mungu wetu, aliyevumilia Msalaba sawa alivyotaka kwa ajili yetu, na aliyebaki siku tatu ndani ya Hadeze waabudu, ufufuko wake katika wafu, kwa ajili yake ulimwengu nzima umeangaziwa.

Ulisulubiwa, ulizikwa, ee Kristu, kama ulivyotaka; ulinyanganya mauti, kwa sababu wewe ni Mungu na Rabi, ukitoa kwa dunia uzima wa milele, na rehema kubwa.

Hakika ninyi wavunja-sheria, mulipofunga jiwe, mulitustahilisha kuona ajabu kubwa; walinzi walijua muzuri sana; leo Kristu alitoka Kaburini, na mulisema: Mutasema, Wanafunzi wake walikuja kumuiba wakati tulipolala. Nani anaiba maiti, na tena mutupu? Huyu alifufuka kwa uwezo wake, kwa kuwa Yeye ni Mungu, akiacha sanda ya maziko ndani ya Kaburi. Kujeni Wayuda mwone, sababu gani hakubomoa muhuri, huyu aliyeshinda mauti, na aliyeleta kwa uzao wa watu, uzima usiyo na mwisho, na rehema kubwa.

Utukufu kwa Baba...**EOTHINON** *Sauti ya mbili*

Wabebaji-Manukato, wenzi wa Maria wakaulizana ginsi gani watafanya kwa kufikia ukomo wao; lakini wakaona jiwe limeondoshwa tena Malaika Mtakatifu akaonekana kwao aliyerudisha amani ku roho yao yenye kufazaika: «Kwani, alivyosema, Bwana Yesu amefufuka; muwapashe Wafwasi habari, Mitume wake, ili waende upesi ku Galilaya huko watamuona amefufuka katika wafu, yeye, Bwana na chemchem ya uzima.

Sasa na siku zote...**THEOTOKION**

Mbarikiwa ukupita, ewe Mzazi-Mungu Bikira......**DOKSOLOGIA KUBWA NA KUAGA**

## MU JUMA YA WABEBAJI-MANUKATO MAGARIBI

*Kisha «Bwana nimekuita...» tunaimba wimbo sita; tatu ya siku Kuu na tatu ya Mineon.*
***Wimbo ya Siku Kuu.***

*Kreris askitikon Sauti ya tano*

Na mikono yako iliyotobolewa na misumari msalabani, ulisimamisha laana iliyoingia duniani kwa kula tunda la muti iliyokataziwa; wakati uliwekwa kaburini, kwa uwezo wako wa umungu, ulifufua wale walikufa tangu zamani; tunatukuza ubwana wako na tunaimba tukisema : Paska takatifu,

Yesu mwenyezi, nuru ya Baba na Uzima wetu! Na mbinguni Malaika wanafurahi pamoja na wanadamu wenye kukuimbia wimbo wa ushindi, ewe Neno wa Mungu mwenyi kuleta duniani neema ya wokovu.

Wanawake wabebaji-manukato walilia na kusema: Uzima amelala katikati ya wafu? Eko tena chini ya udongo huyu aliye Jua letu la alfajiri? Kujeni, twendeni wepesi tuone kaburi takatifu ya Kristu. Na huko, walipomuona Malaika mumoja mwenye kuangaa, wakawa na shaka, hawakujua nini watafanya, lakini Malaika alipogeuza mateso yao kuwa furaha, akawaambia: Amefufuka, Kristu aliye Chemchem ya uzima; enyi marafiki za Mungu, musiogope: Bwana anatawala na analeta duniani neema ya wokovu.

Mbele ya alfajiri Wanawake watakatifu walimutafuta Jua la mbele ya jua huyu walizania kuwa ndani ya kaburi, lakini Malaika mumoja mwenye kuangaa aliwatokea na akawaambia: Nuru amesimama, amewangazia wale waliolala katika giza ya mauti; basi wapasheni habari Wafwasi wenye kuangaziwa ya kwamba maombolezo yanakuwa furaha; pigeni mikono, shangilieni na furaha rohoni mwenu sababu ya hii Paska ya furaha yenyi kutuokoa: Kristu alifufuka, alileta duniani neema ya wokovu.

***Wimbo ya Mineon***

Utukufu kwa Baba…Sasa na siku zote… *Sauti ya kwanza*

Malaika mwenyi kuangaa alisema: Enyi wanawake wabebaji-manukato, nini munakuja kufanya kaburini? Sababu gani munamutafuta katika wafu Yeye aliye hai? Muwe na moyo: Bwana amefufuka!

**APOSTIKHA** *Sauti ya mbili*

Kujeni tumwabudu huyu aliyezaliwa kwa Baba mbele ya milele, Mungu neno aliyechukuwa mwili kwa Bikira Maria; kwa sababu alivumilia Msalaba, alijitoa ku maziko kama alivyotaka, na alifufuka katika wafu, aliniokoa mimi mpotevu.

Mimi mwana mupotevu, nimekosa mbele yako, ee Mwokozi: Ee Baba pokea toba yangu na unihurumie, ewe Mungu wangu.

Walipokataa furaha za hapa chini, Mashahidi. Watakatifu wakapokea hazina za mbinguni, wakawa Wenzao wa malaika: Kwa maombezi yao, ee Bwana, utuhurumie na utuokoe.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya kwanza.*

Wanawake walikuja na woga ku kaburi yako sababu ya kupakaa mwili wako manukato, lakini wasipoipata wakaulizana mumoja kwa mwingine kwa kutokujuwa Ufufuo, Malaika mumoja aliwatokea na kuwaambia: Kristu amefufuka, ametupatia neema ya wokovu.

*Apolitikion ya tatu, sawa mu posho mangaribi ya hii Siku Kuu.*

# MU KAZI MOJA ASUBUI YA JUMA YA WABEBAJI-MANUKATO

*Kisha Eksapsalmos na Apolitikia tunaimba*

**KATHISMA YA KWANZA** *Sauti ya mbili*

Wewe usiyekataza jiwe lisifungwe kaburini, katika Ufufuo wako, ukatupatia jiwe la imani, ee Bwana, ututukufu kwako.

Zambi zangu zimetokea nyingi juu yangu kama mawimbi ya bahari na kama mashua baharini na kubwa na mawimbi ya uovu; ee Bwana, uniongoze ku bandari ya amani na uniokoe ukinirudisha tena kwako.

Utukufu kwa Baba...

Ewe Bwana mwenye kuvika mbingu na mawingu, umekuwa duniani humo vazi la Mashahidi: Walivumilia mateso ya makafiri na wakaharibu uwongo wa miungu ya uwongo; kwa maombezi yao, utuopoe kwa adui msiyeonekana na utuokoe, ee Mungu Mwokozi.

Sasa na siku zote...**THEOTOKION**

Chemchem ya rehema, ewe Mzazi-Mungu, utustahilishe na huruma yako; tazama watu wenye zambi, onyesha uwezo wako wa siku zote; tunakutumainia wewe na tunakulalamikia: Salamu! Kama alivyofanya zamani Malaika mkuu Gabrieli.

**KATHISMA YA MBILI** *Sauti ya mbili. Ta ano ziton.*

Mwokozi, Wanawake watakatifu walileta manukato kaburini na juhudi, na roho yenyi kufurahishwa na Malaika mwenye kuangaa walikutangaza kama Mungu wa ulimwengu, wakawaambia Wafwasi na furaha: Amefufuka, Bwana aliye Uzima wetu.

Utukufu kwa Baba…Sasa na siku zote…*(mara ya mbili)*

*Kisha tunasoma: Tukiona ufufuo wa Kristu...Zaburi 50 (51). Kanuni ya Siku Kuu na Mineon, Kontakion na Eksapostilarion ya Siku Kuu.*

**MASIFU** *Sauti ya mbili.*

Kila mwenye pumuzi na kila Kiumbe, kila kusifu, ee Bwana, kwa sababu kwa Musalaba uliharibu mauti, kusudi ya kuonyesha kwa mataifa, ufufuo wako katika wafu, kwa maana ni wewe peke Mpenda-wanadamu.

Ninapoona matendo yangu ya mazimu, nakimbilia ku rehema yako kwa mfano wa Mtoza-kodi, kama mwana mpotevu na kahaba, na nasujudu mbele yako: Mbele ya kunihukumu, ee Mungu wangu, unisamehe na unihurumie kwa wema wako.

Mulipoteswa kwa ajili ya Kristu mpaka kufa, enyi Washuhuda Washindaji wa Bwana, mukatoa mbinguni roho yenu mikononi mwa MUngu, na masalio yenu yanapelekwa duniani kote; makohani na Wafalme wanasujudu mbele hii, na mataifa yote yanapaza sauti kwa furaha: Ni ya samani ku macho ya Bwana; lufu ya marafiki zake.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya kwanza.*

Maria Magdalena na Maria mwingine walikwenda kaburini kumutafuta Bwana, wakamuona Malaika mumoja mwenyi kuangaa kama umeme amekaa pembeni ya jiwe na akawaambia: Sababu gani munamutafuta katika wafu Yeye aliye hai? Hayuko hapa, amefufuka kama alivyosema, anawatangulia kwenda Galilea. Tunaposujudu mbele yake, tunaimba: Ee Mfufuliwa katika wafu, Bwana, utukufu kwako.

**APOSTIKHA** *Sauti ya sita. Triimeros anestis.*

Enyi mataifa, imbeni nyimbo sababu ya kumutukuza Kristu na furaha: Paska isiyofanana na ingine, Mfufuliwa toka kaburi amesimama kwa ajili yetu, Kristu aliye chemchem ya uzima, Mkombozi wa vyumbe vyote.

Shairi: Unapenda inchi yako, ee Bwana, unarudisha wafungwa wa Yakobo.

Ulipowaambia Wanawake wabebaji-manukato: Furahini, uligeuza mateso ya Eva kuwa furaha, unawatuma Mitume wako kutangaza Ufufuo wako toka kaburi siku ya tatu.

Shairi: Mapendo na Ukweli yanakutana, haki na amani yanakumbatiana.

Paska tukufu na takatifu, Kristu aliangaa juu yetu; kujeni, waaminifu wote, tuangazishe roho zetu na nuru, maana tazama mchana inaonekana na nuru yake yote : shangilieni na kufurahiwa.

Utukufu kwa Baba… Sasa na siku…*Sauti ya mbili*

Wanawake watakatifu walimwanga manukato na machozi yao juu ya kaburi yako, kinywa chao kilijazwa na furaha kwa kutangaza wakisema: Bwana amefufuka!

## MU KAZI MOJA MANGARIBI KISHA JUMA YA WABEBAJI-MANUKATO

*Kisha «Bwana nimekuita...» tunaimba wimbo sita; tatu ya siku Kuu na tatu ya Mineon.*

***Wimbo ya Siku Kuu.***

*Sauti ya mbili. Ote ek tu ksilu.*

Ee Kristu, wakati Wanawake wabebaji-manukato walikutafuta asubui mapema Wewe uliye Uzima wa ulimwengu, walibeba manukato ya harufu nzuri sababu ya kukupakaa; na walipolia na mapendo wakasikia toka kaburi kijana mumoja akawaambia: Musilie, furahini, kwa sababu mumepewa wokovu, muwaambie wote ya kwamba Bwana amefufuka.

Mtukufu Yosefu, katika wewe tunaona gari la Wakheruvi, maana ulibeba Kristu Mfalme wetu juu ya mabega yako wakati ulimushusha msalabani;na tunataja heri mikono yako iliyobeba mpaka kwa kaburi Jua letu aliye Neno wa Mungu; na kwa furaha tunatukuza makumbusho yako takatifu.

Sikukuu ya Wanawake watakatifu wabebaji-manukato na ya Mtukufu Yosefu inaonekana kwetu kuwa Paradizo ingine yenyi kuwa na chemchem ya uzima: maana inamwangia dunia neema mingi, kwa Ufufuo inaleta maji mengi; makutano ya waaminifu yanashangilia na kupaza sauti: Utukufu kwa huyu mwenye kuleta duniani zawadi ya Ufufuo wake takatifu.

***Wimbo tatu ya Mineon***

Utukufu kwa Baba… Sasa na siku…*Sauti ya mbili*

Ee Kristu, Wanawake wabebaji-manukato walienda na haraka asubui mapema kaburini kwako kukutafuta sababu ya kupakaa mwili wako manukato; lakini kisha kusikia maneno Malaika aliwaambia, wakaenda wepesi kwa Mitume kuwapasha habari ya furaha wakisema: Mfalme wa wokovu wetu amefufuka; Mshindi wa mauti analeta duniani uzima wa milele na neema ya wokovu.

## APOSTIKHA *Sauti ya mbili*

Kristu Mwokozi wetu, alizimisha maandiko mabaya ya ndani zetu, kwa kuipigilia Msalabani, na aliharibu nguvu ya mauti. Tuabudu Ufufuo wake wa siku tatu.

Ee Kristu Mwokozi wangu, nafananisha sauti ya mtoza-kodi: Unirehemu na unihurumie, ewe Mungu wangu.

Kwa imani mumepata utukufu kubwa: apana paka mulishinda adui mulipoteswa, lakini munafukuza tena mashetani na munaponyesha ugonjwa wowote, enyi Waganga wa roho na wa miili, ee Mashahidi Watakatifu, ombeni kwa Mungu ili ahurumie roho zetu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya mbili.*

Sababu gani munachanganya machozi yenu na manukato munabeba? Jiwe limesukumwa, kaburi ni wazi; tazameni namna gani uzima imeshinda mauti, tazameni jiwe limekuwa ushuhuda wa nuru, tazameni usingizi gani walilala walinzi makafiri; ile ilikuwa zamani chini ya utumwa wa mauti imeokolewa kwa mwili wa Mungu wetu, Hadeze inalia na uchungu; lakini kwendeni upesi mukawaambie Mitume ya kwamba: Kristu mshindi wa mauti na Mzaliwa wa kwanza katika wafu anawatangulia kwenda Galilea.

**Apolitikia tatu ya Siku Kuu**

# MU KAZI MBILI ASUBUI YA JUMA YA WABEBAJI MANUKATO

*Kisha Eksapsalmos na Apolitikia tunaimba:*

**KATHISMA YA KWANZA.** *Sauti ya mbili*

Kundi ya Wafwasi, ewe Mzazi-Mungu, Mtukufu kuliko wote, lufu imevunjwa kwa lufu, na Hadeze imeshindwa kwa Msalaba wa mwana wako; alitufufua ku lufu, akatupatia uzima, wa milele; paradizo inapewa mara ingine kwa sisi, sababu ya kufurahiwamo kama zamani; tena tunatukuza na shukrani mapendo na uwezo wa Kristu Mungu wetu.

Mimi ni muti kavu, ee Bwana, sitoe tunda la toba, naogopa shoka na moto usiyozimika; ndiyo maana nakuomba, mbele ya mwisho, uniokoe, ee Bwana, ukinirudisha tena kwako.

Uliwaangaza Mashahidi wako kupita zahabu, na ukawatukuza Watakatifu wako katika wema wako; kwa maombezi yao, ee Kristu Mungu wetu. Mpenda-wanadamu, leta amani ku uzima wetu, pokea ombi letu kama ubani, wewe mwenye kupumzika kati ya Watakatifu.

Ewe Mzazi-Mungu, ndiwe msaada wa wenye kuteswa, mlinzi wa Wamaskini, matumaini ya wale wenye kutotumainia, mganga wa maginjwa yasiyoweza kupona, ee Bikira mstahili kamili wa nyimbo zetu, utuombee kwa Bwana.

**KATHISMA YA MBILI** *Sauti ya mbili*

Wanawake Wabebaji-manukato walipokuja asubui mapema na walipokuta kaburi ya Bwana ni wazi, wakaenda wepesi kuwaambia Mitume ya kwamba: Mwenyezi ameharibu nguvu ya mauti, na amewaokoa wale wote walikuwa wafungwa wa Hadeze; tangazeni na matumaini ya kwamba kweli amefufuka, Kristo Mungu wetu mwenye kutupatia neema ya wokovu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*(mara mbili).*

*Kisha tunasoma: Tukiona ufufuo wa Kristu...Zaburi 50 (51). Kanuni ya Siku Kuu na Mineon, Kontakion na Eksapostilarion ya Siku Kuu.*

## MASIFU *Sauti ya mbili*

Wayuda walisema namna gani wakati askari walipochunga Mfalme walimupotesha? Sababu gani jiwe halikuchunge mwamba wa uzima? Ao watupatiye huyu aliyezikwa, ao wamwabudu huyu aliyefufuka, wakisema pamoja na sisi: Utukufu kwa wingi wa rehema Yako, ee Mwokozi wetu, utukufu kwako.

Ee Bwana, usitazame zambi zangu, wewe uliyezaliwa kwa Bikira, lakini takasa moyo wangu uifanye kuwa hekalu la Roho Mtakatifu; usinitupe mbali ya uso wako, wewe mwenye wokovu mingi.

Mashahidi Watakatifu walipochukua Msalaba wa Kristu kama ukumbusho wa ushindi, waliharibu nguvu ya Shetani, na walipotukuzwa mbinguni, wakawa walinzi wetu wenye kutuombea daima.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya mbili*.

Asubui mapema, Wanawake wabebaji-manukato walipokuja ku kaburi ya Bwana na wakati hawakupata ile walitafuta, wakasikitika sababu ya hii mabadiliko na mbele ya jiwe lilisukumwa wakaambiana mumoja kwa mwingine: Wapi mlango wa kaburi? Wapi walinzi Pilato alituma? Lakini sikitiko yao ikaondolewa wakati walimuona Malaika mumoja mwenye kuangaa aliyewauliza akisema: Sababu gani munamutafuta na machozi huyu aliye hai na mwenyi kuwapa wanadamu uzima? Amefufuka katika wafu, Kristu Mungu wetu mwenyezi mwenyi kutupatia wote uzima wa milele, nuru na neema ya wokovu.

## APOSTIKHA *Sauti ya mbili. Ote ek tu ksilu.*

Nuru ya Jua tatu inangaa leo duniani, inafukuza giza ya mateso; leo Ufufuo wa Kristu inangaa kwa sababu ni ulinzi wa waaminifu; Mitume wanashangilia na furaha; Mtukufu Yosefu anashangilia pamoja nao; makumbusho ya nuru ya Wanawake watakatifu wabebaji-manukato inavika taji ya maua wale wenye kuimbia na kutukuza Ufufuo takatifu.

Shairi: Unapenda inchi yako, ee Bwana, unarudisha wafungwa wa Yakobo.

Ee Yosefu, ulibeba juu ya mabega yako Mwana mwenye kuketi kuume kwa Baba mbinguni; unapakaa marasi Manukato yetu isiyokwisha; unaweka kaburini Ufufuo wa dunia; unamufunika jiwe huyu mwenyi kujifunika nuru kama nguo; na kwa nyimbo zetu tunatukuza Mateso yake ya nuru na Ufufuo wake takatifu.

Shairi: Mapendo na Ukweli yanakutana, haki na Amani yanakumbatiana.

Ee Yosefu, Malaika walitetemeka wakati walikuona unamuzika Kristu; dunia inakutanga kuwa mwenye heri, na sisi waaminifu tunakutukuza, tunajaa na bidii juu ya Ufufuo takatifu; tunapokuimbia pamoja na Wanawake wabebaji manukato, tunapaza sauti na kusema: Utuombee pamoja nao sababu ya kutuokoa toka hatari yote.

Utukufu kwa Baba… Sasa… *Sauti ya kwanza*

Wanawake walikuja na woga ku kaburi yako sababu ya kupakaa mwili wako manukato, lakini wasipoipata wakaulizana mumoja kwa mwingine kwa kutokujuwa Ufufuo, Malaika mumoja aliwatokea na kuwaambia: Kristu amefufuka, ametupatia neema ya wokovu.

## MU KAZI MBILI MANGARIBI YA JUMA YA WABEBAJI-MANUKATO

*Kisha «Bwana nimekuita...» tunaimba wimbo sita; tatu ya siku Kuu na tatu ya Mineon.*

***Wimbo ya Siku Kuu.***

*Sauti ya mbili. Ote ek tu ksilu.*

Wanawake wabebaji-manukato walifurahi kwa kusikia Malaika ambaye maneno yake yaliwapa imani kwa Ufufuo wa huyu alihesabiwa katika wafu kwa ajiliyetu: walisadiki japo walienda kaburini na nyimbo zao za kilio na japo jiwe lililosukumwa liliwasangaza.

Wanawake wabebaji-manukato wa Kristu walifurahi sana wakati walionekana mbele ya Wafwasi wa Bwana kuwapasha habari ya Malaika Mtakatifu ambaye manguo yake mweupe yaliwaopesha,wakasema: Hadeze imeshimdwa kwa Ufufuo wa huyu alikufa kwa ajili yetu, Kristu Mfalme wetu.

Kisha kulia kwao, sasa Wanawake wabebaji-manukato wa Kristu wanapasha habari ya furaha kwa washuhuda wa neema ya Mungu, wanawatangazia Ufufuo wa Neno takatifu, furaha yenye kutoka kaburini na furaha nzuri ilimaliza kulia kwao wakati walisikia: Salamu.

***Wimbo tatu ya Mineon***

Utukufu kwa Baba… Sasa na siku zote… *Sauti ya sita*

Wanawake Wabebaji-manukato walipofika kaburini na walipoona kaburi wazi na hawakupata mwili wako takatifu japo kuja kwao wepesi, wakalia na kusema: Nani alituiba matumaini yetu? Nani alibeba mwili tupu wenyi kupakaa manukato ambaye kwa Mama yake alikuwa kitulizo? Ole wetu! Namna gani aliuawa huyu mwenyi kuwapa watu uzima? Namna gani Mshindi wa Hadeze aliwekwa kaburini? Lakini kwa uwezo wako, ee Mwokozi, fufuka siku ya tatu kama ulivyosema sababu ya kuleta neema ya wokovu rohoni mwetu.

**APOSTIKHA** *Sauti ya mbili*

Uniokoe, ee Kristu Mwokozi, kwa uwezo wa Msalaba wako, wewe uliyemuokoa Petro pa mawimbi, na unihurumie,ee Mungu wangu.

Tuimbeni Ufufuo wa Kristu pamoja na malaika wakuu; kwa maana huyu ni Mkombozi, na Mwokozi wa roho zetu; na maogopesho ya utukufu, na nguvu ya uwezo, eko nakuja tena, kuhukumu dunia aliyeumba.

Washahidi Watakatifu waliposhika Msalaba wa Kristu kama ushindi, wakavunja nguvu ya shetani, na walipotukuzwa mbinguni, wakawa walinzi wetu wenye kutuombea daima.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya sita.*

Yosefu aliomba mwili wako takatifu, akauweka ndani ya kaburi yake mupya: ulitoka kaburini kama katika nyumba ya arusi, ee Kristu uliyeharibu ufalme wa mauti sababu ya kuwafungulia wanadamu milango ya Paradizo, Bwana, utukufu kwako.

# MU KAZI TATU ASUBUI YA JUMA YA WABEBAJI-MANUKATO

*Kisha Eksapsalmos na Apolitikia tunaimba:*

**KATHISMA YA KWANZA.** *Sauti ya mbili*

Ulitimiza wokovu duniani ee Kristu Mungu wetu, ulipanua mikono yako takatifu Msalabani kwa kuwakusanya mataifa yote yenye kukuimbia: Ee Bwana, utukufu kwako.

Ee Bwana, ulipofufuka kaburini, ulivunja minyororo ya Hadeze na ulipasua hati ya hukumu ilituhukumu ku mauti; ulituokoa sisi wote ku mutego wa adui na ulionekana katikati ya Mitume wako ulituma duniani kote kuhubiri na katika wao ulileta amani deniani, ewe peke yako Bwana mwenye kutujaza na rehema yako.

Heri ni udongo wenye kunyunyiziwa na damu yenu, enyi Washindani wa Bwana, na takatifu ni makao yenye kufunika miili yenu, kwani katika uwanja mulimushinda adui wakati mulimutangaza Kristu na uhodari: Kwa maombezi yenu mutupokelee ku wema wake neema ya wokovu wa roho zetu.

**STAVROTHEOTOKION**

Bikira aliyekuzaa akasimama chini ya Msalaba, na hakuweza kuvumilia akikuona umeteswa bila haki, akalia na akapaza sauti akasema: Ee Mwanangu, hali isiyo na mateso, namna gani umeteswa? Naimba na natyukuza wema wako mkuu.

**KATHISMA YA MBILI** *Sauti ya mbili. Efsplaknias iparkusa.*

Mwokozi, Wanawake watakatifu wabebaji-manukato walikuja kwa haraka ku kaburi yako sababu ya kukupakaa manukato wewe Bwana sawa mufu, lakini Malaika mumoja akawatangazia furaha kubwa akasema: Bwana amefufuka! kwendeni mukawaambie Mitume ya kwamba kweli Amefufuka kaburini.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*(mara mbili).*

*Kisha tunasoma: Tukiona ufufuo wa Kristu...Zaburi 50 (51). Kanuni ya Siku Kuu na Mineon, Kontakion na Eksapostilarion ya Siku Kuu.*

**MASIFU** *Sauti ya mbili*

Kwa kutaka kwako ulipenda kuwa na umaskini wa ubinadamu wetu, ee Kristu Mungu wetu, ulikuja duniani na ukajifanya mtu kwa Bikira na ukateswa hata kufa Msalabani kwa kutukomboa ku utumwa wa adui. Ee Bwana, utukufu kwako.*(mara mbili)*

Furahini, mataifa na mushangilie; malaika alikaa juu ya jiwe la Kaburi; huyu akatuletea sisi habari njema, akatwambia: Kristu Mwokozi wa watu, alifufuka katika wafu, na akajaza ulimwengu kwa marasi. Furahini, mataifa na mushangilie.

Ee Kristu, Mashahidi wengi wanakuomba: Katika wema wako kwa wanadamu, utuhurumie.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya kwanza.*

Wanawake walikuja na woga ku kaburi yako sababu ya kupakaa mwili wako manukato, lakini wasipoipata wakaulizana mumoja kwa mwingine kwa kutokujuwa Ufufuo, Malaika mumoja aliwatokea na kuwaambia: Kristu amefufuka, ametupatia neema ya wokovu.

**APOSTIKHA** *Sauti ya mbili. Ote ek tu ksilu*

Wanawake wabebaji manukato walipaza sauti na kusema: Eko katika wafu, Mukombozi wetu? Jua letu Mtukufu analala tena chini ya udongo ao amesimama kama alivyosema? Wakati walikuwa wakilia, toka kaburi Malaika mumoja akawaletea habari ya furaha ya umungu akisema: Kristu amefufuka, kwendeni wepesi kuwapasha wote habari ya kwamba amesimama kaburini kama Mungu.

Shairi: Unapenda inchi yako, ee Bwana, unarudisha wafungwa wa Yakobo.

Walipotayarisha manukato yao siku ya kwanza kisha Sabato Wanawake wabebaji-manukato walikuenda asubui mapema ku kaburi yako sababu ya kukupakaa mwili wako takatifu manukato, ee Kristu; walipofundishwa Ufufuo wako, wakaenda kwa haraka kuwapasha marafiki zako habari; ukakutana nao inje ya kaburi na kwa wema wako ukawaambia: Salamu.

Shairi: Mapendo na Ukweli yanakutana, haki na Amani yanakumbatiana.

Walipotaka kutimiza duniani maziko ya Mungu aliye juu, Wanawake wabebaji manukato wakaenda haraka sababu ya kupakaa mwili wake manukato ya bei mingi; lakini walipoona kijana mumoja amekaa pembeni ya kaburi, wakaogopa kwa kwangaa kwake; lakini wakati walisikia ya kwamba Neno ametoka kaburini, wakawapasha Mitume habari ya Ufufuo wake siku ya tatu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya tano.*

Wewe mwenye kuvaa nuru kama nguo, Yosefu na Nikodemu walikushusha pa mti wa Msalaba na mbele ya mwili wako, bila kaburi, wakaomboleza kwa uchungu na wakasema wakilia: Ole, ee Yesu mpole kamili! Jua lililokuona Msalabani limepata giza na inchi imetikisika kwa woga; pazia la Hekalu likapasuka na nimekuona ukivumilia kwa ajili yangu kifo cha kutaka. Namna gani nitakuzika, ee Mungu wangu? Sanda gani nitakufunika? Na mikono gani nitagusa Mwili wako Takatifu? Wimbo gani nitaimbia kifo chako? Ewe mwenye rehema kamili, natukuza mateso yako! Naimbia maziko yako na Ufufuo wako nikilalamika: Ee Bwana, utukufu kwako!

## MU KAZI TATU MANGARIBI YA JUMA YA WABEBAJIMANUKATO

*Kisha «Bwana nimekuita...» tunaimba wimbo sita; tatu ya siku Kuu na tatu ya Mineon.*

***Wimbo ya Siku Kuu.***

*Sauti ya mbili. Ote ek tu ksilu.*

Wanawake watakatifu wabebaji-manukato waliposikia maneno ya furaha kwa Malaika aliyekaa juu ya kaburi ya Neno wa Mungu wakaenda mbiyo, walipofurahi, wakawa wenye kufundisha furaha, wakawapasha Wafwasi habari ya Ufufuo wa huyu aliyejifanya mutu sababu ya kutuokoa.

Asubui mapema wanawake wabebaji-manukato walikuja ku kaburi kumupakaa manukato Kristu chemchem ya uzima aliye Mshindi wa Hadeze, lakini Malaika mumoja wa Mungu akawatokea na kuwaambia: Sababu gani munamutafuta katika wafu huyu aliye hai na mwenye kutupatia uzima? Kwendeni mukatangaze Ufufuo wake.

Ee mwenye heri Yosefu, Neno mwenye kukaa juu ya mabega ya Wakheruvi, juu ya mabega yako,ulimubeba wewe mwenyewe kama gari ingine; ya kwanza alijifanya mutu, tazama sasa anauawa huyu mwenyi kuwapa wanadamu uzima; lakini ulipomwona amefufuka, ulifurahi pamoja na Wanawake wabebaji-manukato kisha nyimbo za kilio mulimusindikiza nazo.

***Wimbo tatu ya Mineon.***

Utukufu kwa Baba… Sasa na siku… *Sauti ya kwanza*

Maria Magdalena na Maria mwingine walikwenda kaburini kumutafuta Bwana, wakamuona Malaika mumoja mwenyi kuangaa kama umeme amekaa pembeni ya jiwe na akawaambia: Sababu gani munamutafuta katika wafu Yeye aliye hai? Hayuko hapa, amefufuka kama alivyosema, anawatangulia kwenda Galilea. Tunaposujudu mbele yake, tunaimba: Ee Mfufuliwa katika wafu, Bwana, utukufu kwako.

### APOSTIKHA *Sauti ya mbili*

Ufufuo wako, ee Kristu Mwokozi, uliangaza ulimwengu nzima, na uliita tena kiumbe chako; Bwana mwenyezi, utukufu kwako.

Shairi: Habari yao ilisikilika duniani kote, neno lao mpaka ku mwisho wa dunia.

Ee Mwokozi, ulitukuza ulimwengu kote jina la Mitume wakuu: Walifunza mbinguni siri isiyokadirika, wakawa chemchem ya kuponyesha kwa ajili ya watu, paka kivuli yao iliponyesha

wagonjwa; wa kwanza akafanya miujiza, yeye aliyekuwa mvuvi; wa pili, aliyechaguliwa kati ya Wayuda, akasiri na neema Kanuni za Mungu; kwa maombezi yao, ewe Mungu wa mapendo, unipe neema ya wokovu.

Shairi: Bwana ni wa ajabu katikati ya Watakatifu, yeye Mungu wa Israeli.

Kwa imani mulipata utukufu kubwa: Apana paka mulishinda adui mulipoteswa, lakini tena mulifukuza mashateni, na munaponyesha magonjwa yote, enyi waganga wa roho na wa miili; enyi Mashahidi Watakatifu, ombeni kwa Mungu ili ahurumie roho zetu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya mbili.*

Wanawake walimimia manukato na machozi juu ya Kaburi yako, na vinywa vyao vilijazwa na furaha, wakati waliposema: Bwana amefufuka.

**Apolitikia ya Siku Kuu tatu**

# MU KAZI INE ASUBUI YA JUMA YA WABEBAJI MANUKATO

*Kisha Eksapsalmos na Apolitikia tunaimba:*

**KATHISMA YA KWANZA.** *Sauti ya mbili*

Asubui mapema, wanawake wabebaji-manukato walikuja kwa siri ku kaburi yako sababu ya kukupakaa manukato, wakaogopa majivuno ya Wayuda na waaskari aliyolinda kaburi; hali yao ya kike ilishinda kiume kwa sababu mapendo inapata neema kwa Mungu; ndio maana walipaza sauti na kusema: Ee Bwana, utulinde ne kutokoa kwa mapendo ya jina lako.

Uliwapa Wavuvi hekima mingi kuliko Wasemaji na ukawatuma duniani kote kama Watangazaji; kwa sababu ya mapendo yako isiyokadirika, ee Kristu Mungu wetu, kwa tegemeo lao uipatie Eklezya yako nguvu, tuma baraka yako kwa waamini wako, ewe peke yako Mpenda-wanadamu na Bwana mwenyi hurumu.

Enyi Mitume, Manabii na Mashahidi, Watakatifu wakuu na Wenyi haki wote, ninyi muliyoshindana vema na kukesha kwa kulinda imani, kwa waminifu wenu kwa Mwokozi mtupokelee sisi kwa wema wake neema ya wokovu wa roho zetu.

**THEOTOKION**

Kwa ajili yako, ee Maria Mzazi-Mungu na Bikira daima, tuliweza kushariki ku hali ya Mungu; lakini kwa ajili yetu umemzaa Mungu aliyechukua mwili wetu; na tena, kama alivyo mwenye haki, sisi wote tunakutukuza na ibada.

**KATHISMA YA MBILI.** *Sauti ya mbili. Ta ano ziton.*

Ee Mwokozi, wanawake watakatifu walipotayarisha manukato yao wakaenda haraka kukupakaa manukato, ewe Mungu mwema; ndani ya kaburi Malaika mumoja akawaambia : " Amefufuka, Bwana chemchem ya uzima ameshinda Hadeze na mauti!'

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*(mara mbili).*

*Kisha tunasoma: Tukiona ufufuo wa Kristu...Zaburi 50 (51). Kanuni ya Siku Kuu na Mineon, Kontakion na Eksapostilarion ya Siku Kuu.*

**MASIFU** *Sauti ya mbili*

Malaika alileta salamu kwa Mujaliwa neema, mbele ya kuchukuwa miimba yako, ee Bwana; tena Malaika alisukuma jiwe la Kaburi yako tukufu, katika ufufuko wako. Malaika wa kwanza pahali pa sikitiko, akapasha habari ya alama ya furaha; Malaika mwengine pahali pa mauti, alitutangazia ya kama Rabi na Muletaji-uzima kwa sisi; kwa hii tunakupazia sauti: Ewe Bwana, Mufazili wa wote, utukufu kwako. (*mara mbili).*

Tunaposhambuliwa ngambo yote bila haki, tunakimbilia kwako, ewe Mungu wa ukweli, tunakutolea mlio wa Wafuasi wako tukisema: Utuokoe, ee Bwana, tunakufa na tunakuomba, onyesha

kwa maadui zetu ya kama unalinda watu wako na unawaokoa hatarini, kwa maombi ya Mitume wako usamehe makosa yetu mengi katika wema wako kubwa: Ee Rabi na Bwana, utukufu kwako.

Enyi Mashahidi Washindaji masalio yenu yanaheshimiwa katika mji wote, mu inchi yote, kwani mulishindana na ukarimu na mulipokea taji mbinguni, ninyi ni utukufu wa makohani na wa Wafalme tena mapambo ya ma Eklezya takatifu ya Mungu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya mbili.*

Asubui mapema, Wanawake wabebaji-manukato walipokuja ku kaburi ya Bwana na wakati hawakupata ile walitafuta, wakasikitika sababu ya hii mabadiliko na mbele ya jiwe lilisukumwa wakaambiana mumoja kwa mwingine: Wapi mlango wa kaburi? Wapi walinzi Pilato alituma?" Lakini sikitiko yao ikaondolewa wakati walimuona Malaika mumoja mwenye kuangaa aliyewauliza akisema: Sababu gani munamutafuta na machozi huyu aliye hai na mwenyi kuwapa wanadamu uzima? Amefufuka katika wafu, Kristu Mungu wetu mwenyezi mwenyi kutupatia wote uzima wa milele, nuru na neema ya wokovu.

**APOSTIKHA** *Sauti ya mbili. Ote ek tu ksilu.*

Wakati ulifufuka kama Mungu, uliwaamuru Wanawake wabebaji-manukato wafurahi, ee Neno, na uliwaambia: Sijapanda bado kwa Baba yangu, ndio maana musinishike, lakini kwendeni mukawaambie marafiki zangu ya kwamba; Tazama, ninawatangulia kwenda Galilea. Kisha mambo hayo, ulionekana katikati yao na kwa pumzi yako, ee Kristu Mwokozi, uliwapa Roho Mtakatifu.

Shairi: Unapenda inchi yako, ee Bwana, unarudisha wafungwa wa Yakobo.

Wafwasi hawakusadiki maneno ya Wanawake waliotangaza Ufufuo wa Kristo, wakaenda wepesi kuona kaburi: sanda na utepe zilikuwa mule ndani, lakini hawakumuona Huyu walitafuta. Basi walipoona Ufufuo wakawa washuhuda duniani na wakaitangaza kwa mataifa yote.

Shairi: Mapendo na Ukweli yanakutana,haki na amani yanakumbatiana.

Tuliona Nuru isiyokaribika aliyetoka kaburini mwenyi kuangaa na uzuri, Kristu Bwana wetu; Hadeze imefungwa, Shetani amevunjwa, mipaka ya dunia inafurahi, viumbe vinashangilia; Kanisa inashangilia kwa kutukuza makumbusho ya Wanawake wabebaji-manukato na ya Mtukufu Yosefu.

Utukufu kwa Baba… Sasa… *Sauti ya mbili*

Sababu gani munachanga machozi yenu na manukato munabeba? Jiwe limesukumwa, kaburi ni wazi; oneni namna gani uzima inashinda mauti, oneni jiwe ni ushuhuda tazameni usingizi gani walinzi walilala; ile zamani ilikuwa chini ya utumwa wa mauti imeokolewa kwa mwili wa Mungu wetu, Hadeze inalia kwa uchungu; lakini kwendeni na furaha kwa Mitume mukawaambie ya kwamba: Kristu mshindi wa mauti na mzaliwa wa kwanza katika wafu anawatangulia kwenda Galilea.

# MU KAZI INE MANGARIBI YA JUMA YA WABEBAJI-MANUKATO

*Kisha «Bwana nimekuita...» tunaimba wimbo sita; tatu ya siku Kuu na tatu ya Mineon.*
***Wimbo ya Siku Kuu.***

*Sauti ya munane. O tu paradoksu thavmatos.*

Wanawake wabebaji manukato, mulifwata njia ya Kristu aliyeonekana, mulimusindikiza na kumutumikia na bidii ya moyo wenu; hamukumwacha ndani ya mauti, lakini mulipomuonea huruma, mulitayarisha manukato mukaichanga na machozi yenu; ndio maana tunatukuza makumbusho yenu takatifu.

Wanawake watakatifu walipotaka kumuona Uzima aliyelala kaburini walikuja asubui mapema, lakini Malaika akawaambia: Kama alivyosema, Kristu amefufuka. Kwendeni wepesi mukawapashe Wafwasi wake habari, rafiki zake, ondoeni sikitiko mioyoni mwenu, geuzeni machozi yenu kuwa furaha isiyokadirika.

Enyi Wanawake watakatifu wabebaji-manukato, leo sisi waaminifu tunashangilia kwa ajili yenu, tunatukuza Bwana mwema kamili aliyewatukuza ninyi; mumuombe daima ili tusharikie utukufu wa milele, kwa nuru ya Watakatifu wake; maana wakati wote muko na heri ya kumwambie.
***Wimbo tatu ya Mineon.***

Utukufu kwa Baba… Sasa na siku… *Sauti ya mbili*

Asubui mapema wanawake wabebaji manukato wakaenda kwa haraka ku kaburi yako kukutafuta, ee Kristu, sababu ya kupakaa manukato mwili wako takatifu; lakini kisha maneno Malaika aliyowaambia wakaenda wepesi kwa Mitume kuwapasha habari ya furaha wakasema: Amefufuka, Mfalme wa wokovu wetu; Mshindi wa mauti ameleta duniani uzima wa milele na neema ya wokovu.

**APOSTIKHA** *Sauti ya mbili*

Asulubiwe, ndivyo walilalamika wale uliaza na mema yako, wakaomba wamufungue muovu pahali pa mfazili; na wewe Kristu, ulinyamaza na ulivumilia makelele yawauaji wa wenyi haki, kwani ulipenda kuteswa na kutuokoa katika mapendo yako.

Kujeni tumwabubu huyu aliyezaliwakwa Baba mbele ya milele Neno wa Mungu na aliyezaliwa kwa Bikira Maria, sababu alivumiliya Msalaba, alijitoa ku maziko kama alivyotaka, na alifufuka katika wafu, aliniokoa mimi mpotevu.

Walipokataa furaha za hapa chini, Mashahidi. Watakatifu wakapokea hazina za mbinguni, wakawa Wenzao wa malaika: Kwa maombezi yao, ee Bwana, utuhurumie na utuokoe.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya sita.*

Yosefu aliomba mwili wa Yesu, akauweka ndani ya kaburi mupya; kwa sababu ilifai Kristu atoke ndani ya kaburi kama katika nyumba ya arusi. Wewe uliyeharibu nguvu ya mauti sababu ya kuwafungulia wanadamu milango ya Paradizo, Bwana, utukufu kwako.

# MU KAZI TANO ASUBUI YA JUMA YA WABEBAJI MANUKATO

*Kisha Eksapsalmos na Apolitikia tunaimba:*

**KATHISMA YA KWANZA**. *Sauti ya mbili.*

Tunasujudu mbele ya Ikona yako Takatifu, ewe Mungu wa wema, tukiomba maondoleo ya makosa yetu, ee Kristu Mungu wetu, kwani ulipenda kuteswa ulipopanda Msalabani kwa kuokoa kiumbe chako ku utumwa wa adui; na kwa shukrani tunakulalamikia: Umejaza ulimwengu na furaha, ewe Mwokozi wetu, ulipokuja kuleta wokovu duniani.

Wewe usiyekataza jiwe lisifungana kaburini, katika ufufuo wako, ukatupatia jiwe la imani, ee Bwana, utukufu kwako.

Kwa imani mulipata utukufu kubwa: Hapana paka mulishinda Adui mulipoteswa, lakini tena mulifukuza mashetani, na munaponyesha magonjwa yote, enyi waganga wa roho na wa miili; enyi Mashahidi Watakatifu, ombeni kwa Mungu ili ahurumie roho zetu.

Alipotazama, ee Kristu, lufu yako Msalabani, Bikira Mama yako akalia na uchungu akasema: ee mwanangu, ni fumbo gani hii ya kuogopesha? Wewe mwenye kuleta uzima wa milele kwa wote, namna gani unaweza kuteswa na haya kwa kutaka kwako Msalabani na lufu?

**KATHISMA YA MBILI** *Sauti ya mbili. Ta ano ziton*

Mwokozi, Wanawake watakatifu walileta manukato kaburini na juhudi, na roho yenyi kufurahishwa na Malaika mwenye kuangaa walikutangaza kama Mungu wa ulimwengu, wakawaambia Wafwasi na furaha : Amefufuka, Bwana aliye Uzima wetu."

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*(mara mbili).*

*Kisha tunasoma: Tukiona ufufuo wa Kristu...Zaburi 50 (51). Kanuni ya Siku Kuu na Mineon, Kontakion na Eksapostilarion ya Siku Kuu.*

## MASIFU.*Sauti ya mbili*

Ee Kristu Mungu wetu, kwa mti wa Msalaba wako, ukafanya mti wa uzima kwa ajili yetu sisi mwenye kukuamini wewe, katika hii uliharibu adui aliyekuwa na ufalme wa mauti, ukatupatia tena uzima sisi tuliyouawa na zambi; tena tunakulalamikia: Ewe Mfazili wa ulimwengu, Bwana, utukufu kwako. *(mara mbili).*

Kila mwenye pumuzi na kila Kiumbe, kila kusifu, ee Bwana, kwa sababu kwa Musalaba uliharibu mauti, kusudi ya kuonyesha kwa mataifa, ufufuo wako katika wafu, kwa maana ni wewe peke Mpenda-wanadamu.

Mulipoteswa kwa ajili ya Kristu mpaka kufa, enyi Washuhuda Washindaji wa Bwana, mukatoa mbinguni roho yenu mikononi mwa Mungu, na masalio yenu yanapelekwa duniani kote; makohani na Wafalme wanasujudu mbele hii, na mataifa yote yanapaza sauti kwa furaha: Ni ya samani ku macho ya Bwana; lufu ya marafiki zake.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya kwanza.*

Malaika mumoja mwenye kuangaa alisema: Ninyi wanawake wabebaji manukato, nini munakuja kufanya kaburini? Sababu gani munamutafuta katika wafu Huyu aliye hai? Muwe na moyo: Bwana amefufuka.

## APOSTIKHA *Sauti ya mbili. Ote ek tu ksilu.*

Wanawake wabebaji-manukato walifurahi kwa kusikia Malaika ambaye maneno yake yaliwapa imani kwa Ufufuo wa huyu alihesabiwa katika wafu kwa ajiliyetu: walisadiki japo walienda kaburini na nyimbo zao za kilio na japo jiwe lililosukumwa liliwasangaza.

Shairi: Unapenda inchi yako, ee Bwana, unarudisha wafungwa wa Yakobo.

Wanawake wabebaji-manukato wa Kristu walifurahi sana wakati walionekana mbele ya Wafwasi wa Bwana kuwapasha habari ya Malaika Mtakatifu ambaye manguo yake mweupe yaliwaopesha,wakasema: Hadeze imeshimdwa kwa Ufufuo wa huyu alikufa kwa ajili yetu, Kristu Mfalme wetu.

Shairi: Mapendo na Ukweli yanakutana, haki na Amani yanakumbatiana

Kisha kulia kwao, sasa Wanawake wabebaji-manukato wa Kristu wanapasha habari ya furaha kwa washuhuda wa neema ya Mungu, wanawatangazia Ufufuo wa Neno takatifu, furaha yenye kutoka kaburini na furaha nzuri ilimaliza kulia kwao wakati walisikia: Salamu.

Utukufu kwa Baba… Sasa na siku zote…, *Sauti ya kwanza*

Ee Kristu, Wanawake wabebaji-manukato walienda na haraka asubui mapema kaburini kwako kukutafuta sababu ya kupakaa mwili wako manukato ; lakini kisha kusikia maneno Malaika

aliwaambia, wakaenda wepesi kwa Mitume kuwapasha habari ya furaha wakisema : “ Mfalme wa wokovu wetu amefufuka; Mshindi wa mauti analeta duniani uzima wa milele na neema ya wokovu.

# MU KAZI TANO MANGARIBI YA JUMA YA WABEBAJI MANUKATO

*Kisha «Bwana nimekuita...» tunaimba wimbo sita; tatu ya siku Kuu na tatu ya Mineon.*

***Wimbo ya Siku Kuu.***

*Sauti ya mbili. Idiomelon.*

Asubui mapema, Wanawake wabebaji-manukato walipokuja ku kaburi ya Bwana na wakati hawakupata ile walitafuta, wakasikitika sababu ya hii mabadiliko na mbele ya jiwe lilisukumwa wakaambiana mumoja kwa mwingine: Wapi mlango wa kaburi? Wapi walinzi Pilato alituma? Lakini sikitiko yao ikaondolewa wakati walimuona Malaika mumoja mwenye kuangaa aliyewauliza akisema: Sababu gani munamutafuta na machozi huyu aliye hai na mwenyi kuwapa wanadamu uzima? Amefufuka katika wafu, Kristu Mungu wetu mwenyezi mwenyi kutupatia wote uzima wa milele, nuru na neema ya wokovu.

Sababu gani munachanga machozi yenu na manukato munabeba? Jiwe limesukumwa, kaburi ni wazi; oneni namna gani uzima inashinda mauti, oneni jiwe ni ushuhuda tazameni usingizi gani walinzi walilala; ile zamani ilikuwa chini ya utumwa wa mauti imeokolewa kwa mwili wa Mungu wetu, Hadeze inalia kwa uchungu; lakini kwendeni na furaha kwa Mitume mukawaambie ya kwamba: Kristu mshindi wa mauti na mzaliwa wa kwanza katika wafu anawatangulia kwenda Galilea.

Ee Kristu, Wanawake wabebaji-manukato walienda na haraka asubui mapema kaburini kwako kukutafuta sababu ya kupakaa mwili wako manukato; lakini kisha kusikia maneno Malaika aliwaambia, wakaenda wepesi kwa Mitume kuwapasha habari ya furaha wakisema: Mfalme wa wokovu wetu amefufuka; Mshindi wa mauti analeta duniani uzima wa milele na neema ya wokovu.

***Wimbo tatu ya Mineon***

Utukufu kwa Baba.. *Sauti ya sita*

Wanawake Wabebaji-manukato walipofika kaburini na walipoona kaburi wazi na hawakupata mwili wako takatifu japo kuja kwao wepesi, wakalia na kusema : “ Nani alituiba matumaini yetu? Nani alibeba mwili tupu wenyi kupakaa manukato ambaye kwa Mama yake alikuwa kitulizo? Ole wetu! Namna gani aliuawa huyu mwenyi kuwapa watu uzima? Namna gani Mshindi wa Hadeze aliwekwa kaburini? Lakini kwa uwezo wako, ee Mwokozi, fufuka siku ya tatu kama ulivyosema sababu ya kuleta neema ya wokovu rohoni mwetu.

Sasa na siku zote...**THEOTOKION**

Kivuli cha Sheria kinafifia, kwani ilikuja neema; sawa kichaka kiliwaka moto bila kuteketezwa, hivyo ulizaa Bikira, na ulibaki Bikira; pahali pa nguzo ya moto, Jua la uhaki lilipanda pa fasi ya Musa, Kristu, wokovu wa mioyo zetu.

**APOSTIKHA.** *Sauti ya mbili.*

Kujeni tumwabudu huyu aliyezaliwa na Baba mbele ya milele, Mungu neno aliyechukuwa mwili, kwa Bikira Maria; kwa sababu alivumiliya Msalaba, alijitoa ku maziko, kama alivyotaka, na alifufuka katika wafu, aliniokoa mimi mtu mpotevu.

Shairi: Bwana anatawala mwenye kuvaa utukufu, Bwana anatawala anajifunga uwezo wake

Kristu Mwokozi wetu, alizimisha maandiko mabaya ya ndani zetu, kwa kuipigilia Msalabani, na aliharibu nguvu ya mauti. Tuabudu Ufufuo wake wa siku tatu.

Shairi: Ulikaza ulimwengu isitikisike,utawala wako ni imara daima.

Tuimbeni Ufufuo wa Kristu pamoja na malaika wakuu; kwa maana huyu ni Mkombozi, na Mwokozi wa roho zetu; na maogopesho ya utukufu, na nguvu ya uwezo, eko nakuja tena, kuhukumu dunia aliyeumba.

Shairi: Ee Bwana, makao yako inastahili utakatifu siku nyingi.

Ufufuo wako, ee Kristu Mwokozi, uliangaza ulimwengu nzima, na uliita tena kiumbe chako; Bwana mwenyezi, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya tano.*

Wewe mwenye kuvaa nuru kama nguo, Yosefu na Nikodemu walikushusha pa mti wa Msalaba na mbele ya mwili wako, bila kaburi, wakaomboleza kwa uchungu na wakasema wakilia: Ole, ee Yesu mpole kamili! Jua lililokuona Msalabani limepata giza na inchi imetikisika kwa woga; pazia la Hekalu likapasuka na nimekuona ukivumilia kwa ajili yangu kifo cha kutaka. Namna gani nitakuzika, ee Mungu wangu? Sanda gani nitakufunika? Na mikono gani nitagusa Mwili wako Takatifu? Wimbo gani nitaimbia kifo chako? Ewe mwenye rehema kamili, natukuza mateso yako! Naimbia maziko yako na Ufufuo wako nikilalamika: Ee Bwana, utukufu kwako.

## MU POSHO ASUBUI YA JUMA YA WABEBAJI MANUKATO

*Kisha Eksapsalmos na Apolitikia tunaimba:*

**KATHISMA YA KWANZA** *Sauti ya mbili.*

Wewe usiyekataza jiwe lisifungana kaburini, katika ufufuo wako, ukatupatia jiwe la imani, ee Bwana, utukufu kwako.

Kundi ya Wafwasi, ewe Mzazi-Mungu, Mtukufu kuliko wote, lufu imevunjwa kwa lufu, na Hadeze imeshindwa kwa Msalaba wa mwana wako; alitufufua ku lufu, akatupatia uzima, wa milele; paradizo inapewa mara ingine kwa sisi, sababu ya kufurahiwamo kama zamani; tena tunatukuza na shukrani mapendo na uwezo wa Kristu Mungu wetu.

**THEOTOKION**

Siri zako zote, zinapita wazo lolote na zote ni utukufu sana, ee Mzazi-Mungu, wewe uliyechapiwa alama ya safi, uliyelindwa kwa ubikira, ulijulikana mama msema kweli, ulizaa Mungu kweli; umwombe aokoe roho zetu.

**KATHISMA YA MBILI** *Sauti ya mbili.*

Kundi la Wafwasi wako linaungana na lile la Miroforo katika furaha; wote pamoja nao tunashangilia hii siku Kuu kwa kutukuza ufufuo wako Takatifu; kwa haki zao, ee Bwana, Mpenda-wanadamu, tunakuomba, uwape watu wako neema ya wokovu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote... *(mara mbili).*

*Kisha tunasoma: Tukiona ufufuo wa Kristu...Zaburi 50 (51). Kanuni ya Siku Kuu na Mineon, Kontakion na Eksapostilarion ya Siku Kuu.*

**MASIFU.** *Sauti ya mbili.*

Kila mwenye pumuzi na kila Kiumbe, kila kusifu, ee Bwana, kwa sababu kwa Musalaba uliharibu mauti, kusudi ya kuonyesha kwa mataifa, ufufuo wako katika wafu, kwa maana ni wewe peke Mpenda-wanadamu.

Wayuda wa wewe namna gani wakati askari walipochunga Mfalme walimupotesha? Sababu gani jiwe halikuchunge mwamba wa uzima? Ao watupatiye huyu aliyezikwa, ao wamwabudu huyu aliyefufuka, wakisema pamoja na sisi: Utukufu kwa wingi wa rehema Yako, ee Mwokozi wetu, utukufu kwako.

Furahini, mataifa na mushangilie; malaika alikaa juu ya jiwe la Kaburi; huyu akatuletea sisi habari njema, akatwambia: Kristu Mwokozi wa watu, alifufuka katika wafu, na akajaza ulimwengu kwa marasi. Furahini, mataifa na mushangilie.

Malaika alileta salamu kwa Mujaliwa na neema, mbele ya kuchukuwa miimba yako, ee Bwana; tena Malaika alisukuma jiwe la Kaburi yako tukufu, katika ufufuko wako. Malaika wa kwanza pahali pa sikitiko, akapasha habari ya alama ya furaha; Malaika mwengine pahali pa mauti, alitutangazia ya kama Rabi na Muletaji-uzima kwa sisi; kwa hii tunakupazia sauti: Ewe Bwana, Mufazili wa wote, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya kwanza.*

Maria Magdalena na Maria mwingine walikwenda kaburini kumutafuta Bwana, wakamuona Malaika mumoja mwenyi kuangaa kama umeme amekaa pembeni ya jiwe na akawaambia : Sababu gani munamutafuta katika wafu Yeye aliye hai? Hayuko hapa, amefufuka kama alivyosema, anawatangulia kwenda Galilea." Tunaposujudu mbele yake, tunaimba : " Ee Mfufuliwa katika wafu, Bwana, utukufu kwako.

**APOSTIKHA** *Sauti ya mbili. Sauti ek tu ksilu.*

Wakati mtu wa Arimathea alipokushusha umekufa Msalabani, wewe Uzima wa wote, akakumimia manukato, ee Kristu, akakufunga sanda. Tena mwenye kujaa na mapendo akakumbatia kwa moyo na kwa midomo Mwili wako Takatifu kamili. Lakini aliposhikwa na woga, akasema na furaha akitetemeka: Utukufu kwa ukubwa wako, ewe Mpenda-wanadamu.

Shairi:Unapenda inchi yako, ee Bwana, unarudisha wafungwa wa Yakobo

Wakati ulipowekwa kaburini mpya kwa ajili ya wokovu wa wote kama ukombozi wa wote, hadeze ilizihakiwa na ikaogopa; makomeo yake ikavunjwa, milango yake iliondolewa. Makaburi yalifunguka, wafu wakafufuka. Kwa hii wakati Adamu mwenyi shukrani akakulalamikia: Utukufu kwa ukubwa wako, ewe mpenda-wanadamu.

Shairi: Mapendo na Ukweli yanakutana, haki na Amani yanakumbatiana

Ee Kristu, wakati majeshi ya mbinguni yalikuona wamekuchongea kwa uwongo, wamekutendea kama mwenyi kudanganya kwa wasiyo na sheria, yakatetemeka pakuona uvumilivu wako wa kweli. Lakini mbele ya jiwe lililowekwa kaburini kwa mikono iliyochoma ubavu wako Takatifu, yakafurahiwa kwa ajili ya wokovu wako na ya kalalamika: Utukufu kwa ukubwa wako, ewe mpenda-wanadamu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya sita.*

Yosefu alikwenda kwa Pilato kumwomba mwili wa Yesu, akauweka ndani ya kaburi mupya; kwa sababi ilifai Kristu atoke kaburini kama katika nyumba ya arusi. Wewe uliyeharibu nguvu ya mauti sababu ya kuwafungulia wanadamu milango ya Paradizo, Bwana, utukufu kwako.

# MU JUMA YA MWENYE KUPOOZA

## MU JUMA MANGARIBI YA MWENYE KUPOOZA

*Elezo: Kisha: «Bwana nimekuita...» tunaimba wimbo kumi; Wimbo saba ya Ufufuo na tatu ya mwenye kupooza.*

*Sauti ya tatu*

Nguvu ya mauti ilivunjwa kwa Msalaba wako Kristu Mwokozi, na udanganyifu wa Shetani uliharibiwa, basi uzao wa watu, wenye kuokolewa kwa imani, unakutolea nyimbo kila siku.

Ulimwengu uliangazwa, kwa Ufufuo wako Bwana, na Paradizo tena ilifunguliwa; na kiumbe chote mukukusifu, kinakutolea nyimbo kila siku.

Ninatukuza nguvu ya Baba, na ya Mwana, na ninaimba uwezo wa Roho Mtakatifu, umungu usiyogawanywa na usiyoumbwa, Utatu wa asili moja (omousion), unaotawala milele na milele.

Tunaabudu, ee Kristu, Msalaba wako muheshimiwa, tunaimba na tunatukuza, Ufufuo wako; kwa sababu ya alama ya mapigo yako, sisi wote tumepona.

Tunamwimba Mwokozi, aliyepata mwili kwa Bikira; Alisulubiwa juu ya sisi, na siku ya tatu alifufuka, kwa ajili ya kutupatia rehema yake kubwa.

Wakati alishuka kwa wale walikua kuzimu, Kristu alitangaza habari njema; akisema, muwe sabiti, sasa minashinda; mimi ni Ufufuo; nitamipandisha ninyi, pa kuvunja milango ya mauti.

Tunasimama bila kustahili, mu makao yako takatifu, tunakutolea wimbo wetu wa mangaribi, na ndani yetu tunapaza sauti; ee Kristu Mungu, uliyeangaza ulimwengu, kwa ufufuo wako siku ya tatu, opoa watu wako, ku mukono wa adui wako, ewe Mpenda-wanadamu.

***Wimbo ya mwenye kupooza. Idiomela***

*Sauti ya kwanza*

. Ee Kristu, wewe kwa mkono wako takatifu kamili uliumba mwili wa mwanadamu, kwa wema wako ulikuja kuponyesha wagonjwa; kwa neno lako uliamusha Mwenye kupooza kule ku kisima cha Kondoo; ulituliza mateso ya mwanamuke mwenye kutoka damu, uliponyesha binti wa mwanamuke mkanana; haukukataa ombi la mkubwa wa waaskari; ndio maana tunakulalamikia tukisema: Ee Bwana mwenyezi, utukufu kwako. *(mara mbili).*

Kama mufu mzima, Mwenye kupooza alipokuona akapaza sauti na kusema : Unihurumie, Bwana, maana kinywa changu kimekuwa kaburi yangu; uzima inaniletea nini? Kisima cha kondoo kinanisaidia nini? Sina na mutu wa kuniingiza ndani wakati maji yanapotikiswa; lakini nakuja kwako wewe uliye Chemchem ya maponyesho ili nipaze sauti pamoja na wote nikisema: Ee Bwana mwenyezi, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba.....*Sauti ya tano.*

Yesu alienda Yerusalema ku kisima cha Kondoo kinachoitwa katika kiebrania Betesaida, wagonjwa wengi walikuwa wamelala katika baraza, Malaika wa Mungu alishuka mara kwa mara na kuingia katika kile kisima, akatikisa maji na waaminifu waliingia wa kwanza walipona. Kristo alipomuona mutu mumoja aliyekuwa mgonjwa muda wa siku nyingi, akamuuliza: Unataka kupona? Yule mgonjwa akamujibu: Bwana, sina na mutu wa kuniingiza katika kisima wakati maji yanapotikiswa; nimepoteza mali yangu yote kwa waganga na sikuweza kupona. Lakini mganga wa roho na wa mwili akamwambia: Simama, chukua mukeka wako na wende kutangaza duniani kote uwezo wangu na neema ya wokovu .

Sasa na siku zote...**THEOTOKION**. *Sauti ya tatu.*

Namna gani hatutashangaa, Muheshimiwa kamili, uzao wa Mungu na mtu? Kwa sababu bila kujua mwanaume, ee Bikira usiye na doa, ulizaa Mwana kwa namuna ya mwili pasipo baba, mwenye aliyezaliwa na Baba mbele ya milele pasipo mama, bila kupokea geuzo, ao mchanganyo, ao mgawanyo, lakini mwenye kushika tabia zake nzima za kila moja asili ya yote mbili. Kwa hii, Mama Bikira bibi malkia, umusihi kwa sababu ya wokovu, wa roho ya wale wanakusadiki kwa namuna ya kiorthodoksi, ya kama uko Mzazi-Mungu.

**Kuingia.** Mwangaza upole (ilaron)...

**L I T I A** Utukufu kwa Baba...*Sauti ya tano*

Bwana, karibu ya kisima cha Kondoo kulilala mutu mumoja mwenyi kupooza, alipokuona, akapaza sauti na kusema: Sina na mutu wa kuniingiza katika kisima wakati maji yanapotikiswa; ninapojaribu kuingia katika maji mutu mwingine anaingia mbele yangu na anapona, mimi nabaki mwenyi kupooza. Mwokozi akamuhurumia na akamwambia palepale: Kwa ajili yako nimejifanya mutu, kwa ajili yako nilichukua mwili, unasema hauna na mutu wa kukusaidia? Chukua mukeka wako, nakuamuru wende. Vitu vyote vinakutii, ee Bwana, vitu vyote vinakutii, unaweza kufanya ile unataka; utukumbuke sisi wote, ee Mungu Mtakatifu; na kwa mapendo yako kwa wanadamu utuhurumie.

Sasa na siku zote...**THEOTOKION**

Bikira Muheshimiwa kamili, uko hekalu na mulango, nyumba na kiti cha Mufalme; kwa wewe Kristu, Bwana na Mukombozi wangu, alifunuliwa kwa wale waliokaa katika giza; eko jua la haki, akitaka kwangaza wale walioumbwa kwa mufano wake kwa mikono yake; kwa hii, Mwimbiwa kamili, kwa sababu uko na uhodari ya umama mbele yake, upatanishe bila kuacha, kwa kuokoa nafsi yetu.

**APOSTIKHA** *Sauti ya tatu*

Kwa mateso yako, ee Kristu, ulileta giza ku jua, kwa nuru ya Ufufuo wako, ulifurahisha ulimwengu, pokea wimbo wetu wa mangaribi, ewe Mpenda-wanadamu.

*Tangazo:Kisha tunaimba WIMBO YA PASKA (Angalia Masifu ya Orthros ya Paska): Sauti ya tano*

1. Paska zabihu leo imeonekana kwetu, Paska mupya Takatifu. . .
2. Kujeni Wanawake. . .
3. Wanawake Wabebaji manukato. . .
4. Paska ya furaha, Paska ya Bwana Paska. . .

Utukufu kwa Baba. . . *Sauti ya mnane*.

Wagonjwa wengi walilala karibu ya Mulango ya Hekalu ya Solomoni: Katikati ya Sikukuu Yesu alikuta mutu mumoja mwenyi kupooza tangu miaka makumi tatu na munane; kwa sauti yake ya ubwana akamwambia: Unataka kupona? Mgonjwa akamujibu: Bwana, sina na mutu wa kuniingiza katika kisima wakati maji yanatikisiwa. Lakini Bwana akamwambia: Chukua mukeka wako, umeponyeshwa, tangu sasa usitende tena zambi. Kwa maombezi ya Mzazi-Mungu, ee Bwana, ututumie neema ya wokovu.

Sasa na siku zote. . . *Sauti ya tano.*

Ufufuo ni leo na tuangazwe kwa Karamu. . .

**APOLITIKION.** *Sauti ya tatu.*

Mbingu zifurahiwe, na inchi ishangilie, kwa sababu Bwana ametenda nguvu, kwa mukono wake; na kwa lufu alishinda mauti; na akawa muzaliwa wa kwanza katika wafu; akatuondosha katika tumbo la kuzimu, na akaleta ku dunia huruma kubwa.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote..**THEOTOKION.**

Bikira Mzazi-Mungu tunakuimbia, wewe mupatanishi wa wokovu juu ya ukoo wetu; katika mwili alipata Kwako, Mwana wako na Mungu wetu, alitaka kuteswa msalabani, juu ya kutukomboa ku lufu, sawa Mpenda-wanadamu. **KUAGA**

# MU JUMA YA MWENYE KUPOOZA ASUBUI

**KATHISMA YA KWANZA** *Sauti ya tatu*

Kristu amesimama katika wafu, malimbuko ya wale waliyolala; mzaliwa wa kwanza wa kiumbe, fundi wa ulimwengu wote, ndani yake alifanya upya hali ya ubinadamu iliyoharibika. Ewe mauti, hautawala tena: Ufalme wako umevunjwa na Bwana wa ulimwengu.

Utukufu kwa Baba

Ee Bwana, kwa mwili wako ulionja mauti, ukaondoako uchungu kwa ufufuo wako; kwa hii ulisabitisha ubinadamu, ukaondoa ushindo uliyoazibiwa na laana ya zamani. Ewe Mlinzi wa uzima wetu, Bwana, utukufu kwako.

Sasa na siku zote. **THEOTOKION**

Ee Mzazi-Mungu mbele ya neema isiyoweza kufafanishwa ya ubikira wako, mbele ya uzuri na ya nuru kimungu ya utakatifu wako, alipoogopa, Gabrieli akapaza sauti akasema: Sifa gani yenye kustahili utakaitfu wako nitaweza kukutolea? Kwa jina gani kubwa nitakutaja? Sijui na imekatazwa. Na tena, nikishika amri niliyopewa, nakuimbia: Salamu, ewe Mjaliwa neema.

**KATHISMA YA MBILI.** *Sauti ya tatu. Tin oreotita.*

Ee Bwana, mbele ya hali imara ya umungu wako, mbele ya mateso ya kutaka uliyoteswa, ilipoogopa, Hadeze ikalia juu ya bahati yake, ikalalamika: Naogopa sana mwili wako usiyoharibika; naona msiyeonekana akinigombanisha na akili; na wale ninaofunga nawasikia wakilalamika: Utukufu ku ufufuo wako takatifu, ee Kristu Mungu wetu.

Utukufu kwa Baba...

Sisi waamini tunatangaza fumbo isiyokadirika wakati tunapotazama kusulubiwa kwako ambako mtu hata mmoja hawezi kusikia na ufufuo wako ambao mtu hata mmoja hawezi kueleza: Kwa hii siku mauti na Hadeze zimenyanganywa, ubinadamu umevaa umilete; na kwa ushukuru tunaweza kuimba: Utukufu ku ufufuo wako Takatifu, ee Kristu Mungu wetu.

Sasa na siku zote...**THEOTOKION**.

Majeshi ya mbinguni yalifurahiwa na mapendo, wanadamu waliogopa wakati salamu ya Malaika ilitolewa kwako, ewe Mzazi-Mungu; duniani kama mbinguni ni Siku Kuu ileile inatoa nuru yake kwa sababu Baba wa kwanza amekombolewa ku lufu; pamoja na malaika, sisi pia tunakulalamikia: Salamu, ewe Mama Mzazi-Mungu Mtakatifu kamili tena Bikira.

***Mahimidi ya Ufufuo ya Kristu.***

**IPAKOI**

Wa ajabu ku sura yake, Malaika mwenye kuangaa, kwa maneno yake akamwanga umande, akawaambia wabebaji-manukato: Kwa nini munamutafuta katika wafu huyu aliye hai? Alipotosha

vyote kaburini, amefufuka! Na kwa mabadiliko yenye kufanyika kaburini mutambue huyu hawezi kugeuka na mumuambieni: Matendo yako ni ya ajabu, Bwana! Kwani uliokoa ubinadamu ku lufu.

*Kisha tunaimba Anavathmi ya sauti ya tatu. Tafuta mu Kitabu ya Paraklitiki, mu Juma, sauti ya tatu.*

*Kisha tunaimba Kanuni ya Ufufuo ya siku ya Paska na Kanuni ya Mwenye kupooza.*

**WIMBO YA KWANZA.** *Sauti ya tatu.*

**IRMOS:** Uko Mungu mwenye kutukuzwa kabisa uliyefanya maajabu zamani, uligeuza bahari kuwa inchi kavu na kuangamiza waaskari sababu ya kuoka watu wenye kukuimbia, ee Mkombozi.

Utukufu kwako ee Mungu wetu, utukufu kwako..

Peke yako Mfalme mwenye kufanya miujiza, zamani ulifanya maajabu; ulipanda msalabani kwa kutaka kwako, ee Mungu wa wema, kwa lufu yako uliharibu mauti sababu ya kutupa sisi uzima.

Utukufu kwako ee Mungu wetu, utukufu kwako..

Enyi watu waaminifu, tushangilie leo kwa ajili ya Kristu aliyefufuka : Hadeze imeshindwa, inafunguwa wafungwa wake wa zamani wenye kuimbia maajabu ya Mungu.

Utukufu kwako ee Mungu wetu, utukufu kwako..

Ee Kristu ambaye kwa neno lako na kwa ubwana wako zamani uliponyesha Mwenye kupooza na kumubebesha mukeka wake wakati alipokuwa mgonjwa tangu miaka mingi, ponyesha vilevile roho yangu yenye kujaribiwa kabisa.

Utukufu kwako ee Mungu wetu, utukufu kwako..

Zamani Malaika mumoja alishuka mara na mara ndani ya kiziwa cha Kondoo, aliponyesha paka mgonjwa wa kwanza aliyeingia katika maji yaliyotikiswa; lakini Kristu anatakasa sasa watu wengi kwa Ubatizo takatifu.

Utukufu kwako ee Mungu wetu, utukufu kwako..

Ee Mfalme mkubwa wa Malaika wa juu mbinguni, Mwongozi mkubwa wa watumishi wa mbinguni, linda na chunga salama toka hatari yote waaminifu wenye kukusanyika katika kanisa yako sababu ya kuimbia na kutukuza Bwana.

Utukufu kwa Baba…

Pamoja na Malaika wasiyo na mwili tuimbie daima katika watu tatu hali moja ya Mungu wa milele, Baba, Neno na Roho Mtakatifu ambao utawala na uwezo usiyogawanyika ni wao.

Sasa na siku zote...

Ee Bikira Mtakatifu kamili, uwape watu wako waaminifu wenye kukutukuza daima na imani waepuke hatari ya mashambulio na ya vita kati ya raia.

**WIMBO YA TATU.** *Sauti ya tatu*

**IRMOS:** Roho tasa isiyozaa watoto, chanusha tunda la sifa, ee mama mwenye kutukuzwa katika wana wake, imba ukisema: Roho yangu inasabitishwa kwa Mungu; hakuna aliye mtakatifu, hakuna aliye mwenye haki ila Bwana peke yake.

Utukufu kwako ee Mungu wetu, utukufu kwako..

Ee Neno, zamani jua lilipokuona umetundikwa msalabani, likaficha nuru yake, inchi ikatetemeka pande zote, wafu wakafufuka toka kaburi, ee Mungu mwenyezi, wakati wewe mwenyewe ulikufa.

Utukufu kwako ee Mungu wetu, utukufu kwako..

Mwokozi, wakati na roho yako uliingia katika udongo, Hadeze ikafunguwa kwa haraka roho alizofunga na ziliimbia uwezo wako wimbo wa shukrani, ee Bwana.

Utukufu kwako ee Mungu wetu, utukufu kwako..

Ee Mungu wa wema, tangu miaka mingi roho yangu inateswa vibaya; kama ulivyomutendea Mwenye kupooza zamani, uiponye ili niweze kutembea katika njia humo unaalika wenye kupenda jina lamo.

Utukufu kwako ee Mungu wetu, utukufu kwako..

Ee Mtakatifu Malaika mkuu wa Mungu, pamoja na majeshi ya mbinguni ombea wale wenye kukutukuza na imani: Utuokoe, utulinde, utuchunge sisi wenye kushambuliwa na mateso ya hii uzima.

Utukufu kwa Baba…

Tunatoa utukufu kwa Mungu tukiimbia Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, wenye kutukuwza na majeshi ya mbinguni wakisema na woga kwa Mungu mumoja: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ni wewe, Bwana Mungu wetu.

Sasa na siku zote…

Ulipata mimba bila mbegu, kuokolewa kwako kunapita ufahamu wote, ee tendo la kushangaa, muujiza wa ajabu wanaimbia Malaika na kutukuza na wanadamu, ee Bibi wetu na Bikira Mama Mtakatifu kamili.

**KATHISMA** *Sauti ya tatu. Tin oreotita.*

Neno moja tu lilimuponyesha Mwenye kupooza wakati alisema Neno wa milele ambaye kwa ajili yetu alionekana duniani kwa kutaka kwake; mgonjwa alichukua mukeka wake na akatenbea japo Wayuda wabaya hawakuvumilia kuona muujiza Kristu alifanya, na kwa uovu wao walichukia huyu mwenye kuvunja minyororo ya roho zetu.

Utukufu kwa Baba..Sasa na siku zote...**THEOTOKION**

Ee Mzazi-Mungu mbele ya neema isiyoweza kufafanishwa ya ubikira wako, mbele ya uzuri na ya nuru kimungu ya utakatifu wako, alipoogopa, Gabrieli akapaza sauti akasema: Sifa gani yenye kustahili utakatifu wako nitaweza kukutolea? Kwa jina gani kubwa nitakutaja? Sijui na imekatazwa. Na tena, nikishika amri niliyopewa, nakuimbia: Salamu, ewe Mjaliwa neema.

**KONTAKION**

Ee Kristu, kwa maongozi yako ya umungu, kama kwa Mwenye kupooza wa zamani, ponyesha roho yangu yenyi kupooza sababu ya zambi zangu na maovu yangu, kusudi, nikiokolewa niweze kukutukuza : Ee Mungu wa mapendo, utukufu kwa uwezo wako wa milele.

**IKOS**

Ee Bwana Yesu wa milele pamoja na Baba na kutawala na utukufu pamoja na Roho Mtakatifu, ulionekana mwilini ukiponyesha magonjwa na kufukuza mateso, ulifungua macho ya vipofu, uliponyesha Mwenye kupooza na neno takatifu, ukamuamuru tena atembee na abebe mukeka wake juu ya mabega yake; pamoja naye tunakutukuza na kukuimbia tukisema : Ee Mungu wa mapendo, utukufu kwa uwezo wako wa milele.

**SINAKSARI YA WATAKATIFU**

Leo, Juma ya ine ya Paska, tunakumbuka Mwenye Kupooza na tunashangilia muujiza wa hii namna kama inavyofaa.

Kule ku kisima cha Kondoo Kristu mganga wa hekima, kwa neno lake la uwezo, aliponyesha Mwenye Kupooza. Kwa rehema yako ya milele, ee Kristu Mungu wetu, utuhurumie. Amin.

**KATAVASIA YA UFUFUO YA KRISTU**

**EKSAPOSTILARION YA PASKA.** *Sauti ya mbili*

Kwa mwili, ee Mufalme na Bwana ulipolala kama mutu mwenye kuweza kufa, ulifufuka siku ya tatu; ukisimamisha Adamu toka uharibifu na uliharibu mauti, ewe Paska uzima usiyoharibika Mwokozi wa dunia.

**Ingine ya mwenye kupooza.** *Sauti ya mbili. Ginekes akutisthite.*

Bwana Mpenda-wanadamu, yeye chemchem isiyokauka ya mapendo, alikuja karibu ya kisima cha Kondoo kuponyesha wagonjwa na vilema; alipomukuta mutu mumoja mwenyi kulala tangu miaka mingi, Yesu akamuamuru : " Chukua mukeka wako, na tangu sasa tembea katika uhaki."

**MASIFU** *Sauti ya tatu*

Kujeni, mataifa yote, mujue nguvu ya fumbo ya ajabu; kwani Kristu Mwokozi wetu, Neno aliyekuwa katika mwanzo, alisulibiwa kwa ajili yetu, na alizikwa kwa kutaka kwake, na alifufuka katika wafu kusudi aokoe ulimwengu. Tumwabudu yeye.

Walinzi, ee Bwana, wakaeleza maajabu yako yote; lakini baraza ya ubatili, wakijaza mukono wao wa kuume kwa zawadi, waliwaza ya kama watafuchika Ufufuo wako, uliyotukuzwa na watu. Utuhurumie.

Dunia yote ilijazwa na furaha, wakati ilipopata maarifa ya ufufuo; kwani Maria Magdalena alikuja kwa Kaburi, na akakuta Malaika amekaa juu ya jiwa, kwa mavazi ya kuangaa, na akasema: sababu gani munatafuta yeye aliye hai katika wafu; Hayuko hapa, lakini alifufuka, kama alivyosema, akiwatangulia kwenda Galilaya.

Katika mwangaza yako, ee Rabi Mpenda-wanadamu, tutaona mwangaza; kwa sababu ulifufuka katika wafu, ukitoa wokovu kwa uzao wa watu, kusudi viumbe vyote vikusifu, uliye peke Msiye-zambi. Utuhurumie.

Wanawake wabebaji-manukato, walitoa, ee Bwana, machozi, sawa wimbo wa asubui; kwani wakichukua mikononi mwao manukato ya arufu mzuri, walishika Kaburi yako, wakishugulika kupakaa mwili wako usiyo na doa kwa manukato. Lakini Malaika aliyekaa juu ya jiwe, aliwaletea habari njema; Sababu gani munatafuta Yeye aliyehai wafu. Akishinda mauti; alifufuka, kwa kuwa yeye ni Mungu, akileta rehema kubwa kwa wote.

Malaika aliyeangaa kama umeme, juu ya Kaburi yako iliyoleta uzima, alisema kwa wanawake wabebaji-manukato: Mkombozi aliacha ma kaburi tupu, alinyanganya Hadeze, na alifufuka siku ya tatu kwa kuwa yeye ni Mungu peke na mwenyezi.

Maria Magdalena akikuja kwa kaburi siku ya kwanza ya juma, alikutafuta; lakini sawa hakukupate, akalia, akipaza sauti kwa maombolezo: Ole! Mwokozi wangu, Mfalme wa wote, namna gani uliibwa? Lakini Malaika wawili waletaji-uzima, ndani ya kaburi wakapaza sauti: Kwa nini unalia, ee mwanamuke? Akawaambia: Ninalia, kwani wamemwondoa Bwana wangu toka kaburi, na sijui pahali walipomuweka. Basi alipogeuka nyuma, na waakti alipokuona, akaita mara moja: Bwana wangu, na Mungu wangu, utukufu kwako.

Waebrania walifunga sana Uzima ndani ya kaburi; lakini munyanganyi alifungua Paradizo kwa neno lake, akapaza sauti na akasema: Huyu aliyesulubiwa kwa ajili yangu na kutundikwa pamoja na mimi ameonekana kwangu mwenye kutawala pamoja na Baba; kwa sababu Yeye ni Kristu Mungu wetu, mwenye kuleta neema ya wokovu duniani.

Utukufu kwa Baba...*Sauti ya mnane.*

Bwana, apana kisima cha Kondoo kilimuponyesha Mwenye kupooza, lakini ni neno lako lilimufanya kuwa mutu mupya; apana magonjwa yake ya miaka mingi ilimuzuia kupona, ni uwezo wa msalaba wako ulishinda hii ugonjwa; Mwenye kupooza alitupa mzigo wake mzito, akachukua mukeka wake sababu ya kushuhudia rehema yako. Bwana, utukufu kwako.

Sasa na siku zote....Mbarikiwa ukupita, ewe Mzazi-Mungu Bikira....

**DOKSOLOGIA KUBWA**

# MU JUMA YA MWENYE KUPOOZA MANGARIBI

*Elezo: Kisha : «Bwana nimekuita...» tunaimba wimbo sita; tatu ya siku Kuu na tatu ya Mineon.*

***Wimbo ya siku Kuu.***

*Sauti ya mnane. O tu paradoksu thavmatos*

Ni jambo la ajabu! Muumba wa ulimwengu ameonekana na mwili wetu na kwa kutaka kwake alijifanya masikini katika hali ya ubinadamu; alipoishi pamoja na watu alifanya miujiza ya nuru, aliponyesha Mwenye kupooza, akamwambia: Chukua mukeka wako, simama na usitende tena zambi.

Mwokozi, Bwana wangu na Mungu wangu, ulipotaka kuamusha watu walioanguka, ulikuja duniani kama mwanadamu na kwa mapendo yako uliponya wagonjwa; ulipopita karibu ya kisima cha Kondoo, uliokoa Mwenye kupooza wa zamani: Mgonjwa tangu miaka makumi tatu na minane, aliponyeshwa kwa neno lako, ee Bwana.

Bwana, walipowaka na chuki, Wafarisayo waligeuza mema yako kuwa kisingizio na moto iliyowakisha hasira yao; wao waliovunja daima amri yako, sababu ya Sabato walipenda kukuua Wewe uliye Uzima wa kweli wakati siku moja ya Sabato uliponyesha mutu mumoja katika mwili wake wote pakusimamisha mgonjwa Mwenye kupooza wa zamani.

***Wimbo tatu ya Mineon***

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya kwanza*

Bwana, karibu ya kisima cha Kondoo kulilala mutu mumoja mwenyi kupooza, alipokuona, akapaza sauti na kusema: Sina na mutu wa kuniingiza katika kisima wakati maji yanapotikiswa; ninapojaribu kuingia katika maji mutu mwingine anaingia mbele yangu na anapona, mimi nabaki mwenyi kupooza. Mwokozi akamuhurumia na akamwambia palepale: Kwa ajili yako nimejifanya mutu, kwa ajili yako nilichukua mwili, unasema hauna na mutu wa kukusaidia? Chukua mukeka wako, nakuamuru wende.” Vitu vyote vinakutii, ee Bwana, vitu vyote vinakutii, unaweza kufanya ile unataka; utukumbuke sisi wote, ee Mungu Mtakatifu; na kwa mapendo yako kwa wanadamu utuhurumie.

**APOSTIKHA** *Sauti ya tatu.*

Nguvu ya mauti ilivunjwa kwa Msalaba wako Kristu Mwokozi, na udanganyifu wa Shetani uliharibiwa, basi uzao wa watu, wenye kuokolewa kwa imani, unakutolea nyimbo kila siku.

Shairi:Nitanyanyula macho yangu kwako, ee mwenye kuikaa mbinguni...

Tunakutolea shairi yetu ya mangaribi na ubani na nyimbo za kiroho: Ee Kristu Mwokozi, hurumia roho zetu.

Shairi: Utuhurumie, ee Bwana, utuhurumie, kwani tunayala na kuzarauliwa...

Ee Bwana, uwezo wa Msalaba wako ni kubwa, uliposimikwa kule Kalvario, unatawala dunia yote, uligeuza wavuvi kuwa Mitume na Wapagani kuwa wingu la Washuhuda wanaomba kwa ajili ya wokovu roho zetu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya kwanza.*

. Ee Kristu, wewe kwa mkono wako takatifu kamili uliumba mwili wa mwanadamu, kwa wema wako ulikuja kuponyesha wagonjwa; kwa neno lako uliamusha Mwenye kupooza kule ku kisima cha Kondoo; ulituliza mateso ya mwanamuke mwenye kutoka damu, uliponyesha binti wa mwanamuke mkanana; haukukataa ombi la mkubwa wa waaskari; ndio maana tunakulalamikia tukisema: Ee Bwana mwenyezi, utukufu kwako

**APOLITIKION**

Mbingu zifurahiwe, na inchi ishangilie, kwa sababu Bwana ametenda nguvu, kwa mukono wake; na kwa lufu alishinda mauti; na akawa muzaliwa wa kwanza katika wafu; akatuondosha katika tumbo la kuzimu, na akaleta ku dunia huruma kubwa.

Sasa na siku zote...**THEOTOKION**.

Bikira Mzazi-Mungu tunakuimbia, wewe mupatanishi wa wokovu juu ya ukoo wetu; katika mwili alipata Kwako, Mwana wako na Mungu wetu, alitaka kuteswa msalabani, juu ya kutukomboa ku lufu, sawa Mpenda-wanadamu.

**KUAGA**

# MU KAZI MOJA ASUBUI YA JUMA YA MWENYE KUPOOZA

*Kisha Eksapsalmos: Bwana ndiwe...Apolitikion, Thetokion.*

**KATHISMA YA KWANZA** *Sauti ya tatu.*

Kristu amefufuka katika wafu, malimbuko ya wale waliyolala; mzaliwa wa kwanza wa kiumbe, fundi wa ulimwengu wote, ndani yake alifanya upya hali ya ubinadamu iliyoharibika. Ewe mauti, hautawala tena: Ufalme wako umevunjwa na Bwana wa ulimwengu.

Ee roho yangu, wewe ni mgeni duniani, tubu, kwani uvumbi hauimbake kaburini, na juu ya zambi hakuna ukombozi; tangu sasa lalamikia Kristu Mungu wetu: Nimekosa, ee Bwana mwenyi kuvumba yengi kuwa moyoni, usinihukumu, lakini unihurumie.

Ushujaa wenu na imara yenu zilishinda uerevu wa adui; ee Mashahidi Washindaji, wenyi kustahili heshima yote, mumestahili heri ya milele; ninyi washuhuda wa Mungu kweli; ombeni kwa Bwana ili aokoe kondoo zake wenyi kumpenda Kristu.

Utukufu kwa Baba..Sasa na siku zote...**THEOTOKION**

Ee Mzazi-Mungu mbele ya neema isiyoweza kufafanishwa ya ubikira wako, mbele ya uzuri na ya nuru kimungu ya utakatifu wako, alipoogopa, Gabrieli akapaza sauti akasema: Sifa gani yenye kustahili utakatifu wako nitaweza kukutolea? Kwa jina gani kubwa nitakutaja? Sijui na imekatazwa. Na tena, nikishika amri niliyopewa, nakuimbia: Salamu, ewe Mjaliwa neema.

**KATHISMA YA MBILI** *Sauti ya tatu. Tin oreotita.*

Wale walinungunikia kuponyeshwa kwa mgonjwa Mwenye kupooza siku ya Sabato walisongwa kwa chuki, walipoozwa mwili wao wote, wakasema : “ Hairuhusu kuponyesha mutu hii siku ao kutoshika siku ya mapumzika”, hawakujua ya kwamba Wewe ni Bwana wa Sheria na mganga wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba..Sasa na siku zote...*(mara ingine)*

*Kisha tunasoma: Tukiona ufufuo wa Kristu...Zaburi 50 (51). Kanuni ya Siku Kuu na Mineon, Kontakion na Eksapostilarion ya Siku Kuu.*

## MASIFU. *Sauti ya tatu.*

Kujeni, mataifa yote, mujue nguvu ya fumbo ya ajabu; kwani Kristu Mwokozi wetu, Neno aliyekuwa katika mwanzo, alisulibiwa kwa ajili yetu, na alizikwa kwa kutaka kwake, na alifufuka katika wafu kusudi aokoe ulimwengu. Tumwabudu yeye.

Mara nyingi, wakati niliimba kwa ajili yako, nilipatikana mu hali ya zambi, na wakati kinywa yangu ilikutukuza, roho yangu ilijivuna; kwa ttoba uniadibishe mimi wote, ee Kristu Mungu wetu, unihurumie na uniokoe.

Njooni mataifa yote, tutukuze makumbusho ya Mashahidi wa Bwana, kwani walipokea kwa Kristu mbele ya Malaika na ya Wanadamu taji la washindi na wanamuomba kwa ajili ya roho zetu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya kwanza.*

Kama mufu mzima, Mwenye kupooza alipokuona akapaza sauti na kusema : Unihurumie, Bwana, maana kinywa changu kimekuwa kaburi yangu; uzima inaniletea nini? Kisima cha kondoo kinanisaidia nini? Sina na mutu wa kuniingiza ndani wakati maji yanapotikiswa; lakini nakuja kwako wewe uliye Chemchem ya maponyesho ili nipaze sauti pamoja na wote nikisema : “ Ee Bwana mwenyezi, utukufu kwako.

## APOSTIKHA *Sauti ya tatu.Megali tu Stavru su.*

Japo miujiza na ishara waliona, Wafarisayo wagonjwa wa chuki hawakusaidiki ya kwamba wewe ni Mwana wa Mungu na Bwana wa ulimwengu,wewe ambaye neno lako lilimuponyesha mutu Mwenye kupooza.

Shairi: Bwana, nitatukuza rehema yako milele, kinywa changu kitatangaza uaminifu wako

kizazi na kizazi

Wafarisayo wenye kulinda siku ya Sabato walipoona Mwenye kupooza anaponyeshwa siku ya Sabato, wakajivuna sana na wakasema, kama wanavyojuwa Sheria, ya kama haifai kuvunja siku ya Sabato kwa kuponyesha wagonjwa.

Shairi: Kwani ulisema : rehema ni ya milele; uliweka uaminifu wako mbinguni.

Kwa kutokujua ya kama Wewe ni Muumba na Bwana wa Sabato, wenye kulinda Sabato walikunungunikia sababu ya kuponyesha Mwenye kupooza siku ya Sabato, wakasema : " Hairuhusu kubeba mukeka siku ya Sabato.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*Sauti ya tano.*

Yesu alikuenda Yerusalema ku kisima cha Kondoo kinachoitwa katika kiebrania Betesaida wagonjwa wengi walikuwa wamelala katika baraza, Malaika wa Mungu alishuka mara kwa mara na kuingia katika kile kisima, akatikisa maji na waaminifu waliingia wa kwanza walipona. Kristo alipomuona mutu mumoja aliyekuwa mgonjwa muda wa siku nyingi, akamuuliza: Unataka kupona? Yule mgonjwa akamujibu: Bwana, sina na mutu wa kuniingiza katika kisima wakati maji yanapotikiswa; nimepoteza mali yangu yote kwa waganga na sikuweza kupona. Lakini mganga wa roho na wa mwili akamwambia: Simama, chukua mukeka wako na wende kutangaza duniani kote uwezo wangu na neema ya wokovu .

# MU KAZI MOJA MANGARIBI YA JUMA YA MWENYE KUPOOZA

*Elezo: Kisha : «Bwana nimekuita...» tunaimba wimbo sita; tatu ya siku Kuu na tatu ya Mineon.*

***Wimbo ya siku Kuu*** *Sauti ya kwanza. Idiomelon.*

Ee Kristu, wewe kwa mkono wako takatifu kamili uliumba mwili wa mwanadamu, kwa wema wako ulikuja kuponyesha wagonjwa; kwa neno lako uliamusha Mwenye kupooza kule ku kisima cha Kondoo; ulituliza mateso ya mwanamuke mwenye kutoka damu, uliponyesha binti wa mwanamuke mkanana; haukukataa ombi la mkubwa wa waaskari; ndio maana tunakulalamikia tukisema: Ee Bwana mwenyezi, utukufu kwako.

Kama mufu mzima, Mwenye kupooza alipokuona akapaza sauti na kusema : Unihurumie, Bwana, maana kinywa changu kimekuwa kaburi yangu; uzima inaniletea nini? Kisima cha kondoo kinanisaidia nini? Sina na mutu wa kuniingiza ndani wakati maji yanapotikiswa; lakini nakuja kwako wewe uliye Chemchem ya maponyesho ili nipaze sauti pamoja na wote nikisema: Ee Bwana mwenyezi, utukufu kwako.

***Wimbo tatu ya Mineon***

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*Sauti ya tano.*

Yesu alikuenda Yerusalema ku kisima cha Kondoo kinachoitwa katika kiebrania Betesaida wagonjwa wengi walikuwa wamelala katika baraza, Malaika wa Mungu alishuka mara kwa mara na kuingia katika kile kisima, akatikisa maji na waaminifu waliingia wa kwanza walipona. Kristo alipomuona mutu mumoja aliyekuwa mgonjwa muda wa siku nyingi, akamuuliza: Unataka kupona? Yule mgonjwa akamujibu: Bwana, sina na mutu wa kuniingiza katika kisima wakati maji yanapotikiswa; nimepoteza mali yangu yote kwa waganga na sikuweza kupona. Lakini mganga wa roho na wa mwili akamwambia: Simama, chukua mukeka wako na wende kutangaza duniani kote uwezo wangu na neema ya wokovu .

**APOSTIKHA** *Sauti ya tatu.*

Ulimwengu uliangazwa, kwa Ufufuo wako Bwana, na Paradizo tena ilifunguliwa; na kiumbe chote mukukusifu, kinakutolea nyimbo kila siku.

Shairi: Nitanyanyua macho yangu kwako, ee mwenye kuikaa mbinguni...

Uniokoe, ee Bwana Mungu wangu: Ndiwe wokovu wa Wanadamu; mawimbi ya mateso yananitikisa na nazama kwa uzito wa zambi zangu; unisaidie na mkono wako na uniongoze ku nuru ya toba, ewe Bwana mpenda-wanadamu, peke yako mwenyi huruma.

Shairi: Utuhurumie, ee Bwana, utuhurumie, kwani tunajaa na kuzarauliwa...

Ee Bwana, mashahidi wako walipotegemezwa kwa imani na kusabitishwa kwa matumaini, walipoungana katika roho na mapendo ya Msalaba, wakavunja uzulumu wa adui; walipopokea taji la milele, wanaomba pamoja na malaika wabila-mwili kwa ajili ya roho zetu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*Sauti ya mnane*.

Wagonjwa wengi walilala karibu ya Mulango ya Hekalu ya Solomoni: Katikati ya Sikukuu Yesu alikuta mutu mumoja mwenyi kupooza tangu miaka makumi tatu na munane; kwa sauti yake ya ubwana akamwambia: Unataka kupona? Mgonjwa akamujibu: Bwana, sina na mutu wa kuniingiza katika kisima wakati maji yanatikisiwa. Lakini Bwana akamwambia: Chukua mukeka wako, umeponyeshwa, tangu sasa usitende tena zambi. Kwa maombezi ya Mzazi-Mungu, ee Bwana, ututumie neema ya wokovu.

**APOLITIKION**

Mbingu zifurahiwe, na inchi ishangilie, kwa sababu Bwana ametenda nguvu, kwa mukono wake; na kwa lufu alishinda mauti; na akawa muzaliwa wa kwanza katika wafu; akatuondosha katika tumbo la kuzimu, na akaleta ku dunia huruma kubwa.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote..**THEOTOKION.**

Bikira Mzazi-Mungu tunakuimbia, wewe mupatanishi wa wokovu juu ya ukoo wetu; katika mwili alipata Kwako, Mwana wako na Mungu wetu, alitaka kuteswa msalabani, juu ya kutukomboa ku lufu, sawa Mpenda-wanadamu.

# MU KAZI MBILI ASUBUI YA JUMA YA MWENYE KUPOOZA

*Kisha Eksapsalmos: Bwana ndiwe...Apolitikion, Thetokion.*

**KATHISMA YA KWANZA** *Sauti ya tatu.*

Ee Bwana, kwa mwili wako ulionja mauti, ukaondoako uchungu kwa ufufuo wako; kwa hii ulisabitisha ubinadamu, ukaondoa ushindo uliyoazibiwa na laana ya zamani. Ewe Mlinzi wa uzima wetu, Bwana, utukufu kwako.

Ee roho yangu, mpaka wakati gani utakaa katika zambi? Mpaka wakati gani utazarau toba? Ona hali ya hukumu na lalamikia Bwana: Nimekosa, lakini uniokoe, ee Mungu wangu.

Kwa imani munaangaa kama nyota za mwanga, enyi Mashahidi Watakatifu ambao tunatukuza mashindano; bila woga mbele ya uzulumu wa wazulumu, mukamaliza kufuru ya miungu ya uwongo paka na silala ya ukweli na ushindi wa Msalaba usiyoweza kushindwa.

**THEOTOKION**

Ee Mzazi-Mungu, nguvu yetu na boma yetu, mpatanishi wa nguvu wa ulimwengu, ewe Bikira mbarikiwa katika wote, kwa maombezi yako okoa watumishi wako ku hatari yote.

**KATHISMA YA MBILI** *Sauti ya tatu. Tin oreotita*

Wale walinungunikia kuponyeshwa kwa mgonjwa Mwenye kupooza siku ya Sabato walisongwa kwa chuki, walipoozwa mwili wao wote, wakasema: Hairuhusu kuponyesha mutu hii siku ao kutoshika siku ya mapumzika, hawakujua ya kwamba Wewe ni Bwana wa Sheria na mganga wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote.*(mara mbili).*

*Kisha tunasoma: Tukiona ufufuo wa Kristu...Zaburi 50 (51). Kanuni ya Siku Kuu na Mineon, Kontakion na Eksapostilarion ya Siku Kuu.*

## MASIFU *Sauti ya tatu*

Walinzi, ee Bwana, wakaeleza maajabu yako yote; lakini baraza ya ubatili, wakijaza mukono wao wa kuume kwa zawadi, waliwaza ya kama watafuchika Ufufuo wako, uliyotukuzwa na watu. Utuhurumie. *(mara mbili).*

Ee Bwana, kusanya akili yangu yenye kutawanyika, takasa miiba ya moyo wangu, kama kwa Petro unipe toba, na kama kwa mtoza-kodi unipe pumuzi, kama kahaba unipe machozi ili nikupazie sauti: Uniokoe, ee Mungu wangu, mpenda-wanadamu, peke yako mwenyi huruma.

Maaskari wa Kristu walivunja woga wote mbele ya wafalme na wazulumu na uhodari kubwa walimuungama Bwana wa ulimwengu, Mungu na Mfalme wetu, na sasa wanaombea roho zetu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*Sauti ya mnane.*

Bwana, apana kisima cha Kondoo kilimuponyesha Mwenye kupooza, lakini ni neno lako lilimufanya kuwa mutu mupya; apana magonjwa yake ya miaka mingi ilimuzuia kupona, ni uwezo wa msalaba wako ulishinda hii ugonjwa; Mwenye kupooza alitupa mzigo wake mzito, akachukua mukeka wake sababu ya kushuhudia rehema yako. Bwana, utukufu kwako.

**APOSTIKHA** *Sauti ya tatu. Megali tu Stavru su.*

Ee Neno mwenye kuleta kuzima, kwa viungo vyenye kupooza neno lako ni lenyi kuponyesha na kuleta uzima; mushuhuda ni Mwenye kupooza aliyechukua mukeka wake na matumaini kwa amri yako, yeye aliyelala bila nguvu tangu miaka mingi.

Shairi: Bwana,nitatukuza rehema yako milele, kinywa changu kitatangaza uaminifu wako kizazi na kizazi.

Ee Bwana mwenyezi, Mwenye kupooza alifwata na furaha ile amri ulimuamuru; alipochukua mukeka wake akasimama na kutembea na akatoa ushuhuda akasema : : " Natimiza mapenzi ya Huyu aliniponyesha.

Shairi: Kwani ulisema : rehema ni ya milele; uliweka uaminifu wako mbinguni.

Huyu ambaye tangu miaka mingi mwili wake ulipoozwa na kuhangaika alipaza sauti na kusema: Unihurumie, ee Mukombozi; Kristu Mwokozi alimuokoa na alimwambia abebe mukeka wake.

Utukufu kwa Baba… Sasa na siku zote… *Sauti ya tano*

Bwana, karibu ya kisima cha Kondoo kulilala mutu mumoja mwenyi kupooza, alipokuona, akapaza sauti na kusema: Sina na mutu wa kuniingiza katika kisima wakati maji yanapotikiswa; ninapojaribu kuingia katika maji mutu mwingine anaingia mbele yangu na anapona, mimi nabaki mwenyi kupooza. Mwokozi akamuhurumia na akamwambia palepale: Kwa ajili yako nimejifanya mutu, kwa ajili yako nilichukua mwili, unasema hauna na mutu wa kukusaidia? Chukua mukeka wako, nakuamuru wende. Vitu vyote vinakutii, ee Bwana, vitu vyote vinakutii, unaweza kufanya ile unataka; utukumbuke sisi wote, ee Mungu Mtakatifu; na kwa mapendo yako kwa wanadamu utuhurumie.

# MU KAZI TATU SIKU KUU YA KATI YA PENTIKOSTI

*Kisha Proimiakos tunaimba: «Bwana nimekutia...» na tunaimba wimbo tatu ya kuimba kila moja mara mbili.*

*Sauti ya ine. Kirie anelthon en to Stavro.*

Tazama nusu ya sikukuu inaanza na Ufufuo wa Mwokozi na inamalizika na Sikukuu ya Pentikosti, yote mbili inaungana, inangaa na nuru yao mbili na inatukuzwa kwa kutangulia sikukuu ya Kupanda kwa Mwokozi mbinguni.

Sayuni inasikiliza na kufurahi, kwa sababu Kupanda kwa Kristu mbinguni kumetangaziwa; wana wake waaminifu wanashangilia na furaha; inapoona damu ya Kristu kusafishwa na Roho Mtakatifu, Kanisa inajitayarisha kutukuza kama inavyostahili sehemu ya furaha ya hii sikukuu takatifu mbili.

Tazama Roho Mtakatifu anashukia mwanadamu wote kama alivyoandika Nabii Yoeli; tazama Sikukuu iliyotangulia kuwekwa imefika katikati yake, kwani kisha kufa kwake, kuzikwa kwake na Kufufuka kwake, bila uongo Kristu aliwahidi Wafwasi wake kuwatumia Mfariji.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*Sauti ya sita.*

Ee Kristu, tunapofika katikati ya Ufufuo wako na kuja kwa Roho wako Mtakatifu, wote pamoja tunatukuza miujiza ya ajabu ambayo fumbo imefunuliwa kwetu, na tunapojaa na woga tunakuomba: Ututumie neema ya wokovu.

**KUINGIA**. Mwangaza upole (ilaron)

**Unabii ya Nabii Mika tutasoma (4,2. 6,2. 5,4)**

Bwana anasema hivi: Kwa maana katika Sayuni sheria itatoka, na neno la Bwana toka Yerusalema. Naye atahukumu kati ya mataifa mengi, na atahamakia makabila ya nguvu ya mbali, nao watafua panga zao kuwa majembe, na mikuki yao kuwa miundu; taifa halitanyanyua upanga juu ya taifa, wala hawatajifundisha kupiga vita tena.Sikieni, ee ninyi milima mashindano ya Bwana, na ninyi misingi imara ya dunia, kwa maana Bwana ana mashindano pamoja na watu wake, na atasihi Israeli. Ee watu wangu, nimewafanyia ninyi nini? Na kwa njia gani nimewachokesha ninyi? Unishuhudie. Kwa sababu niliwapandisha ninyi toka inchi ya Misri, niliwakomboa ninyi toka nyumba ya utumwa, na nimetuma mbele yenu Musa, Haruni na Miriamu.Amekuonyesha, ee mutu, nini ni njema, na Bwana anataka nini kwako ila kutenda haki, na kupenda rehem,a na kutembea kwa unyenyekevu na Mungu wako? Kwa sababu hii atawatoa hata wakati wa kuzaa kwake aliye na uchungu, kisha mabaki ya ndugu zake yatarudi kwa wana wa Israeli. Naye atasimama na atakulisha kundi lake kwa nguvu za Bwana kwa enzi ya jina la Bwana Mungu wake, na watakaa, kwa maana sasa atakuwa makubwa hata miisho ya dunia.

**Unabii ya Nabii Isaya tutasoma (55,1-13)**

Haya, kila mutu anayeona kiu, muje kwa maji, naye asiye na feza; muje, mununue na mule; ndiyo, muje, mununue mvinyo na maziwa, pasipo feza na pasipo bei! Kwa nini munatoa feza kwa ajili ya kitu kisicho chakula? Na kazi yenu kwa kitu kisichoshibisha? Munisikilize sana sana, na mule kilicho chema, na nafsi zenu zifurahi katika unono. Tegeni masikio yenu, na muje kwangu; Sikieni, na nafsi zenu zitaishi. Nami nitafanya nanyi agano la milele. Maneno matakatifu ya Daudi yaliyo ya imani. Tazameni nimemuweka kwa mushuhuda kwa watu, mukubwa na jemadari wa watu. Tazama, utaita taifa usilolijua, na taifa lisilokujua litakukimbilia, kwa sababu ya Bwana Mungu wako, na Mutakatifu wa Israeli; maana amekutukuza. Mutafute Bwana angali anaweza kupatikana, mumwitie angali yeye ni karibu; mutu mubaya aache njia yake na mutu asiye haki aache mafikili yake; Na arudi kwa Bwana, naye atamurehemu; na kwa Mungu wetu, naye atamusamehe kabisa kabisa. Maana mafikili yangu si mafikili yenu, wala njia zenu si njia zangu, Bwana anasema. Kwa maana kama vile mbingu ni juu sana kuliko dunia, hivi njia zangu ni juu sana kuliko njia zenu, na mafikili yangu juu kuliko mafikili yenu. Maana kama vile mvua inavyoshuka, na theluji kutoka mbinguni, na hairudi kule; lakini inakunywesha udongo, na kuuzalisha na kuuchipuza, umupe mupandaji mbegu, na mukulaji chakula; ndivyo litavyokuwa neno langu linalotoka kwa kinywa changu: Halitarudi bule, lakini litafanya linalonipendeza litasitawi katika yale niliyolituma. Maana mutatoka kwa furaha, na mutaongozwa kwa salama; Mbele yenu milima ni vilima vitatoa nyimbo; na miti yote ya inchi itapiga mikono. Pahali pa miiba musunobari utatoa, na pahali pa mibigili, muhadesi; litakuwa kwa Bwana kwa jina, litakuwa alama ya milele isiyokatiliwa mbali.

**Somo ya Mezali tutasoma (9,1-11)**

Hekima amejenga nyumba yake, amechonga nguzo zake saba: Ameua nyama zake, amechanganya mvinyo yake, ametandika meza yake. Ametuma vijakazi wake, analia juu ya pahali pa juu pa muji. Mujinga ye yote ageuke na kuingia hapa: Naye asiye na ufahamu, anamwambia: Kuja ule wa mukate wangu, na kunywa ya mvinyo niliyochanganya. Ninyi wajinga, acheni ujinga, mupate kuishi; na mutembee katika njia ya ufahamu. Yeye anayekemea mwenye kuzarau anajipatia haya: Naye anayeonya mutu mwovu anajipatia kipaku. Usionye mwenye kuzarau, asikuchukie: Kemea mwenye hekima, naye atakupenda. Fundisha mwenye hekima, naye atakupenda. Fundisha mwenye hekima, naye atazidi kuwa na hekima: Fundisha mwenye haki, naye atazidi kuwa na elimu. Woga wa Bwana ni mwanzo wa hekima: Na kujua Mutakatifu ni ufahamu. Maana kwa njia yangu siku zako zitazidishwa na miaka ya maisha yako itaongezwa.

**APOSTIKHA** *Sauti ya kwanza. Idiomelao.*

Tazama katikati ya Siku makumi tano Kristo, kisha kufunua ubwana wa umungu wake, aliponyesha Mwenye kupooza na kwa neno lake alimuamusha toka mukeka wake; alipotenda maajabu katika mwili wa mutu aliwapa wanadamu uzima wa milele na neema ya wokovu.

Shairi: Kumbuka watu wako uliriti tangu mwanzo, wale ulikomboa kama kabila ya uriti wako.

Ee Hekima ya Mungu, katikati ya Sikukuu uliingia ndani ya Hekalu kufundisha, ukawavua Waandishi na Wafarisayo, ukawaambia na uwezo wote: Huyu aliye na kiu aje kwangu na anywe maji ya uzima na hatakuwa na kiu tena; akiniamini mimi mito ya maji ya uzima yatatoka ndani yake. Ewe Wema kubwa, ewe rehema ya milele, Kristu Mungu wetu, utukufu kwako.

Shairi: Mungu ni Mfalme wetu tangu milele, ametenda wokovu duniani.

Katikati ya Sikukuu Yesu alienda ku Hekalu na akanza kufundisha akawaambia Wayuda Huyu aliye na kiu aje kwangu na anywe maji ya uzima wa milele na hatakuwa na kiu tena; huyu mwenyi kuniamini mimi, kama inavyosema Maandiko: Mito ya kaji yatatoka ndani yake na atakuwa na nuru na uzima.

Utukufu kwa Baba… Sasa na siku zote… *Sauti ya mnane*

Mwokozi, katikati ya Sikukuu wakati ulipofundisha, Waandishi wakaulizana wakisema : Wapi anafahamia Maandiko, yeye hakufunza? Kwa sababu wao wenyewe hawakujuwa ya kama Wewe ni Hekima yenye kuumba ulimwengu. Bwana, utukufu kwako.

**APOLITIKION** *Sauti ya mnane*

Katikati ya Sikukuu ondosha kiu ya roho yangu, kwani uliwaambia watu wote ya kama : Huyu aliye na kiu aje kwangu na anywe! Ee Chemchem ya uzima, Kristu Mungu wetu, utukufu kwako.*(mara tatu).*

## IBADA YA MU KAZI TATU ASUBUI

*Elezo: Kisha Eksapsalmos, «Bwana ndiwe...», Apolitikion na Theotokion ya Siku Kuu, tunaimba:*

**KATHISMA YA KWANZA** *Sauti ya inne. Takhi prokataleve.*

Ndani ya Hekalu Huyu mwenyi kujua siri za mioyo yote aliwaambia wadanganyifu ukweli akasema: Sababu gani munatafuta kuniuwa mimi chemchem ya uzima? Na kwa uhodari katikati ya sikukuu akawaambia: Musihukumu bila haki, ninyi waamzi wabaya.

Utukufu kwa Baba… Sasa na siku zote*…(mara mbili)*

**KATHISMA YA MBILI** *Sauti ya tano. Ton sinanarkhon Logon.*

Katikati ya Sikukuu ya Siku makumi tano Bwana wa ulimwengu alisimama ndani ya Hekalu, akawafundisha Wayuda, Waandishi na Wafarisayo, na sawa Mfalme na Mungu aliwalaumu hawa wa mwisho sababu ya nguvu ya uzulumu wao. Lakini kwa mapendo yake anatupatia sisi wote neema ya wokovu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*(mara mbili).*

*Kisha tunasoma: Tukiona ufufuo wa Kristu...Zaburi 50 (51). Kanuni ya Siku Kuu na Mineon.*

**KANUNI YA SIKU KUU**

**WIMBO YA KWANZA,** *Sauti ya ine.*

**IRMOS:** Wakati alipovuka pakavu zimu ya Bahari nyekundu, Israeli wa zamani alifukuza jangwani nguvu ya Amaleki kwa mikono ya Musa aliyopanua kwa alama ya msalaba.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Bwana, mema kubwa ya umwilisho wako takatifu wenyi kupita ufahamu yanangaa juu yetu, yanaleta vipaji kubwa kama chemchem ya neema na ya nuru ya Mungu.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Ee Kristu, ulionekana katikakati ya sikukuu yenyi kuangaa, ulionyesha nuru ya Mungu, na wewe mwenyewe uko sikukuu ya furaha ya watu wenye kuokolewa, wewe mwenye kutuletea wokovu.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Ee Bwana, ulipotoka kwa Mungu, kwa ajili yetu uko hekima, utakatifu na ukombozi, unatuchukuwa toka dunia mpaka juu mbinguni, na unatupatia zawadi ya Roho Mtakatifu.

Mtakatifu kamili, ee mzazi-Mungu, utuokoe. **THEOTOKION.**

Bwana, Mwili wako haikuharibika na uvumbi wa kaburi; ilifanyika bila mbegu na ilikaa bila kuharibika, inapita dunia na sheria zake.

**WIMBO WA TATU**. *Sauti ya ine.*

**IRMOS:** Ee Kristu, Kanisa yako inashangilia ndani yako na inakulalamikia ikisema: Bwana, uko nguvu yangu, makimbilio yangu na tegemeo yangu.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Ee Mungu wa mapendo, ulifungulia Kanisa chemchem ya maji ya uzima wakati uliposema: Huyu aliye na kiu aje kwangu anywe maji na furaha!

Utukufu kwa Baba…

Ulipofunua Kupanda kwako toka dunia mpaka mbinguni, uliahidi kutuma toka mbinguni Roho wako Mtakatifu.

Sasa na siku zote… **THEOTOKION**

Kwa mapendo yake, Bwana mwenye kuleta uzima aliyejifanya mutu kwa Bikira alileta kwa kila mwaminifu uzima wa milele.

**KATHISMA**. *Sauti ya mnane. Tin Sofian ke Logon.*

Ndani ya Hekalu na sikukuu ilipofika katikati yake, ulipaza sauti na kusema: Huyu aliye na kiu aje kwangu na anywe, maana kwa kunywa hii maji takatifu ndani yake mutatoka mitoni ya mafundisho yangu; pamoja nami atatukuzwa huyu atanitambua kuwa mjumbe wa Baba Mtakatifu. Ndio maana tunakulalamikia tukisema: Utukufu kwako, ee Kristo Mungu wetu uliyewamwangia watumishi wako maji mengi ya mapendo yako kwa wanadamu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...

Ulipoletea dunia chemchem ya hekima na ya uzima, unaalika wanadamu kushota maji ya wokovu, kwani huyu mwenyi kupokea Sheria yako takatifu ndani yake anazima moto ya udanganyifu; hatakuwa tena na kiu milele na hatakosa mema yako, ee Bwana na Mfalme wa mbinguni. Ndio maana tunatukuza uwezo wako, ee Kristu Mungu wetu; tunakuomba, uzime makosa yetu na uwape watumishi wako neema mingi ya wokovu.

**KONTAKION.** *Sauti ya ine.*

Ee Muumba na Bwana wa ulimwengu, Kristu Mungu wetu katikati ya sikukuu iliyoamuriwa na Sheria,uliwaambia wale waliokuzunguka: Kujeni mushote maji ya uzima wa milele. Ndio maana tunasujudu mbele yako na kupaza sauti na imani na tunasema: Utupe rehema yako, maana wewe ni Chemchem ya uzima wetu.

**IKOS**

Ee Neno wa Mungu, mwanga damu yako juu ya roho yangu isiyozaa matunda sababu ya zambi kusudi izae matunda ya fazila; kwani uliwaambia watu wote waje kwako kushota maji ya uzima wa milele yenyi kusafisha zambi za wale wenyi kutukuza Ufufuo wako tukufu na takatifu; ee Mungu wa wema, uko na nguvu ya Roho Mtakatifu aliyewashukia kweli Wafwasi wako wenyi kujua umungu wako, kwa sababu Wewe ni Chemchem ya uzima wetu.

**SINAKSARI**

Mu Kazi Tatu ya Mwenye kupooza tunashangilia Siku kuu ya Kati ya Pentikosti.

Katikati ya siku kuu Kristu aliwafundisha waalimu waliotaka kumukamata.

Kwa rehema yako ya milele, ee Kristu Mungu wetu, utuhurumie. Amin.

**KATAVASIA.** *Sauti ya mnane.*

Ee Bwana, uligandamisha bahari, ukazamisha Farao na gari zake, uliokoa watu wako kwa kuwavukisha pakavu, uliongoza ku mlima wa utakatifu wale walisema: Tumuimbie Mungu "wetu wimbo wa ushindi sawa mshindi wa vita.

Roho yangu inasabitishwa katika Bwana, nguvu yangu inashangilia ndani ya Mungu wangu, kinywa changu kinafunguka mbele ya addui zangu : maanawokovu wako inanichezesha na "furaha.

Bwana, kwa ono lake nabii Habakukialitangulia kusema kuja kwako, ni kwa hii alisema: Bwana amekuja toka Themani. Utukufu kwa mapendo yako ya milele, ee Kristu.

Bwana Mungu wetu, utupe amani, Bwana Mungu wetu, utulinde; hatujui mungu mwingine ila wewe peke yako, ni jina lako tunaomba, ee Bwana.

Nazama ndani ya mawimbi ya hii uzima kama ndani ya mawimbi ya bahari, na kama Yona, ee Neno, nakulalamikia: Bwana wa mapendo, ondoa uzima kuzimuni.

Ee Mungu msaada, tanuru ya moto ya Wakaldei ilifunikwa na umande kwa Roho Mtakatifu na Vijana walipaza sauti na kusema: Mungu wa baba zetu, umetukuzwa.

Tumwihimidi, tunamutukuza na tumamsujudu Bwana.

Ni kwa ninyi Malaika mbinguni kumutukuza, kumuimbia na kumusifu milele Huyu mwenyi kutawala na utukufu na kutukuzwa kama Mungu.

**WIMBO YA TISA.** *Sauti ya ine*

Ee Bikira, Kristu aliye jiwe la pembe ambaye mkono hata mumoja wa mwanadamu haikuchonga, wewe ulimuchonga, ewe mlima haramu; ni yeye mwenyi kuunganisha hali zenye kutengana: Ndio maana, tunapojaa na sherehe na furaha, ee Mzazi-Mungu, tunakutukuza wewe.

Utukufu kwako, ee Mungtu wetu, utukufu kwako.

Kwa Kristu tulifundishwa namuna ingine mupya ya uzima: kwa moyo wote tufanye haraka kuishika mpaka mwisho sababu ya kupokea Kuja kwa Roho Mtakatifu.

Utukufu kwako, ee Mungtu wetu, utukufu kwako.

Ee Chemchem ya uzima, hali ya kufa nilichukuwa ndani yangu uliivika uzima wa milele, na neema ya kutoharibika, ee Mwokozi, uliifufua pamoja nawe na uliipeleka kwa Baba sababu ya kupata amani.

Utukufu kwa Baba…

Tunapoitwa mara ingine ku uzima wa mbinguni kwa msaada wa uwezo wa huyu aliyejishusha mpaka ku hali ya mtumwa sababu ya kutuinua mpaka kwake, ni haki kweli sisi kumutukuza.

Sasa na siku zote**…** **THEOTOKION.**

Sisi wote, waaminifu, tunasadiki ya kama wewe ni kisa, ni shina, na chemchem huko alitoka huyu mwenye kutupatia uzima wa milele; na kwa nyimbo zetu tunakutukuza, kwani ulichanusha Bwana aliye Uzima wetu.

**Katavasia ya tisa:** Ubikira ni ajabu kwa wamama wazazi, kuzaa ni ajabu kwa mabikira; lakini ndani yako, ee Mzazi-Mungu, hii maajabu mbili yanaungana, vizazi vyote vya mataifa vinakutukuza.

## EKSAPOSTILARION *Sauti ya tatu. O uranon tis astris.*

Wewe uliye na kisima cha zawadi nyingi unipe nishote maji ya maondoleo ya zambi zangu, maana nateswa na kiu, peke yako Bwana wa mapendo na wa huruma.*(mara mbili)*

## MASIFU *Sauti ya ine. Os geneon en martisin.*

Hekima, uwezo wa Baba na nuru yake, Neno wa milele tena Mwana wa Mungu alikuja ku Hekalu mwilini akanza kuwafundisha watu waliosema na kushangaa ufahamu wake kubwa: Namna gani anajua Maandiko, yeye hakufunza? *(mara mbili).*

Aliponyamazisha Waandishi na Wafarisayo, Bwana na Masiya akawaambia: Musihukumu kwa inje kama Waamzi wasio na sheria; niliponyesha mutu Mwenye kupooza siku ya Sabato kwa sababu mimi ni Bwana wa Sabato na wa Sheria; sababu gani munatafuta kuniuwa, mimi mwenyi kufufua wafu?

Watu wasiyo na shukrani, wasiyo na haki na waovu walimutupia Musa mawe na kumukatakata Isaya, walimutupa Yeremia mwenye haki ndani ya matope, na walimusulubisha Bwana juu ya msalaba wakiseema: Wewe mwenye kubomoa Hekalu, ujiokoe wewe mwenyewe na tutakuamini.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*Sauti ya ine.*

Ndugu, tunapoangazwa kwa Ufufuo wa Mwokozi Yesu Kristu, tunapofika katikati ya sikukuu ya Bwana, tushike na hekima mafundisho ya Mungu kusudi tuweze kushangilia tena Kupanda kwake mbinguni na kuja kwa Roho Mtakatifu.

# MU KAZI TATU MANGARIBI YA MWENYE KUPOOZA

*Elezo: Kisha Proimiakos, tunaimnba «Bwana nimekuita...» na wimbo sita; tatu ya Siku Kuu na tatu ya Mineon.*

***Wimbo ya siku Kuu***

*Sauti ya ine. O eks ipsistu klithis.*

Ee Kristu, ulipoharibu ufalme wa mauti kwa lufu yako, uliwapa wanadamu uzima kwa Ufufuo wako tukufu; na kwa kushuka kwako kuzimuni ulifufua wanadamu pamoja nawe; ndio maana kwa shukrani tunatukuza sifa yako katika hii sikukuu tunashangilia Ufufuo wako wa nuru siku ya tatu ambao tumekwisha kumaliza nusu katika nuru yenyi kuangaa toka kwako, ee Yesu Chemchem ya uzima na Mfazili wa roho zetu.

Bwana mwenyezi, mbele ya Mateso yako takatifu msalabani ulifanya miujiza ya uwezo kwa ajili ya watu : Kama inavyoandikwa, katikati ya Sikukuu ulipaza sauti na kusema : “ Huyu aliye na kiu aje kwangu, ashote maji takatifu na ya uzima, kwa sababu nawapa wote maji ya hekima, ya uwezo na ya uzima, mimi nilipenda kufanana na wanadamu kwa mapendo yangu juu yao.

Bwana mwenyi huruma, kwa zambi nimepoozwa katika kitanda cha uchungu, siwezi kutikisa viungo; lakini wewe kwa mapendo yako ya milele ulijifanya mutu kwa kutaka kwako, kama Mwenye kupooza, uniamushushe na kuniongoza katika mafundisho yako takatifu, ee Mwokozi ambaye mbele ya Mateso yako uliwaonyesha watu miujiza mingi, Wewe Mungu uliyeteswa mwilini kwa kutaka kwako.

***Wimbo ya Mineon tatu***

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*Sauti ya mbili.*

Ee Kristu Mungu wetu, wakati ulipokuja ndani ya Hekalu, katikati ya Sikukuu ulifundisha makutano ukasema: Huyu mwenye kuniamini mimi, hata akifa, ataishi! Lakini Wafarisayo, Wasadukayo na Waandishi wakanungunika na wakasema: Ni nani huyu anayekufuru hivi Mungu? Hawakuwazia ya kama uko kweli Mungu wa milele yote mwenyi kutukuzwa pamoja na Baba na Roho Mtakatifu. Bwana Mungu wetu, utukufu kwako.

## APOSTIKHA *Sauti ya tatu.*

Kwa mateso yako, ee Kristu, ulileta giza ku jua, kwa nuru ya Ufufuo wako, ulifurahisha ulimwengu, pokea wimbo wetu wa mangaribi, ewe Mpenda-wanadamu.

Shairi: Habari yao ilisikilika duniani kote,neno lao mpaka ku mwisho wa dunia.

Sauti yenu ilisikika duniani kote, enyi Mitume Watakatifu, mulivunja miungu ya uwongo na kukatangaza maarifa ya Mungu wa kweli, mukashindana hivi vema, enyi wenyi heri tunaoimbia na kutukuza makumbusho.

Shairi: Mungu ni wa ajabu katika Watakatifu wake, Mungu wa Israeli.

Bwana, Mashahidi wako waliposabitishwa kwa imani na matumaini, walipokuwa mu umoja katika roho kwa mapendo ya Msalaba wako, waliharibu uzulumu wa Adui; walipopokea taji ya uzima wa milele,wanaombea pamoja na Malaika roho zetu wokovu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*Sauti ya tatu.*

Katikati ya Sikukuu tunatukuza huyu alileta wokovu duniani; Kristu Uzima wetu alitundikwa msalabani katikati ya wanyanganyi wawili; kwa matusi ya wa kwanza alinyamaza, lakini kwa huyu

alimuamini akamwambia: Leo hii utakuwa pamoja nami katika Paradizo!" Kisha, Kristo alishuka kaburini na akanyanganya Hadeze, siku ya tatu alifufuka sababu ya kuleta wokovu rohoni mwetu.

**Apolitikion ya Siku Kuu ya kati ya Pentikosti.**

# MU KAZI INE ASUBUI YA JUMA YA MWENYE KUPOOZA

*Kisha Eksapsalmos: Bwana ndiwe...Apolitikion, Thetokion.*

**KATHISMA YA KWANZA** *Sauti ya tatu.Tin oreotita*

Ee Bwana, mbele ya hali imara ya umungu wako, mbele ya mateso ya kutaka uliyoteswa, ilipoogopa, Hadeze ikalia juu ya bahati yake, ikalalamika: Naogopa sana mwili wako usiyoharibika; naona msiyeonekana akinigombanisha na akili; na wale ninaofunga nawasikia wakilalamika: Utukufu ku ufufuo wako takatifu, ee Kristu Mungu wetu.

Ee Bwana, uliangaza makumbusho ya Mitume wako, uliwapa nguvu ya kufafanisha Mateso yako; walishinda bora nguvu ya shetani na wakapokea kipaji cha kuponyesha; kwa maombezi yao, ee Bwana, leta amani duniani.

Kwa imani munaangaa kama nyota za mwanga, enyi Mashahidi Watakatifu ambao tunatukuza mashindano; bila woga mbele ya uzulumu wa wazulumu, mukamaliza kufuru ya miungu ya uwongo paka na silala ya ukweli na ushindi wa Msalaba usiyoweza kushindwa.

**THEOTOKION**

Ndiwe kiti cha zahabu cha Mfalme wetu, ee Bikira safi kamili, Paradizo yenyi kujaa na maua; kwa neema yako unatumimina manukato mazuri, kwa sababu ni Mungu yeye mwenyewe ulichukua tumboni mwako; tunatangaza ukweli wa umama wako takatifu na tunakutukuza daima.

**KATHISMA YA MBILI.** *Sauti ya mnane. Tin sofian ke Logon.*

Ndani ya Hekalu na Sikukuu ilipofika katikati yake, ulipaza sauti na kusema: Huyu aliye na kiu aje kwangu na anywe; kwa maana kwa kunywa hii maji takatifu ndani yake mutatoka mito ya mafundisho yangu; pamoja nami atatukuzwa huyu atanitambua kuwa mjumbe wa Baba Mtakatifu. Ndio maana tunakulalamikia tukisema: Utukufu kwako, ee Kristo Mungu wetu uliyewamwangia watumishi wako maji mengi ya mapendo yako kwa wanadamu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*(mara mbili).*

*Kisha tunasoma:* Tukiona ufufuo wa Kristu...*Zaburi 50 (51). Kanuni ya Siku Kuu na Mineon.Kontakion na Eksapostilarion ya Siku Kuu.*

## MASIFU *Sauti ya tatu.*

Katika mwangaza yako, ee Rabi Mpenda-wanadamu, tutaona mwangaza; kwa sababu ulifufuka katika wafu, ukitoa wokovu kwa uzao wa watu, kusudi viumbe vyote vikusifu, uliye peke Msiye-zambi. Utuhurumie.*(mara mbili).*

Ee Mitume Watakatifu, mulichunga bila kosa mafundisho ya Kristu; muliipokea bila kulipa na mukaipokesha na mapendo, mukiponyesha mateso ya roho zetu na ya miili yetu, na kwa deni munayo kwa Mungu mutuombee ili roho zetu ziokolewe.

Kama nyota, munaangaza ulimwengu hata kufa kwenu, ee mashahidi Watakatifu; muliposhindana vema zaidi, muna uwezo wa kumuomba Kristu ili alete neema ya wokovu ku roho zetu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*Sauti ya ine.*

Bwana, mbele ya Kusulubiwa kwako takatifu, Sikukuu ilipofika katikati yake, ulipanda kwenda ku Hekalu sababu ya kufundisha na uwezo ile wewe mwenyewe uliongoza katika Sheria ya Musa; na adui zako, ee Kristo, walipoogopa kwa fumbo ya ndani ya hekima yako, ee Bwana, kwa chuki wakafanya shauri juu yako na wakaulizana: Namna gani huyu anajua Maandiko bila kuyanfuza? Kwa sababu hawakujua ya kuwa Wewe ni Mwokozi wa roho zetu.

## APOSTIKHA *Sauti ya mbil. Ikos tu Efratha*

Wewe ni mkubwa, ee Mfalme wangu, na unapojaa na ukubwa wako : ulijishusha sana sababu ya kujaza ulimwengu na mema yako mengi.

Shairi: Kumbuka watu wako ulipata tangu mwanzo, wale ulikomboa kama kabila la uriti wako.

Uliingia ndani ya Hekalu katikati ya Sikukuu, ndani yako mukatoka mito ya maji ya uzima sababu ya kunywisha wale walio na kiu ya neema yako takatifu, ee Bwana.

Shairi: Mungu ni Mfalme wetu tangu milele, ulitimiza wokovu duniani.

Ni ajabu, ulipotaka kuniokoa, ulijifanya mutu kwa Bikira asiyeolewa; ndani ya Hekalu ulimwangia roho yangu neema ya wokovu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*Sauti ya mnane*.

Bwana, katikati ya sikukuu mbele ya Mateso yako na ya Ufufuo wako tukufu, ulifundisha ndani ya Hekalu, uliwaambia Waandishi na Wafarisayo hivi: Huyu aliye na kiu aje kwangu na anywe! Huyu anayeniamini mimi ndani yake mutatoka mito ya maji ya uzima yenyi kutakaswa kwa Roho Mtakatifu. Ee Hekima isiyokadirika na uwezo wa Mungu, wewe mwenye kujaza ulimwengu, Bwana, utukufu kwako.

# MU KAZI INE MANGARIBI YA JUMA YA MWENYE KUPOOZA

*Elezo: Kisha Proimiakos, tunaimnba «Bwana nimekuita...» na wimbo sita; tatu ya Siku Kuu na tatu ya Mineon.*

***Wimbo ya Siku Kuu***

*Sauti ya tano. Kheris askitikon*

Leo, kama saa ya kusini inavyogawanya siku kwa sehemu mbili, Mesopentikosti inaonekana kwa neema yake na kwa nuru yake katikati ya hii wakati tunashangilia Ufufuo wa Mwokozi; inapoeneza nuru ya Kristu aliyefufuka, inaonyesha alama za uzima wa milele na inatangulia kutuonyesha Kupanda kwake mbinguni; inatangaza kuja kwa Roho Mtakatifu na Sikukuu ya nuru ya Pentikosti, inaleta amani na neema ya wokovu rohoni mwetu.

Katikati ya Sikukuu Bwana anatupa sisi wote maji ya mapendo yake kama mutoni wa utukufu takatifu akisema: Muje, ninyi mulio na kiu, na shoteni. Kwa sababu Yeye ni chemchem ya huruma na bahari ya rehema, anatirikizia wanadamu maondoleo ya zambi; anasafisha zambi, anatakasa wagonjwa, anaokoa wale wenye kushangilia Ufufuo wake, analinda wenye kupenda Kupanda kwake tukufu mbinguni, analeta amani na neema ya wokovu rohoni mwetu.

Bwana ambaye makao hata moja haiwezi kumuzunguka alisimama katikati ya Hekalu kwa sababu Yeye ni Mungu, japo alijifanya mutu kwa ajili yetu, alionekana kwa nyakati katika mwili; na anawamwangia watu wote maji ya uzima ya neno lake akisema: Muje, takaseni mioyo yenu, tulizeni roho yenu sababu ya kivukutu cha mateso; hata mumoja asikose kunywa! Maji ninayoleta ni neema ya Mungu, ni nzuri na inaleta uzima wa milele; huyu anayeikunywa ataweza kutawala pamoja na mimi Muumba wake katika ufalme na utukufu wa Mungu.

***Wimbo tatu ya Mineon***

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*Sauti ya sita*.

Ee Kristu, tunapofika katikati ya Ufufuo wako na Kuja kwa Roho wako Mtakatifu, wote pamoja tunatukuza miujiza ya ajabu ambayo fumbo imefunuliwa kwetu, na tunapojaa na woga tunakuomba: Ututumie neema ya wokovu.

**APOSTIKHA** *Sauti ya tatu.*

Muti uliyokataziwa ukazaa mauti duniani, mti wa Msalaba ukatoa uzima wa milele; tunakuabudu tena, ee Bwana, msulubiwa; nuru ya uso wako ituangazie, ee Mwokozi.

Nguvu ya mauti ilivunjwa kwa Msalaba wako Kristu Mwokozi, na udanganyifu wa Shetani uliharibiwa, basi uzao wa watu, wenye kuokolewa kwa imani, unakutolea nyimbo kila siku.

Nguvu ya mashahidi ni kubwa sana: Wanapolala kaburini, wanafukuza pepo za uovu; walishinda nguvu ya adui waliposhindania imani katika Utatu Mtakatifu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*Sauti ya mnane.*

Bwana, katikati ya sikukuu mbele ya Mateso yako na ya Ufufuo wako tukufu, ulifundisha ndani ya Hekalu, uliwaambia Waandishi na Wafarisayo hivi: Huyu aliye na kiu aje kwangu na anywe! Huyu anayeniamini mimi ndani yake mutatoka mito ya maji ya uzima yenyi kutakaswa kwa Roho Mtakatifu. Ee Hekima isiyokadirika na uwezo wa Mungu, wewe mwenye kujaza ulimwengu, Bwana, utukufu kwako.

# MU KAZI TANO ASUBUI YA JUMA YA MWENYE KUPOOZA

*Kisha Eksapsalmos: Bwana ndiwe...Apolitikion, Thetokion.*

**KATHISMA YA KWANZA** *Sauti ya tatu. Tin oreotita.*

Ulipochagua kufa Msalabani, ukaupanda moyoni mwa viumbe; kwa kutuokoa ukakubali mwili wako upigiliwe Msalabani, alafau jua likaficha miangaza yake; ni hii aliyoona munyanganyi akakutambua kama Mungu na kwa imani yake akaingia Paradizoni wakati alipokulalamikia: Ee Bwana, unikumbuke katika ufalme wako.

Sisi waamini tunatangaza fumbo isiyokadirika wakati tunapotazama kusulubiwa kwako ambako mtu hata mmoja hawezi kusikia na ufufuo wako ambao mtu hata mmoja hawezi kueleza: Kwa hii siku mauti na Hadeze zimenyanganywa, ubinadamu umevaa umilete; na kwa ushukuru tunaweza kuimba: Utukufu ku ufufuo wako Takatifu, ee Kristu Mungu wetu.

Ushujaa wenu na imara yenu zilishinda uerevu wa adui; ee Mashahidi Washindaji, wenyi kustahili heshima yote, mumestahili heri ya milele; ninyi washuhuda wa Mungu kweli; ombeni kwa Bwana ili aokoe kondoo zake wenyi kumpenda Kristu.

**STAYROTHEOTOKION**

Tuna Msalaba wa Mwana wako kama fimbo ya nguvu, ee Mzazi-Mungu; katika hii tunashusha majivuno ya adui, sisi wenye kukutukuza daima na moyo wote.

**KATHISMA YA MBILI** *Sauti ya mnane. Tin sofian ke Logon.*

Ulipotirikizia dunia chemchem ya hekima na ya uzima, unawaalika watu wote washote maji ya wokovu, kwani huyu mwenye kupokea Amri yako ya umungu anazima ndani yake moto ya udanganyifu; hatakuwa tena na kiu milele na hatakosa kupata mema yako, ee Bwana na Mfalme wa mbinguni. Ndio maana tunatukuza uwezo wako, ee kristu Mungu wetu; tunakuomba, uzime makosa yetu na uwape watumishi wako neema mingi ya wokovu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*(mara mbili).*

*Kisha tunasoma:* Tukiona ufufuo wa Kristu...*Zaburi 50 (51). Kanuni ya Siku Kuu na Mineon.Kontakion na Eksapostilarion ya Siku Kuu.*

**MASIFU** *Sauti ya tatu.*

Kwa chuki nilifukuzwa Paradizoni, na kwa uzito wa zambi nikaanguka; lakini haukunizarau, ee Bwana, na kwa ajili yangu ukafanana nami; ukajachilia kusulubiwa na ukawa wokovu wangu: Uniongoze ku utukufu wako. Ee Mungu mwenye kuniokoa, utukufu kwako.*(mara mbili).*

Kujeni, mataifa yote, mujue nguvu ya fumbo ya ajabu; kwani Kristu Mwokozi wetu, Neno aliyekuwa katika mwanzo, alisulibiwa kwa ajili yetu, na alizikwa kwa kutaka kwake, na alifufuka katika wafu kusudi aokoe ulimwengu. Tumwabudu yeye.

Njooni mataifa yote, tutukuze makumbusho ya Mashahidi wa Bwana, kwani walipokea kwa Kristu mbele ya Malaika na ya Wanadamu taji la washindi na wanamuomba kwa ajili ya roho zetu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote. *Sauti ya mnane*.

Ee Yesu Mwokozi wangu, Sikukuu ya Paska ilipofika katikati yake, ulikuja ndani ya Hekalu, na uliposimama katikati ya makutano ukawafundisha na uwezo ukawaambia : " Mimi ni nuru ya dunia, huyu mwenyi kunifwata hatatembea katika giza, lakini atakuwa na nuru ya uzima wa milele.

**APOSTIKHA** *Sauti ya mbili. Ikos tu Efratha.*

Ee Neno, unapokaa wewe wote pamoja na Mungu na unapotaka kuniokoa toka zimu ya zambi, kwa wema wako kubwa kuja ukae ndani yangu.
Shairi; Kumbuka watu wako ulipata tangu mwanzo,wale ulikomboa kama kabila la uriti wako.

Giza imeondolewa, tazama, katikati ya Sikukuu Masiya anangaa na neema ya wokovu kama alfajiri.

Shairi: Mungu ni Mfalme wetu tangu milele, alitimiza wokovu duniani.

Mwokozi alisema: Muje wepesi, ninyi wenye kutaka kunywa maji ya uzima, kunyweni na furaha neema ya Mungu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote. *Sauti ya mnane.*

Tutakaseni siri za mawazo yetu, tuwakisheni taa za roho zetu, hivi tutamwona Kristu Uzima wetu kuingia ndani ya Hekalu kwa wema wake kubwa sababu ya kushinda Adui na kuokoa wanadamu kwa Mateso yake msalabani na kwa Ufufuo wake takatifu; na kwa ajili yake tutaimba : Wewe mwenye kujaa ulimwengu, Bwana, utukufu kwako.

# MU KAZI TANO MANGARIBI YA JUMA YA MWENYE KUPOOZA

*Elezo: Kisha Proimiakos, tunaimnba «Bwana nimekuita...» na wimbo sita; tatu ya Siku Kuu na tatu ya Mineon.*

***Wimbo ya Siku Kuu***

.

*Sauti ya kwanza. Ton uranion tagmaton.*

Kwa mapendo yake kwa wanadamu, Muumba wa ulimwengu, Mfalme wa uzima, Neno wa milele pamoja na Baba Mtakatifu, alipotwaa mwili kwa Bikira kwa kutaka kwake, alileta mafundisho ya hekima yake isiyokadirika.

Ee Bwana, kama inavyoandikwa, katikati ya Sikukuu ulikuja ndani ya Hekalu, ee Bwana wa Sheria, uliwafundisha Wayuda na uwezo, wakashangaa kwa maneno yako ya hekima na kwa miujiza yako ya nuru.

Mfalme wa hekima, Mwenye kuleta fazila, huyu mwenye kuleta maji toka chemchem isiyokauka, anasema : Muje kwangu, ninyi wote muliyo na kiu, muje mushote maji ya uzima na ya wokovu, ndani yenu mutatoka mito ya vipaji takatifu.

***Wimbo tatu ta Mineon***

Utukufu kwa Baba...*Sauti ya kwanza.*

Tazama katikati ya Siku makumi tano Kristo, kisha kufunua ubwana wa umungu wake, aliponyesha Mwenye kupooza na kwa neno lake alimuamusha toka mukeka wake; alipotenda maajabu katika mwili wa mutu aliwapa wanadamu uzima wa milele na neema ya wokovu.

Sasa na siku zote...**THEOTOKION.** *Sauti ya tatu.*

Namna gani hatutashangaa, Muheshimiwa kamili, uzao wa Mungu na mtu? Kwa sababu bila kujua mwanaume, ee Bikira usiye na doa, ulizaa Mwana kwa namuna ya mwili pasipo baba, bila kupokea geuzo, ao mchanganyo, ao mgawanyo, lakini mwenye kushika tabia zake nzima za kila moja asili ya yote mbili. Kwa hii, Mama Bikira bibi malkia, umusihi kwa sababu ya wokovu, wa roho ya wale wanakusadiki kwa namuna ya kiorthodoksi, ya kama uko Mzazi-Mungu.

**APOSTIKHA** *Sauti ya tatu.*

Nguvu ya mauti ilivunjwa kwa Msalaba wako Kristu Mwokozi, na udanganyifu wa Shetani uliharibiwa, basi uzao wa watu, wenye kuokolewa kwa imani, unakutolea nyimbo daima.

Shairi:Bwana anatawala mwenye kuvaa utukufu, Bwana anatawala anajifunga uwezo wake

Ulimwengu uliangazwa, kwa Ufufuo wako Bwana, na Paradizo tena ilifunguliwa; na kiumbe chote mukukusifu, kinakutolea nyimbo kila siku.

Shairi: Ulikaza ulimwengu isitikisike,utawala wako ni imara daima.

Ninatukuza nguvu ya Baba, na ya Mwana, na ninaimba uwezo wa Roho Mtakatifu, umungu usiyogawanywa na usiyoumbwa, Utatu wa asili moja (omousion), unaotawala milele na milele.

Shairi: Bwana,makao yako inastahili utakatifu,milele.

Kwa mateso yako, ee Kristu, ulileta giza ku jua, kwa nuru ya Ufufuo wako, ulifurahisha ulimwengu, pokea wimbo wetu wa mangaribi, ewe Mpenda-wanadamu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote.... *Sauti ya kwanza.*

Ee Hekima ya Mungu, katikati ya Sikukuu uliingia ndani ya Hekalu sababu ya kufundisha, ukawalaumu Waandishi na Wafarisayo na ukawaambia na uwezo wako wote : “ Huyu aliye na kiu aje kwangu anywe maji ya uzima na hatakuwa tena na kiu; akiniamini mimi ndani yake mutatoka mito ya maji ya uzima. Ewe wema kubwa, ewe rehema ya milele, Kristu Mungu wetu, utukufu kwako.

# MU POSHO ASUBUI YA JUMA YA MWENYE KUPOOZA

*Kisha Eksapsalmos: Bwana ndiwe...Apolitikion, Thetokion.*

**KATHISMA YA KWANZA** *Sauti ya tatu.*

Kristu amesimama katika wafu, malimbuko ya wale waliyolala; mzaliwa wa kwanza wa kiumbe, fundi wa ulimwengu wote, ndani yake alifanya upya hali ya ubinadamu iliyoharibika. Ewe mauti, hautawala tena: Ufalme wako umevunjwa na Bwana wa ulimwengu.

Utukufu kwa Baba

Ee Bwana, kwa mwili wako ulionja mauti, ukaondoako uchungu kwa ufufuo wako; kwa hii ulisabitisha ubinadamu, ukaondoa ushindo uliyoazibiwa na laana ya zamani. Ewe Mlinzi wa uzima wetu, Bwana, utukufu kwako.

Sasa na siku zote. **THEOTOKION**

Bikira Mzazi-Mungu tunakuimba, wewe mupatanishi ya wokovu juu ya ukoo wetu; katika mwili alipata kwako, Mwana wako na Mungu wetu, alitaka kuteswa Msalabani, juu ya kutukomboa ku lufu, sawa mpenda-wanadamu.

**KATHISMA YA MBILI** *Sauti ya mnane. Tin sofian ke Logon.*

Ee Mwokozi wangu, katikati ya Sikukuu iliyoamuriwa na Sheria ulifundisha ndani ya Hekalu, ukawalaumu Wayuda wasioamini sababu ya kutokuamini kwao, na kwa sauti yako ya umungu uliwaambia makutanoHuyu aliye na kiu aje kwangu na anywe. Na uliwahidi waaminifu kuwapa maji ya hekima yenyi kutoka ku Chemchem yako isiyokauka. Ndio maana tunakulalamikia, ee Kristu Mungu wetu tukisema: Wewe peke yako uliye na mapendo ya milele, ututumie Roho wako Mtakatifu kamili na utuokoe.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*(mara mbili)*

*Kisha tunasoma:* Tukiona ufufuo wa Kristu...*Zaburi 50 (51). Kanuni ya Siku Kuu na Mineon.Kontakion na Eksapostilarion ya Siku Kuu.*

## MASIFU. *Sauti ya tatu.*

Kujeni, mataifa yote, mujue nguvu ya fumbo ya ajabu; kwani Kristu Mwokozi wetu, Neno aliyekuwa katika mwanzo, alisulibiwa kwa ajili yetu, na alizikwa kwa kutaka kwake, na alifufuka katika wafu kusudi aokoe ulimwengu. Tumwabudu yeye.

Walinzi, ee Bwana, wakaeleza maajabu yako yote; lakini baraza ya ubatili, wakijaza mukono wao wa kuume kwa zawadi, waliwaza ya kama watafuchika Ufufuo wako, uliyotukuzwa na watu. Utuhurumie.

Dunia yote ilijazwa na furaha, wakati ilipopata maarifa ya ufufuo; kwani Maria Magdalena alikuja kwa Kaburi, na akakuta Malaika amekaa juu ya jiwa, kwa mavazi ya kuangaa, na akasema: sababu gani munatafuta yeye aliye hai katika wafu; Hayuko hapa, lakini alifufuka, kama alivyosema, akiwatangulia kwenda Galilaya.

Katika mwangaza yako, ee Rabi Mpenda-wanadamu, tutaona mwangaza; kwa sababu ulifufuka katika wafu, ukitoa wokovu kwa uzao wa watu, kusudi viumbe vyote vikusifu, uliye peke Msiye-zambi. Utuhurumie.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote. *Sauti ya ine.*

Ndugu, tunapoangazwa kwa Ufufuo wa Mwokozi Yesu Kristu, tunapofika katikati ya hii sikukuu ya Bwana, tuchunge na hekima mafundisho ya Mungu sababu ya kuweza kushangilia tena Kupanda kwake mbinguni na kuja kwa Roho Mtakatifu.

**APOSTIKHA** *Sauti ya mbili. Ikos tu Efratha.*

Ee Bwana, Chemchem ya hekima yako inaleta maji ya kiroho na wakati tunapoikunywa tunajazwa na mafundisho yako takatifu.
Shairi; Kumbuka watu wako ulipata tangu mwanzo,Wale ulikomboa kama kabila la uriti wako.

Ee Neno, Waandishi na Wafarisayo walichukizwa kwa majivuno wakati walikuona unafundisha makutano mafundisho yako ya wokovu.

Shairi: Mungu ni Mfalme wetu tangu milele,alitimiza wokovu duniani.

Ee Mungu Muumba, ulikuja katika Sayuni, ukasimama katikati ya watu wako sababu ya kuwafundisha watu wote neema ya wokovu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote. *Sauti ya ine*.

Bwana, mbele ya Kusulubiwa kwako Msalabani, wakati sikukuu ilipofika katikati, ulipanda kwenda ku Hekalu sababu ya kufundisha na uwezo ile wewe mwenyewe uliongoza ndani ya Sheria ya Musa; ee kristo, na adui zako walipoogopa sababu ya siri ya ndani ya hekima yako, Bwana, kwa chuki wakafanya shauri juu yako na wakaulizana wakisema : “ Namna gani huyu anajuwa Maandiko bila kuyafunza?” Kwa maana hawakujuwa ya kwamba wewe ni Mwokozi wa roho zetu.

# JUMA YA MWANAMUKE MSAMARIA

*Kisha* «Kristu alifufuka...» *mara tatu na Zaburi Proimiakos tunaimba:* «Bwana nimekuita....» *na wimbo kumi; ine ya ufufuo ya Paraklitiki, tatu ya Siku Kuu ya Kati ya Pentikosti na tatu ya Mwanamuke Msamaria.*

***Wimbo ya Ufufuo ya Paraklitiki :*** *Sauti ya ine*

Tukiabudu bila kuacha Msalaba wako unaoleta uzima, ee Kristu Mungu, tunatukuza ufufuo wako wa siku tatu; kwa sababu ya hii ulifanya mupya asili ya watu iliyoharibika, ee Mwenyezi, na ukatuonyesha njia ya kupanda mbinguni, kwa kuwa wewe ni peke yako Mwema na Mpenda-wanadamu.

Ee Mwokozi, kwa kuondoa mateso iliyoletwa na zambi juu ya muti iliyokataziwa, ulisulubiwa juu ya muti wa msalaba; na kwa kushuka kwako kuzimuni ulivunja milango ya mauti, ee Mungu mwenyezi; ndio maana tunabudu Ufufuo wako katika wafu, na kwa shangwe tunakutukuza tukisema: Ee Bwana mwenyezi, utukufu kwako.

Ulivunja milango ya Hedeza, ee Bwana, na kwa lufu yako, uliharibu ufalme wa mauti; na uliopoa ukoo wa watu toka uharibifu, mukuleta ku dunia uzima na usiyoweza kuharibika na rehema kubwa.

Kujeni mataifa tuimbe, ufufuo wa Mwokozi wa siku tatu; sababu ya hii tulikumbolewa toka minyororo isiyofunguliwa ya Hadeze, na wote tulipata uzima na usiyoweza kuharibika, tukipaza sauti: Ewe uliyesulibiwa, uliyezikwa na uliyefufuka, utuokoe kwa ufufuo wako, wewe peke mupenda-wanadamu.

***Wimbo ya Siku Kuu Kati ya Pentikosti.*** *Sauti ya ine*.

Tazama katikati ya siku zenyi kwanza na Ufufuo wa Mwokozi na kumalizika na sikukuu ya Pentikosti, kati ya hii mbili tunaangazwa na nuru yao na inajitukuza kwa kutangulia shangilio ya Kupanda kwake Bwana mbinguni.

Sayuni inasikiliza na inafurahi, maana inatangaziwa sikukuu ya Kupanda kwa Kristu mbinguni; wana wake waaminifu wanashangilia na furaha; inapoona damu ya Kristu kusafishwa na Roho Mtakatifu, Kanisa inajitayarisha kushangilia kama inavyofaa hii nusu ya wakati wa furaha ya hii sikukuu mbili takatifu.

Tazama kushuka kwa Roho Mtakatifu juu ya kila mwanadamu kama alivyoandika nabii Yoeli; tazama katikati yake hii siku iliyotangulia kuwekwa, maana Kisha kufa kwake, kuzikwa kwake na kufufuka kwake, bila uwongo Kristu aliahidi Wafwasi wake Kuja kwa Mfariji.

**Wimbo tatu ya mwanamuke wa Samaria**. *Sauti ya kwanza. Idiomelon.*

Ee Chemchem ya miujiza, katika saa ya sita ya mchana ulikuja ku kisima cha Yakobo kukamata tunda la mama yake ya walio hai, kwani katika hii saa Eva alipodanganywa kwa nyoka alipoteza Paradizo! Mwanamuke Msamaria akajongea sababu ya kushota maji, na Mwokozi wakati ulipomwona, ukamwomba ukisema: Unipe maji ya kunywa na mimi nitakupa maji ya uzima wa milele. Mwanamuke aliendа katika muji na hekima kuwapasha watu habari akisema: Muje mukamwone Kristo Bwana, Mwokozi wa roho zetu.

*Sauti ya mbili*

Bwana alikaa pembeni ya kisima cha Yakobo na Mwamamuke Msamaria akamwomba akisema: Unipa maji ya imani, nitapokea maji ya ubatizo, ya furaha naukombozi; ee Chemchem ya uzima, Bwana, utukufu kwako.

*Sauti ya mbili*

Mwana na Neno wa Mungu mwenye kutawala na Baba wa milele alikuja ku kisima, yeye aliye Chemchem ya maponyesho; alafu, Mwanamuke Msamaria alikuja kushota maji na wakati alimwona, Mwokozi akamwambia: Unipe maji ya kunywa, na wende kumwita mume wako. Lakini huyu mwanamuke akajiharikisha kuficha sawa anazungumuza na mutu apana na Mungu, akasema: Sina mume! Bwana akamujibu: Unasema kweli kwamba huna mume, kwani ulikuwa na wanaume watano, na yule unayeishi naye sasa si mume wako! Kwa hii maneno mwanamuke akaogopa, akaenda katika muji kuwaambia watu: Muje mukamuone Kristo, huyu mwenyi kuleta neema ya wokovu duniani.

Utukufu kwa Baba... *Sauti ya sita.*

Yesu alipomukuta Mwanamuke Msamaria karibu ya kisima cha Yakobo, akamuomba maji, yeye mwenyi kufunika inchi na mawingu! Ni ajabu! Huyu mwenyi kutembea juu ya Wakheruvi anazungumuza na mwanamuke mwovu; anaomba maji, yeye mwenyi kutundika inchi juu ya maji anatafuta maji, yeye mwenyi kujaza mitoni na viziwa; Lakini, kweli anataka kuokoa mwanamuke muovu toka mtego wa Adui, kumunywisha maji ya uzima sababu ya kuzima moto ya mateso yake, kwa wema wake na kwa mapendo yake kwa wanadamu.

Sasa na siku zote...**THEOTOKION.** *Sauti ya ine.*

Nabii Daudi aliyekuwa Babu-Mungu kwa ajili yako, alikutabiri katika zaburi kwa yule aliyekufanya maajabu: Malkia anasimama ku mukono wako wa kuume. Kwa sababu Mungu alikuonyesha wewe mama muletaji-uzima, yeye aliyetwaa mwili toka wewe kwa mapenzi yake bila baba, kusudi aumbe mara ingine mufano yake, iliyoharibika kwa tamaa, na kupata kondoo alliyepotea mulimani, kumubeba ku mabega yake, na kumutoa kwa Baba, kwa kuiunganisha pamoja na Ezi za mbinguni kwa kutaka kwake, na kuokoa dunia, ee Mzazi-Mungu; yeye ni Kristu, mwenye kuwa na rehema kubwa zaidi.

**L I T I A** *Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...Sauti ya tatu.*

Leo mbingu na inchi zinashangilia, kwani Kristu anaonekana kama mutu mwenye kuchukua mwili wetu sababu ya kuokoa Adamu na wanadamu wote toka laana ya zamani; kwa miujiza yake yenyi kushangaza alikuja katika inchi ya Samaria; alionekana kwa mwanamuke mumoja akitafuta maji, yeye mwenyi kuvaa mawingu ya mbinguni yenyi maji; na sisi wote waaminifu tunasujudu mbele ya huyu ambaye kwa nia yake ya wema alitwaa hali yetu ya umaskini.

**APOSTIKHA** *Sauti ya Ine.*

Ee Bwana, ulipopanda juu ya Msalaba, ulizimisha laana yetu yakutoka kwa mababu zetu; na uliposhuka ndani ya hadeze, uliopoa wafungwa tangu zamani, ukaleta uzima usiyoharibika ku uzao wa watu; kwa hii tukiimba tunasifu ufufuo wako, uletao uzima na wokovu.

Tangazo:Kisha tunaimba WIMBO YA PASKA (Angalia Masifu ya Orthros ya Paska: *Sauti ya tano*

1. Paska zabihu leo imeonekana kwetu, Paska mupya Takatifu. . .
2. Kujeni Wanawake. . .
3. Wanawake Wabebaji manukato. . .
4. Paska ya furaha, Paska ya Bwana Paska. . .

Utukufu kwa Baba. . . *Sauti ya mnane.*

Ee Kristu Mungu wetu, wakati ulionekana duniani sababu ya kutimiza wokovu wetu, Mwanamuke Msamaria aliposikiliza neno la Mungu mwenye kutupenda sana, aliacha mutungi wake wa maji pembeni ya kisima, akaenda katika muji kuwaambia watu ya kama: Muje mukamwone huyu mwenyi kujua siri za mioyo yetu; huyu si Kristu, Masiya atakayekuja, huyu eko na neema ya wokovu.

Sasa na siku zote. . . *Sauti kimoja.*

Mwokozi, katikati ya sikukuu wakati ulipokuwa umefundisha, Waandishi waliulizana wakisema: Wapi anajuwia Maandiko, yeye hakufunza? Kwa sababu wao wenyewe hawakujua ya kama wewe ni Hekima yenye kuumba ulimwengu; Bwana, utukufu kwako.

**Apolitikion ya ufufuo**. *Sauti ya ine.*

Wakati wanawake-wanafunzi wa Bwana, walipofundisha na Malaika kuhubiri habari ya furaha ya ufufuo, na walipotupa hukumu kwa mababu zetu, wakasema kwa Mitume kwa kujisifu: Mauti imenyanganywa, Kristu Mungu alisimama, kwa kuleta duniani rehema kubwa.

**Apolitikion ya Siku Kuu Kati ya Pentikosti.**

Utukufu kwa Baba...*Sauti ya munane*

Katikati ya Sikukuu ondosha kiu ya roho yangu, kwani uliwaambia watu wote ya kama : Huyu aliye na kiu aje kwangu na anywe! Ee Chemchem ya uzima, Kristu Mungu wetu, utukufu kwako.

Sasa na siku zote...**THEOTOKION.** *Sauti ya mnane.*

Wewe uliyezaliwa kwa Bikira kwa ajili yetu, na uliyevumilia usulubisho, ee Mwema, uliyenyanganya mauti kwa lufu, na uliyeonyesha usimamao sawasawa na Mungu, usikengue walioumbwa kwa mukono wako; onyesha mapendo yako kwa wanadamu. Murehemu; pokea Mzazi Mungu aliyekuzaa, aliyepatanisha juu yetu, na okoa, ee Mwokozi wetu, taifa isiyotumainia.

**Kuaga.**

## IBADA YA ASUBUI

**KATHISMA YA KWANZA** *Sauti ya ine.*

Walipoona mlango wa kaburi, na wasipoweza kuvumilia mwangaza wa Malaika wa nuru, Wanawake Watakatifu Wabebaji0manukato wakaogopa na wakasema: Wamemuimba huyu aliyemfungulia Mnyanganyi Paradizo? Ameamka, huyu mbele ya Mateso yake alitangaza Ufufuo wake? Kweli amefufuka, Kristu Mungu wetu, akiwapa wale wa ku Hadeze uzima wa milele na kuwafufua.

Utukufu kwa Baba... *Takhi prokatalave.*

Ee Mwokozi msiyekufa, umefufuka, ukisanyika dunia yote pamoja nawe; kwa uwezo wako, ee Kristu Mungu wetu, ulivunja ufalme wa mauti, ee Mungu wa mapendo, uliwaonyesha watu wote Ufufuo. Wewe mwenye kutupenda, tunakutukuza.

Sasa na siku zote...**THEOTOKION**

Siri ya kificho tangu milele iliyokuwa isijulikane na Malaika, imeonekana duniani katika wewe, ee Mzazi-Mungu; maana Mungu alitwaa mwili kwa ushirika, bila muchanganyo, na alikubali msalaba kwa kutaka kwake kwa ajili yetu; juu ya hii akifufua Muumbwa wa kwanza, akaokoa toka lufu nafsi yetu.

**KATHISMA YA MBILI** *Sauti ya ine. kateplagi Iosif.*

Aliposhuka toba uwanja wa mbinguni, Gabrieli akajongea ku jiwe huko kulipatikana mwamba wa uzima wetu; mwenyi kuvaa mavazi meupe, akawaambia wanawake wenyi kulia: Msilie, maana muna daima huyu munapenda, muwe na moyo, kwani amefufuka kweli, huyu munayetafuta mukilia; nendeni mukawaambie Mitume: Bwana amefufuka.

Utukufu kwa Baba...umoja.

Ee Mungu Mwokozi, ulipenda kuteswa Msalabani kwa kutaka kwako, wanadamu wakakuweka kaburini mupya wewe ambaye neno linakusanya mipaka ya ulimwengu; na katika Ufufuo wako wenyi kuleta uzima mauti ikafungwa monyororo na ikanyanganywa, wafungwa wa Hadeze wakalalamika: Kristu amefufuka, anakaa milele kama chemchem ya uzima.

Sasa na siku zote.**THEOTOKION**. *Kateplagi Iosif. Aftomelon.*

Yosefu aliogopa alipoona siri yenye kupita ubinadamu, akakumbuka manyonya yenyi kufunikwa na umande, ee Mzazi-Mungu, wakati ulipopata mimba bila mbegu, akakumbuka kichaka kilichowaka moto bila kuteketezwa, akakumbuka tawi la Haaroni lililochamuka; mume wako na mlinzi wako akakushuhudia mbele ya makohani akalalamika: Bikira amezaa na amekaa bikira hata kisha kuzaa.

## MAHIMIDI YA UFUFUO YA KRISTU
## IPAKOI

Ee Kristu, Wabebaji manukato, watangazaji wa kwanza wa ufufuo wako, wa ajabu, wakaenda mbio kwa Mitume wakasema: Kristu amefufuka kama Mungu, analeta duniani neema kubwa.

**ANAVATHMI NA PROKIMENON YA PARAKLITIKI**

*Tafuta mu Kitabu Paraklitiki. Sauti ya ine.*

KANUNI YA UFUFUO YA PASKA ***Sauti ya kwanza***

**KANUNI YA KATI YA PENTIKOSTI**

*Sauti ya mnane. Thalassan epiksas.*

**KANUNI YA MWANAKUKE MSAMARIA *Sauti ya ine.***

**WIMBO YA KWANZA**

**IRMOS:** Huyu alipiga Misri na mzulumu wake na kuwangamiza ndani ya bahari aliokoa toka utumwa wa Farao watu wake wenye kuimba wimbo wa Musa mshindi: Maana amevaa utukufu.
Utukufu kwako ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Huyu aliyezikwa ameamuka, anafufua wanadamu pamoja naye: viumbe vyote vishangilie na mawingu ya kiroho yanyesheshe haki leo.
Utukufu kwako ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Ee Kristu, wewe uliyeteswa mwilini kwa kutaka kwako, siku ya tatu ulifufuka katika wafu, ukafungua makaburi ya Hadeze na ukaokoa roho za wafungwa kama Mfalme wa uzima.
Utukufu kwako ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Wanawake wabebaji-manukato walimuona Malaika mwenye kuangaa, wakaenda mbali na kaburi, wakawaendea Wafwasi kwa haraka kuwaambia Ufufuo wa Kristu.
Utukufu kwako ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Ee Bwana uliye maji ya uzima na uliyejenga makao yako makubwa juu ya maji, ulimupa Mwanamuke Msamaria maji takatifu aliyokuomba, akatambua rehema yako ya milele.

Utukufu kwa Baba…

Ee Utatu Mtakatifu, kwa waaminifu wenye kukutukuza kweli uwape wokovu, Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, Muumba wa ulimwengu, kwa wema wako, utupe maondoleo ya zambi zetu.

Sasa na siku zote…**THEOTOKION**

Salamu, kiti cha moto, kinara cha zahabu na wingu la nuru, Makao ya Neno, salamu, Meza ya siri iliyostahili kumubeba Kristu aliye mukate wa uzima.

**WIMBO YA TATU**

Moyo wangu inasabitishwa katika Bwana mwenye kuwafundisha waaminifu namuna gani inafaa kuomba; anaregeza silaha ya vita, na wazaifu anawavika uwezo.

Ee Neno, ulisulubiwa msalabani kwa kutaka kwako, na mawe yalipasuka kwa kukuona, viumbe vyote vilitetemeka na woga, kama ndoto, wafu waliamuka toka kaburini.

Ee Neno, roho za wenye haki zilipokuona umeshuka na roho yako kuzimuni, vilifunguliwa toka minyororo iliyozifunga tangu milele, na zikatukuza uwezo wako wenyi kupita ufahamu wote.

Malaka mumoja mwenyi kuangaa aliwaambia wanawake wabebaji manukato : “ Enyi wanawake, sababu gani hii fujofujo? Sababu gani munamutafuta na manukato Bwana kaburini? Amesimama, na watu wote wameamuka pamoja naye!”

Ee Mfalme wa uzima na Chemchem ya uzima wa milele, ulipokaa pembeni ya kisima, kwa wema wako ulimujaza Mwanamuke Msamaria maji ya hekima aliyokuomba wewe.

Utukufu kwa Baba…

Peke yake na Mukubwa ni Mungu tunayetukuza, Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, Utatu majeshi ya mbinguni wanatukuza wakisema: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ni wewe milele.

Sasa na siku zote…**THEOTOKION.**

Ee Bikira Mzazi, ulipopata mimba ya Mungu wa ulimwengu tumboni mwako, ulimuzaa kwa namuna yenyi kupita ufahamu, ulikaa Bikira kama mbele ya kuzaa.

*Elezo: Kisha kuimba wimbo ya tatu, tunasoma Kontakion ya Siku Kuu ya Kati ya Pentikosti;*

**KONTAKION YA SIKU KUU KATI YA PENTIKOSTI** *Sauti ya ine.*

Ee Muumba na Bwana wa ulimwengu, Kristu Mungu wetu katikati ya sikukuu iliyoamuriwa na Sheria,uliwaambia wale waliokuzunguka: Kujeni mushote maji ya uzima wa milele. Ndio maana tunasujudu mbele yako na kupaza sauti na imani na tunasema: Utupe rehema yako, maana wewe ni Chemchem ya uzima wetu.

**KATHISMA YA MWANAMUKE MSAMARIA**

*Sauti ya ine. O Ipsothis en to Stavro.*

Mbingu ifurahiwe, wanadamu washangilie! Kwa sababu Kristu aliyezaliwa kwa Bikira ameonekana katika mwili wetu, kwa lufu yake aliokoa wanadamu toka uvumbi wa kaburi; alipomuomba Mwanamuke Msamaria maji, kwa nuru ya muujiza yeye anamupa chemchem ya neema na ya uzima wa milele.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...

**KATHISMA YA KATIKATI YA PENTIKOSTI**

Ee Mfalme wa hekima na Bwana wa ufahamu, katikati ya sikukuu iliyoamuriwa na Sheria, ulipokaa ndani ya Hekalu ulifundisha, ukawaambia makutano waliyokusanyika ya kama: Huyu aliye na kiu aje kwangu, na anywe maji ninayoleta sasa; katika hii watu wote watapata uzima takatifu na furaha.

**KONTAKION YA MWANAMUKE MSAMARIA** *Sauti ya ine*

Ee Chemchem ya hekima, alipokuja karibu ya kisima, Mwanamuke Msamaria alikuona na macho yake ya imani; alishotako ufalme wa juu mbinguni; makumbusho yake inatukuzwa milele.

**IKOS**

Tusikilize kama inavyostahili Evangeli huko Mtakatifu Yoane anatufundisha waziwazi mafumbo takatifu yaliyotokea zamani katika inchi ya Samaria: Alipozungumuza na mwanamuke, Bwana akamwomba maji, Yeye zamani aliyeamuru maji yakusanyike fasi moja, Neno wa Mungu mwenyi kutawala pamoja na Baba na Roho Mtakatifu, maana alikuja kutafuta sura yake iliyopotea, makumbusho yake inatukuzwa milele.

**SINAKSARI**

Leo, Juma ya tano ya Paska, tunashangilia sikukuuu ya Mwanamuke Msamaria.

Ewe Mwanamuke, maji ulikuja kutafuta ilikuwa ya mbaya, alafu ulishota maji ya uzima huko ulisafisha roho yako.

Kwa maombezi ya Shahidi wako Mtakatifu Fotini, ee Kristu Mungu wetu, utuhurumie. Amin.

**KATAVASIES YA UFUFO YA KRISTU**

Bwana Mungu wetu ndiye Mtakatifu *(mara tatu).*

**EKSAPOSTILARION YA PASKA.** *Sauti ya mbili.*

Kwa mwili, ee Mufalme na Bwana ulilala kama mutu mwenye kuweza kufa, ulifufuka siku ya tatu; ukasimamisha Adamu toka uharibifu, maana ulishinda mauti, ewe Paska huko tnashota uzima usiyoku, Paska huko dunia inapata wokovu..

**Ingine ya mwanamuke wa Samaria. G***inekes akutisthite. Sauti ya mbili.*

Ee Mwokozi, ulipokutana na mwanamuke katika muji mumoja wa Samaria, ukamwomba maji ya kunywa, Wewe zamani jangwani ulitirikiza maji toka mwamba ambayo wana wa Israeli walikunywa. Ee Chemchem ya uzima, unaamusha imani katika roho ya Mwanamuke Msamaria mwenyi kuonja daima furaha na maji ya uzima mbinguni.

**Ingine ya Siku Kuu ya Kati ya Pentikosti.** *Umoja.*

Ee Bwana Mpenda-wanadamu, ulionekana ndani ya Hekalu katikati ya sikukuu, ukasema : “ Kujeni kwangu ninyi wote mulio na kiu, shoteni maji ya uzima; ndani ya hii maji mutapata furaha, neema na uzima wa milele.

**MASIFU** *Sauti ya ine.*

Ewe uliyevumilia, Msalaba na lufu, na ulifufuka katika wafu, Bwana Mwenyezi, tunasifu Ufufuo wako.

Pa Msalaba wako, ee Kristu, ulituopoa toka fingo ya Kale, na kwa lufu yako uliharibifu Shetani, mwenye jeuri kwa hali yetu, na kwa ufufuo wako ulijaza vyote kwa furaha; kwa hii tunapaza sauti kwako: Ewe Bwana, uliyefufuka katika wafu, utukufu kwako.

Pa Msalaba wako, ee Kristu Mwokozi, utuongoze kwa ukweli wako, na utuokoa toka mitego ya adui; Ewe uliyefufuka katika wafu, utufufue sisi tuliyoanguka katika zambi, myolosha mukono wako, ee Bwana Mpenda-wanadamu, kwa upatanisho ya watakatifu wako.

Pasipo kujitenga toka kifua cha Baba yako, ee Mwana wa pekee Neno la Mungu, ulikuja duniani kwa kupenda-wanadamu, ukijifanya mtu bila ugeuzo, na ulivumilia katika mwili Msalaba na lufu, ee Msiyeteswa katika umungu; ukifufuka katika wafu, ulipatia uzima usiyokufa kwa uzao wa watu, sawa yako Mwenyezi.

Ulikubali lufu kwa mwili, ukifanya biashara kusudi ya kutupatia uzima usiyokufa, ee Mwokozi; na ulikaa ndani ya kaburi, kusudi utuopoe katika Hadeze, ukitufufua pamoja nawe, ukiteswa sawasawa na mtu, lakini ukifufuka sawasawa na Mungu; kwa hii tunakupaza sauti: Utukufu kwako, ee Bwana mletaji-uzima, peke yako mpenda-wanadamu.

Mawe ilipasuka, ee Mwokozi, wakati Msalaba wako ulipozamishwa ndani ya pahali pa mufupa wa kichwa; wakati uliwekwa ndani ya kaburi sawa mwenye kufa, zamu ya milango wa hadeze walitetemeka; na kwa sababu uliharibu nguvu ya mauti, uliwapa wafu wote uzima usiyoharibika, kwa ufufuo wako, ee Mwokozi; Bwana mletaji-uzima, utukufu kwako.

***Wimbo Idiomela ya mwanamuke Msamaria.*** *Sauti ya tatu*

Shairi: Tembea katika nuru ya ufalme wako, linda ukweli, wena, na uhaki.

Leo mbingu na inchi zinafurahi, kwa sababu Kristu ameonekana kama mutu mwenyi kuchukua mwili wetu sababu ya kuokoa adamu na wanadamu wote toka laana ya zamani. Kwa miujiza yake ya ajabu alikuja katika inchi ya Samaria; akaonekana kwa mwanamuke mumoja alikuja kushota maji, Yeye mwenye kuvaa mawingu ya maji ya mbinguni; na sisi wote waaminifu tunasujudu mbele ya huyu ambaye kwa wema wake alitwaa mwili wetu wa umaskini.

*Sauti ya sita*

Shairi: Unapenda haki, unachukia uovu, ndio maana Bwana Mungu wako alikukapaa mafuta ya furaha kuliko hata mumoja waadui zako.

Bwana anamwambia hivi mwanamuke Msamaria: Kama ungalijua zawadi ya Mungu, na ni nani anakwaambia unipe maji ya kunywa, wewe ndiye ungalimwomba, naye angalikupa maji yaliyo hai kusudi usiwe na kiu tena hata milele.

Utukufu kwa Baba...*Sauti ya sita.*

Yesu Mwokozi wetu aliye Chemchem ya uzima alipofika ku kisima cha Yakobo, akaomba maji kwa mwanamuke mumoja Msamaria; lakini kama vile huyu mwanamuke alisema juu ya uadui kati ya Wasamaria na Wayuda, Muumba mwenye hekima kwa maneno yake upole akamushauria kumupa maji ya uzima wa milele; na alipoipokea, akawapasha watu wote habari akasema: Muje mukamuone huyu mwenyi kujua siri za mioyo yetu, Mungu aliyeonekana katika mwili sababu ya kuokoa wanadamu wote.

Sasa na siku zote...Mbarikiwa ukupita, ewe Mzazi-Mungu Bikira.....

**DOKSOLOGIA KUBWA**

# MU JUMA MANGARIBI YA MWANAMUKE MSAMARIA

*Kisha Proimiakos na «Bwana nimekuita...» tunaimba wimbo sita; tatu ya Siku kuu ya kati ya Pentikosti na tatu ya Mineon.*

***Wimbo ya Siku Kuu ya kati ya Pentikosti.***

*Sauti ya tano*. Kheris askitikon

Leo, kama saa ya kusini inavyogawanya siku kwa sehemu mbili, Mesopentikosti inaonekana kwa neema yake na kwa nuru yake katikati ya hii wakati tunashangilia Ufufuo wa Mwokozi; inapoeneza nuru ya Kristu aliyefufuka, inaonyesha alama za uzima wa milele na inatangulia kutuonyesha Kupanda kwake mbinguni; inatangaza kuja kwa Roho Mtakatifu na Sikukuu ya nuru ya Pentikosti, inaleta amani na neema ya wokovu rohoni mwetu.

Katikati ya Sikukuu Bwana anatupa sisi wote maji ya mapendo yake kama mutoni wa utukufu takatifu akisema : " Muje, ninyi mulio na kiu, na shoteni." Kwa sababu Yeye ni chemchem ya huruma na bahari ya rehema, anatirikizia wanadamu maondoleo ya zambi; anasafisha zambi, anatakasa wagonjwa, anaokoa wale wenye kushangilia Ufufuo wake, analinda wenye kupenda Kupanda kwake tukufu mbinguni, analeta amani na neema ya wokovu rohoni mwetu.

Bwana alisimama katikati ya Hekalu kwa sababu kwa hali yake yeye ni Mungu, japo alijifanya mutu kwa ajili yetu; kwa neno lake anawapa watu wote maji ya uzima akisema : " Muje, takaseni moyo wenu, tulizeni roho yenu toka moto ya tamaa; mutu hata mumoja asikose kunywa hii maji! Maji ninayoleta ni neema ya Mungu, ni maji nzuri na inaleta uzima wa milele; huyu anayeikunywa atatawala pamoja na mimi Muumba wake katika utukufu wa Mungu.

***Wimbo tatu ya Mineon.***

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...Sauti ya mnane.

Bwana, katikati ya sikukuu mbele ya Mateso yako na ya Ufufuo wako tukufu, ulifundisha ndani ya Hekalu, uliwaambia Waandishi na Wafarisayo hivi: Huyu aliye na kiu aje kwangu na anywe! Huyu anayeniamini mimi ndani yake mutatoka mito ya maji ya uzima yenyi kutakaswa kwa Roho Mtakatifu. Ee Hekima isiyokadirika na uwezo wa Mungu, wewe mwenye kujaza ulimwengu, Bwana, utukufu kwako.

**APOSTIKHA** *Sauti ya ine.*

Tukiabudu bila kuacha Msalaba wako unaoleta uzima, ee Kristu Mungu, tunatukuza ufufuo wako wa siku tatu; kwa sababu ya hii ulifanya mupya asili ya watu iliyoharibika, ee Mwenyezi, na ukatuonyesha njia ya kupanda mbinguni, kwa kuwa wewe ni peke yako Mwema na Mpenda-wanadamu.

Shairi:Nitanyanyula macho yangu kwako, ee mwenye kuikaa mbinguni...

Ee Bwana, nilitaka kuzima katika vidonda vyangu daftari ya zambi zangu ili kuamini kuangu kukupendeze katika muda wa maisha yangu, lakini kwa hila yake adui akasirika juu ya roho yangu: Ee Bwana, mbele ya mwisho uniokoe.

Shairi: Utuhurumie, ee Bwana, utuhurumie, kwani tunayala na kuzarauliwa...

Ee Kristu Mungu wetu, unapotukuzwa katika makumbusho ya Watakatifu wako, kwa maombezi yao ututumie neema ya wokovu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya sita*.

Ee Kristu, tunapofika katikati ya Ufufuo wako na Kuja kwa Roho wako Mtakatifu, wote pamoja tunatukuza miujiza ya ajabu ambayo fumbo imefunuliwa kwetu, na tunapojaa na woga tunakuomba: Ututumie neema ya wokovu.

# MU KAZI MOJA ASUBUI YA JUMA YA TANO YA MWANAMUKE MSAMARIA

*Elezo: Kisha Eksapsalmos, Bwana ndiwe...» na Apolitikia, tunaimba:*

**KATHISMA YA KWANZA.** *Sauti ya ine.*

Walipoona mlango wa kaburi, na wasipoweza kuvumilia mwangaza wa Malaika wa nuru, Wanawake Watakatifu Wabebaji0manukato wakaogopa na wakasema: Wamemuimba huyu aliyemfungulia Mnyanganyi Paradizo? Ameamka, huyu mbele ya Mateso yake alitangaza Ufufuo wake? Kweli amefufuka, Kristu Mungu wetu, akiwapa wale wa ku Hadeze uzima wa milele na kuwafufua.

Ee Bwana, rudisha kwako roho yangu maskini, kwani nimetumia vibaya maisha yangu yote katika zambi, unipokee kama mwanamuke mwenye zambi na uniokoe.

Leo Majeshi ya mbinguni wanapoikumbuka Mashahidi washindaji, wanakuja kuangaza moyo wa waaminifu na wanaangazisha neema ulimwenguni; kwa maombezi yao, ee Mungu Mwenyezi, utupe neema ya wokovu.

**THEOTOKION**

Ni wewe kweli Mzazi-Mungu na kama Mama unauwezo wa kumuomba Mwana wako na Mungu wetu alinde waaminifu wenye kukukimbilia; katika wewe kuna nguvu yetu na makimbilio yetu, ndiwe boma letu bandari yetu ya wokovu na peke yako mlinzi wa wanadamu.

**KATHISMA YA MBILI** *Sauti ya munane. Tin Sofian ke Logon*

Hekima na Neno la Baba aliyewapa Mitume amri takatifu ya kutangaza ku mipaka ya ulimwengu kuja kwake duniani, makafiri waongo walimutukana, wakamushitaki kuwa mudanganyifu na mwenye kushikwa na mashetani; lakini yeye akawaambia : „ Musinihukumu bila haki, ninyi waamzi wasio na imani na haki.“ Ndio maana tunamulalamikia tukisema : „ Ee Mpenda-wanadamu, Kristo Mungu wetu, uwape waaminifu wenyi kuimbia utukufu wako usamehe na maondoleo ya zambi.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*(mara mbili).*

*Elezo: Kisha tunasoma:* Tukiona ufufuo wa Kristu, tumusujudu Yesu...*Kanuni ya Siku Kuu na Mineon. Kontakion na Eksapostilarion ya Siku Kuu ya mu Juma*.

## MASIFU. *Sauti ya ine.*

Ewe uliyevumilia, Msalaba na lufu, na ulifufuka katika wafu, Bwana Mwenyezi, tunasifu Ufufuo wako.*(mara mbili).*

Mimi ni mpotevu kati ya kondoo zako wa siri na nakimbilia kwako, ewe Mchungaji mwema: Ee Mungu, unihurumie.

Ee Mashahidi Watakatifu, mumukuwa marafiki ya malaika mulipomtangaza Kristu uwanjani, mulizarau furaha za hii dunia, mukishika kweli nanga ya imani, ninyi ni Chemchem ya kuponyesha ya Wazaifu: Ombeni daima kwa ajili ya roho zetu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya mnane.*

Ee Yesu Mwokozi wangu, Sikukuu ya Paska ilipofika katikati yake, ulikuja ndani ya Hekalu, na uliposimama katikati ya makutano ukawafundisha na uwezo ukawaambia : “ Mimi ni nuru ya dunia, huyu mwenyi kunifwata hatatembea katika giza, lakini atakuwa na nuru ya uzima wa milele.

## APOSTIKHA *Sauti ya mbili. Ikos tu Efratha.*

Ee Mungu Mwokozi wangu, ulipoinamisha mbingu, ulitwaa mwili kwa Bikira bila kugeuka, na ukanimwangia maondoleo ya zambi zangu.

Shairi: Mungu ni Mfalme wetu tangu milele, alitimiza wokovu duniani.

Ee Neno, unapokaa wewe wote pamoja na Mungu na unapotaka kuniokoa toka zimu ya zambi, kwa wema wako kubwa kuja ukae ndani yangu.

Shairi: Kumbuka watu wako ulipata tangu mwanzo, Wale ulikomboa kama kabila la uriti wako

Ee Mfalme mkubwa, wewe ni Hekima ya milele Baba wa milele aliumba nayo na hekima ulimwengu kwa ushirika wa Roho Mtakatifu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya sita*

Tutakaseni siri za mawazo yetu, tuwakisheni taa za roho zetu, hivi tutamwona Kristu Uzima wetu kuingia ndani ya Hekalu kwa wema wake kubwa sababu ya kushinda Adui na kuokoa wanadamu

kwa Mateso yake msalabani na kwa Ufufuo wake takatifu; na kwa ajili yake tutaimba : Wewe mwenye kujaa ulimwengu, Bwana, utukufu kwako.

# MU KAZI MOJA MANGARIBI YA JUMA YA TANO YA MWANAMUKE MSAMARIA

*Kisha Proimiakos na «Bwana nimekuita...» tunaimba wimbo sita; tatu ya Siku kuu ya kati ya Pentikosti na tatu ya Mineon.*

***Wimbo ya Siku Kuu ya kati ya Pentikosti.***

*Sauti ya kwanza. Ton uranion tagmaton.*

Kwa mapendo yake kwa wanadamu, Muumba wa ulimwengu, Mfalme wa uzima, Neno wa milele pamoja na Baba Mtakatifu, alipotwaa mwili kwa Bikira kwa kutaka kwake, alileta mafundisho ya hekima yake isiyokadirika.

Ee Bwana, kama inavyoandikwa, katikati ya Sikukuu ulikuja ndani ya Hekalu, ee Bwana wa Sheria, uliwafundisha Wayuda na uwezo, wakashangaa kwa maneno yako ya hekima na kwa miujiza yako ya nuru.

Mfalme wa hekima, Mwenye kuleta fazila, huyu mwenye kuleta maji toka chemchem isiyokauka, anasema : Muje kwangu, ninyi wote muliyo na kiu, muje mushote maji ya uzima na ya wokovu, ndani yenu mutatoka mito ya vipaji takatifu.

***Wimbo tatu ya Mineon.***

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya mbili.*

l Ee Kristu Mungu wetu, wakati ulipokuja ndani ya Hekalu, katikati ya Sikukuu ulifundisha makutano ukasema: Huyu mwenye kuniamini mimi, hata akifa, ataishi. Lakini Wafarisayo, Wasadukayo na Waandishi wakanungunika na wakasema: Ni nani huyu anayekufuru hivi Mungu? Hawakuwazia ya kama uko kweli Mungu wa milele yote mwenyi kutukuzwa pamoja na Baba na Roho Mtakatifu. Bwana Mungu wetu, utukufu kwako.

**APOSTIKHA.** *Sauti ya mbili.*

Ee Mwokozi, kwa kuondoa mateso iliyoletwa na zambi juu ya muti iliyokataziwa, ulisulubiwa juu ya muti wa msalaba; na kwa kushuka kwako kuzimuni ulivunja milango ya mauti, ee Mungu mwenyezi; ndio maana tunabudu Ufufuo wako katika wafu, na kwa shangwe tunakutukuza tukisema: Ee Bwana mwenyezi, utukufu kwako.

Shairi: Nitanyanyua macho yangu kwako, ee wewe mwenye kukaa mbinguni...

Mwenyi kuzama gani akifika ku bandari yako hataokolewa? Mgonjwa gani hatapata maponyesho kwako? Ee Muumba wa wote na mganga wa wagonjwa, Bwana, mbele ya mwisho uniokoe.

Shairi: Utuhurumie, ee Bwana, utuhurumie, kwani tunajaa na kuzarauliwa...

Ee Bwana Mpenda-wanadamu uliyepokea uvumilivu wa Mashahidi wako Watakatifu, pokea pia heshima ya nyimbo zetu, ukitupatia kwa maombezi yao neema ya wokovu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya tatu.*

Katikati ya Sikukuu tunatukuza huyu alileta wokovu duniani; Kristu Uzima wetu alitundikwa msalabani katikati ya wanyanganyi wawili; kwa matusi ya wa kwanza alinyamaza, lakini kwa huyu alimuamini akamwambia : " Leo hii utakuwa pamoja nami katika Paradizo!" Kisha, Kristo alishuka kaburini na akanyanganya Hadeze, siku ya tatu alifufuka sababu ya kuleta wokovu rohoni mwetu.

# MU KAZI MBILI ASUBUI YA JUMA YA TANO YA MWANAMUKE MSAMARIA

*Elezo: Kisha Eksapsalmos, Bwana ndiwe...» na Apolitikia, tunaimba:*

**KATHISMA YA KWANZA.** *Sauti ya ine. Kateplagi Iosif.*

Ee Mungu Mwokozi, ulipenda kuteswa Msalabani kwa kutaka kwako, wanadamu wakakuweka kaburini mupya wewe ambaye neno linakusanya mipaka ya ulimwengu; na katika Ufufuo wako wenyi

kuleta uzima mauti ikafungwa monyororo na ikanyanganywa, wafungwa wa Hadeze wakalalamika: Kristu amefufuka, anakaa milele kama chemchem ya uzima.

Tazama, ee roho yangu, namna gani tutahuzuria ku hukumu: Kwa hii wakati wa woga viti vitasimikwa; hapo Mwamzi wa haki atahukumu matendo ya kila mmoja; tazama, moto wa hatari umetayarishwa sababu ya kufunika vitu vyote kama bahari kali. Ee roho yangu, tubu mbele ya mwisho.

Mashahidi wako walipamba Eklezya kwa damu yao ulimwenguni kote: Inapovaa sufi na kitani, kwa kinywa yao, inakuimbia, ee Kristu Mungu wetu: Onyesha huruma yako kwa hawe watu walio wako, leta amani kwa watawala wetu wote na neema ya wokovu ku roho zetu.

**THEOTOKION**

Wewe peke yako ulipata mimba ya Muumba wa ulimwengu na peke yako ulipamba wanadamu na uzazi, ee Bikira safi kamili, uniokoe ku nyavu za Adui, uniweke pa mwamba wa mafundisho ya Kristu, ukimusihi daima huyu aliyepata mwili tumboni mwako.

**KATHISMA YA MBILI** *Sauti ya mnane. Tin Sofian ke Logon*

Ulipotirikizia dunia chemchem ya hekima na ya uzima, unawaalika watu wote washote maji ya wokovu, kwani huyu mwenye kupokea Amri yako ya umungu anazima ndani yake moto ya udanganyifu; hatakuwa tena na kiu milele na hatakosa kupata mema yako, ee Bwana na Mfalme wa mbinguni. Ndio maana tunatukuza uwezo wako, ee kristu Mungu wetu; tunakuomba, uzime makosa yetu na uwape watumishi wako neema mingi ya wokovu.

Utukufu kwa Baba…Sasa na siku zote…*(mara mbili)*

*Elezo: Kisha tunasoma:* Tukiona ufufuo wa Kristu, tumusujudu Yesu...*Kanuni ya Siku Kuu na Mineon. Kontakion na Eksapostilarion ya Siku Kuu ya mu Juma*.

**MASIFU** *Sauti ya ine.*

Pa Msalaba wako, ee Kristu, ulituopoa toka fingo ya Kale, na kwa lufu yako uliharibifu Shetani, mwenye jeuri kwa hali yetu, na kwa ufufuo wako ulijaza vyote kwa furaha; kwa hii tunapaza sauti kwako: Ewe Bwana, uliyefufuka katika wafu, utukufu kwako. *(mara mbili).*

Ee Mwokozi, unisafishe na machozi yangu, mimi mwenyi kuchafuka na zambi nyingi; tena nasujudu mbele yako: Nimekosa, ee Mungu; unihurumie.

Ee Mashahidi Watakatifu, tunashangaa mashindano yenu, kwani, mulipovaa mwili usiyokufa, mulifukuza adui msiyeonekana; mumeteswa mateso kali zaidi bila woga mbele ya wazulumu; sasa mumepata kwa Kristu utukufu wenyi kustahili, yeye mwenyi kuleta neema ya wokovu ku roho zetu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya ine.*

Bwana, mbele ya Kusulubiwa kwako Msalabani, wakati sikukuu ilipofika katikati, ulipanda kwenda ku Hekalu sababu ya kufundisha na uwezo ile wewe mwenyewe uliongoza ndani ya Sheria ya Musa; ee kristo, na adui zako walipoogopa sababu ya siri ya ndani ya hekima yako, Bwana, kwa chuki wakafanya shauri juu yako na wakaulizana wakisema : " Namna gani huyu anajuwa Maandiko bila kuyafunza?" Kwa maana hawakujuwa ya kwamba wewe ni Mwokozi wa roho zetu.

**APOSTIKHA** *Sauti ya mbili. Ikos tu Efratha*.

Wewe ni mwanzo na mwisho, uko tena kichwa cha vitu vyote, na ndani ya Kanisa katikati ya sikukuu, ee Kristu, ulinimwangia maondoleo ya zambi zangu.

Shairi: Kumbuka watu wako ulipata tangu mwanzo, wale ulikomboa kama kabila la uriti wako.

Ee Neno, Yerusalema ilifahamu, Sayuni inatangaza nguvu ya umungu ya Ufufuo wako takatifu na inafurahi pamoja na wana wake wote, wakiimbia wema wako kubwa, ee Kristu.

Shairi: Mungu ni Mfalme wetu tangu milele, alitimiza wokovu duniani.

Ee Neno, wewe ni nuru ya Baba, lakini kwa nyakati za mwisho ulionekana kama mwanadamu sababu ya kunipa maondoleo ya zambi zangu.

Utukufu kwa Baba... Sasa… *Sauti ya mnane*

Ee Yesu Mwokozi wangu, Sikukuu ya Paska ilipofika katikati yake, ulikuja ndani ya Hekalu, na uliposimama katikati ya makutano ukawafundisha na uwezo ukawaambia: Mimi ni nuru ya dunia, huyu mwenyi kunifwata hatatembea katika giza, lakini atakuwa na nuru ya uzima wa milele.

***Elezo**: Mu Kazi Mbili mangaribi na kesho mu Kazi Tatu asubui tunafanya Sidikizo ya Siku ya kati ya Pentikosti. Tunasoma yote, bila masomo ya Unabii na Polieleo na Litia.*

# MU KAZI TATU MANGARIBI YA JUMA YA TANO YA MWANAMUKE MSAMARIA

*Kisha Proimiakos na «Bwana nimekuita...» tunaimba wimbo sita; tatu ya mwanamuke Msamaria na tatu ya Mineon.*

***Wimbo ya mwanamuke wa Samaria***

*Sauti ya ine. O eks Ipsistu*

Kristu alipokutana na Mwanamuke Msamaria karibu ya kisima, akamwomba maji ya kunywa, alikuwa na kiu ya kumwondoa toka zambi kusudi amuokoe, hii akaitimiza kama inavyohakikishwa; kwa sababu wakati aliposhota maji ndani ya kisima, yeye mwenyewe alimuvua na kumujaza na maji ya uzima, akaenda katika muji kuwaambia watu wote: Tazama Kristu, Masiya! Huyu aliyetajwa hivi katika Sheria ameonekana katika mwili na anafunua siri za mioyo yetu.

Mwanamuke Msamaria aliwaambia watu wa muji: Tazameni Masiya, ndiye Kristu, huyu ameandikwa katika Sheria ya kwamba atakuja, Nabii mkubwa, Mungu-mutu, aliniambia hii yote nilifanya na alinifunulia siri zote za moyo wangu. Halafu watu wa muji wakaenda kuona na wakahakikisha maneno yake, wakashangaa hii mambo ya ajabu iliyowaongoza ku imani.

Bwana, wewe ambaye zamani karibu ya saa ya sita ya mchana ulitembea katika Paradizo kama Mungu, binti wa babu wa kwanza alikuona mara ingine karibu ya saa ya sita ya mchana umekaa pembeni ya chemchem na ya kisima cha Yakobo, ukamwomba maji ya kunywa kusudi ya kumunywisha yeye mwenyewe maji ya uzima na ya wokovu kama ulivyoifanya kweli; Mwanamuke Msamaria alipokunywa maji ya uzima yenyi kutoka kwako akatambua uzuri wa chemchem yako, ee Bwana, na akaenda kuitangaza katika muji.

***Wimbo tatu ya Mineon.***

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya kwanza.*

Ee Chemchem ya miujiza, katika saa ya sita ya mchana ulikuja ku kisima cha Yakobo kukamata tunda la mama yake ya walio hai, kwani katika hii saa Eva alipodanganywa kwa nyoka alipoteza Paradizo! Mwanamuke Msamaria akajongea sababu ya kushota maji, na Mwokozi wakati ulipomwona, ukamwomba ukisema: Unipe maji ya kunywa na mimi nitakupa maji ya uzima wa milele. Mwanamuke alienda katika muji na hekima kuwapasha watu habari akisema: Muje mukamwone Kristo Bwana, Mwokozi wa roho zetu.

## APOSTIKHA *Sauti ya ine.*

Ulivunja milango ya Hedeza, ee Bwana, na kwa lufu yako, uliharibu ufalme wa mauti; na uliopoa ukoo wa watu toka uharibifu, mukuleta ku dunia uzima na usiyoweza kuharibika na rehema kubwa.

Shairi: Habari yao ilisikilika duniani kote, neno lao mpaka ku mwisho wa dunia.

Uliangaza kundi la Mitume, ee Kristu, kwa Roho yako Mtakatifu; kwa maombezi yao, ee Bwana, safisha pia uovu wa zambi zetu na utuhurumie.

Shairi: Mungu ni wa ajabu katika Watakatifu wake, Mungu wa Israeli.

Enyi Mashahidi watakatifu, kwa deni munayo kwa Bwana, mutuombee sisi wakosefu maondoleo ya zambi zetu na neema ya wokovu wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba. Sasa na siku zote...*Sauti ya mbili.*

Bwana alikaa pembeni ya kisima cha Yakobo na Mwamamuke Msamaria akamwomba akisema: Unipa maji ya imani, nitapokea maji ya ubatizo, ya furaha naukombozi; ee Chemchem ya uzima, Bwana, utukufu kwako.

# MU KAZI INE ASUBUI YA JUMA YA TANO YA MWANAMUKE MSAMARIA

*Elezo: Kisha Eksapsalmos, Bwana ndiwe...» na Apolitikia, tunaimba:*

**KATHISMA YA KWANZA.** *Sauti ya inne. O Ipsothis en to Stavro.*

Wewe uliyesulubiwa kwa ajili yetu na kuhesabiwa katika wafu, Chemchem ya uzima, ee Kristu Mungu, ulifufuka siku ya tatu, kwa uwezo wako uliharibu ufalme wa mauti na kwa Ufufuo wako takatifu ulifufua wafungwa wa Hadeze; na sisi waaminifu wote tunaimbia na kutukuza Ufufuo wako, ee Bwana msiyekufa.

Ee Kristu, Mitume wako waliangaa kama mwanga ulimwenguni, wanaangaza roho zetu na nuru ya mafundisho yako takatifu; katika wao uliondoa uwongo wa miungu ya uwongo, wanaangaza dunia na mafundisho ya imani. Kwa maombezi yao okoa roho zetu.

Walipovaa silaha ya Msalaba wako, ee Kristu Mungu wetu, Mashahidi wako wakashinda uerevu wa adui; wakaangaa kama nyota, wakaongoza wanadamu; kwa wale wenyi kuwaomba na imani wanawaponyessha kwa maombezi yao, okoa roho zetu.

**THEOTOKION.**

Ee Malkia sikiliza mtumishi wako ambaye roho yenyi huzuni inalalamika kwako; uniondolee zambi zangu hizi nyingi zaidi; kwani mchana na usiku ni wewe uliye ulinzi wangu imara; uniopoe ku gehena ya moto, ee Mzazi-Mungu na uniweke kuume kwa Mwana wako na Mungu wetu.

**KATHISMA YA MBILI.** *Sauti ya sita*

Ee Mungu wa wema, kama ulivyomufungulia Mwanamuke Msamaria chemchem ya umungu wako na kumumwangia maarifa ya Mungu kwa kumunywisha maji yenye kutakaswa, sasa ututumie na sisi pia maondoleo ya zambi zetu.

Utukufu kwa Baba. Sasa na siku zote..*(mara mbili)*..

*Elezo: Kisha tunasoma:* Tukiona ufufuo wa Kristu, tumusujudu Yesu...*Kanuni ya Siku Kuu na Mineon. Kontakion na Eksapostilarion ya Siku Kuu ya mu Juma*.

## MASIFU *Sauti ya ine.*

Pasipo kujitenga toka kifua cha Baba yako, ee Mwana wa pekee Neno la Mungu, ulikuja duniani kwa kupenda-wanadamu, ukijifanya mtu bila ugeuzo, na ulivumilia katika mwili Msalaba na lufu, ee Msiyeteswa katika umungu; ukifufuka katika wafu, ulipatia uzima usiyokufa kwa uzao wa watu, sawa yako Mwenyezi.*(mara mbili).*

Wafwasi wako wasipo kufunza Roho Mtakatifu aliwafanya kuwa Waalimu na kwa uzuri wa maneno yao yenyi kusikilika katika lugha yote akapoteza kosa, ee Kristu Mungu wetu Mwenyezi.

Ee Mashahidi Watakatifu, tunashangaa mashindano yenu, kwani, mulipovaa mwili usiyokufa, mulifukuza adui msiyeonekana; mumeteswa mateso kali zaidi bila woga mbele ya wazulumu; sasa mumepata kwa Kristu utukufu wenyi kustahili, yeye mwenyi kuleta neema ya wokovu ku roho zetu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote. *Sauti ya mbili.*

Mwana na Neno wa Mungu mwenye kutawala na Baba wa milele alikuja ku kisima, yeye aliye Chemchem ya maponyesho; alafu, Mwanamuke Msamaria alikuja kushota maji na wakati alimwona, Mwokozi akamwambia: Unipe maji ya kunywa, na wende kumwita mume wako. Lakini huyu mwanamuke akajiharikisha kuficha sawa anazungumuza na mutu apana na Mungu, akasema: Sina mume. Bwana akamujibu: Unasema kweli kwamba huna mume, kwani ulikuwa na wanaume watano, na yule unayeishi naye sasa si mume wako. Kwa hii maneno mwanamuke akaogopa, akaenda katika muji kuwaambia watu: Muje mukamuone Kristo, huyu mwenyi kuleta neema ya wokovu duniani.

## APOSTIKHA *Sauti ya ine. Os geneon en martisin.*

Ee Bwana wa huruma, Chemchem ya wema, Bahari ya mapendo, wewe mwenye kuleta uzima, namna gani ulimwomba mwanamuke Msamaria wakati ulikutana naye: Unipe maji ya kunywa kusudi

upokee maondoleo ya zambi? Tunatukuza rehema yako ya milele uliokoa nayo wanadamu wote kwa wema wako kubwa.

Shairi: Tembea katika nuru ya ufalme wako, linda ukweli, wena, na uhaki

Muje mukamwone mutu ambaye leo alipokaa pembeni ya kisima aliniambia mambo yote niliyotenda; kweli ni Nabii mkubwa, anajua siri zote za mioyo yetu na anawapa wale walio na kiu maji ya uzima kusudi tusiwe tena na kiu katika uzima wa milele.

Shairi: Unapenda haki, unachukia uovu, ndio maana Bwana Mungu wako alikupakaa mafuta ya furaha kuliko hata mumoja

Njiani, Chemchem ya milele, Uzima msiyekufa, maji safi isiyokauka alikaa pembeni ya kisima, akatuma Wafwasi wake kununua chakula; alipomuona mwanamuke mumoja aliyekuja kushota maji, akazungumuza naye kwa sababu alipenda kumuvua akiangaza macho ya roho yake

Utukufu kwa Baba... Sasa na siku zote...Sauti ya tatu.

Leo mbingu na inchi zinafurahi, kwa sababu Kristu ameonekana kama mutu mwenyi kuchukua mwili wetu sababu ya kuokoa adamu na wanadamu wote toka laana ya zamani. Kwa miujiza yake ya ajabu alikuja katika inchi ya Samaria; akaonekana kwa mwanamuke mumoja alikuja kushota maji, Yeye mwenye kuvaa mawingu ya maji ya mbinguni; na sisi wote waaminifu tunasujudu mbele ya huyu ambaye kwa wema wake alitwaa mwili wetu wa umaskini.

# MU KAZI INE MANGARIBI YA JUMA YA TANO YA MWANAMUKE MSAMARIA

*Kisha Proimiakos na «Bwana nimekuita...» tunaimba wimbo sita; tatu ya mwanamuke wa Samaria na tatu ya Mineon.*

***Wimbo ya mwanamuke wa Samaria***

*Sauti ya ine. Kirie anelthon en to Stavro.*

Mwanamuke Msamaria aliwaambia watu wa muji wa Sukari: Muje mukamwone Yesu Masiya yule Musa aliagua kuja katika Sheria yake; duniani anaonekana kama mutu pembeni ya kisima cha Yakobo na nilizungumuza naye; kweli ni Kristu anakuja duniani kutuokoa.

Ku midomo nzuri kulitoka maji ambayo watu wa muji walikunywa kama kinywaji kitamu : palepale wakaenda karibu ya kisima sababu ya kupata maji mengi ya umungu na kumuona Chemchem ya uzima mwenye kutuliza roho zetu.

Walipoona ya kama Chemchem anafanana nao, mwenyi hali sawasawa ya wanadamu, watu wa muji wakamwaambia mwanamuke wakasema: Si kwa sababu ya maneno yako tu sasa tunaamini, lakini kweli analeta duniani ukombozi na wokovu wa milele.

***Wimbo tatu ya Mineon.***

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya sita.*

Yesu alipomukuta Mwanamuke Msamaria karibu ya kisima cha Yakobo, akamuomba maji, yeye mwenyi kufunika inchi na mawingu! Ni ajabu! Huyu mwenyi kutembea juu ya Wakheruvi anazungumuza na mwanamuke mwovu; anaomba maji, yeye mwenyi kutundika inchi juu ya maji anatafuta maji, yeye mwenyi kujaza mitoni na viziwa; Lakini, kweli anataka kuokoa mwanamuke muovu toka mtego wa Adui, kumunywisha maji ya uzima sababu ya kuzima moto ya mateso yake, kwa wema wake na kwa mapendo yake kwa wanadamu.

**APOSTIKHA** *Sauti ya ine.*

Ee Kristu, tukiwa daima na msaada wa Msalaba wako, tunaweza kuokoka ku mutego wa adui.

Shairi:Nitanyanyula macho yangu kwako, ee mwenye kuikaa mbinguni...

Ee Bwana, ulipopanda juu ya Msalaba, ulizimisha mafingo yetu yakutoka kwa mababu zetu; na uliposhuka ndani ya hadeze, uliopoa wafungwa tangu zamani, ukaleta uzima usiyoharibika ku uzao wa watu; kwa hii tukiimba tunasifu ufufuo wako, uletao uzima na wokovu.

Shairi: Utuhurumie, ee Bwana, utuhurumie, kwani tunayala na kuzarauliwa...

Zabihu mzima, sadaka za kiroho, ee Mashahidi Watakatifu, zabihu zenyi kumpendeza Bwana Mungu wetu, Kondoo wenyi kumjua Bwana wao Mtakatifu na mwenyi kuwajua ambao zizi halifunguliwa kwa mbwa-mwitu, ombeni kwa Mchungaji Mwema ili pamoja nanyi atupeleke pia ku fasi ya mapmziko.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya sita*.

Bwana anamwambia hivi mwanamuke Msamaria: Kama ungalijua zawadi ya Mungu, na ni nani anakwaambia unipe maji ya kunywa, wewe ndiye ungalimwomba, naye angalikupa maji yaliyo hai kusudi usiwe na kiu tena hata milele.

# MU KAZI TANO ASUBUI YA JUMA YA TANO YA MWANAMUKE MSAMARIA

*Elezo: Kisha Eksapsalmos, Bwana ndiwe...» na Apolitikia, tunaimba:*

**KATHISMA YA KWANZA.** *Sauti ya ine. Takhi prokatalave.*

Ulipogiliwa Msalabani sababu ya kutuita kati ya wapagani, ee Bwana Mpenda-wanadamu, ulipanua mikono kwa kutaka kwako, na ukaitika ili ubavu wako uchomwe mkuki. Ee Mungu wa mapendo, utukufu kwako.

Ee Mwokozi msiyekufa, umefufuka, ukisanyika dunia yote pamoja nawe; kwa uwezo wako, ee Kristu Mungu wetu, ulivunja ufalme wa mauti, ee Mungu wa mapendo, uliwaonyesha watu wote Ufufuo. Wewe mwenye kutupenda, tunakutukuza.

Mashahidi wako, ee Bwana, kwa ajili ya mashindano walioshindana walipokea kwako, Mungu wetu, taji ya milele, waliposukumwa na nguvu yako waliangusha wazalimu na kuondoa nguvu ya mashetani; kwa maombezi yao okoa roho zetu, ee Kristu Mungu wetu.

**STAYROTHEOTOKION**

Alipokuona umetukuzwa Msalabani, Mama yako Mtakatifu, ee Neno la Mungu, akalia kwa umama na akasema: Hii ni mambo gani ya ajabu, ee Mwanangu? Wewe uliye uzima wa ulimwengu namna gani unaweza kushuka ku mauti? Lakini kwa rehema yako unataka kufufua wafu.

**KATHISMA YA MBILI.** *Sauti ya ine. Takhi prokatalave.*

Kama desturi, alipokuja kushota maji ku kisima chenyi kuharibika na cha dunia, Mwanamuke Msamaria alishota maji ya uzima wakati alimukuta Bwana Chemchem ya uzima amekaa pembeni ya chemchem na ya kisima cha Yakobo, Yeye mwenye kutuliza mateso ya dunia kama umande.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*(mara mbili)*

*Elezo: Kisha tunasoma:* Tukiona ufufuo wa Kristu, tumusujudu Yesu...*Kanuni ya Siku Kuu na Mineon. Kontakion na Eksapostilarion ya Siku Kuu ya mu Juma*.

**MASIFU** *Sauti ya ine.*

Kwa Kwa wale wenyi kukuogopa, ee Bwana, uliwapa alala ya Msalaba wako mheshimiwa: Katika hii ulishinda ufalme na nguvu za Gehena na ukatuleta ku furaha ya zamani; na tena tunatukuza mapendo yako kwa ajili yetu na tendo lako la wokovu, ee Bwana mwenyezi na Mwokozi wa roho zetu.*(mara mbili).*

Kwa Msalaba wako, ee Kristu Mwokozi, utuongoze kwa ukweli wako, na utuokoa toka mitego ya adui; Ewe uliyefufuka katika wafu, utufufue sisi tuliyoanguka katika zambi, myolosha mukono wako, ee Bwana Mpenda-wanadamu, kwa upatanisho ya watakatifu wako.

Ee Bwana, lufu ya marafiki zako ni tukufu : Kwa upanga, kwa moto ao kwa baridi, walitoa uzima wao katika matumaini ya kupata tunzo ya matendo yao, na uvumilivu wao uliwafaidia kwako, ee Mwokozi, neema ya wokovu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya sita.*

Yesu Mwokozi wetu aliye Chemchem ya uzima alipofika ku kisima cha Yakobo, akaomba maji kwa mwanamuke mumoja Msamaria; lakini kama vile huyu mwanamuke alisema juu ya uadui kati ya Wasamaria na Wayuda, Muumba mwenye hekima kwa maneno yake upole akamushauria kumupa maji ya uzima wa milele; na alipoipokea, akawapasha watu wote habari akasema:  Muje mukamuone huyu mwenyi kujua siri za mioyo yetu, Mungu aliyeonekana katika mwili sababu ya kuokoa wanadamu wote.

**APOSTIKHA** *Sauti ya ine. Os geneon en martisin.*

Alipokuja ku kisima cha Yakobo, Mwanamuke Msamaria akaacha mutungi wake bila maji, akaenda peke yake katika muji kuwaambia watu ya kwamba alimupata Chemchem ya uzima huyu alimupa maji ya wokovu na kutuliza roho yake yenye kukauka na mateso.

Shairi: Tembea katika nuru ya ufalme wako, linda ukweli, wena, na uhaki.

Mwokozi alimwambia Mwanamuke Msamaria:  Unasema kweli kwamba huna mume, kwani ulikuwa na wanaume watano, na yule unayeishi naye sasa si mume wako. Saa ileile akaenda kuwaambia watu wa muji ya kama:  Nimemuona mutu mumoja na ameniambia yote nilitenda kwa siri.

Shairi: Unapenda haki, unachukia uovu, ndio maana Bwana Mungu wako alikupakaa mafuta ya furaha kuliko hata mumoja.

Ku kisima cha Yakobo Mwanamuke Msamaria alishota ku kisima cha mbinguni maji ingine yenyi kuleta uzima : ilitelemuka toka chemchem huko alizoea kushota maji ya kuharibika yenyi kutoka katika udongo, lakini ikawa moyoni mwake maji yenyi kuchemuka, chemchem isiyojulikana yenyi kueneza umande juu ya tamaa zake.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya mnane.*

Ee Kristu Mungu wetu, wakati ulionekana katika mwili kama ilivyopenda wewe mwenyewe kwa ajili ya wokovu wetu, Mwanamuke Msamaria aliposikiliza neno lako na ukweli, akacha mutungi wake karibu ya kisima, akaenda kuwaambia watu wa mugini : „ Muje mumuone mutu mumoja mwenye kujua siri za mioyo yetu! Huyu si Kristu, Masiya aliyeongojewa, huyu aliye na neema ya wokovu?

# MU KAZI TANO MANGARIBI YA JUMA YA TANO YA MWANAMUKE MSAMARIA

*Kisha Proimiakos na «Bwana nimekuita...» tunaimba wimbo sita; tatu ya mwanamuke wa Samaria na tatu ya Mineon.*

***Wimbo ya mwanamuke wa Samaria***

*Sauti ya kwanza.* Idiomelon

Ee Chemchem ya miujiza, katika saa ya sita ya mchana ulikuja ku kisima cha Yakobo kukamata tunda la mama yake ya walio hai, kwani  katika hii saa  Eva alipodanganywa kwa nyoka alipoteza Paradizo. Mwanamuke Msamaria akajongea sababu ya kushota maji, na Mwokozi wakati ulipomwona, ukamwomba ukisema: Unipe maji ya kunywa na mimi nitakupa maji ya uzima wa milele. Mwanamuke alienda katika muji na hekima kuwapasha watu habari akisema: Muje mukamwone Kristo Bwana, Mwokozi wa roho zetu.

*Sauti ya mbili*

Bwana alikaa pembeni ya kisima cha Yakobo na Mwamamuke Msamaria akamwomba akisema:  Unipa maji ya imani, nitapokea maji ya ubatizo, ya furaha naukombozi; ee Chemchem ya uzima, Bwana, utukufu kwako.

*Sauti ya mbili*

Mwana na Neno wa Mungu mwenye kutawala na Baba wa milele alikuja ku kisima, yeye aliye Chemchem ya maponyesho; alafu, Mwanamuke Msamaria alikuja kushota maji na wakati alimwona, Mwokozi akamwambia: Unipe maji ya kunywa, na wende kumwita mume wako. Lakini huyu mwanamuke akajiharikisha kuficha sawa anazungumuza na mutu apana na Mungu, akasema: Sina mume. Bwana akamujibu: Unasema kweli kwamba huna mume, kwani ulikuwa na wanaume watano, na yule unayeishi naye sasa si mume wako. Kwa hii maneno mwanamuke akaogopa, akaenda katika muji kuwaambia watu: Muje mukamuone Kristo, huyu mwenyi kuleta neema ya wokovu duniani.

***Wimbo tatu ya Mineon.***

Utukufu kwa Baba...*Sauti ya sita.*

Yesu alipomukuta Mwanamuke Msamaria karibu ya kisima cha Yakobo, akamuomba maji, yeye mwenyi kufunika inchi na mawingu! Ni ajabu! Huyu mwenyi kutembea juu ya Wakheruvi anazungumuza na mwanamuke mwovu; anaomba maji, yeye mwenyi kutundika inchi juu ya maji anatafuta maji, yeye mwenyi kujaza mitoni na viziwa; Lakini, kweli anataka kuokoa mwanamuke muovu toka mtego wa Adui, kumunywisha maji ya uzima sababu ya kuzima moto ya mateso yake, kwa wema wake na kwa mapendo yake kwa wanadamu.

Sasa na siku zote...*Sauti ya ine***. THEOTOKION**

Nabii Daudi aliyekuwa Babu-Mungu kwa ajili yako, alikutabiri katika zaburi kwa yule aliyekufanya maajabu: Malkia anasimama ku mukono wako wa kuume. Kwa sababu Mungu alikuonyesha wewe mama muletaji-uzima, yeye aliyetwaa mwili toka wewe kwa mapenzi yake bila baba, kusudi aumbe mara ingine mufano yake, iliyoharibika kwa tamaa, na kupata kondoo alliyepotea mulimani, kumubeba ku mabega yake, na kumutoa kwa Baba, kwa kuiunganisha pamoja na Ezi za mbinguni kwa kutaka kwake, na kuokoa dunia, ee Mzazi-Mungu; yeye ni Kristu, mwenye kuwa na rehema kubwa zaidi.

**APOSTIKHA** *Sauti ya ine.*

Tukiabudu bila daima wako unaoleta uzima, ee Kristu Mungu, tunatukuza ufufuo wako wa siku tatu; kwa sababu ya hii ulifanya mupya asili ya watu iliyoharibika, ee Mwenyezi, na ukatuonyesha njia ya kupanda mbinguni, kwa kuwa wewe ni peke yako Mwema na Mpenda-wanadamu.

Shairi: Bwana anatawala mwenye kuvaa utukufu, Bwana anatawala anajifunga uwezo wake

Ee Mwokozi, kwa kuondoa mateso iliyoletwa na zambi juu ya muti iliyokataziwa, ulisulubiwa juu ya muti wa msalaba; na kwa kushuka kwako kuzimuni ulivunja milango ya mauti, ee Mungu mwenyezi; ndio maana tunabudu Ufufuo wako katika wafu, na kwa shangwe tunakutukuza tukisema: Ee Bwana mwenyezi, utukufu kwako.

Shairi: Ulikaza ulimwengu isitikisike, utawala wako ni imara daima.

Ulivunja milango ya Hadeze, ee Bwana, na kwa lufu yako, uliharibu ufalme wa mauti; na uliopoa ukoo wa watu toka uharibifu, mukuleta ku dunia uzima na usiyoweza kuharibika na rehema kubwa.

Shairi: Bwana, makao yako inastahili utakatifu, milele.

Ee Bwana, ulipopanda juu ya Msalaba, ulizimisha mafingo yetu yakutoka kwa mababu zetu; na uliposhuka ndani ya hadeze, uliopoa wafungwa tangu zamani, ukaleta uzima usiyoharibika ku uzao wa watu; kwa hii tukiimba tunasifu ufufuo wako, uletao uzima na wokovu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya mnane*.

Ee Kristu Mungu wetu, wakati ulionekana katika mwili kama ilivyopenda wewe mwenyewe kwa ajili ya wokovu wetu, Mwanamuke Msamaria aliposikiliza neno lako na ukweli, akacha mutungi wake karibu ya kisima, akaenda kuwaambia watu wa mugini: Muje mumuone mutu mumoja mwenye kujua siri za mioyo yetu! Huyu si Kristu, Masiya aliyeongojewa, huyu aliye na neema ya wokovu?

# MU POSHO ASUBUI YA JUMA YA TANO YA MWANAMUKE MSAMARIA

*Elezo: Kisha Eksapsalmos, Bwana ndiwe...» na Apolitikia, tunaimba:*

**KATHISMA YA KWANZA.** *Sauti ya ine.*

Walipoona mlango wa kaburi, na wasipoweza kuvumilia mwangaza wa Malaika wa nuru, Wanawake Watakatifu Wabebaji manukato wakaogopa na wakasema: Wamemuimba huyu aliyemfungulia Mnyanganyi Paradizo? Ameamka, huyu mbele ya Mateso yake alitangaza Ufufuo wake? Kweli amefufuka, Kristu Mungu wetu, akiwapa wale wa ku Hadeze uzima wa milele na kuwafufua.

Utukufu kwa Baba... *Sauti ya inne. Takhi prokatalave.*

Ee Mwokozi msiyekufa, umefufuka, ukisanyika dunia yote pamoja nawe; kwa uwezo wako, ee Kristu Mungu wetu, ulivunja ufalme wa mauti, ee Mungu wa mapendo, uliwaonyesha watu wote Ufufuo. Wewe mwenye kutupenda, tunakutukuza.

Sasa na siku zote...**THEOTOKION**

Siri ya kificho tangu milele iliyokuwa isijulikane na Malaika, imeonekana duniani katika wewe, ee Mzazi-Mungu; maana Mungu alitwaa mwili kwa ushirika, bila muchanganyo, na alikubali msalaba kwa kutaka kwake kwa ajili yetu; juu ya hii akifufua Muumbwa wa kwanza, akaokoa toka lufu nafsi yetu.

**KATHISMA YA MBILI** *Sauti ya ine. O Ipsothis en to Stavro.*

Mbingu ifurahiwe na wanadamu washangilie, kwa maana Kristu aliyezaliwa kwa Bikira ameonekana kama mwanadamu, kwa lufu yake anaokoa wanadamu wote toka uvumbi wa kaburi; kwa miujiza yake anaomba maji lakini anamupa mwanamuke Msamaria chemchem ya maponyesho, yeye aliye peke yake msiyekufa.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...Umoja

Tukiona…Zaburi 50 (51) *na kanuni ya Siku Kuu na Mineon. Kisha Kontakion na Eksapostilarion ya Siku Kuu ya mu Juma.*

## MASIFU *Sauti ya ine.*

Ewe uliyevumilia, Msalaba na lufu, na ulifufuka katika wafu, Bwana Mwenyezi, tunasifu Ufufuo wako.

Pa Msalaba wako, ee Kristu, ulituopoa toka fingo ya Kale, na kwa lufu yako uliharibifu Shetani, mwenye jeuri kwa hali yetu, na kwa ufufuo wako ulijaza vyote kwa furaha; kwa hii tunapaza sauti kwako: Ewe Bwana, uliyefufuka katika wafu, utukufu kwako.

Pa Msalaba wako, ee Kristu Mwokozi, utuongoze kwa ukweli wako, na utuokoa toka mitego ya adui; Ewe uliyefufuka katika wafu, utufufue sisi tuliyoanguka katika zambi, myolosha mukono wako, ee Bwana Mpenda-wanadamu, kwa upatanisho ya watakatifu wako.

Pasipo kujitenga toka kifua cha Baba yako, ee Mwana wa pekee Neno la Mungu, ulikuja duniani kwa kupenda-wanadamu, ukijifanya mtu bila ugeuzo, na ulivumilia katika mwili Msalaba na lufu, ee Msiyeteswa katika umungu; ukifufuka katika wafu, ulipatia uzima usiyokufa kwa uzao wa watu, sawa yako Mwenyezi.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya sita.*

Yesu Mwokozi wetu aliye Chemchem ya uzima alipofika ku kisima cha Yakobo, akaomba maji kwa mwanamuke mumoja Msamaria; lakini kama vile huyu mwanamuke alisema juu ya uadui kati ya Wasamaria na Wayuda, Muumba mwenye hekima kwa maneno yake upole akamushauria kumupa maji ya uzima wa milele; na alipoipokea, akawapasha watu wote habari akasema: Muje mukamuone huyu mwenyi kujua siri za mioyo yetu, Mungu aliyeonekana katika mwili sababu ya kuokoa wanadamu wote.

## APOSTIKHA *Sauti ya ine. Os geneon en Martisin.*

Mwanamuke mumoja alipomwona Chemchem isiyokauka amekaa pembeni ya kisima, kwa kuponyesha vidonda vya mateso yake, akamuomba maji ya uzima yenyi kutoka ndani yake, akaipokea kwa Neno kama zawadi ya bure kusudi asihitaji tena sasa kwenda ku kisima cha dunia na chenyi kuharibika cha hapa chini.

Shairi: Tembea katika nuru ya ufalme wako, linda ukweli, wena, na uhaki.

Mwanamuke alipokataa desturi za Wayuda na kusema Wayuda hawana mapatano na Wasamaria, Kristu akamushauria anywe maji yake na kwa maneno yake ya upole Muumba mwenye hekima akamuonya amuombe Yeye maji ya uzima, maji takatifu ambayo alikunywa yeye wa kwanza mbele ya kuyagawanya kwa watu wa muji wote.

Shairi: Unapenda haki, unachukia uovu, ndio maana Bwana Mungu wako alikupakaa mafuta ya furaha kuliko hata mumoja.

Mwanamuke Msamaria alimwambia Kristu: Hauna na chombo cha kushotea, na kisima kinakwenda chini sana, namuna gani utanipa hii maji ya uzima unasema? Alizani ya kama alikuwa mutu, apana Mungu, na alishangaa maneno yake; lakini Bwana akamunywisha neno lake la upole, akamuamini kama Mungu na Mwokozi wa ulimwengu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya sita.*

Bwana anamwambia hivi mwanamuke Msamaria: Kama ungalijua zawadi ya Mungu, na ni nani anakwaambia unipe maji ya kunywa, wewe ndiye ungalimwomba, naye angalikupa maji yaliyo hai kusudi usiwe na kiu tena hata milele.

# SIKU YA MUNGU YA KIPOFU TANGU KUZALIWA

## SIKU YA POSHO MANGARIBI KWA ESPERINOS

*Kisha: «*Bwana nimekuita...*», tunasimama pa shairi kumi; tunaimba wimbo saba ya Paraklitiki na mbili ya kipofu.*

*Sauti ya tano*

Kwa Msalaba wako muheshimiwa, ee Kristu, ulipatiya shetani haya, na kwa ufufuo wako ulifanya uchungu wa zambi kuwa bure, na ulituokoa toka milango ya mauti; tunakutukuza, ee Mwana wa pekee.

Huyu anayeleta ufufuo ku ukoo wa watu, alipelekwa kama kondoo kuchinjwa; wafalme wa hadeze wakatetemeka mbele yake, na milango ya maumivu iliyanyuliwa; kwani Kristu, Mfalme wa ututuku, aliingia, akiwaambia wafungwa: Tokeni, na wale walio katika giza, mujionyeshe.

Ajabu kubwa! Muumba wa wasioonekana, akiteswa kwa mwili kwa ajili ya kupenda wanadamu, akafufuka sawasawa na musiyekufa. Kujeni wazao wa mataifa, tumuabudu huyu; kwani kwa wema wake tukiondoshwa toka udanganyifu, tumefundishwa kuimba Mungu mmoja, katika aine tatu.

Tunautoa kwako uabudu wa mangaribi, ewe Nuru isiyomwisho uliyeangaza dunia kama katika kioo kwa mwili katika mwisho ya milele, na ulishuka mupaka Hadeze, na kule ulizambalisha giza, ukaonyesha nuru ya ufufuo kwa mataifa; Bwana muletaji-nuru, utukufu kwako.

Tumusifu Kristu, mkubwa wa wokovu wetu; kwani wakati huyu alipofufuka katika wafu, dunia imeokolewa katika udanganyifu, kundi la Malaika wanafurahi, udanganyifu wa mashetani unatoka; Adamu aliyeanguka amefufuka, na Shetani ameharibiwa.

Askari walinzi waliambiwa kwa wavunja-sheria: Mufich ufufuo wa Kristu, na mukamate feza, na museme: waakti tulipolala mufu aliimbwa toka kaburi. Nani aliona, nani alisikia siku moja watu wanaimba mufu? Na tena mwenye kupakaliwa na manukato na uchi, mwenye kuacha manguo yake ya maziko ndani ya kaburi? Musidanganyiwe, Wayuda; mufundishwe maneno ya manabii, na mujue ya kama kweli huyu ni Mwokombozi wa dunia na mwenyezi.

Bwana, uliyenyanganya Hadeze, na ulishinda mauti, Mwokozi wetu, uliyeangaza dunia, kwa Msalaba wako muheshimiwa, utuhurumie.

***Wimbo ya kipofu.*** *Sauti ya mbili*

Kipofu akasema ndani yake: Ni sababu ya zambi za wazazi wangu nimekuwa kipofu? Ni kwa kutukwamini kwa wapagani mimi nitakuwa mshuhuda? Sisubutu kuuliza kama ni mchana ao usiku! Miguu yangu yanakwaa mawe, maana sione nuru ya jua hata sura na mfano wa Muumba wangu; ndio maana nakuomba, ee Kristu Mungu wetu unitazame na unihurumie. *(mara mbili).*

Alipotoka hekaluni, Yesu akakutana na kipofu tangu kuzaliwa, akamuonea huruma; akamupakaa matope machoni: Akamwambia, wende ukanawe katika kisima cha Siloamu! Akasimama na akaona, akamushukuru Mungu. Jirani zake wakamwambia: Ni nani alikufungua macho? Kipofu akawajibu: Huyu anaitwa Yesu aliniambia: Wende ukanawe katika kisima cha Siloamu, na nimeona; kweli, mutu huyu ni ule Musa aliagua katika sheria yake ya kama ni Kristu, ni Masiya na Mwokozi wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba... *Sauti ya tano.*

Ee Bwana, njiani mwako ulikuta kipofu tangu kuzaliwa, Wafuasi wakakuuliza wakishangaa: Ee Rabi, nani basi alitenda zambi, ni Yeye ao ni wazazi wake? Lakini Mwokozi akawajibu: Ao yeye, ao wazazi wake hawakutenda zambi, lakini hii ilifanyika kusudu yaonekane ndani yake maajabu ya Mungu; kwani imenipaswa nitimize kazi ya huyu aliyenituma, na hakuna hata mumoja ataweza kuifanya kama mimi. Kisha kusema hivi, akatema mate chini akafanya utope, akaipakaa pa macho ya kipofu na akamwambia: Wende ukanawe katika kisima cha Siloamu! Kipofu akanawa na akapona, akapaza sauti na kusema: Ninaamini Bwana! Akasujudu mbele yake. Kama yeye na sisi pia tupaze sauti: Utuhurumie, ee Bwana.

Sasa na siku zote...**THEOTOKION.**

Katika Bahari Nyekundu, wakati moja mufano wa Bibi-arusi musiyeolewa ulijionyesha. Kule Musa alikuwa mugawanyi wa maji, hapa Gabrieli alikuwa mutumishi wa ajabu. Wakati ule Israeli alipita vilindini bila kulowanishwa, sasa Bikira alizaa Kristu bila mbegu; Bahari kisha kupita kwa Israeli ilibaki isiyowezekana kupita; Musiyeolewa kisha kuchukua Emmanueli, alibaki bila kuharibiwa. Mungu ndiwe uliye na uliyekuwako, na uliyefunuliwa sawasawa na mutu, utuhurumie.

**Kuingia**. *Kisha*: Mwangaza upole (ilaron)...

**PROKIMENON** *Sauti ya mbili.*

Bwana anatawala, amevikwa utukufu *(mara tatu).*

## APOSTIKHA *Sauti ya tano*

***Wimbo ya Paraklitiki****.*

Tunakutukuza kwa sauti ya nyimbo, ee Kristu Mwokozi, mwenye kutwaa mwili bila kugawanyika toka mbingu; kwani ulikubali Msalaba na lufu, kwa ajili ya ukoo wetu, kwa kuwa wewe ni Bwana mpenda-wanadamu; ukinyanganya milango ya Hadeze, ulifufuka katika siku tatu kwa kuokoa nafsi yetu.

*Tangazo: Kisha tunaimba WIMBO YA PASKA (Angalia Masifu ya Orthros ya Paska):*

*Sauti ya tano*

1. Paska zabihu leo imeonekana kwetu, Paska mupya Takatifu. . .
2. Kujeni Wanawake. . .
3. Wanawake Wabebaji manukato. . .
4. Paska ya furaha, Paska ya Bwana Paska. . .

Utukufu kwa Baba. . .*Sauti ya mnane.*

Jua la hai, ee Kristu Mungu wetu, kwa mkono wako safi kamili uliangaza huyu aliyekuwa kipofu tangu tumboni mwa mama yake; angaza pia macho ya roho zetu, utufanye sisi kuwa wana wa nuru na wa mchana kusudi kwa imani tuweze kukulalamikia: Kubwa na isiyokadirika ni rehema yako kwa ajili yetu, ee Bwana mpenda-wanadamu, utukufu kwako.

Sasa na siku zote. . .

Ufufuo ni leo na tuangazwe kwa Karamu. . .

Apolitikion ya Ufufuo. *Sauti ya tano.*

Neno lasipo mwanzo pamoja na Baba na Roho, huyu alizaliwa kwa Bikira kwa ajili ya wokovu wetu; basi, waaminifu, tumwimbie na tumwabudu; kwani mapenzi yake katika mwili, alipanda juu ya msalaba, akavumilia lufu, na alifufua wafu, katika ufufuo wake muheshimiwa.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...**THEOTOKION**

Salamu, mulango wa Bwana usioweza kupitwa; Salamu, ukuta na kivuli cha wale waliokimbilia kwako; salamu, kivuko bila kutikisika, na musiyeolewa, uliyezaa katika mwili Muumba na Mungu wako; usiache kupatanisha kwa ajili ya wale walikuimbia, na walioabudu Mwana wako.

**Kuaga.**

## SIKU YA MUNGU ASUBUI YA KIPOFU TANGU KUZALIWA

**KATHISMA WA KWANZA**. *Sauti ya tano.*

Kwa mashairi na nyimbo zetu tusifuni Msalaba mweshimiwa wa Bwana, tutukuzeni Kaburi, tutukuzeni Ufufuo wako takatifu, kwani Mungu wetu amewafufua wafu kaburini, akanyanganya ufalme wa mauti na kuharibu nguvu ya shetani, nuru yake ikasimama juu ya wafungwa kuzimuni.

Utukufu kwa Baba...

Ee Bwana, ulihesabiwa kati ya wafu, wewe uliyeua mfalme wa mauti, uliwekwa kaburini, wewe mwenye kwacha makaburi tupu; duniani kaburi yako ikalindwa na maaskari, kuzumuni ukawafufua wafu walioyolala tangu milele. Ee Mungu mwenyezi ambaye ulimwengu hauwezi kuzungusha, ee Bwana, furaha yetu, utukufu kwako.

Sasa na siku zote...**THEOTOKION**.

Salamu, mlima takatifu aliyopanda Bwana, salamu, kichaka kisipoteketezwa, salamu, kilalo cha dunia cha kwenda kwa Mungu, wewe mwenyi kupoleka ku uzima wa milele, salamu, ee Bikira msiyeolewa uliyezaa wokovu wa roho zetu.

**KATHISMA WA MBILI.** *Sauti ya tano*

Ee Bwana, makafiri walikusulubisha msalabani katikati ya wanyanganyi, walichoma ubavu wako kwa mkuki; ee Mungu wa mapendo, uliitika kuzikwa kaburini, wewe uliyevunja milango ya Hadeze, na ukafufuka siku ya tatu; wanawake walikuja wapezi kukuona, wakawatangazia Mitume Ufufuo. Ee Mungu aliye-juu ambaye Malaika wanaimbia, umetukuzwa, ee Bwana, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba...

Ee Mwokozi, fumbo yako ya ajabu kwa ajili ya ulimwengu inaonyesha wokovu: Ulipofufuka kaburi kama Mungu, ee Mungu, ulifufua wanadamu pamoja nawe; ee Chemchem ya uzima, Bwana, utukufu kwako.

Sasa na siku zote..**THEOTOKION**.

Bibi arusi asiyeolewa na mzazi-Mungu aliyebadilisha mateso ya Eva kuwa furaha, sisi waaminifu tunakuimbia na tunasujudu kwako; kwa maana ulituondoa toka laana ya zamani, ee Bikira Mtakatifu kamili mwenye kustahili nyimbo zetu, umuombe kwa ajili ya wokovu wetu.

*Kisha waimbaji wanaimba Mahimidi ya Ufufuo na kisha msomaji anasoma Ipakoi:*

**IPAKOI (UTII)**

Walipoogopeshwa kwa mwangaza wa malaika, walipoangazwa kwa nuru ya ufufuo, Mirofori wakaenda mbio kwa Mitume wakasema: Tangazieni mataifa yote habari njema ya Ufufuo wa Bwana wenye kutenda hapa chini maajabu ya nuru na kutupatia neema kubwa.

**ANAVATHMI NA PROKIMENON**

*(Tafuta mu Kitabu ya Paraklitiki) Sauti ya tano.*

**EVANGELION EOTHINON YA MNANE**

Tukiona ufufuo wa Kristu...Zaburi 50 (51).

*Kisha tunaimba Kanuni ya Paska na ya Kipofu. Ni hii:*

## KANUNI YA KIPOFU

**WIMBO WA KWANZA**. *Sauti ya tano.*

**IRMOS:** Inchi huko jua halijaonekana, zimu ambako halijaona mbingu wazi, Izraeli alipitako pakavu, na, ee Bwana, uliwaongoza mpaka kwa mlima wa utakatifu, kwa wimbo wa ushindi.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Uliteswa mwilini Msalabani kwa kutaka kwako, ulieneza uzima na baraka duniani, peke yako Bwana utukufu wa wote na Muumba wa ulimwengu: Tunakuimbia, tunakutukuza, tunakuhimidi kwa wimbo wa ushindi.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Ee Bwana mvumilivu, Mtukufu Yosefu aliweka mwili wako takatifu kaburini, akaweka jiwe katika mlango wa kaburi, lakini ulifufuka kwa utukufu, ukafufua dunia pamoja nawe kwa wimbo wa ushindi.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Malaika mwenye kuangaa aliwaambia wanawake «sababu gani munachanganya machozi yenu na manukato munayoleta? Kristu amefufuka! Kwendeni mbio mukawapashe Mitume watakatifu habari, wao wanaomboleza na kulia, kusudi wafurahi.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Mkombozi mwenyi kufanya miujiza ya ajabu anaponyesha pia na matope kipofu tangu kuzaliwa na anamwambia: Wende ukanawe katika kisima cha Siloamu sababu ya kumutambua Mungu wako anapotembea inchini, mwenyi kuvaa mwili na nzuri wake.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Enyi waaminifu, tutukuzeni umoja wa wafu tatu tutukuzeni Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, Muumba tena Mkombozi wa ulimwengu, peke yake Mungu asiyeumbwa ambaye tunaimbia pamoja na malaika: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ni wewe Bwana Mfalme wetu.

Mtakatifu kamlili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe…**THEOTOKION**

Ee Bikira kwa wema wake Bwana alipotaka kuokoa mwanadamu aliyeanguka kwa werevu wa adui, akakaa tumboni mwako usiyeolewa: Umuombe alinde wakristu kwa makamio yote yenyi kuwaelemewa.

**WIMBO YA TATU**

**IRMOS:** Ee Bwana mvumilivu, ulisabitisha roho zetu zenyi kuzama wakati dunia yote ilitikisika kwa kusulubiwa kwako mwilini.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Ee Mungu wa mapendo, mtukufu Uosefu alikuweka ndani ya kaburi mupya, na ulitufanya kuwa wapya kwa Ufufuo wako katika wafu ya tatu.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Malaika wenye kwangaa na nuru ya Mungu aliwaambia wanawake? Sababu gani munamutafuta Bwana katika wafu? Amefufua kama alivyoahidi.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Ee Mungu wa mapendo, zamni uliponyesha kipofu tangu kuzaliwa wakati alikujongea, akatukuza maajabu yako na tendo lako la wokovu.

Utukufu kwa Baba...

Tunaabudu kama Mungu mumoja watu tatu ambao hata mumoja wao hakuumbwa Baba, Mwana na Roho Mtakatifu.

Sasa na siku zote...**THEOTOKION**

Ee Bibi Mtakatifu kamili, ulizaa tumboni mwako mwa bikira Mungu mwenye kuvaa mwili: Umuombe atuhurumie.

**KATHISMA** *Sauti ya mnane. Tin sofian ke logon*.

Rabi na Muumba wa ulimwengu alipotembea njiani akakutana na kipofu tangu kuzaliwa mwenyi kukaa, akilia na kusema: tangu kuzaliwa kwangu sijaona nuru ya jua wale mwezi kutoa mwanga wake, ndio maana nakulalamikia, ee Bwana uliyezaliwa kwa Bikira sababu ya kuwangazia ulimwengu wote: Kwa rehema yako angazia pia mutumishi wako kusudi nikuimbie nikisujudu mbele yako; Ee Kristu Mungu wetu, kwa wema wako kubwa unisamehe makosa yangu, peke yako mupenda-wanadamu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*(mara ingine).*

**KONTAKION** *Sauti ya ine.*

Ee Bwana, kama kipofu tangu kuzaliwa, macho ya roho yangu ni yenye kufunga kwa toba nakuja kwako na napaza sauti: Kwa wale wenye kuwa katika giza wewe ni nuru kubwa.

**IKOS**

Ee Kristu, unipe hekima nyingi isiyokadirika na maarifa ya Jua mbinguni, wewe Nuru ya roho zenyi kupofuka tena mwongozi wa wakosefu, ili nitangaze miujiza ya kipofu tangu kuzaliwa kama inavyofundisha kitabu takatifu, Habari njema ya amani; kipofu tangu kuzaliwa anaona na macho pia ya roho, na kwa imani anapaza sauti: Kwa wale wenye kuwa katika giza wewe ni nuru kubwa.

**SINAKSARI**

Leo, Juma ya sita kisha Paska, tunashangilia muujiza wa Bwana wetu, Mungu na Mwokozi Yesu Kristu kwa Kipofu tangu kuzaliwa.

Nuru toka Nuru na Chemchem ya nuru, ee Neno, unafungua macho hata ya Kipofu tangu kuzaliwa!

Kwa rehema yako kubwa, ee Kristu Mungu wetu, wewe mwenye kuleta nuru, utuhurumie na utuokoe. Amin.

**KATAVASIA**

Wimbo ya Kwanza. *Sauti ya Tano*. t

Mungu Mwokozi aliyeongoza wana wa Israeli pakavu baharini Nyekundu, akizamisha Farao na jeshi lake lote, tumwimbe kama peke yake ni mstahili wa nyimbo zetu, kwani amevaa utukufu.

Wimbo ya Tatu.

Ee Kristu, kwa uwezo wa Msalaba wako sabitisha nia zetu, sababu ya kuturuhusu kuimba na kutukuza kupaa kwako kwenyi kuleta wokovu.

Wimbo ya Ine.

Bwana, nilisikia sauti yako, niliungama nguvu ya Msalaba wako, maana kwa hii Paradizo ilifunguliwa na nilisema: Utukufu ku uwezo wako, ewe Bwana.

Wimbo ya Tano.

Bwana kwa hii zamu na kwa matumaini ya asubui, tunakulalamikia: Hurumia na utuokoe, kwani ndiwe kweli Mungu wetu, hatujui mwengine ila Wewe.

Wimbo ya Sita.

Shimo ilinizunguka pande zote, nyama alinikamata kama kaburiri; Mpenda-Wanadamu, nililalamika kwako na kume kwako, ee Bwana, kuliniokoa.

Wimbo ya Saba.

Mwokozi uliyekinga katika tanuru ya moto Vijana waliokuimba, umetukuzwa, Bwana, Mungu wa Baba zetu.

Wimbo ya Mnane.

Mwana wa Mungu, aliyezaliwa kwa Baba mbele ya nyakati, akajifanya mtu Bikira Mzazi-Mungu: Ninyi makohani, mutukuzeni, enyi mataifa yote, makuzeni milele.

Wimbo ya Tisa.

Ewe Mzazi-Mungu, uliposhinda akili yetu na usikilizi wetu, ukamzaa mu wakati Bwana wa milele; kwa sauti moja na kwa moyo moja, sisi waaminifu, tunakusifu.

## EKSAPOSTILARION *Sauti ya mbili.*

Ya Ufufuo ya Kristu.

Kwa mwili, ee Mufalme na Bwana ulipolala kama mutu mwenye kuweza kufa, ulifufuka siku ya tatu; ukisimamisha Adamu toka uharibifu na uliharibu mauti, ewe Paska uzima usiyoharibika Mwokozi wa dunia.

Ya Kipofu. *Sauti ya mbili.*

Ee Bwana, tuma nuru yako na ukweli wako kwa macho yangu ya roho yenyi kupofuka na giza ya zambi, ee Mungu wa mapendo, uyaongoze na macho ya unyenyekevu, na kwa machozi ya toba unitakase mimi wote.

Ingine. *Sauti ya mbili. Ginekes akutisthite.*

Kama alivyipita njiani, Mwokozi wetu akakutana na mtu mmoja mwenyi kupofuka macho, ni kipofu tangu kuzaliwa; Kristu akatema mate chini akafanya matope, akayapakaa machoni mwa kipofu; kisha akamwambia ende kunawa katika kisima cha Siloamu: Kipofu aliponawa akarudi mwenyi kuona vizuri nuru yako, ee Kristu.

## MASIFU *Sauti ya tano.*

Bwana, wakati kaburi ilipotiliwa muhuri kwa wavunja-sheria ulitoka katika kaburi, sawa ulizaliwa kwa Maza-Mungu; Malaika wako wasiyo-mwili hawakujua namna gani ulitwaa mwili; Askari waliokuchunga, hawakusikia wakati gani alifufuka; kwa sababu hii mambo ya ajabu ilifichwa kwa wenye kutafuta; lakini miujiza hii zimeonekana kwa wenye kuabudu siri kwa imani na wanaoimba: Uturudishie shangwe na rehema kubwa.

Bwana, ukivunja mapingo ya milele, ukikata minyororo, ulifufuka toka kaburi, ukiacha sanda, kusudi ya kuishuhudia kweli maziko yako ya siku tatu; na ulitangulia kwa Galilaya, mwenye kulindwa katika pango. Rehema yako ni kubwa, ee Mwokozi msiyesikilikwa! Utuhurumie.

Bwana, wanawake walienda kwa haraka kaburini, kusudi wakuone, ewe Kristu, uliyeteswa kwa ajili yetu; na wakifika, walikutanisha Malaika mwenye kukaa juu ya jiwe, lenye kufingirishwa kwa sababu ya woga, naliwapazia sauti, akisema: Bwana alifufuka; museme kwa Wanafunzi, ya kama alifufuka katika wafu, mwenye kuokoa nafsi yetu.

Bwana, kama vile ulitoka japokuwa kaburi imefungwa, vivyo hivyo uliingia waakti milango ilipofungwa, na ulionekana mbele ya Wanafunzi wako, kwa kuwaonyesha mateso ya mwili wako, uliyokubali, ee Mwokozi muvumilivu; sawa na mutu, muzaliwa wa ukoo wa Daudi, ulivumiulia mapigo; lakini sawasawa na Mwana wa Mungu, uliopoa dunia. Rehema yako ni kubwa, ee Mwokozi msiyesikilikwa! Utuhurumie.

Bwana, mfalme wa milele, Muumba wa vyote, mwenye kukubali kwa ajili yetu katika mwili usulubisho na maziko, kwa kutuopoa sisi wote toka Hadeze, wewe ni Mungu wetu; hatumujui mwengine ila wewe peke yako. Bwana, nani atakayehadisia maajabu yako ya nuru kabisa? Ao nani atakayejulisha siri ya ajabu? Kwa maana ukijifanya mtu kwa ajili yetu, kama ulivyotaka, ulionyesha uwezo wako kwa mamlaka; kwa sababu kwa msalaba wako ulifungua Paradizo mbele ya munyanganyi, na kwa maziko yako ulivunja mapingo ya Hadeze, na kwa ufufuo wako uliwinisha ulimwengu. Ewe mwenye rehema, utukufu kwako.

Wanawake mabebaji-manukato, asubui mapema wakishika kaburi yako, walitafuta kupakaa manukato, ewe Neno na Mungu msiyekufa; na wakati waliposikia maneno ya Malaika, walirudi kwa furaha, kusudi wajulishe wazi kwa Mitume, ya kama ulifufuka, Uzima wa wote na unaleta duniani usamehe na rehema kubwa.

***Wimbo ya Kipofu***

*Sauti ya mnane.*

Shairi: Unitazame na unihurumie.

Ee Kristu Mungu wetu uliyejifanya mtu kwa kutaka kwako, kwa mapendo yako isiyokadirika ulimupa kipofu tangu kuzaliwa nuru ya umungu; kwa kidole chako cha Muumba uliweka matope machoni mwake, na Wewe mwenyewe Bwana mwenyi kuleta nuru, angazia sasa roho yetu kwa ukarimu wako wa mfalme.

Utukufu kwa Baba...Sauti ya mnane.

Ee Kristu, nani ataweza kusema uwezo wako ao kueleza miujiza yako ya milele? Na kama ulivyoonekana duniani katika hali mbili, uliwapa wagonjwa maponyesho mbili, kwani kwa kipofu tangu kuzaliwa haukumufungua paka macho ya mwili bure, lakini uliangaza macho ya roho yake; ndio maana alikutambua wewe kuwa Mungu mwenye kujificha machoni mwetu na mwenyi kuleta duniani neema kubwa.

Sasa na siku zote...Mbarikiwa ukupita, ewe Mzazi-Mungu...

## MU JUMA MANGARIBI YA KIPOFU TANGU KUZALIWA

*Kisha : «*Bwana nimekuita...*» tunaimba waimbo tatu ya kipofu na tatu ya Mineon.*

***Wimbo tatu ya Kipofu***

*Sauti ya tano. Kheris askitikon.*

Ee Neno, wewe ni taa yenyi kuangazia viungo vyetu vyote vya wanadamu, ee Mungu, wewe ni jicho la mwili wetu hapa chini, wewe Muumba wa macho mwenyi kuyafanya mara ingine tena, maana kwa mchanganyo wa mate na matope unafungua macho ya kipofu kwa vidole vyako zamani uliumba navyo pia udongo na nuru; na kipofu aliyejulikana kwa wote ya kwamba haonake nuru ya jua sasa

anakuona kama Jua la nuru ya furaha, anaona sura ya huyu, kwa mapendo yake isiyokadirika, alituumba na kututengeneza.

Alipojaliwa na yote yenye kuunga mwili wa mwanadamu, huyu aliyezaliwa kipofu kwa mama yake hakuwazia ya kama hali ingine inaweza kuwako, kwa sababu alipofuka macho, miguu yake na mwili wake yalikwaa njiani, lakini wakati kwa ajili yako alipata hii hazina, alipoona nuru ya dunia akakutangaza kama Rabi na Bwana wa nuru yote, Muumba wa viumbe vyote.

Alileta shaka kwa Waandishi wa sheria, huyu kipofu wa zamani maana ameona kama macho yake hayakufunguliwa, lakini kwa wao alidanganya kuona sababu ya Mwokozi, maana wao wenyewe walipenda giza kuliko nuru Kristu alileta yeye aliye Jua la nuru ya furaha, kwa ajili yetu alifanya siku Kuu mpya ya Sabato, anangazia giza ya Sheria, anaondoa pazia sababu ya kuwangazia vipofu wa zamani ambao sasa wanatangazia dunia huyu waliona: Ndiye Bwana, Chemchem yetu ya nuru.

***Wimbo tatu ya Mineon***

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya mbili*

Kipofu tangu kuzaliwa aliulizana ndani yake: Ni kwa sababu ya zambi za wazazi wangu nimekuwa kipofu? Ni kwa kutokuamini kwa wapagani nitakuwa mshuhuda? Sisibutu kuuliza kama ni mchana ao ni usiku. Miguu yangu hayaepuke kukwaa, maana sione nuru ya jua ao sura na mfano wa Muumba wangu; ndio maana nakuomba, ee Kristu Mungu wangu, unitazame sababu ya kunihurumia.

## APOSTIKHA. *Sauti ya tano.*

Kwa Msalaba wako muheshimiwa, ee Kristu, ulipatiya Shetani haya, na kwa ufufuo wako ulifanya uchungu wa zambi kuwa bure, na ulituokoa toka milango ya mauti; tunakutukuza, ee Mwana wa pekee.

Shairi: Nitanyanyula macho yangu kwako, ee mwenye kuikala mbinguni, tazama macho ya watumishi yanaangalia kwa mkono wa Bwana kama macho ya kijakazi kwa mkono wa bibi yake, hivyo macho yetu yanavyoangalia kwa Bwana Mungu wetu hata akatuhurumia.

Ee Bwana, siache kutenda zambi, nasahau mapendo uliyonizungusha: Ponyesha ugumu wa moyo wangu, peke yako Mungu wa wema, unihurumie.

Shairi: Utuhurumie, ee Bwana, utuhurumie, kwani tunayala na kuzarauliwa. Nafsi yetu inayala na kuzarauliwa kwa wenye kuikala na salama tena na kuzarau kwa wenye kiburi.

Mashahidi wakuu muliyozarau mema ya hii uzima sababu ya kupambana na mateso, katika matumaini yenu hamukunyanywe furaha yenu, lakini mumeriti ufalme wa mbinguni, na kwa maana munaweza kumdai Mungu mwema, mumuombe amani ya dunia na neema ya wokovu wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya mbili*.

Alipotoka hekaluni, Yesu alikutana na kipofu tangu kuzaliwa, akamuhurumia; akamupakaa matope machoni, akamwambia: Wende ukanawe katika kisima cha Siloamu! Akasimama na akaona, akamushukuru Mungu. Jirani zake wakamuuliza: Ni nani alikufungua macho ambayo mutu hata mumoja mwenyi kuona hawezi kuponyesha? Kipofu akawajibu: Ni huyu anayeitwa Yesu aliniambia: Wende ukanawe katika kisima cha Siloamu! Na nimeona; Mutu huyu eko kweli huyu Muza alisema katika Sheria yake ya kama ni Kristu, ni Masiya na Mwokozi wa roho zetu.

**Apolitikion**: Neno lasipo mwanzo....

**Theotokion**: Salamu mulango wa Bwana...

# MU KAZI MOJA ASUBUI KWA ORTHROS

### KATHISMA YA KWANZA *Sauti ya tano.Ton Sinanarkhon Logon.*

Kwa mashairi na nyimbo zetu tusifuni Msalaba mweshimiwa wa Bwana, tutukuzeni Kaburi, tutukuzeni Ufufuo wako takatifu, kwani Mungu wetu amewafufua wafu kaburini, akanyanganya ufalme wa mauti na kuharibu nguvu ya shetani, nuru yake ikasimama juu ya wafungwa kuzimuni.

Tukesheni juu ya kwenda kukutana na Kristu, na vyombo vyetu vyenyi kujaa na mafuta na taa zetu zenyi kuwaka sababu ya kuweza kuingia katika chumba chake; kwani mbele ya milango yanye kufunga ni bure tutamulalamikia Mungu: Utuhurumie.

Utukufu kwa Baba...

Mashahidi wako, ee Bwana, kisha wewe walikunywa kikombe cha mateso yako, walikataa furaha za hii uzima; wakawa wenzao wa Malaika. Kwa maombezi yao, ee Bwana, samehe roho zetu na leta neema ya wokovu ku roho zetu.

Sasa na siku zote.. **THEOTOKION**

Pamoja na malaika mbinguni, pamoja na wanadamu duniani, tunakuimbia kwa furaha, ee Mzazi-Mungu: Salamu, ewe mlango pana kuliko mbingu, salamu, wewe peke yako msaada wa wanadamu, salamu, ewe mjaliwa neema uliyezaa Mungu mwilini.

**KATHISMA YA MBILI** *Sauti ya tano. Ton sinanarkhon Logon.*

Mbele ta Msalaba wako na Ufufuo wako, ee Mungu wa mapendo, ulikutana na kipofu tangu kuzaliwa aliyekulalamikia na furaha: Ee Mwana wa Mungu, unihurumie, leta nuru machoni mwangu ili niweze kuona, mimi pia! Hapo, ee Neno, ukapakaa machoni mwake mate yako yenyi kuchanganyika na udongo sababu ya kumupa nuru yako ya furaha.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...(*mara mbili).*

Tukiona ufufuo wa Kristu...Zaburi 50 (51).

*Kisha tunaimba Kanuni ya Paska na ya Kipofu. Tena tunasoma Kontakion, Ikos na Eksapostilarion ya Siku Kuu ya Kipofu.*

## MASIFU. *Sauti ya tano.*

Bwana, wakati kaburi ilipotiliwa muhuri kwa wavunja-sheria ulitoka katika kaburi, sawa ulizaliwa kwa Maza-Mungu; Malaika wako wasiyo-mwili hawakujua namna gani ulitwaa mwili; Askari waliokuchunga, hawakusikia wakati gani alifufuka; kwa sababu hii mambo ya ajabu ilifichwa kwa wenye kutafuta; lakini miujiza hii zimeonekana kwa wenye kuabudu siri kwa imani na wanaoimba: Uturudishie shangwe na rehema kubwa. *(mara mbili).*

Ole wangu! Mara ngapi ninafanana na mtini isiyozaa matunda! Naogopa laana na shaka, lakini wewe mtunza shamba wa mbinguni, ee Kristu Mungu wetu, stawisha roho yangu kukauka, unipokee kama Mwana mpotevu na unihurumie.

Litukuzwe jeshi la mfalme wa mbinguni maana walipozaliwa duniani Mashahidi Washindaji hawakutamainia cheo cha Malaika: Walipozarau mwili na kuteswa mateso yao, wakastahili utukufu wa malaika; kwa maombezi yao, okoa roho zetu, ee Bwana.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya mbili.*

Ee Bwana, kipofu alipoishi uzima wake wote katika giza, akalalamika: Unifungua macho, ee Mwana wa Daudi tena Mwokozi wangu, kusudi pamoja na watu wote niimbie mimi pia uwezo wako.

## APOSTIKHA. *Sauti ya tano. Osie pater.*

Katika kipofu wenye kuona waliona paka upofu wenye kupofusha roho yao, moyo wao na akili yao wakati waliona kuona kwake kuwa regevu; kwa sauti kali wakauliza; Namna gani macho yako yamefunguliwa kama yale ya mutu mwenye kuona, wewe uliye kipofu tangu kuzaliwa na zamani ulikaa njiani kwa kuomba? Halafu akawaonyesha Chemchem ya nuru, huyu mwenye kutangaziwa kama Mwana wa Mungu wa milele na ambaye kwa nyakati za mwisho alionekana kwama mwanadamu aliyezaliwa kwa Bikira na kwa Roho Mtakatifu, kwa mapendo yake kwa ajili yetu.

Shairi: Unitazame na unihurumie.

Kama mzito na mzigo ni hivi alionekana duniani kipofu akitembea na kukwaa katika mawe njiani; akatumia bakora pahali pa nuru ilimukosa, anamujongea Vhemchem ya nuru mwenye kumupa nuru juu ya macho yake; anamuona Muumba wake aliuumba zamani wanadamu toka udongo kwa sura yake na mfano wake na sasa kwa mate na matope anangaza mboni za macho yake, na kwa wema wake anamupa kuona jua.

Shairi: Kwa neno lako ongoza batua zangu ili uovu isiwe na nguvu juu yangu.

Alipofanana na wanadamu Neno la Baba anaonekana kwa kipofu akimufunulia nuru; kama wengine, anaona Jua mubebaji-nuru tena Chemchem ya mchana, akafurahia zawadi mpya ya kuona

iliyomuwezesha kutembea sawa bila kosa njiani; alipomtambua mletaji-nuru kama Mwana wa Mungu alipotwa mwili kwa wema wake kubwa, Mungu aliyejifanya mtu akakaa kama alivyokuwa sababu ya kuchukua hali ya vile yeye mwenyewe hakuwa, akaunganisha hali mbili bila kuchanganyika.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya tano.*

Ee Bwana, njiani mwako ulikuta kipofu tangu kuzaliwa, Wafwasi wakakuuliza wakishangaa: «Ee Rabi, nani basi alitenda zambi, ni yeye ao wazazi wake ili azaliwe hivi kipofu? Lakini uliwajibum ee Mwokozi: Ao yeye ao wazazi wake hawakutenda zambi, lakini ili maajabu ya Mungu yaonekanendani yake; kwa sababu imenifai kutimiza kazi ya huyu aliyenituma na hakuna hata mumoja anaweza kuifanya». Aliposema hivi, akatema mate chini akafanya matope, akaipakaa machoni kwa kipofu na kumwambia: Wende ukanawe katika kisima cha Siloamu! Kipofu akaamka na akapona, akapaza sauti: «Ninamini, ee Bwana». na akamusujudu. Kama yeye, sisi pia tunapaza sauti: Utuhurumie, ee Bwana.

# MU KAZI MOJA MANGARIBI YA JUMA YA SITA

**ELEZO:** *Leo tunafanya Sindikizo ya siku Kuu ya Kipofu. Kisha: Bwana nimekuita tunaimba wimbo sita ya Siku Kuu ya Kipofu. Kisha tunafuata desturi ya Apostikha.*

**Kama mpadri hasitake kufanya hii Sindikizo, atafata desturi hii ifwatayo:**

*Kisha : Bwana nimekuita, tunaimba wimbo tatu ya Siku Kuu ya Kipofu na tatu ya Mineon.*

***Wimbo ya Siku Kuu ya Kipofu***

*Sauti ya tano. Kheris askitikon.*

Kwa kinywa kwa moyo na kwa akili yake kipofu wa zamani alimutambua huyu ambaye kwa mate yenyi kuchanganya na udongo alifungua mboni za macho yake ili aone nuru; katika yeye akamkiri Muumba wa ulimwengu ambaye kwa mapendo yake kwa ajili yetu alitwaa mwili wetu, akamtangaza kama Mungu mwenyezi; ndio maana Waandishi wasiyoweza kuvumilia bidii yake na ukweli wa masemo yake walimufukuza toka Sinagogi, wakaonekana kwa mwili na kwa roho kuwa vipofu kabisa kupita kipofu wa zamani.

Kwa kiasi chake alifanya ushindi wa ushijaa juu ya wenye kuona, kwa maana japo na kipofu, anaona Muumba wake, huyu aliyeumba ulimwengu na kwa mate yake anafanya mpya mboni za macho yake ili aone; kwa hii, peke yake akamutambua Mletaji-nuru yake kama ni Mwana wa Mungu tena Bwana wa ulimwengu ambaye hawakuona wenye kuona ambao walipofuka kwa uovu na wivu hata kama waliona miujiza mikubwa sana, ishara ya ajabu neno peke aliweza kufanya.

Alileta shaka kwa Waandishi wa Sheria, huyu kipofu wa zamani, maana ameona kama macho yake hayakufunguliwa. Lakini kwa wao alidanganya kuona sababu ya Mwokozi, maana wao wenyewe walipenda giza kuliko nuru Kristu alileta, yeye aliye Jua la nuru ya furaha, kwa ajili yetu alifanya siku Kuu mpya ya Sabato, anangazia giza ya sheria, anaondoa pazia sababu ya kuwangazia vipofu wa zamani ambao sasa wanatangazia dunia huyu waliona: Ndiye Bwana, Chemchem yetu ya nuru.

***Wimbo tatu ya Mineon.***

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya mnane.*

Ewe Jua ya haki, Kristu Mungu wetu, kwa mkono wako takatifu kamili uliangaza huyu alikuwa kipofu tangu tumboni mwa mama yake; angaza pia macho ya roho zetu, mtufanye sisi kuwa wana wa nuru na wa mchana kusudi kwa imani tuweze kukulalamikia: «Kubwa na isiyokadirika ni rehema yako kwa ajili yetu, ee Bwana mpenda-wanadamu, utukufu kwako.

**APOSTIKHA** *Sauti ya tano.*

Huyu anayeleta ufufuo ku ukoo wa watu, alipelekwa kama kondoo kuchinjwa; wafalme wa hadeze wakatetemeka mbele yake, na milango ya maumivu iliyanyuliwa; kwani Kristu, Mfalme wa ututuku, aliingia, akiwaambia wafungwa: Tokeni, na wale walio katika giza, mujionyeshe.

Shairi: Nitanyanyula macho yangu kwako, ee mwenye kuikala mbinguni, tazama...

Ee Bwana, sina hata na woga juu yako, makosa daima; mtu gani asiyeogopa mwamzi wa baraza ya hukumu? Mgonjwa gani akishurulika kupona atasirikisha nganga wake kama mimi. Ee Bwana mvumilivu na mwenye kujaa na mapendo tazama uzaifu wangu na unihurumie.

Shairi: Utuhurumie, ee Bwana, utuhurumie, kwani tunayala na kuzarauliwa.

Ee Bwana, walipolindwa kwa ngao ya imani waliposabitishwa kwa alama ya Msalaba, Mashahidi wako watakatifu walivumilia mateso; kwa utukufu walishinda uwongo na nguvu ya shetani; kwa maombezi yao, ee Mungu mwenyezi, tuma amani yako duniani na neema ya wokovu rohoni mwetu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya mnane.*

Ee Kristu Mungu wetu ambaye kwa kutaka kwako ulitwaa mwili, kwa mapendo yako isiyokadirika ulileta nuru takatifu kwa kipofu tangu kuzaliwa; na kidole chako uliweka matope machoni mwake, wewe mwenyewe mwenye kuleta nuru kwa ukarimu wako mfalme angaza sasa macho ya roho yetu.

## MU KAZI MBILI ASUBUI YA JUMA YA SITA

**KATHISMA WA KWANZA.** *Sauti ya tano.*

Ee Bwana, ulihesabiwa kati ya wafu, wewe uliyeua mfalme wa mauti, uliwekwa kaburini, wewe mwenye kwacha makaburi tupu; duniani kaburi yako ikalindwa na maaskari, kuzimuni ukawafufua wafu walioyolala tangu milele. Ee Mungu mwenyezi ambaye ulimwengu hauwezi kuzungusha, ee Bwana, furaha yetu, utukufu kwako.

Wakati atakapoketi Mwamzi mwenye kuzungukwa na malaika, kwa sauti ya baragumu na mbele ya tanuru ya moto, utafanya nini ee roho yangu ile wakati wa hukumu? Hapo yataonekana matendo yako ya giza, hapo yatafunuliwa mawazo yako ya siri; ndio maana mbele ya mwisho umwambie Kristu Mungu wetu: Wewe mwenye kusoma mioyo, unihurumie mimi mkosefu.

Utukufu kwa Baba...

Leo inangaa makumbusho ya Mashahidi, na mbingu inaongezako nuru yake: Malaika wanashangilia pamoja na sisi kama wanadamu duniani; Mashahidi wanamuomba Mungu kusudi ahurumie roho zetu.

Sasa na siko zote. **THEOTOKION**

Ee Mzazi-Mungu Mtakatifu kamili, wewe mlinzi wa wakristu, okoa watu wako wenyi kukuita na matumaini na moyo; fukuza haya ya mawazo, yetu bure ili tukulalamikia: Ee Mama bikira daima, salamu.

**KATHISMA YA MBILI** *Sauti ya tano. Ton sinanarkhon Logon.*

Kipofu ambaye tangu kuzaliwa hajaona jua anapata kuona kwa mate ya huyu zamani aliumba mwili ya wanadamu; kwa roho yake yote anamushukuru Mungu kwa sababu anaweza kuona mfano wa Muumba wake aliyetuumba kwa sura yake.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*(mara ingine).*

Tukiona ufufuo wa Kristu...Zaburi 50 (51).

*Kisha tunaimba Kanuni ya Paska na ya Kipofu. Tena tunasoma Kontakion, Ikos na Eksapostilarion ya Siku Kuu ya Kipofu.*

## MASIFU. *Sauti ya tano.*

Bwana, ukivunja mapingo ya milele, ukikata minyororo, ulifufuka toka kaburi, ukiacha sanda, kusudi ya kuishuhudia kweli maziko yako ya siku tatu; na ulitangulia kwa Galilaya, mwenye kulindwa katika pango. Rehema yako ni kubwa, ee Mwokozi msiyesikilikwa! Utuhurumie. *(mara mbili).*

Ee Bwana, usiangalie wingi wa zambi zangu, wewe uliyezaliwa kwa Bikira; makosa yangu yote unyazima na unipe mawazo ya toba, ewe peke yako mpenda-wanadamu, unihurumie.

Ee Bwana, waliposhinda kwa mashindano yao, washandani wa Malaika Wabila-mwili Mashahidi wako walivumilia mateso; kwa tumaini moja walifurahia mema iliyoahidiwa: Kwa maombezo yao, ee Kristu Mungu wetu, leta amani duniani na rehema kubwa rohoni mwetu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya mnane.*

Ee Kristu, nani ataweza kuhadisia uwezo wako kubwa ao kueleza miujiza yako ya milele? Na kama ulivyoonekana duniani katika hali mbili kwa wagonjwa unawapa maponyesho mawili, kwani kwa kipofu tangu kuzaliwa haukumufungua paka macho ya mwili lakini uliangaza tena macho ya roho yake kwako; ndio maana alitambua ndani yako Mungu mwenye kujificha machoni mwetu ambaye analeta duniani neema ya wokovu.

**APOSTIKHA** *Sauti ya tano. Osie Pater.*

Siku moja ya Sabato walipoona waziwazi nuru imemushukia kipofu aliyeangazwa kimungu, wale walioadibishwa chini ya sheria ya Musa wakawa vipofu rohoni mwao, hawakujua giza gani inafunika Sheria; ndio maana hawakumuona Bwana wa nuru ambaye kwa neno lake yeye ni Rabi wa Sabato, anamufungua kipofu macho kwa kunawa katika kisima cha Siloamu na kwa mate ya kinywa chake juu ya udongo kama ile siku ya kuumba mtu; enyi waaminifu, tuungane na kipofu ili tumuone Mungu mwenyewe na tufukuze upofu wa Wafarisayo wenyi kutazama tangu juu.

Shairi: Unitazame na unihurumie.

Juu ya kipofu aliyetembea katika giza na kuteswa daima na giza ya upofu wake nuru imepanda wakati, kwa amri ya Mungu, alinawa machoni mwake katika kisima cha Siloamu; hapo akaonekana kama nyota mpya yenye kufukuza giza ya Waandishi, ikichoma kwa nuru yake giza yao ya upofu; tokea sasa hati ya giza ya zamani imekuwa ya nuru kwa mwanga wa Neno la Mungu.

Shairi: Kwa neno lako ongoza hatua zangu, uovu isiwe na nguvu juu yangu.

Kipofu alipoangazwa kwa maarifa ya Mungu akapanda juu ya ncha ya nuru na hata kama alikuwa kipofu wa macho yote mbili alitambua Muumba na Chemchem ya nuru aliyetokea siku ya tatu kaburini akiangazia inchi kwa Ufufuo wake takatifu; katika hii anawangazia na nuru mpya wanadamu wafungwa wa kivuli na wa mauti sababu ya kuleta duniani neema ya wokovu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya mnane*.

Ee Kristu Mungu wetu, wewe uliye Jua la haki, kwa mkono wako safi kamili uliangaza huyu aliyekuwa kipofu tangu tumboni mwa mama yake; angaza pia macho ya roho zetu, utufanye kuwa wana wa nuru na wa mchana kusudi kwa imani tuweze kukulalamikia: Kubwa na isiyokadirika ni rehema yako kwa sisi, ee Bwana mpenda-wanadamu, utukufu kwako.

# MU KAZI MBILI MANGARIBI YA JUMA YA SITA KWA ESPERINOS.

# (SINDIKIZO YA SIKU KUU YA UFUFUO YA BWANA YESU KRISTU)

**Elezo:** *Padri anavaa manguo yake takatifu yote, anakamata pa mukono ya kuhume chetezo na ku mukono ya kushoto mushumaa ya kuwaka, anaanza kufukiza Meza Takatifu na kusema hivi:*
**PADRI**: Utukufu kwa Utatu Mtakatifu, wenye asili moja, Muumba wa uzima, usiotengana, daima, sasa na siku zote, hata milele na milele.
**WAIMBAJI**: Amina.
**PADRI**: Kristu alifufuka *(mara tatu).*
**Elezo***: Mwisho ya mwimbo: "Kristu alifukuka… hile ya tatu, wataimba waimbaji na padri atakuwa pa mulango Bora na atafukiza na chetezo ma pichaTakatifu na kisha waaminifu pempeni.*
**WAIMBAJI**: Kristu alifukuza *(mara sita).*
Na mistari ya Zaburi 67 (68) sawa ku mwanzo ya Liturgia ya Ufufuo.
*Kisha **PADRI** Ektenia mkubwa .*
**WAIMBAJI**: Bwana nimekuita. . . Sauti ya kwanza.
**Elezo: Tunaimba Ibada ya Ufufuo ya Yesu Kristu, bila mageuzo.**

**Elezo: Kama Mpadri anataka kufata paka desturi ya hii siku atafata desturi, sawa ifwatayo:**
*Kisha Bwana nimekuita wataimba:*

***Wimbo sita ya Kipofu***

*Sauti ya mbili. Idiomela.*

Kipofu tangu kuzaliwa aliulizana ndani yake: Ni kwa sababu ya zambi za wazazi wangu nimekuwa kipofu? Ni kwa kutokuamini kwa wapagani nitakuwa mshuhuda? Sisibutu kuuliza kama ni mchana ao ni usiku! Miguu yangu hayaepuke kukwaa, maana sione nuru ya jua ao sura na mfano wa Muumba wangu; ndio maana nakuomba, ee Kristu Mungu wangu, unitazame sababu ya kunihurumia.

*Sauti ya mbili*

Alipotoka hekaluni, Yesu alikutana na kipofu tangu kuzaliwa, akamuhurumia; akamupakaa matope machoni, akamwambia: Wende ukanawe katika kisima cha Siloamu! Akasimama na akaona, akamushukuru Mungu. Jirani zake wakamuuliza: Ni nani alikufungua macho ambayo mutu hata mumoja mwenyi kuona hawezi kuponyesha? Kipofu akawajibu: Ni huyu anayeitwa Yesu aliniambia: Wende ukanawe katika kisima cha Siloamu! Na nimeona; Mutu huyu eko kweli huyu Muza alisema katika Sheria yake ya kama ni Kristu, ni Masiya na Mwokozi wa roho zetu.

*Sauti ya ine*

Ee Bwana, kipofu alipoishi uzima wake wote katika giza, akalalamika: Unifungua macho, ee Mwana wa Daudi tena Mwokozi wangu, kusudi pamoja na watu wote niimbie mimi pia uwezo wako.

*Sauti ya tano*

Ee Bwana, njiani mwako ulikuta kipofu tangu kuzaliwa, Wafwasi wakakuuliza wakishangaa: «Ee Rabi, nani basi alitenda zambi, ni yeye ao wazazi wake ili azaliwe hivi kipofu? Lakini uliwajibum ee Mwokozi: Ao yeye ao wazazi wake hawakutenda zambi, lakini ili maajabu ya Mungu yaonekanendani yake; kwa sababu imenifai kutimiza kazi ya huyu aliyenituma na hakuna hata mumoja anaweza kuifanya». Aliposema hivi, akatema mate chini akafanya matope, akaipakaa machoni kwa kipofu na kumwambia: Wende ukanawe katika kisima cha Siloamu! Kipofu akaamka na akapona, akapaza sauti: «Ninamini, ee Bwana». na akamusujudu. Kama yeye, sisi pia tunapaza sauti: Utuhurumie, ee Bwana.

*Sauti ya mnane*

Ee Kristu Mungu wetu, wewe uliye Jua la haki, kwa mkono wako safi kamili uliangaza huyu aliyekuwa kipofu tangu tumboni mwa mama yake; angaza pia macho ya roho zetu, utufanye kuwa wana wa nuru na wa mchana kusudi kwa imani tuweze kukulalamikia: Kubwa na isiyokadirika ni rehema yako kwa sisi, ee Bwana mpenda-wanadamu, utukufu kwako.

*Sauti ya mnane*

Ee Kristu Mungu wetu ambaye kwa kutaka kwako ulitwaa mwili, kwa mapendo yako isiyokadirika ulileta nuru takatifu kwa kipofu tangu kuzaliwa; na kidole chako uliweka matope machoni mwake, wewe mwenyewe mwenye kuleta nuru kwa ukarimu wako mfalme angaza sasa macho ya roho yetu.

Utukufu kwa Baba..Sasa na siku zote....*Sauti ya mnane*.

Ee Kristu, nani ataweza kusema uwezo wako ao kueleza miujiza yako ya milele? Na kama ulivyoonekana duniani katika hali mbili, uliwapa wagonjwa maponyesho mbili, kwani kwa kipofu tangu kuzaliwa haukumufungua paka macho ya mwili bure, lakini uliangaza macho ya roho yake; ndio maana alikutambua wewe kuwa Mungu mwenye kujificha machoni mwetu na mwenyi kuleta duniani neema kubwa.

**APOSTIKHA** *Sauti ya tano.*

Tunakutukuza kwa sauti ya nyimbo, ee Kristu Mwokozi, mwenye kutwaa mwili bila kugawanyika toka mbingu; kwani ulikubali Msalaba na lufu, kwa ajili ya ukoo wetu, kwa kuwa wewe ni Bwana mpenda-wanadamu; ukinyanganya milango ya Hadeze, ulifufuka katika siku tatu kwa kuokoa nafsi yetu.

Tangazo: Kisha tunaimba WIMBO YA PASKA (Angalia Masifu ya Orthros ya Paska): *Sauti ya tano*
1. Paska zabihu leo imeonekana kwetu, Paska mupya Takatifu. . .
2. Kujeni Wanawake. . .
3. Wanawake Wabebaji manukato. . .
4. Paska ya furaha, Paska ya Bwana Paska. . .
Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .
Ufufuo ni leo na tuangazwe kwa Karamu. . .
Kristu alifufuka *(mara tatu)*
Padri: Sasa Bwama umuache mutumishi wako...
Msomaji: Trisagion
Apolitikion: Neno lasipo mwanzo...
Theotokion: Salamu mulango wa Bwana...

**Kuaga.**

# MU KAZI TATU ASUBUI YA JUMA SITA YA KIPOFU, MBELE YA KUPANDA YESU MBINGUNI

***Elezo: Kama tutafanya Sindikizo ya Bwana Yesu Kristu, katika Desturi ya Kanisa yetu, tutaimba paka Ibada ya Asubui ya Ufufuo ya Kristu. Hakuna wimbo ingine. Kama hatutafata hii Desturi tutaimba hii wimbo ifwatayo.***

**KATHISMA YA KWANZA** *Sauti ya tano. Ton sinanarkhon Logon.*

Kwa mashairi na nyimbo zetu tusifuni Msalaba mweshimiwa wa Bwana, tutukuzeni Kaburi, tutukuzeni Ufufuo wako takatifu, kwani Mungu wetu amewafufua wafu kaburini, akanyanganya ufalme wa mauti na kuharibu nguvu ya shetani, nuru yake ikasimama juu ya wafungwa kuzimuni.

Utukufu kwa Baba...

Ee Bwana, ulihesabiwa kati ya wafu, wewe uliyeua mfalme wa mauti, uliwekwa kaburini, wewe mwenye kwacha makaburi tupu; duniani kaburi yako ikalindwa na maaskari, kuzumuni ukawafufua wafu walioyolala tangu milele. Ee Mungu mwenyezi ambaye ulimwengu hauwezi kuzungusha, ee Bwana, furaha yetu, utukufu kwako.

Sasa na siku zote...**THEOTOKION** .

Salamu, mlima takatifu aliyopanda Bwana, salamu, kichaka kisipoteketezwa, salamu, kilalo cha dunia cha kwenda kwa Mungu, wewe mwenyi kupoleka ku uzima wa milele, salamu, ee Bikira msiyeolewa uliyezaa wokovu wa roho zetu.

**KATHISMA YA MBILI** Ya kipofu. *Sauti ya tano. Ton sinanarkhon Logon.*

Neno wa miele pamoja na Baba na Roho Mtakatifu, mwenye kuvaa nuru kama vazi, amevaa mwili kwa kutaka kwake kwa ajili yetu; alipofukuza magonjwa yote kwa watu, kwa uwezo wake wa umungu aklifungua macho ya huyu alikuwa kipofu tangu tumboni mwa mama yake.

Utukufu kwa Baba..Sasa na siku zote....*(mara mbili)*

Tukiona ufufuo wa Kristu...Zaburi 50 (51). *Kisha tunaimba Kanuni ya Paska na ya Kipofu. Kisha Ode ya tatu tunasoma Kontakion na Ikos ya Kipofu.*

## KONTAKION YA KIPOFU *Sauti ya ine.*

Ee Bwana, kama kipofu tangu kuzaliwa, macho ya roho yangu ni yenye kufunga kwa toba nakuja kwako na napaza sauti: Kwa wale wenye kuwa katika giza wewe ni nuru kubwa.

## IKOS

Ee Kristu, unipe hekima nyingi isiyokadirika na maarifa ya Jua mbinguni, wewe Nuru ya roho zenyi kupofuka tena mwongozi wa wakosefu, ili nitangaze miujiza ya kipofu tangu kuzaliwa kama inavyofundisha kitabu takatifu, Habari njema ya amani; kipofu tangu kuzaliwa anaona na macho pia ya roho, na kwa imani anapaza sauti: Kwa wale wenye kuwa katika giza wewe ni nuru kubwa.

## KATHISMA YA KIPOFU *Sauti ya kwanza. Ton tafon su Sotir*

Ee Kristu, ulifungua macho ya Kipofu tangu kuzaliwa na uliwaonyesha Wayuda utukufu wako; Mwokozi, wewe ni nuru ya ulimwengu, lakini kwa chuki vipofu wa roho wanafanya shauri juu yako sababu ya kuuwa Chemchem ya uzima wetu.

Utukufu kwa Baba… Sasa…**THEOTOKION**

Mwokozi, ulizaliwa kama ulivyopenda na ulionekana kwa kutaka kwako; ulipoteswa mwilini ulifufuka kama Mungu na ulipanda kwa utukufu mbinguni, ulichukua hali ya wanadamu pamoja nawe ambayo ulipamba na utukufu na uzuri.

### KONTAKION YA UFUFUO.

*Sauti ya Mnane*

Ulipolala Kaburini, ee Bwana msiyekufa ulivunja nguvu ya Gehena na ulifufuka kwa ushindi, ee Kristu Mungu wetu, ukiwamuru wabebaji-manukato kwa wafurahiwe; ukiwaangalia Mitume wako ukawapa amani, ee wewe unayetuokoa na kutupa ufufuo.

### IKOS

Wakati jua ya mbele ya jua zamani uliposhuka Kaburini, wanawake wabebaji manukato walikutafuta kama siku, walijiharikisha asubui mapema mumoja kwa mwingine wakiambiana: Rafiki zangu wapenzi, tuendeni tupakae marasi, mwili wenye-kuleta uzima wa yule aliyezikwa unayefufua adamu wenye kuanguka kulala Kaburini; tuendeni, tujiharikishe, sawa Waakili, na tumuabudu na tumutolee marasi sawa zawadi, yeye mwenye kufungwa si kwa sanda ya kitoto,
lakini kwa sanda ya maziko; na tulie, na tulalamike: Simama, ee Rabi, wewe mwenye kuleta Ufufuo kwa wenye kuanguka.

### SINAKSARION YA WATAKATIFU YA LEO.

*Kisha tunaimba Katavasies ya ufufuo ya Kristu.*

### KATAVASIES YA UFUFUO

### EKSAPOSTILARION YA UFUFUO *Sauti ya mbili*

Kwa mwili, ee Mufalme na Bwana ulipolala kama mutu mwenye kuweza kufa, ulifufuka siku ya tatu; ukisimamisha Adamu toka uharibifu na uliharibu mauti, ewe Paska uzima usiyoharibika Mwokozi wa dunia. *(mara tatu).*

**EKSAPOSTILARION YA KIPOFU** *Sauti ya mbili*

Ee Bwana, tuma nuru yako na ukweli wako kwa macho yangu ya roho yenyi kupofuka na giza ya zambi, ee Mungu wa mapendo, uyaongoze na macho ya unyenyekevu, na kwa machozi ya toba unitakase mimi wote.

**MASIFU** *Sauti ya mbili. Idiomela*

*Tunaimba wimbo ya kipofu ine na ya Ufufuo ya Kristu ine.*

Kipofu tangu kuzaliwa aliulizana ndani yake: Ni kwa sababu ya zambi za wazazi wangu nimekuwa kipofu? Ni kwa kutokuamini kwa wapagani nitakuwa mshuhuda? Sisibutu kuuliza kama ni mchana ao ni usiku! Miguu yangu hayaepuke kukwaa, maana sione nuru ya jua ao sura na mfano wa Muumba wangu; ndio maana nakuomba, ee Kristu Mungu wangu, unitazame sababu ya kunihurumia.

*Sauti yas mbili.*

Alipotoka hekaluni, Yesu alikutana na kipofu tangu kuzaliwa, akamuhurumia; akamupakaa matope machoni, akamwambia: Wende ukanawe katika kisima cha Siloamu! Akasimama na akaona, akamushukuru Mungu. Jirani zake wakamuuliza: Ni nani alikufungua macho ambayo mutu hata mumoja mwenyi kuona hawezi kuponyesha? Kipofu akawajibu: Ni huyu anayeitwa Yesu aliniambia: Wende ukanawe katika kisima cha Siloamu! Na nimeona; Mutu huyu eko kweli huyu Muza alisema katika Sheria yake ya kama ni Kristu, ni Masiya na Mwokozi wa roho zetu.

*Sauti ya ine.*

Ee Bwana, kipofu alipoishi uzima wake wote katika giza, akalalamika: Unifungua macho, ee Mwana wa Daudi tena Mwokozi wangu, kusudi pamoja na watu wote niimbie mimi pia uwezo wako.

*Sauti ya tano*

Ee Bwana, njiani mwako ulikuta kipofu tangu kuzaliwa, Wafwasi wakakuuliza wakishangaa: Ee Rabi, nani basi alitenda zambi, ni yeye ao wazazi wake ili azaliwe hivi kipofu? Lakini uliwajibum ee Mwokozi: Ao yeye ao wazazi wake hawakutenda zambi, lakini ili maajabu ya Mungu yaonekanendani yake; kwa sababu imenifai kutimiza kazi ya huyu aliyenituma na hakuna hata mumoja anaweza kuifanya. Aliposema hivi, akatema mate chini akafanya matope, akaipakaa machoni kwa kipofu na kumwambia: Wende ukanawe katika kisima cha Siloamu! Kipofu akaamka na akapona, akapaza sauti: Ninamini, ee Bwana». na akamusujudu. Kama yeye, sisi pia tunapaza sauti: Utuhurumie, ee Bwana.

Tangazo: Kisha tunaimba: **STIKHIRA YA PASKA** *Sauti ya tano***.**

Kituo: 1. Mungu asimame, adui zake zote wasambazwe; wenye kumuchukia wakimbie vilevile mbele ya uso wake.

Paska zabihu leo

Kituo: 2. Kama moshi inavyopeperushwa, hivi uwapeperushe; kama taa inavyoyeyuka mbele ya moto.

Kujeni Wanawake mulioona

Kituo: 3. Hivi waovu wapotee mbele ya uso wa Mungu na wenye haki wafurahi.

Wanawake wabebaji manukato

Kituo: 4. Hii ni siku aliyofanya Bwana, tufurahi na kushangilia ndani yake.

Paska ya furaha, Paska Bwana Paska,

**DOKSASTIKON.**

*Sauti ya tano.*

Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa roho Mutakatifu. Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Ufufuo ni leo, tuangazwe ku Karamu,

*Na mara ingine*: Kristu alifufuka. . . *(mara tatu)***. DOKSOLOGIA KUBWA.**

Apolitikion: Neno lasipo mwanzo... **Kuaga.**

## SIKU KUU KUBWA YA KUPANDA MBINGUNI YESU KRISTU

### MU KAZI TATU MANGARIBI KWA ESPERINOS KUBWA.

*Kisha Zaburi 103 (104)ao Proimiakos na : «Bwana nimekuita...» tunaimba wimbo sita. Sawa hivi:*

*Sauti ya Sita. Idiomela.*

Bwana alipanda mbinguni sababu ya kutuma duniani Roho Mtakatifu; kiti chake kimetayarishwa mbinguni, mawingu ni pa kufinyayangia miguu yake; Malaika wanashangaa kwa kuona mwanadamu amekuwa juu yao, Baba anapokea huyu anakaa milele kifwani mwake, Roho Mtakatifu anaamuru katika majumbe wake: Enyi Milango, funguni, ukuta wenu, enyi mataifa yote, pigeni mikono, maana Kristu amepanda kule alikuwa zamani. *(mara mbili).*

Ee Bwana, kwa Kupanda Kwako mbinguni Wakheruvi waliogopa pa kukuona umependa juu ya mawingu, wewe Mungu mwenye kukaa juu yao; tunatukuza neema wema wako.*(mara mbili).*

Ee Kristu, mlimani takatifu tunapoona utukufu wako, ee Nuru ya utukufu wa Baba, tunaimbia nuru ya uso wako; tunasujudia mateso yako, tunaheshimu Ufufuo wako takatifu na kutukuza Kupanda kwako; utuhurumie. *(mara mbili).*

Ee Bwana, wakati Mitume walikuona umenyanyuliwa juu ya mawingu, moyo wenye kujaa na machozi na sikitiko, ee Kristu uliye chemchem ya uzima, wakakuambia wakilia: Ee Rabi, usiache mayatima watumishi ulipanda na mapendo kubwa, lakini kama ulivyotuahidia, ututumie Roho Mtakatifu kusudi angazie roho zetu na nuru yako. *(mara mbili).*

Ee Bwana, ulipotimiza fumbo ya wokovu, ulichukua Wafuasi wako pamoja nawe sababu ya kuwapeleka juu ya mulima wa Mzeituni, na ulipanda katika anga ya mbinguni; ee Bwana wewe uliyejifanya maskini kwa ajili yangu mpaka kuvaa ubinadamu wangu na kupanda kwa utukufu ambako haukutengana nayo, tuma toka mbinguni Roho wako Mtakatifu sababu ya kuangazia roho zetu na nuru yako. *(mara mbili).*

Utukufu kwa Baba...sasa na siku zote...*Sauti ya Sita.*

Ee Yesu mupole kabisa, bila kuacha kifua cha Baba, duniani ulikua na ubinadamu wetu, unapanda leo mbinguni na utukufu tangu mulima wa Mzeituni, ukiinua kwa huruma yako hali yetu yenye kuanguka, sababu ya kuiweka karibu ya Baba pamoja na wewe; majeshi ya Wabila-mwili mbinguni wanaposhangaa na kuogopa, wanatukuza mapendo unapenda nayo wanadamu; na sisi duniani, pamoja nao tunatukuza mapendo yako kwa sisi na Kupanda kwako mbinguni tukisema: Ee Bwana uliyezaza na furaha kubwa siku ya Kupanda Kwako Wafuasi wako na Mzazi-Mungu aliyekuzaa, utupe na sisi pia, kwa maombezi yao, furaha ya mateule wako na neema ya wokovu.

**KUINGIA**

Mwangaza upole na Prokimenon ya hii siku na Masomo:

**Unabii ya Isaya tutasoma. (2,2-4).**

Bwana akasema: Na itakuwa siku za mwisho, mulima wa nyumba ya Bwana utasimamishwa juu ya milima; na utanyanyuliwa juu ya vilima, na mataifa yote wataukimbilia. Na wakabila mengi watakwenda na kusema: Kujeni, tupande kwea mulima wa Bwana, kwa nyumba ya Mungu wa Yakobo; na yeye atatufundisha katika njia zake, nasi tutatembea kwa njia zake.

**Unabii ya Isaya tutasoma. (61,10-62,1)**

Bwana akasema: Mupite, mupite katika malango; mutengeneze njia ya watu, tutieni, tutieni barabara; mutoe mawe yake; Munyanyue bendera kwa makabila ya watu. Tazama, Bwana ametangaza habari mupaka mwisho wa dunia, mumwambie binti ya Sayuni, tazama, wokovu wako unakuja; Tazama, zawabu yake ni pamoja naye, na malipo yake mbele yake. Nao watawaita: Watu watakatifu, wenye kukombolewa na Bwana; nawe utaitwa, aliyetafutwa, muji usioachwa. Ni nani huyu anayetoka Edomu, Mwenye mavazi ya rangi nyekundu sana, kutoka Bosara? Huyu aliye na nguo ya utukufu, akikwenda katika ukubwa wa uwezo wake? Mimi ninayesema kwa haki, hodari wa kuokoa. Kwa nini mavazi yako ni mekundu, na nguo zako kama za mutu anayekanyaga zabibu? Mimi peke yangu nimekanyaga pahali pa kukamua pamoja nami; niliwakanyaga kwa kasirani yangu, na niliwaponda kwa kasirani yangu kali; na damu yao imerukia mavazi yangu, nami nimechafua nguo zangu zote. Maana siku ya kisasi ilikuwa katika moyo wangu, na mwaka wao niliowakomboa umefika. Nikatazama, na hakuna wa kusaidia; nikashangaa kwa kuwa hakuna mwenye kutegemeza; Basi, mukono wangu mwenyewe uliniletea wokovu; kasirani yangu kali ilinitegemeza. Nikakanyaga makabila ya watu kwa kasirani yangu, na niliwalewesha klwa gazabu yangu, nami nitamwanga damu yao chini. Nitataja rehema ya bwana, sifa za Bwana sawasawa na yote Bwana aliyotufanyia, na wingi

wa wema wake kwa nyumba ya Israeli, aliowafanyia wao sawasawa na rehema zake, na kwa wingi wa wema wake. Maana alisema: Kweli ndio watu wangu hawa, wana wasio na uwongo; naye akakuwa Mwokozi wao. Katika mateso yao yote yeye aliteswa, na malaika mbele ya uso wake aliwaokoa; kwa mapendo yake na kwa huruma zake aliwakomboa; akawanyanyua na kuwachukua siko zote za zamani.

**Unabii ya Zakharia tutasoma. (14, 4-11).**

Tazama, siku ya bwana inakuja, wakati nyara zako zitakapogawiwa katikati yako. Kwa maana nitakusanya kataifa yote juu ya Yerusalema kwa vita; na muji utakamatwa, na nyumba zitatekwa, na wanawake watachukuliwa kwa nguvu, na nusu ya muji itakwenda kwa kufungwa, na baki la watu halitakatiliwa mbali na muji. Halafu Bwana atatoka, na atapigana na mataifa yale, sawasawa alivyopigana kwa siku ya vita. Na miguu yake itasimama siku ile juu ya mulima wa Zeituni ulio mbele ya Yerusalema kwa mashariki, na mulima wa Zeituni utapasuka katikati yake kwa upande wa mashariki na kwa upande wa mangaribi, na litakuwa bonde kubwa sana; na nusu ya mulima itaondoka kwa kaskazini na nusu yake kwa kusini. Na mutakimbia kwa njia ya bonde la milima yangu, kwani bopnde la milima litafika hata Azeli; ndiyo, mutakimbia, sawasawa mulivyokimbia mbele ya tetemeko la inchi katika siku za Uzia, mufalme wa Yuda. Na Bwana, Mungu wangu, atakuja na watakatifu wote pamoja naye. Na itakuwa siku ile nuru haitakuwa na kungaa, wala usiku; lakini itakuwa siku moja iliyojulikana kwa Bwana, si muchana, wala usiku; lakini itakuwa wakati wa mangaribi, nuru itakuwa. Na itakuwa siku ile maji ya uzima yatatoka Yerusalema; nusu yao kwa bahri ya mashariki na nusu yao kwa bahari ya mangaribi; itakuwa kwa wakati wa kipwa na kwa wakati wa baridi. Na Bwana atakuwa mufalme juu ya inchi yote; siku ile Bwana atakuwa mumoja na jina lake moja. Inchi yote itageuzwa kama Araba; toka Geba hata Rimoni kwa kusini wa Yerusalema; nayo itanyanyuliwa na itakaa kwa pahali pake, toka lango la Benyamina hata pahali pa lango la kwanza, hata kwa langho la pembeni, na toka munara wa Hananeli hata mashinikizo ya mufalme. Na watu watakaa ndani yake wala laana haitakuwa tena; lakini Yerusalema utakaa salama.

## LITIA

*Sauti ya kwanza. Idiomela.*

Ee Bwana, unapopanda mbinguni huko ulishuka, usituache mayatima, lakini akuje juu yetu Roho Mtakatifu mwenye kuleta amani duniani; kwa watu wote onyesha matendo ya uwezo wako, ee Bwana.

Ee Kristu, ulipanda kwa Baba yako wa milele ambaye haukwache kifua kubwa na malaika hawakuongeza chochote kwa utukufu wa Utatu Mtakatifu; hata kisha umwilisho waliona katika wewe paka Mwana wa pekee wa Baba ambaye kwa mapendo yake kubwa, ee Bwana, utuhurumie.

*Sauti ya ine.*

Ee Bwana, wakati ulipofika juu ya milima wa Mzeituni kwa kutimiza nia ya wema ya Baba yako, malaika mbinguni walishangaa, na duniani mashetani walitetemeka; Mitume walijazwa na woga na furaha wakati ulizungumuza nao katikati yao; wingu liliongojea mbele yako kama kiti chenye kutayarishwa mbingu ilifungua milango yake ikiangaa na uzuri, incghi ilitambua mashimo yake sababu ya kuonyesha kuanguka kwa Adamu na kupanda kwake mpaka kwako; wakati nguvu isiyoonekana ilikunyanyua toka inchi ukasema maneno ya baraka kwa sauti kubwa sababu ya kusikilika; wingu likakuchukua na mbingu ikafungulika kwa kukupokea. Ee Bwana, hii ni tendo kubwa na la ajabu ulilotenda kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

*Sauti umoja*

Ee Bwana, ubinadamu iliyoanguka katika Adamu mpaka chini kabisa ya udongo, uliitengeneza kuwa mpya katika wewe mwenyewe: Leo unaipandishja juu ya majeshi na ya matawala wa mbinguni; ulipopenda, unaipa kukaa pamoja nawe, kwa huruma uliiungamisha kwa hali yako, kwa hii ushirika, unateswa pamoja nayo; kwa mateso yako, ee Mungu mvumilivu, uliitukuza; lakini majeshi ya Wabila-mwili wakaulizana: Huyu ni mutu gani mwenye kuvaa utukufu? Hayuko paka mutu, yeye ni Mutu-Mungu, kwani eko na hali zote mbili; na malaika wenye kuvaa mavazi ya kuangaa wakawazunguka pambeni wakawaambia: Enyi watu wa Galilea, huyu Yesu Mutu-Mungu aliyeondoka kwenu, kwa umungu-umutu wake atarudi tena kuhukumu wazima na wafu, kwa wenye kuamini atawapa maondoleo ya zam,bi na neema kubwa.

*Sauti umoja*

Ee Kristu Mungu wetu, wakati ulinyanyuliwa katika utukufu, machobni mwa Wafwasi wako wawingu yakakuchukuwa na mwili wako? Milango yakafunguliwa mbinguni, Malaika wakafurahiwa, majeshi ya mbinguni-juu ya kapaza sauti ya kisema: Enyi milango, inueni kuta zenu ili Mfalme wa utukufu aingie; Wafwasi walioshikwa na woga wakasema: Usituache, ee Mchungaji mwema, lakini ututumie sisi Roho wako Mtakatifu kamili awe mwongozi na msaada wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote... *Sauti ya ine*

Ee Bwana, kwa wema wako, kwa kutimiza fumbo iliyofichwa milele, ulikuja pamoja na Wafwasi wako kwa mlima wa Mzeituni, pamoja na huyu aliyekuzaaewe Bwana na Muumba wa ulimwengu wote; kwani alipokuwa mama, aliteswa kuliko wote katika mateso yako na akastahili kuonja furaha kubwa ya kukuona umetukuzwa mwilini mwako; na sisi wenyewe tunaposharikia hii furaha leo ya kupanda kwako mbinguni, tunatukuza, ee Bwana rehema yajko kwa ajili yetu.

## APOSTIKHA

*Sauti ya mbili. Idiomela.*

Kwa kutaka kwako ulipata mwili, kwa kutaka kwako ulionekana; ee Mungu wetu, uliteswa mwilini mwako; ulifufuka katika wafu, ulishinda matui kwa utukufu ulipanda mbinguni, wewe mwenye kujaza ulimwengu wote, na ulitutumia Roho Mtakatifu sababu ya kuimbia na kutukuza umungu wako.

Shairi: Enyi mataifa yote, pigeni mikono shangilieni Mungu kwa furaha.

Ee Kristu, wakati ulinyanyuliwa tangu mulima wa Mzeituni, yalipoona hivi, Majeshi ya mbinguni moja kwa ingine ya kasema: «Huyu ni nani?» Na sauti ikajibu toka mbingu: «Ni Mweza, ni shujaa, ni mwenyi nguvu katika mashindano, ni mfalme kweli wa utukufu! Sababu gani amevaa nguo nyekundu? Nikusema anatokea kwa Bossori, maana kwa mwili! Yeye mwenyewe amekaa kama Mungu kuume kwa ufalme wa Mungu, anatutumia Roho Mtakatifu, sababu ya kuongoza roho zetu na kuziokoa.

Shairi: Mungu anapanda katika shangwe, Bwana, kwa sauti ya baragumu.

Tangu mulima wa Mzeituni ulipanda katika utukufu mbele ya Wafwasi wako, ee Kristu Mungu wetu; unakaa kuume kwa Baba, wewe mwenyewe kujaza uliwemgu wote kwa umilele wa umungu wako, na uliwatumia Roho Mtakatifu kusudi roho zetu zipate katika yeye msaada, nuru na utakatifu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya sita.*

Mungu anapanda katika shangwe, Bwana, kwa s auti ya baragumu sababu ya kuinua sura iliyoanguka katika Adamu na toka mbingu mbinguni atatuma Roho Mfariji kusudi roho zetu zitakaswe.

**Apolitikion.** *Sauti ya Ine.*

Unapanda katika utukufu, ee Kristu Mungu wetu, ukiwajaza wafwasi wako na furaha kwa ahadi ya Roho Mtakatifu, ukawapa nguvu na kuwabariki na mikono yako, kwani ndiwe Mwana wa Mungu, Mkombozi wa dunia. *(mara tatu)*

## MU KAZI INE ASUBUI SIKU KUU YA KUPANDA YESU KRISTU MBINGUNI

**KATHISMA YA KWANZA** *Sauti ya kwanza. Tu lithu sfragisthentos.*

Ee Mwokozi, Malaika waliposhangaa kupanda kwako na Wafwasi waliposangaza kwa kuchukuliwa kwako kwa ajabu, ulichukuliwa na utukufu kama Mungu, milango yalifunguliwa mbele yako; ndio maana majeshi ya mbinguni wakashangaa yakipaza sauti: Utukufu kwa mapendo yako, ee Mwokozi, utukufu kwa Ufalme wako, utukufu kwa kupanda kwako, ewe peke yako mpenda-wanadamu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*(mara ingine).*

**KATHISMA YA MBILI** *Sauti ya tatu. Tin oreotita.*

Mungu wa mbele ya milele alipogeuza kwa siri ubinadamu aliyochukua, leo amechukuliwa mbinguni, Malaika wanamutangulia na wanawaonyesha Wafwasi Bwana akichukuliwa na utukufu

kubwa mpaka mbinguni, na wanaposujudu, wanasema: Utukufu kwa Mungu mwenye kupanda mbinguni.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*(mara ingine).*

**KATHISMA KISHA POLIELEO.** *Sauti ya tano. Ton sinanarkhon Logon.*

Ee Kristu, uliposhuka toka mbinguni mpaka duniani, sababu ya kuinua kwa umungu ukoo wa Adamu mwenye kulala chini ya kifungo cha Hadeze, kwa kupanda kwako ulipomupandisha mbinguni, pamoja nawe amekaa katika kiti cha ufalme cha Baba, kwa huruma na mapendo yako kwa wanadamu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*(mara ingine).*

**ANTIFONON** *Sauti ya ine*

Tangu ujana wangu, tamaa zenye kunishambulia zilinizunguka, lakini wewe, ee Mwokozi wangu, unilinde na uniokoe.

Adui wa Sayuni wanyamazishwe na Bwana; Wawe kama nyasi yenye kuungua inapokauka!

Utukufu kwa Baba...

Roho yote inaishi kwa neema ya Roho Mtakatifu na inaishi na usafi wote kwa kwangaa ku Utatu moja katika siri takatifu.

Sasa na siku zote...

Mawimbi ya neema yenye kunywesha kiumbe yote sababu ya kuchanua uzima yanach irizika kwa Roho Mtakatifu.

**PROKIMENON:**

Kwa shangwe Bwana anapanda kwa sauti ya baragumu. *(mara mbili).*

Kituo: Enyi Mataifa yote, pigeni mikono, shangilieni Mungu kwa furaha.

Kwa shangwe Bwana anapanda kwa sauti ya baragumu.

**EVANGELION EOTHINON YA TATU**. *(Marko 16, 9-20).*

*Msomaji anasoma na sauti nzuri hii sala ya chini.*

MSOMAJI: Tukiona ufufuo wa Kristu, tumsujudu Yesu Bwana Mtakatifu aliye peke yake bila zambi. Tunausujudu msalaba wako, ee Kristu, tena tunausifu na kuutukuza ufufuo wako takatifu. Kwa kuwa wewe Mungu wetu, la wewe peke yako hatumjui mwengine, jina lako tunaliita. Njoni enyi waaminifu wote, tuusujudu ufufuo takatifu wa Kristu. Kwa kuwa. je! Kwa ajili ya msalaba umefika furaha katika dunia mzima. Tukimhimidi Bwana daima, tunasifu ufufuo wako; kwa sababu akiuvumilia masalaba kwa ajili yetu, aliangamiza kifo kwa kifo chake.

ZABURI 50 (51)

*Sauti ya pili.*

Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu.

Kwa ajili ya maombezi ya Mitume, ee Mrahimu, uufute wingi wa zambi zangu.

Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Kwa ajili ya maombezi ya Mzazi-Mungu, ee Mrahimu, uufute wingi wa zambi zangu.

Mrahimu, unihurumie, ee Mungu, sawasawa na huruma yako kubwa,...

*Sauti ya sita.*

Leo Majeshi ya juu-mbinguni wanapoona hali yetu mbinguni, wanashangaa kwa kupanda kwajko kwa ajabu na wanaulizana mumoja kwa mwingine wakisema: «Ni nani huyu anakuja?» Lakini walipotambua Bwana wao, wanaamuru milango ya mbinguni yafunguliwe. pamoja nao tunakuimbia daima wewe utakayerudi toka mbinguni na mwili wako kama Mwamzi wa ulimwengu tena Mungu Mwenyezi.

## KANUNI.

**WIMBO YA KWANZA** *Sauti ya tano. To Sotiri Theo.*

**IRMOS:** Mungu Mwokozi aliyeongoza wana wa Israeli pakavu baharini Nyekundu, akizamisha Farao na jeshi lake lote, tumwimbe kama peke yake ni mstahili wa nyimbo zetu, kwani amevaa utukufu.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Enyi mataifa yote, tumwimbieni Kristu aliyechukuliwa na utukufu juu ya mabega ya Wakheruvi sababu ya kutuikalisha pamoja na yeye kuume kwa Baba: Tumwimbieni wimbo wa ushindi, kwani amevaa utukufu.

Utukufu kwako ee Mungu wetu, utukufu kwako

Malaika walipoona Kristu aliye mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu anapanda juu-mbinguni na mwili, wakashikwa na woga, na kwa sauti moja wakaimba wimbo wa ushindi.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Mungu aliyeonekana juu ya mlima Sinayi na kumupa Musa Sheria alipomuona, akachukuliwa na mwili wake tangu mlima wa Mzeituni: Pamoja tumwimbieni, kwani amevaa utukufu.

Mtakatifu kamili, ee mzazi-Mungu, utuokoe. **THEOTOKION**.

Ee Bikira asiye na doa tena Mzazi-Mungu, umuombe daima Mungu aliyetwaa mwili tumboni mwake bila kuacha kifua cha Baba mbinguni: Aokoe toka hatari yote wale aliumba kwa mikono yake.

**KANUNI INGINE** *Sauti ya ine. Anikso to stoma mu.*

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu wako.

Ulifufuka siku ya tatu, wewe uliye msiyekufa, ulionekana kwa Wafwasi wote, kisha ukapanda kwa baba yako, ee Kristu, mwenye kuchukuliwa juu ya mawingu, wewe uliye Muumba wa ulimwengu.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu wako.

Katika zaburi moja Daudi mwenye kuongozwa na Mungu alitangaza waziwazi: «Bwana anapanda mbinguni kwa shangwe na sauti ya baragumu, anarudi kwa Baba yake, Yeye aliye chemchem ya nuru.

Utukufu kwa Baba...

Ee Bwana, dunia yenye kuzekea katika zambi zake nyingi Mateso yako na kwa ufufuo wako uliifanya kuwa mpya, kisha ulipanda mbinguni mwenye kuchukuliwa katika mawingu.

Sasa na siku zote....**THEOTOKION**.

Ee Malkia uisye na doa, ulizaa Rabi wa vitu vyote: Aliteswa kwa kutaka Kwake, kisha alipanda kwa Baba yake bila kumuacha kama alitwaa mwili wetu.

W**IMBO YA TATU.** *Sauti ya tano.*

**IRMOS:** Ee Kristu, kwa uwezo wa Msalaba wako sabitisha nia zetu, sababu ya kuturuhusu kuimba na kutukuza kupaa kwako kwenyi kuleta wokovu.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu wako.

Ee Kristu, uliye chemchem ya uzima, ulipanda mbinguni kwa Baba yako, ulichukua hali yetu pamoja nawe, ee mpenda-wandamu, kwa wema wako isiyokadirika.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu wako.

Ee Mwokozi Malaika wanapoona umechukua hali ya wanadamu, kwa kushangaa wanakuimbia daima mbinguni.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu wako.

Ee Kristu, malaika walishangaa kwa kukuona umechukuliwa mbinguni na mwili wako kwa utukufu, na waliimbia kupanda kwako kama Mungu.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu wako.

Ee Kristu, hali ya wanadamu iliyotiishwa kwa uvumbi wa Kaburi unainyanyua na kuitukuza kwa kupanda kwako mbinguni huko unatutukuza pamoja na wewe.

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe. **THEOTOKION**.

Ee Bikira usiye na doa, umuombe daima huyu aliyezaa kusudi aokoe toka upotevu wote wale wenye kukuimbia kama Mzazi-Mungu.

**KANUNI INGINE** *Sauti ya inne. Tus sus imnologus Theotoke.*

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu wako.

Majeshi ya mbinguni yaliambiana moja kwa ingine: «Fungueni milango ya mbinguni! Tazama amefika, yeye aliye Mfalme, Bwana wetu, amevaa mwili wa wanadamu.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu wako.

Ulipokuja kutafuta hali ya mwanadamu iliyopotea kwa werevu wa nyoka, ulivaa wewe mwenyewe na ulipanda kuikalisha pamoja nawe kuume kwa Baba yako ambaye Malaika wanaimbia mbinguni.

Utukufu kwa Baba...

Mbingu na dunia zinashangilia kwa furaha siku ya kupanda kwa Muumba wa ulimwengu mwenye kuunganisha ile ilitengana zamani.

Sasa na siku zote...**THEOTOKION**.

Ee Bikira Mama Mtakatifu kamili, ulipozaa mshindi wa mauti, Mungu aliye peke yake msiyekufa, umuombe daima aniokeo toka tamaa zangu mbaya.

**KATHISMA** *Sauti ya mnane. Tin sofian ke Logon.*

Unapoenda juu ya mawingu ya mbinguni kisha kuwapa wanadamu amani duniani unachukuliwa sababu ya kukaa juu ya kiti taaktifu kama ulivyo wa asili moja na Baba na Roho Mtakatifu; ul;ionekana mwilini bila kugeuka na unaongojea ukamilifu wa vitu vyote sababu ya kuja tena duniani kuhukumu dunia yote. Ee Mwamzi mwenye haki, samehe roho zetu, ee Bwana, uwaondolee watumishi wako zambi zao, ee Mungu wa mapendo.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*(mara ingine).*

**KONDAKION.** *Sauti ya sita.*

Ulipotimiza kwa ajili yetu tendo lako la wokovu, kisha kuunganisha mbingu na dunia, watu na Mungu, katika utukufu, ee Kristu Mungu wetu, ukapanda mbinguni bila kutwacha, lakini umekaa siku zote katikati yetu na ukawaambia wale wanaochunga mapendo yako: Mimi ni pamoja nanyi siku zote na mutu hata mumoja hawezi kufanya chochote juu yenu.

**IKOS**

Tunapoacha inchini shuruli za dunia, udongoni ile iliyo matope na yenye kusumbua, kujeni, tuamukeni toka usingizi, tunanyueni macho yetu na roho zetu juu, tuelekezeni pia macho yetu na mawazo yetu kwa milango ya mbinguni, kama tulikua juu ya mlima wa Mzeituni, tukimutazama Mkombozi akichukuliwa juu ya mawingu; ni huko Bwana alipanda kwenda mbinguni, ni huko pia aliwagawanyia Mitume vipaji, akawapa nguvu na kuwatuliza kama Baba, akawaongoza kama wana na kuwaambia: Siwache ninyi; mimi ni pamoja nanyi siku zote na hakuna hata mumoja atawatendea ninyi ubaya.

**SINAKSARI YA WATAKATIFU YA LEO.**

*Kisha Hii:*

Leo, mu Kazi Inne ya Juma ya Sita ya paska, tunashangilia Kupanda mbinguni kwa Bwana Mungu na Mwokozi wetu Yesu Kristu.

Ee Neno, unakaa kuume kwa Baba, unasabitisha imani ya Mitume wako Watakatifu.

Ee Kristu Mungu wetu, ulipochukuliwa kwa utukufu mbinguni, utuhurumie. Amina.

**KATAVASIA** *Sauti ya Ine.*

Wingu wa kimungu ulifunika Musa mwenye-ulimi muzito, na Yeye alihubiri sheria iliyoandikwa na Mungu. Kwani akiondosha uchafu toka macho ya roho aliona Mungu Aliye, na aliingiza katika mafikili ya Roho, akimwimbia kwa wimbo kimungu.

Minyororo la tumbo ya tasa ilikatika, na tena laumu isiyovumiliwa ya Muzazi, paka kwa maombi ya Hana nabii wakate, mwenye-kuwa moyo uliovunjika mbele ya Mufalme wa uwezo, na Mungu wa kujua yote.

Mufalme wa wafalme. Mwana wa pekee na Neno, uliyezaliwa na Baba peke yake asiye mwanzo, ulituma Roho kweli sawa na wewe kwa mitume, kwa sababu wewe ni mwema, na wao waliimba: Utukufu kwa uwezo wako, ee Bwana.

Mupokee usafisho unaozimisha zambi, mupokee upepo wa Roho ya umande na ya moto, enyi watoto wa Kanisa kwa uso ya nuru. Kwa maana sasa katika sayuni sheria ilitoka, neema ya Roho ilionekana ndini kama za moto.

Kristu Rabi, uko usamehe na wokovu, ukianga toka Bikira, ili utoshe toka uharibifu Adamu mwenye kuanguka na wote, kama ulitosha toka matumbo ya samaki nabii Yona.

Upatanisho wa viombo vya musiki ilinguruma, kusudi mataifa waabudu sanamu isiyo na nafsi iliyofanywa kwa zahabu. Lakini neema ya Mufariji ilitayonuru iliwapatia moyo ya ukimya kwa waaminifu wapaze sauti: Utatu wa usawa pasipo mwanzo, uko peke yako mubarikiwa.

Tunasifu, tunamuhimidi na tunamusujudu Bwana.

Mufano wa nuru tatu ya Umungu unafungula minyororo na unapoza moto. Watoto wanaimba na viumbe vyote vilivyoumbwa na Mungu, Mwokozi na Muumba peke yake, vinamubarikia, kwaq kuwa Yeye ni Mwema.

**WIMBO YA TISA**

**IRMOS:** Ewe Mzazi-Mungu, uliposhinda akili yetu na usikilizi wetu, ukamzaa mu wakati Bwana wa milele; kwa sauti moja na kwa moyo moja, sisi waaminifu, tunakusifu.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu wako.

Ee Kristu Mungu wetu, Mkombozi wa dunia, Mitume walipotazama kutukuzwa kwako, wakakutukuza kwa woga na furaha.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu wako.

Ee Kristu, walipoona mwili wako inakuwa ya umungu, kule juu-mbinguni Malaika wakasemezana mumoja kwa mwingine: Kweli mutu huyu ni Mungu.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu wako.

Ee Kristu Mungu wetu, walipokuona umechukuliwa juu ya mawingu, malaika wakapaza sauti wakasema: «Kwa ajili ya Mfalme wa utukufu, fungueni milango ya mbinguni».

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu wako.

Uliposhuka kuzimuni, uliokoa dunia na ulinyanyua kwa kupanda kwako mbinguni: Ee Kristu Mungu wetu, tunakutukuza.

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe. **THEOTOKION**.

Salamu, ee Mama Mtakatifu wa Kristu Mungu wetu: Kwani huyu uliyezaa leo umemutukuza pa kumuona amepanda pamoja na Malaika toka dunia mpaka mbinguni.

**KANUNI INGINE.** *Sauti ya ine. Apas gigenis.*

*Shairi:* Malaika walipoona kupanda kwa Bwana, wakashangaa: «namna gani amechukuliwa kwa utukufu toka inchi mpaka mbinguni?

Ni ukarimu yenye kupita ufahamu! Ni fumbo yenye kuchokoza msangao! Rabi wa ulimwengu alipopanda toka dunia kwenda mbinguni anawatumia Wafwasi wake Roho Mtakatifu sababu ya kuangazia roho yao na kuwakisha neema yake ndani yao.

*Shairi:* Malaika walipoona kupanda kwa Bwana,......

Bwana aliwaambia Wafwasi wake: Kaeni katika Yerusalema nitawatumia ninyi Mfariji mwenye kukaa pamoja na Baba na Mimi munayeona nikichukuliwa mbinguni kwa wingu la nuru.

Utukufu kwa Baba... Malaika walipoona kupanda kwa Bwana,......

Waziwazi amechukuliwa Mfalme aliyetoka katika mbingu kubwa sababu ya kuwa maskini katika mwili wetu na kuikalisha karibu ya Baba hali yetu yenye kuanguka: Kwa hii siku Kuu tuimbieni wote kwa sauti moja, tumushukuru Mungu kwa furaha.

Sasa na siku zote...**THEOTOKION**.

Nuru toka nuru, Kriustu ameinuliwa Kwako, ee Mtakaitfu kamili usiye na doa, aliondoa upofu wa makafiri, aliamusha wale waliolala katika giza ya usiku; ndio maana, ee Bikira mwenye kustahili nyimbo zetu, tunakutukuza milele.

**Wimbo ya Katavasia ya tisa.**

Salamu, Malkia, utukufu kwa wazazi na wabikira. Katika kila kinywa kisemaji wepesi, wakati kinasema, hakitaweza kukusifu kwa kustahili. Tena kila akili kinapata kizunguzungu bila kuweza kusikia kulala kwako. Kwa hii sisi wote tunakusifu kwa sauti moja.

**EKSAPOSTILARION.** *Sauti ya mbili. Ton mathiton oronton se.*

Ee Kristu, ulichukuliwa mbinguni machoni mwa Wafwasi wako, ulipanda kwa Baba yako, unakaa pamoja naye katika kiti chake; karibu ya mlango wa mbingu Malaika walikuja kukutana nawe wakasemezana mumoja kwa mwingine: Fungueni milango! Enyi milango, nyanyueni kuta zenu ili aingie mfalme wa utukufu, kwani Mfalme wetu anapanda kwa chemchem ya nuru. *(mara tatu).*

**MASIFU** *Sauti ya kwanza. Ton uranion tagmaton.*

Kama Malaika mbinguni, duniani tutukuzeni Mungu anayepanda juu ya kiti chake cha utukufu na tumwimbieni: Wewe ni Mtakatifu, ee Baba wa mbinguni, Neno wa milele na Roho Mtakatifu. *(mara mbili).*

Ee Mwokozi, Malaika wanapoona ajabu ya kupanda kwako, wakaambiana mumoja kwa mwingine: Ni ndoto gani tunaona machoni mwetu? Ni mwanadamu tunaona, lakini kama Mungu anachukuliwa mbinguni na mwili wake.

Ee Neno watu wa Galilaya walipokuona umepanda na mwili wako huko mulima wa Mzeituni, wakasikia malaika wakawaambia: «Sababu gani munakaa hapa kwa kutazama mbinguni? Atarudi na mwili wake kama mulivyomuona akipanda».

Utukufu kwa Baba... Sasa na siku zote...*Sauti ya mbili*

Ulipata mwili kwa kutaka kwako, ulionekana kwa kupenda kwako, ee Mungu wetu, uliteswa mwilini; ulifufuka katika wafu, ulishinda mauti, ulipanda mbinguni kwa utukufu wewe mwenye kujaza ulimwengu wote, na ulitutumia Roho Mtakatifu sababu ya kuimbia na kutukuza umungu wako.

**DOKSOLOGIA KUBWA**

**KUAGA** ni hivi: Yeye aliyepanda mbinguni katika utukufu tena anayekaa kuume kwa Mungu Baba, Kristu Mungu wetu kweli, kwa maombezi...

## LITURGIA TAKATIFU.

### ANTIFONON YA KWANZA

Pigeni mikono, ninyi mataifa yote; Kwa maombi...

Kwa kuwa Bwana aliye juu ni mwenye kuogopesha yeye ni mufalme mukubwa juu ya inchi yote.
Kwa maombi...

Atatiisha watu chini yetu, na mataifa chini ya miguu yetu. Kwa maombi...

Utukufu... Sasa... Kwa maombi ya Mzazi-Mungu...

### ANTIFONON YA MBILI.

Bwana ni mukubwa na mwenye kusifiwa sana.

Utuokoe, ee Mwana wa Mungu, Wewe uliyepanda kwetu na utukufu mbinguni, tunaokuimbia, Alliluia.

Mungu amejijulisha katika nyumba zake kubwa pahali pa kukimbilia... Utuokoe,...

Kwa sababu, tazama, wafalme walijikusanya wakapita pamoja. Utuokoe...

Utukufu... Sasa... Uliye Mwana wa pekee...

### ANTIFONON YA TATU.

Sikieni maneno haya, ninyi mataifa yote;

Apolitikion ya Siku Kuu hii:

Sauti ya ine. Unapanda katika utukufu, ee Kristu Mungu wetu, ukiwajaza Wafwasi wako na furaha kwa ahadi ya Roho Mtakatifu, ukiwapa nguvu na kuwabariki na mikono yako, kwani ndiwe Mwana wa Mungu, Mwokozi wa dunia.

Kinywa changu kitasema akili na mawazo ya moyo wangu yatakuwa ya ufahamu.

Apolitikion ya Siku Kuu.

Nitatega sikio langu nisikie mezali; nitafumbua fumbu langu kwa kinubi.

Apolitikion ya Siku Kuu.

Isodikon (Kuingia): Mungu amepanda kwa mashangilio, Bwana kwa mlio wa baragumu. Utuokoe, ee Mwana wa Mungu, Wewe uliyepanda kwetu na utukufu mbinguni, tunaokuimbia. Alliluia. Apolitikion ya Siku Kuu, mara tatu. Kontakion ya Siku Kuu.
Trisagion: Mungu Mutakatifu... Apostolos na Evangelion ya Siku Kuu.
*Pahali ya fasi:* Niwajibu kweli... tunaimba Hirmos ya Tisa ya Kanuni ya Siku Kuu. Kinonikoni: Mungu amepanda kwa mashangilio, Bwana kwa mlio wa baragumu.
*Pahali ya fasi:* Tumeona,... tunaimba leo Apolitikion ya Siku Kuu.

# MU KAZI INE MANGARIBI YA SIKU KUPANDA YESU MBINGUNI

*Kisha: «Bwana nimekuita...» tunaimba waimbu sita; tatu ya Siku Kuu ya Kupanda Yesu Kristu mbinguni na tatu ya Mineon.*
***Wimbo ya Siku Kuu**. Sauti ya kwanza.*

Ee Bwana, unapopanda mbinguni huko ulishuka, usituache mayatima lakini atushukie Roho Mtakatifu mwenye kuleta amani duniani; kwa watu wote onyesha matendo ya uwezo wako, ee Bwana.

Ee Kristu, ulipanda kwa Baba yako wa milele ambaye haukuacha kifua kubwa na Malaika hawakuongeza chochote kwa utukufu wa Utatu Mtakatifu; hata kisha umwilisho waliona katika wewe paka Mwana wa pekee wa Baba ambaye kwa mapendo yake kubwa, ee Bwana, utuhurumie.

Ee Bwana, Malaika wako waliwaambia Mitume wako: «Ninyi watu wa Galilaya sababu gani munatazama hivi mbinguni? Kama mulivyomuona Kristu Mungu wetu akichukuliwa katikati yenu kwenda mbinguni, yeye mwenyewe atarudi vilevile. Mtumikieni basi kwa uhaki na utakatifu wote.
***Wimbo tatu ya Mineon.***

Utukufu kwa Baba...*Sauti ya mbili.*

Ulipata mwili kwa kutaka kwako, ulionekana kwa kupenda kwako, ee Mungu wetu, uliteswa mwilini; ulifufuka katika wafu, ulishinda mauti, ulipanda mbinguni kwa utukufu wewe mwenye kujaza ulimwengu wote, na ulitupatia Roho Mtakatifu sababu ya kuimbia na kutukuza umungu wako.

**KUINGIA.** Mwangaza upole. **PROKIMENON** *Sauti ya saba.*

Mungu wako eko mbinguni na duniani, aliumba vitu vyote kwa kutaka kwake.
Shairi: Wakati wana wa Israeli walitoka mu Misri na nyumba ya Yakobo katikati ya watu wabaya, Yudasi akawa patakatifu pa Bwana.
Mungu wako eko mbinguni na duniani, aliumba vitu vyote kwa kutaka kwake.
Shairi: Bahari ilipoona hivi ikakimbia, yorodani ikarudi nyuma.
Mungu wako eko mbinguni na duniani, aliumba vitu vyote kwa kutaka kwake.
Ewe Bahari kwa nini unakimbia? Yorodani kwa nini unarudi nyuma?
Mungu wako eko mbinguni na duniani, aliumba vitu vyote kwa kutaka kwake.

**APOSTIKHA** *Sauti ya mbili. Ote ek tu ksilu se nekron.*

Huyu mwenye kujaza ulimwengu yote anawaambia Mitume wake wakati wanapanda mlima wa Mzeituni: Rafiki zangu, tazameni imefika waakti wa kuondoka kwangu; kwendeni kuwafundisha mataifa yote neno mulilofundishwa kwa sauti yangu. Kisha, akapanda katika utukufu kama juu ya gari; Wafwasi wakashikwa kwa woga kubwa.
Shairi: Enyi mataifa yote, pigeni mikono shangilieni Mungu kwa furaha.

Ee Kristu, wakati ulinyanyua mikono kwa kubariki Mama yako na Wafwasi wako waliokuja pamoja kule Betania na machoni mwao wingu la nuru likakuchukua, ulipanda kwa utukufu na ukaonekana mbinguni kuume kwa Baba, ukapokea ibada ileile.
Shairi: Mungu anapanda katika shangwe, Bwana, kwa sauti ya baragumu.

Kujeni, ninyi waaminifu wote, tupande juu ya mlima kubwa wa Mzeituni na kule, kama walipokusanyika Mitume, tuinue mioyo yetu na akili yetu sababu ya kutazama Bwana akichukuliwa na kwa shukrani tumulalamikie na furaha. Ee Bwana, utukufu kwa Kupanda kwako.

Utukufu kwa Baba... Sasa na siku zote...*Sauti ya sita.*

Ee Kristu, mlimani takatifu tunapotazama utukufu wako, ee kianga ya utukufu wa Baba, tunaimbia nuru ya uso wako; tunaposujudia Mateso yako, tunatukuza Ufufuo wako takatifu na Kupanda kwako; utuhurumie.
***Apolitikion ya kupanda Yesu mbinguni.***

# MU KAZI TANO ASUBUI KISHA KUPANDA YESU MBINGUNI

**KATHISMA YA KWANZA.** *Sauti ya mnane. To prostakthen mistikos.*

Ee Mwokozi mwenye huruma, ulipopanda juu ya mlima wa Mzeituni, ukachukuliwa mbinguni; maana wingu la nuru likakuondoa duniani machoni mwa Wafwasi wako wenye kushangaa wakati mbinguni Malaika wakapaza sauti wakisema: Enyi Milango, kwa woga inueni kuta zenu! Pamoja na majeshi ya juu-mbinguni viumbe vyote vinakuimbia, ee Mfalme wa ulimwengu yote.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*(mara ingine).*

**KATHISMA YA MBILI.** *Sauti ya mnane, Tin sofian ke Logon.*

Unapoenda juu ya mawingu ya mbinguni kisha kuwapa wanadamu amani duniani unachukuliwa sababu ya kukaa juu ya kiti taaktifu kama ulivyo wa asili moja na Baba na Roho Mtakatifu; ul;ionekana mwilini bila kugeuka na unaongojea ukamilifu wa vitu vyote sababu ya kuja tena duniani kuhukumu dunia yote. Ee Mwamzi mwenye haki, samehe roho zetu, ee Bwana, uwaondolee watumishi wako zambi zao, ee Mungu wa mapendo.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*(mara ingine).*

*Kisha tunaimba Kanuni, tunasoma Kontakion, Ikos, Eksapostilarion na Masifu ya Siku Kuu na kisha:*

**APOSTIKHA** *Sauti ya mbili. Ikos tu efratha.*

Hii ni mambo ya ajabu, mwili ya wanadamu inapanda mbinguni, inaungana na Neno la Mungu, Yeye Bwana mwenyezi.

Shairi: Enyi mataifa yote, pigeni mikono shangilieni Mungu kwa furaha.

Siku ya nuru ya kupanda kwa Bwana mbinguni inangaa na mwanga wake wote, inangaza dunia yote.

Shairi: Mungu anapanda katika shangwe, Bwana, kwa sauti ya baragumu.

Ee Kristu Mwokozi, kama ulivyowatumia toka mbinguni Wafwasi Roho Mtakatifu wa asili moja, tumia pia watu neema na nuru yako.

Utukufu kwa Baba... Sasa na siku zote...*Sauti ya tano.*

Ee Bwana, wakati ulichukulia mbinguni huko haukwacha, Malaika wakapaza sauti na furaha mumoja kwa mwingine: Ninyi Milango, inueni kuta zenu ili Mfalme wa utukufu aingie! Kwani kiti cha Wakheruvi ilikupokea na mwili wako, ee Bwana, matumaini yetu, utukufu kwako.

# MU KAZI TANO MANGARIBI KISHA KUPANDA YESU MBINGUNI

*Kisha :»Bwana nimekuita...» tunaimba wimbo sita; tatu ya Siku Kuu na tatu ya Mineon.*

***Wimbo ya Siku Kuu.*** *Sauti ya ine. Edokas simiosin.*

Kama mutu uliteswa, ee Mungu usiyeteseka, ulifufuka siku ya tatu mwenye kushinda mauti, ulifufua pamoja nawe wanadamu wote kaburini, ee Kristu, na ulipanda kwa Baba yako, ukaahidi Mitume wako Roho Mtakatifu, ee Bwana Mwenyezi na Mwokozi wa roho zetu.

Malaika waliyowatokea Wafwasi wakawauliza: Sababu gani munatazama mbinguni? Huyu muliona akipanda juu ya wingu la nuru atarudi sawasawa kuhukumu dunia kama alivyosema; kuendeni basi na fanyeni hii aliwaamuru ninyi.

Ee Bwana mwenyezi, kisha Ufufuo wako kaburini, ulichukua marafiki zako, ee Neno, ukawapeleka kule Bethania; na ukawabariki juu ya mlima wa Mzeituni mbele ya wewe kupanda mbinguni mwenye kuchukuliwa na malaika wa Mungu, ee Bwana Mwenyezi na Mwokozi wa Roho zetu.

***Wimbo tatu ya Mineon.***

Utukufu kwa Baba... Sasa na siku zote...*Sauti ya sita.*

Leo Majeshi ya juu-mbinguni wanapoona hali yetu mbinguni, wanashangaa kwa kupanda kwajko kwa ajabu na wanaulizana mumoja kwa mwingine wakisema: Ni nani huyu anakuja? Lakini walipotambua Bwana wao, wanaamuru milango ya mbinguni yafunguliwe. pamoja nao tunakuimbia

daima wewe utakayerudi toka mbinguni na mwili wako kama Mwamzi wa ulimwengu tena Mungu Mwenyezi.

**APOSTIKHA.** *Sauti ya mbili. Ikos tu efratha*

Ulipotimiza kwa kutaka kwako mapenzi ya Baba yako kisha kuunganisha inchi na mbingu, ulipanda kwa utukufu huko ulikuwa zamani.

Shairi: Enyi mataifa yote, pigeni mikono shangilieni Mungu kwa furaha.

Ulipanda kwa Baba yako bila kumuacha, ee Mungu wa mapendo, na uliinua, ee Bwana, mateso yetu ya hapa chini.

Shairi: Mungu anapanda katika shangwe, Bwana, kwa sauti ya baragumu.

Ee Bwana, wingu la nuru lilikuchukua mbinguni, na kwa mwito wako Malaika walikutumikia na woga wakitetemeka.

Utukufu kwa Baba... Sasa na siku zote...*Sauti ya saba*.

Ee Bwana, kwa mapendo yako kwa wanadamu ulikuja juu ya mlima wa Mzeituni; ulipochukuliwa kwa wingu ukatoweka machoni mwa Wafwasi wako, wakaogopa kwa ono la ajabu lakini walifurahiwe kwa kuongojea Roho Mtakatifu; ulipotusabitisha katika yeye, utuhurumie, ee Mungu Mwokozi.

**Apolitikion ya Siku Kuu na Kuaga.**

# MUPOSHO ASUBUI KISHA KUPANDA YESU MBINGUNI

## KATHISMA YA KWANZA.

*Sauti ya kwanza. Tu lithu sfragisthentos*.

Ee Mwokozi, Malaika waliposhangaa kupanda kwako na Wafwasi waliposangaza kwa kuchukuliwa kwako kwa ajabu, ulichukuliwa na utukufu kama Mungu, milango yalifunguliwa mbele yako; ndio maana majeshi ya mbinguni wakashangaa yakipaza sauti: Utukufu kwa mapendo yako, ee Mwokozi, utukufu kwa Ufalme wako, utukufu kwa kupanda kwako, ewe peke yako mpenda-wanadamu.

Utukufu kwa Baba... Sasa na siku zote... *(mara ingine).*

**KATHISMA YA MBILI.** *Sauti ya kwanza. Tu lithu sfragisthentos.*

Ee chemchem ya uzima, uliponyanganya Hadeze na kwangazia ulimwengu, ulipanda na utukufu wewe mwenye kushika ulimwengu mkononi mwako; ndivyo maana tunakutukuza pamoja na Malaika, ee Bwana Mwenyezi. Utukufu kwa kupanda kwako, ee Kristu, utukufu kwa Ufalme wako, utukufu kwa rehema yako, peke yako mpenda-wanadamu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*(mara ingine).*

*Kisha tunaimba Kanuni, Kontakion, ikos, eksapostilarion na Masifu ya Siku Kuu na kisha:*

**APOSTIKHA.** *Sauti ya mbili. Ikos tu efratha.*

Bwana aliwaambia marafiki zake: Sitawacha mayatima ninyi nilikusanya na kuchagua, lakini nitawatumia ninyi Roho Mtakatifu.

Shairi: Enyi mataifa yote, pigeni mikono shangilieni Mungu kwa furaha.

Malaika waliwaambia Mitume Watakatifu: Ninyi watu wa Galilaya, kama mulivyomuona akienda, Bwana atarudi vivyo hivyo.

Shairi: Mungu anapanda katika shangwe, Bwana, kwa sauti ya baragumu.

Ee Bwana, waliposhuka kwa furaha mlima wa Mzeituni, Wafwasi wako walitukuza na kuimbia Kupanda kwako takatifu.

Utukufu kwa Baba... Sasa na siku zote...*Sauti ya ine*.

Ulipanda toka dunia mpaka mbinguni kwa utkufu, wewe ambaye umungu inajaa ulimwengu; unakaa kuume kwa Baba, wewe Neno uliyekuwako tangu mwanzo karibu ya Mungu; walipoona hivi Malaika wa mbinguni wakaogopa na wakawaambia Mitume: Sababu gani munakaa kwa kutazama mbinguni? Huyu muliyeona atarudi na utukufu duniani kuhukumu wanadamu na kumulipa kila

mumoja kadiri ya matendo yake. Tumwaambie: «Wewe mwenye kujaa duniani, ee Bwana mwenyezi, utukufu kwako.

# SIKU YA MUNGU YA WAPADRI WATAKATIFU YA MKUTANO IKUMENIKI MKUBWA YA KWANZA KATIKA MJI NIKEA

*Elezo: Kisha Zaburi Proimiakos tunaimba: «Bwana nimekuita...» na kisha wimbo tatu ya Ufufuo ya Kristu, tatu ya Siku Kuu ya Kupanda Kristu mbinguni na ine ya Wapadri Watakatifu wetu.*

***Wimbo ya Ufufuo.*** *Sauti ya sita.*

Ee Kristu, ikiweza kushinda juu ya Hadeza, ulipanda juu ya Msalaba, kusudi ufufue pamoja nawe,wao waliokaa katika giza ya mauti, wewe uliye na uhuru katikati ya wafu. Wewe uliyechirizika uzima toka nuru yako, ee Mwenyezi na Mwokozi, utuhurumie.

Leo Kristu akishinda mauti, alifufuka, kama alivyosema na akaleta shangwe ku ulimwengu, kusudi wote tupaze sautim, na tuseme wimbo hivi: Chemchem ya uzima, Nuru isiyoweza kukaribiwa, Mwenyezi na Mwokozi, utuhurumie.

Ewe Bwana, uliye katika viumbe vyote, tutakimbilia wapi sisi wenye zambi? Juu ya mbinguni? Wewe unakaa. katika Hadeze? Ulishinda mauti. Katika chini ya bahari? Kule ni mukono wako, ee Rabi. Tunakimbilia kwako, tukikusujudu tunakusihi: Ewe Uliyefufuka katika wafu, utuhurumie.

***Wimbo tatu ya Siku Kuu ya Kupanda Yesu mbinguni***

*Sauti ya Sita.*

Bwana alipanda mbinguni sababu ya kutuma duniani Roho Mtakatifu; kiti chake kimetayarishwa mbinguni, mawingu ni pa kufinyayangia miguu yake; Malaika wanashangaa kwa kuona mwanadamu amekuwa juu yao, Baba anapokea huyu anakaa milele kifwani mwake, Roho Mtakatifu anaamuru katika majumbe wake: Enyi Milango, funguni, ukuta wenu, enyi mataifa yote, pigeni mikono, maana Kristu amepanda kule alikuwa zamani.

Ee Bwana, kwa Kupanda Kwako mbinguni Wakheruvi waliogopa pa kukuona umependa juu ya mawingu, wewe Mungu mwenye kukaa juu yao; tunatukuza neema wema wako.

Ee Kristu, mlimani takatifu tunapoona utukufu wako, ee Nuru ya utukufu wa Baba, tunaimbia nuru ya uso wako; tunasujudia mateso yako, tunaheshimu Ufufuo wako takatifu na kutukuza Kupanda kwako; utuhurumie.

***Wimbo ine ya Wapadri Watakatifu.****Sauti ya sita. I apegnosmeni*

Baba alikuzaa tangu mwanzo wa nyakati bila mama hata kama Arius anakutukuza kama kiumbe, apana kama Mungu, akichanganya vibaya kiumbe na Muumba wake, na kwa hii anastahili moto ya milele, lakini Makutano ya Nikea inakutangaza kuwa Mwana wa Mungu, wewe Bwana mwenye kutawala pamoja na Baba na Roho Mtakatifu.

Ee Mwokozi, nani alipasua nguo yako? Na Arius mwenye kutenga na kugawanya utukufu na ufalme wa milele wa Utatu Mtakatifu; hakubali ya kama wewe ni Mumoja wa Utatu Mtakatifu, inamuwazisha Nestorius kukataa neno. «Mzazi-Mungu», lakini Makutano ya Nikea inakutangaza kuwa Mwana wa Mungu, wewe Bwana mwenye kutawala pamoja na Baba na Roho Mtakatifu.

Ameanguka katika zimu ya makafiri, huyu Arius ambaye kwa yeye nuru haiwezi kuonekana, na haki ya Mungu ilipasua tumbo lake, akafa vibaya kama Yudas kwa matendo na mawazo yake, lakini Makutano ya Nikea inakutangaza kuwa Mwana wa Mungu, wewe Bwana mwenye kutawala pamoja na Baba na Roho Mtakatifu.

Arius aligawanya katika hali tatu asili moja ya Utatu Mtakatifu, lakini Wapadri Wabebaji-Mungu walipokusanyika na bidii kama Elia Mthesviti katika makutano, wakamukatakata kwa upanga wa Roho huyu alifundisha kufuru la haya: Waliifanya kwa shauri la Roho Mtakatifu.

Utukufu kwa Baba. *Sauti ya sita.*

Tutukuzeni leo Wapadri Wabebaji-Mungu, hawa waimbaji wa siri wa Roho Mtakatifu waliovumisha katika Eklezya umoja wa Mungu wakatangaza hali moja ya Utatu Mtakatifu; juu ya Arius wakashika imani ya kweli na wanamuomba daima Mungu kusudi ahurumie roho zetu.

Sasa na siku zote... **THEOTOKION**. *Sauti ya sita*

Nani hatakuita wewe Mwenye heri, Bikira Mtakatifu kamili? Nani hataimba kuzaliwa kwa Mwana wako bila mume? Kwani Mwana wa pekee aliyeangaa mbele ya wakati kwa Baba, yeye vilevile alitokea kwa wewe uliyesafi, akitwaa mwili usiyosemwa; yeye ni Mungu sawasawa na hali yake, na akajifanya mtu kwa kadiri ya hali ya watu kwa ajili yetu; yeye hagawanyike kwa uso mbili, lakini anajulikana kwetu katika hali mbili bila muchanganyo. Umusihi, ee Bikira mutaratibu na heriu daima, kwa murehemu nafsi yetu.

**KUINGIA.** Kisha: Mwangaza upole (ilaron)... **PROKIMENON.**

**Somo ya Mwanzo tutasoma.** *(14,14-20).*

Na wakati Abramu aliposikia ya kama ndugu yake ametwaliwa mufungwa, aliongoza watu wake waliofundishwa, waliozaliwa nyumbani mwake, mia tatu kumi na wanane, akawafuata hata Dani. Akajigawa juu yao usiku, yeye na watumihsi wake, akawapiga na kuwafuata hata Hoba ulio kwa upande wa kushoto wa Damasiki. Akarudisha mali zote, akaleta tena ndugu yake Loti vilevile na mali zake, na wanawake vilevile, na watu. Mufalme wa Sodomo akatoka kukutana naye nyuma ya kurudi kwake toka uuaji wa Kedori-Laomeri, na wafalme waliokuwa pamoja naye, kwa bonde la Sawe (lililo bonde la Mufalme). Melkisedeki, mufalme wa Salemi, akatoa mukate na mvinyo; naye alikuwa kuhani la Mungu aliye juu; akamubariki na kusema: Abarikiwe Abramu na Mungu aliye juu, mwenye mbingu na inchi; na abarikiwe Mungu aliye juu aliyetoa adui zako mukononi mwako.

**Somo ya Kumbukumbu la Torati, tutasoma** (*1,8-17).*

Tazama, nimeweka inchi mbele yenu: mwingie na kuriti inchi Bwana aliyoapia baba zenu, Abrahamu, na Isaka, na Yakobo, kwamba atawapa na uzao wao nyuma yao. Nami niliwaambia ninyi kwa wakati ule nikisema: Siwezi mimi mwenyewe peke yangu kuwachukua ninyi: Bwana Mungu wenu amewafanya ninyi kuwa wengi, na tazama, leo ninyi ni kama nyota za mbingu kwa wengi. Bwana Mungu wa baba zenu, awafanye ninyi kuwa wengi mara elfu kuliko mulivyo, na awabariki ninyi kama alivyowaahidi ninyi! Namna gani mimi peke yangu, ninaweza kuchukua usumbufu wenu na muzigo wenu na magomvi yenu? Mujitwalie watu wenye akili na ufahamu na wenye kujulikana, sawasawa na makabila yenu, nami nitawafanya wawe vichwa juu yenu. Nanyi mulinijibu na kusema: Neno ulilolisema ni jema kwa kufanya. Hivi nikatwaa vichwa vya makabila yenu, watu wenye akili, na wenye kujulikana, nikawafanya wawe vichwa juu yenu, maakida juu ya elfu, na maakida juu ya mia, na maakida juu ya makumi tano, na maakida juu ya kumi, na wenye amri, kwa kadiri na kamabila yenu. Nikaagiza waamuzi wenu kwa wakati ule nikisema: Sikieni ninyi maneno kati ya ndugu zenu, na hukumuni kwa haki kati ya mutu na ndugu yake, na kati ya mugeni aliye pamoja naye.

**Somo ya Kumbukumbu la Torati, tutasoma** (*10,14-21 ).*

Tazama mbingu ni mali ya Bwana Mungu wako, na mbingu za mbingu, na inchi na vyote vilivyo ndani yake. Tena Bwana alifurahia baba zako ili kuwapenda, akachagua uzao wao nyuma yao, hata ninyi, zaidi ya mataifa yote, kama na leo. MUtahiri basi ngovi ya moyo wenu, yeye ni Mungu wa miungu na Bwana wa wabwana, Mungu mukubwam, mwenye uwezo na mwenye kuogopesha, asiyeangalia nyuso za watu wala hapokei rushwa. Anafanyia yatima na mujane hukumu basi: Maana ninyi mulikuwa wageni katika inchi ya Misri. Ogopa Bwana Mungu wako; umutumikie, na uambatane naye, na kuapa kwa jina lake. Yeye ni sifa yako, na yeye ni Mungu wako, aliyekutendea maneno haya makubwa na ya kuogopesha, macho yako yaliyoona.

**L I T I A** *Utukufu kwa Baba...Sauti ya tatu.**(**Ya Watakatifu)*

Enyi Wapadri Watakatifu, mulikuwa walinzi wa mafundisho ya Mitume; Waalimu wa imani ya kweli mulifundisha Utatu Mtakatifu wa asili moja, na mulikataa kufuru la Arius katika Makutano;

mulimukataa pia Makedonius aliyekana Utatu Mtakatifu, mulimuhukumu Nestorius, Eftiki na Dioskori, Sabellius na Severi «asiye na mkubwa», kwa maombezi yenu mutuokoe toka mafundisho ya uwongo na lindeni uzima yetu katika imani safi.

Sasa na siku zote...*Ya Siku Kuu*. *Sauti ya sita.*

Ee Bwana, ulipotimiza fumbo ya wokovu, ulichukua Wafuasi wako pamoja nawe sababu ya kuwapeleka juu ya mulima wa Mzeituni, na ulipanda katika anga ya mbinguni; ee Bwana wewe uliyejifanya maskini kwa ajili yangu mpaka kuvaa ubinadamu wangu na kupanda kwa utukufu ambako haukutengana nayo, tuma toka mbinguni Roho wako Mtakatifu sababu ya kuangazia roho zetu na nuru yako.

## APOSTIKHA. *Sauti ya sita*

Ufufuo wako, ee Kristu Mwokozi, unaimbiwa kwa malaika mbinguni; na utustahilishe sisi wa dunia, tunakutukuza kwa mioyo safi.

Ulivunja milango ya shaba, na ulikata mapingo ya Hadeze, kwa kuwa wewe ni Mungu Mwenyezi, ukifufua uzao wa watu walioanguka; kwa hii na sisi tunaita kwa sauti moja: Ewe Bwana, uliyefufuka katika wafu, utukufu kwako.

Kristu akitaka kutusimamisha tena toka anguko la zamani, anapigiliwa musalabani na anawekwa kaburini; lakini wanawake wabebaji-manukato wakimutafuta kwa machozi na maombolezo, walisema: Ole kwetu! Ee, Mwokozi wa wote! Namna gani ulikubali kukaa kaburini? Japo ulitaka kukaa kule, namna gani uliibwa? namna gani uliondoshwa? Pahali gani mwili wako uletaji-uzima ulifichwa? Lakini, ee Rabi, kama ulivyoahidi, onekana kwetu, na simamisha machozi ya maombolezo yetu. Wakati wanawake walipolia, Malaika aliwaambia kwa sauti kubwa: Musilie, na museme kwa Mitume ya kama Bwana alifufuka, akileta duniani usamehe na rehema kubwa.

Ukisulubiwa kama ulivyotaka, ee Kristu, na kwa maziko yako ukinyanganya mauti, ulifufuka siku ya tatu, kwa wewe ni Mungu kwa utukufu, ukileta duniani usiyomwisho, na rehema kubwa.

Utukufu kwa Baba... (ya Watakatifu) *Sauti ya ine*.

Enyi Waaminifu Orthodoksi, tutukuzeni leo makumbusho ya Wapdri Wabebaji-Mungu waliokuja katika mji wa Nikea toka pande zote za ulimwengu; walikataa mafundisho ya kafiri Arius na wakaiondoa kwa Ekklezya ya ulimwengu; wakaamuru kukiri Mwana wa Mungu wa asili moja na wa milele, mwenyi kuwako hata mbele ya nyakati; wakayandika waziwazi katika simvolo (Fundisho) ya Imani, na sisi wenye kufwata mafundisho yao takatifu, kwa matumaini ya imani tunaabudu pamoja na Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, Utatu wa asili moja katika Mungu mumoja.

Sasa na siku zote...(Ya siku Kuu) *Sauti ya kwanza*

Ee Bwana, kwa wema wako, kwa kutimiza fumbo iliyofichwa milele, ulikuja pamoja na Wafwasi wako kwa mlima wa Mzeituni, pamoja na huyu aliyekuzaaewe Bwana na Muumba wa ulimwengu wote; kwani alipokuwa mama, aliteswa kuliko wote katika mateso yako na akastahili kuonja furaha kubwa ya kukuona umetukuzwa mwilini mwako; na sisi wenyewe tunaposharikia hii furaha leo ya kupanda kwako mbinguni, tunatukuza, ee Bwana rehema yajko kwa ajili yetu.

**APOLITIKION** *Sauti ya sita.*

Majeshi ya Malaika pa kaburi yako, na walinzi walikuwa kama wafu; Maria alisimama kaburini, akitafuta mwili wako usiye na doa. Ulinyanganya Hadeze bila kujaribiwa kwake. Ulikuta Bikira, ukileta uzima. Ewe Bwana uliyefufuka katika wafu, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba...Ya Wapadri Watakatifu. *Sauti ya mnane.*

Utukuzwe, ee Kristu Mungu wetu, wewe uliyeweka duniani Wapadri wetu Watakatifu, kama taa na kwa ajili yao ulituongoza wote kwa imani ya kweli: Ee Mungu wa huruma Bwana, utukufu kwako.

Sasa na siku zote... Apolitikion ya Kupanda Yesu Kristu Mbinguni. *Sauti ya ine*

Unapanda katika utukufu, ee Kristu Mungu wetu, ukiwajaza wafwasi wako na furaha kwa ahadi ya Roho Mtakatifu, ukawapa nguvu na kuwabariki na mikono yako, kwani ndiwe Mwana wa Mungu, Mkombozi wa dunia.

*Elezo: Hii Apolitikio tutaimba na kesho asubui, kisha* «Bwana ndiwe Mungu...»

# IBADA YA ASUBUI YA SIKU KUU YA WAPADRI WATAKATIFU

**KATHISMA YA KWANZA** *Sauti ya sita.*

Hadeze ilisikitikia kufungwa kwa kaburi na Maria Magdalena aliwalalamikia Mitume waliyofichama: Enyi Watumishi wa mzabibu, tokeni, tangazeni habari ya Ufufuo; kwani Bwana amefufuka akileta duniani neema ya wokovu.

Utukufu kwa Baba.

Ee Bwana, Maria Magdalena alisimama karibu ya Kaburi yako na akazania ya kama mwenye shamba, na machozi yake akalalamika: wapi umeweka Uzima wa milele? Wapi ulificha huyu mwenye kukaa pa kiti cha Wakheruvi? Kwani walinzi wake wameogopa; unirudishie Bwana wangu ao lalamika pamoja nami: Wewe ambaye unapotoka kaburini, unafufua wafu, ee Bwana, utukufu kwako.

Sasa na siku zote...**THEOTOKION**.

Wewe uliyemuita Mama yako «Mwenyi heri» na uliyeteswa kwa kutaka kwako, nuru yake iliangaa msalabani, kwani ulitaka kwenda kumutafuta Adamu; ukawaambia malaika: Furahini pamoja nami, kwani imepatikana drakma iliyototea. Wewe uliyefanya yote kwa hekima, utukufu kwako, ee Bwana Mungu wetu.

**KATHISMA YA MBILI.** *Sauti ya sita*

Uzima wetu Ililala kaburini na jiwe lilifunjwa, maaskari walimuchunga Kristu kama ni juu ya kukesha kwa kumulinda Mfalme; lakini alipopofusha maadui zake, Bwana akafufuka kaburini.

Utukufu kwa Baba...

Ee Mwokozi mwenyezi, kwa lufu yako ya kutaka sisi tulipata uzima wa milele, kwani kwa Ufufuo wako tamatifu, ulifufua wanadamu wote, uliondoa ushindi wa Hadeze na kuvunja uchungu wa mauti.

Sasa na siku zote. **THEOTOKION**.

Ee Mzazi-Mungu na Bikira mubarikiwa, umuombe Mwana wako, Kristu Mungu wetu alisulubiwa msalabani kwa kutaka kwake na aliyefufuka katika wafu alete wokovu ku roho zetu.

*Elezo: Kisha waimbaji wanaimba Mahimidi ya Ufufuo ya Kristu. Kisha wanasoma Ipakoi.*

**IPAKOI.**

Ee Kristu, kwa lufu yako ya kutaka na yenye kuleta uzima, ulivunja milango ya Hadeze; ee Mungu, unatufungulia Paradizo ya zamani; ulipofufuka katika wafu, unanyanganya uzima wetu kuzimuni.

**ANAVATHMI NA PROKIMENON.**

*(Tafuta mu kitabu ya Paraklitiki).* *Sauti ya sita.*

**EVANGELION EOTHINON YA KUMI** *(Yoane 21,1-14).*

Tukiona Ufufuo wa Kristu...Zaburi 50 (51).

**KANUNI YA UFUFUO YA KRISTU YA PARAKLITIKI**

**KANUNI YA SIKU KUU YA KUPANDE YESU KRISTU MBINGUNI.**

**KANUNI YA WAPADRI WATAKATIFU YA LEO**

**WIMBO YA KWANZA Sauti ya sita. Os en ipiro pezefsas.**

Watakatifu wa Mungu mutuombee kwa sisi.

Ninapotukuza Makutano ya Wapadri watakatifu, ee Kristu nakuomba, nakusihi nichunge moyoni mwangu mafundisho yao takatifu.

Watakatifu wa Mungu mutuombee sisi.

Ee Kristu, Wapadri Wabebaji-Mungu wanapokusanyika leo kama taa zenye kuangaa na nuru, wamekutambua kuwa Mwana wa pekee wa Mungu, wa asili moja na baba na mwenye kuwako milele kama yeye.

Utukufu kwa Baba...

Ee Bwana, wasindikizi wenye kuangaa wa Ekklezya iliyo mchumba wako, waliitolea mafundisho ya imani kama johari na waliipamba kwa pambo la uwezo.

Sasa na siku zote...**THEOTOKION**.

Alipovaa nguo za harizi zenyi kusukwa, Malkia Mtakatifu aliyenda kwa Mfalme, aliye Mwana wake na Mungu wake, na anaombea roho zetu wokovu.

**WIMBO YA TATU**
**KANUNI YA UFUFUO YA KRISTU YA PARAKLITIKI**
**KANUNI YA KUPANDA MBINGUNI.**

**KANUNI YA WATAKATIFU**. *Uk estin Agios, os o Theos imon.*

Watakatifu wa Mungu mutuombee sisi.

Kwa ukafiri wake Arius anachanganya kwa kizazi chako cha umungu njia ya ustawi, mateso na mtanguo, lakini yeye mwenyewe alikatwa kwa upanga wa Roho Mtakatifu.

Watakatifu wa Mungu mutuombee sisi.

Ee Bwana wa wema, Waalimu watakatifu walipopangwa kwa kushindana kama Abrahamu zamani juu ya wafalme, wakawashinda maadui zako wakali kwa uwezo wa mikono yako.

Utukufu kwa Baba...

Ee Mwokozi, Makutano tukufu na ya kwanza ya maaskofu wako Watakatifu ilikutangaza na imani kama ulizaliwa mbele ya nyakati na uko wa aili moja na Baba wa milele tena Muumba wa ulimwengu.

Sasa na siku zote...**THEOTOKION**.

Ee Bikira, hata neno moja, hata luga moja ya wanadamu haiwezi kuacha kukutukuza kama inavyostahili, kwa sababu ilimupendeza kristu aliye chemchem ya uzima ajifanye mtu bila mbegu tumboni mwako, ee Bikira usiye na doa.

**KONTAKION YA KUPANDA MBINGUNI.** *Sauti ya mnane.*

Ulipotimiza kwa ajili yetu tendo lako la wokovu, kisha kuunganisha mbingu na dunia, watu na Mungu, katika utukufu, ee Kristu Mungu wetu, ukapanda mbinguni bila kutwacha, lakini umekaa siku zote katikati yetu na ukawaambia wale wanaochunga mapendo yako: Mimi ni pamoja nanyi siku zote na mutu hata mumoja hawezi kufanya chochote juu yenu.

**KATHISMA YA WATAKATIFU.** *Sauti ya inne. Takhi prokatalave.*

Enyi Wapadri wenye heri, kweli duniani ninyi mumekuwa kwa ajili ya ukweli wa Kristu, taa zenye kuangaa, munayeyusha uhalifu wa wasemaji waongo, munazima moto ya makafiri: Enyi Maaskofi wa Kristu, ombeni kwa ajili ya wokovu wetu.

Utukufu kwa Baba...

Leo mji wa nuru wa Nikea inakusanya maaskofu mia tatu kumi na nane wa dunia yote juu ya kufuru ya Arius alishusha Mumoja wa Utatu Mtakatifu, Mwana na Neno la Mungu; walipomukataa, wanasabitisha imani ya kweli.

Sasa na siku zote...Kwa Kupanda mbinguni

Ee Kristu mpenda-wanadamu ulipanda mbinguni kwa utukufu na kukaa kuume kwa Baba bila kumuacha; uliwaahidi Wafwasi wako wenye hekima kuwatumia Roho Mtakatifu; ututumie sisi wote nuru yako yangaze roho zetu na mawazo yetu ili tukuimbie daima, ee Bwana.

**KONTAKION YA WATAKATIFU**. *Sauti ya mnane*.

Mafundisho ya Mitume na ya Wapadri inaifundisha, wanasabitisha umoja wa imani: Inapovaa nguo ya ukweli yenyi kufuma kwa ufunuo wa mbinguni, inafundisha na uaminifu na kutukuza fumbo kubwa ya imani.

**IKOS**

Tusikilizeni Ekklezya ya Mungu inatulalamikia kwa kutuhubiri ukweli kubwa: Huyu aliye na kihu aje kwangu anywe ni katika kisima cha hekima ninachanga divai yangu; nimeichanga na neno la ukweli; na hii maji ninamimina haiko ile ya ubishi, lakini ni ile ya mapatano katika imani ambayo anakunywa Israeli mupya anatokea Mungu akimwambia: Tazama na ona, mimi ni yuleyule, sikubadilika, Mimi ni Mungu kwa mwanzo kama kisha wakati hakuna mwingine kuliko mimi. Wale watashariki watashiba na watatukuza fumbo kubwa ya imani.

**SINAKSARION YA LEO**. *Kisha hii:*

Leo siku ya Yenga ya saba toka Paska, tunatukuza Makutano (Sinodi) Ikumeniki (na maaskofu ya ma fasi yote ya dunia) ya Kwanza ya mji Nikea, inje ya muji kubwa Konstantinopoli walikusanyika Wapadri Wabebaji Mungu miya tatu na kumi na mnane.

Enyi Nyota wenye kuangaa wa mbingu ya roho, angazeni roho yangu na nuru yenu.
Alipomukatalia Mwana kwa hali ya Baba, Arius atakuwa mgeni kwa utukufu wa Mungu.

Kwa maombezi ya Wapadri Watakatifu na Wabebaji-Mungu, Miya tatu, kumi na mnane, ee Kristu Mungu wetu, utuhurumie. Amina.

**KATAVASIA** *Sauti ya Ine.*

Wingu wa kimungu ulifunika Musa mwenye-ulimi muzito, na Yeye alihubiri sheria iliyoandikwa na Mungu. Kwani akiondosha uchafu toka macho ya roho aliona Mungu Aliye, na aliingiza katika mafikili ya Roho, akimwimbia kwa wimbo kimungu.

Minyororo la tumbo ya tasa ilikatika, na tena laumu isiyovumiliwa ya Mzazi, paka kwa maombi ya Hana nabii wakate, mwenye-kuwa moyo uliovunjika mbele ya Mufalme wa uwezo, na Mungu wa kujua yote.

Mufalme wa wafalme. Mwana wa pekee na Neno, uliyezaliwa na Baba peke yake asiye mwanzo, ulituma Roho kweli sawa na wewe kwa mitume, kwa sababu wewe ni mwema, na wao waliimba: Utukufu kwa uwezo wako, ee Bwana.

Mupokee usafisho unaozimisha zambi, mupokee upepo wa Roho ya umande na ya moto, enyi watoto wa Kanisa kwa uso ya nuru. Kwa maana sasa katika sayuni sheria ilitoka, neema ya Roho ilionekana ndini kama za moto.

Kristu Rabi, uko usamehe na wokovu, ukianga toka Bikira, ili utoshe toka uharibifu Adamu mwenye kuanguka na wote, kama ulitosha toka matumbo ya samaki nabii Yona.

Upatanisho wa viombo vya musiki ilinguruma, kusudi mataifa waabudu sanamu isiyo na nafsi iliyofanywa kwa zahabu. Lakini neema ya Mufariji ilitayonuru iliwapatia moyo ya ukimya kwa waaminifu wapaze sauti: Utatu wa usawa pasipo mwanzo, uko peke yako mubarikiwa.

Tunasifu, tunamuhimidi na tunamusujudu Bwana.

Mufano wa nuru tatu ya Umungu unafungula minyororo na unapoza moto. Watoto wanaimba na viumbe vyote vilivyoumbwa na Mungu, Mwokozi na Muumba peke yake, vinamubarikia, kwaq kuwa Yeye ni Mwema.

**WIMBO YA TISA**
**YA KANUNI YA UFUFUO YA KRISTU YA PARAKLITIKI**
**YA KANUNI YA KUPANDA YESU MBINGUNI**
**KANUNI YA WATAKATIFU** *Sauti ya sita. Theon antropis..*

Watakatifu wa Mungu mutuombee sisi.

Neno wa mbele ya wakati mwenye kukaa pamoja na Baba mbinguni katika kiti cha ufalme na kuishi naye milele aliwavika ninyi uwezo wa Roho Mtakatifu na kuwakusanya katika Makutano aliwafanya ninyi kuwa wenzake katika mashindano, na sasa enyi Wapadri watakatifu, pamoja na majeshi ya mbinguni munamutukuza milele.

Watakatifu wa Mungu mutuombee sisi.

Kama waganga wenye hekima wa roho na mwili, mulisimamisha mafundisho ya Arius na ya uhalifu wake mbaya, mukawekea Waaminifu wote Simvolo (fundisho) ya imani na sisi wenye kuitangaza sasa tunatukuza daima makumbusho yenu takatifu.

Utukufu kwa Baba...

Ee Kristu, wewe Nuru safi, uliokoa roho yangu toka giza ya tamaa kwa maombezi ya maaskofu wako watakatifu ambao Sinodi inakutangaza kama wa milele na usiyeumbwa, Muumba wa ulimwemgu tena Mungu wa milele pamoja na Baba.

Sasa na siku zote...**THEOTOKION**.

Ee Mzazi-Mungu na malkia, kwa kuzaa kwako kwa ajabu wafu wanafufuliwa, kwani kwako alitoka Bwana aliye Uzima wetu, mwenye kuvaa mwili wetu, na alipoondoa giza ya mauti, aliangaza ulimwengu.

**Wimbo ya Katavasia ya tisa.**

Salamu, Malkia, utukufu kwa wazazi na wabikira. Katika kila kinywa kisemaji wepesi, wakati kinasema, hakitaweza kukusifu kwa kustahili. Tena kila akili kinapata kizunguzungu bila kuweza kusikia kulala kwako. Kwa hii sisi wote tunakusifu kwa sauti moja.

*Kunafwata Shairi za ufufuo zifwatazo:* WAIMBAJI: Bwana Mungu wetu ndiye Mtakatifu. *(mara tatu)*

**EKSAPOSTILARION YA UFUFUO YA KRISTU.** *Sauti ya mbili.*

Zamani bahari ya Tiberia ikawashauria Simon Petro na Toma, nathanaeli na Waana wawili wa Zebedeo pamoja na wafwasi wengine wawili kwenda kuvua samaki; kwa amari ya Kristu, walipotupa wavu wao upande wa kuume, hawakuweza kuukokota sababu ya wingi wa samaki; Petro alipomtambua Bwana akajitupa bajharini mpaka kwa yeye; Hii ndiyo mara ya tatu alionekana, na pa moto wa makaa akawaonyesha samaki na mukate.

**YA WATAKATIFU.** *Sauti ya mbili. Ginekes akutisthite.*

Leo tunaposhangilia makumbusho ya Wapateri wetu watakatifu,, kwa maombezi yao tunakuomba, ee Rabi wa mapendo: okoa watu wako toka udanganyifu wote na uhalifu wote, Bwana, utupe tuimbie utukufu wa Baba, wa Neno na wa Roho Mtakatifu.

**YA KUPANDA YESU MBINGUNI.**

Ee Kristu, ulichukuliwa mbinguni machoni mwa Wafwasi wako, ulipanda kwa baba yako, unakaa pamoja naye katika kiti chake; karibu ya mlango wa mbingu Malaika walikuja kukutana nawe wakasemezana mumoja kwa mwingine: Fungueni milango! Enyi milango, nyanyueni kuta zenu ili aingie mfalme wa utukufu, kwani Mfalme wetu anapanda kwa chemchem ya nuru.

***Nyimbo ine za ufufuo wa Kristu**..*

**MASIFU.** *Sauti ya sita.*

Msalaba wako, ee Bwana, ni uzima na ufufuo kwa watu wako; na tukitumainia kwake, tunakuimbia wewe, Mungu wetu, uliyefufuka. Utuhurumie.

Maziko yako, ee Rabi, ilifungua Paradizo kwa uzao wa watu; na tukikombolewa katika uharibifu, tunakuimbia wewe, Mungu wetu, uliyefufuka. Utuhurumie.

Pamoja na Baba na Roho, tumwimbie Kristu, aliyefufuka katika watu, na tupaze sauti kwa yeye: Ewe ni uzima na ufufuo wetu. Utuhurumie.

Katika siku tatu ulifufuka, ewe Kristu, toka kaburi, kama ilivyoandikwa, ukiamusha pamoja nawe Baba yetu; kwa hii uzao wa watu tunakutukuza na tunaimba ufufuo wako.

***Wimbo ya Watakatifu.***

*Sauti ya sita. Olin apothemeni.*

Walipokusanya maarifa yao yote ya kiroho kwa maongozi ya Roho Mtakatifu, Wapadri watakatifu wakandika Simvolo ya imani ambamo walitangaza waziwazi kabnisa ya kama Neno ni wa milele pamoja na Baba aliyemzaa na wa asili moja kweli kufwatana na mafundisho ya Mitume Watakatifu.*(mara mbili).*

Shairi: Utukufu kwako, ee Bwana, Mungu wa Baba zetu, sifa ni kwa jina lako, na utukufu milele.

Walipopokea nuru yote ya Roho Mtakatifu, Wapadri Watakatifu wakatangaza, kwa maombezi ya Mungu, fumbo ya imani iliyo fupi kwa maneno lakini tajiri kwa maana, na kama watangazaji wa Kristu wenye kuongozwa na mafundisho ya habari njema na ya mapokeo takatifu, walipokea juu mbinguni ufumbulio wa nuru, na walipoangazwa wote kwa nuru wakafasiria makanuni takatifu.

Shairi: Kusanyeni mbele yake Watakatifu wote ambao kwa sadaka yao walisabitisha agano pamoja naye.

Walipokusanya maarifa yao yote na walipochukizwa kwa chuki, Wachungaji Watakatifu wakafukuza, kwa kombeo ya Roho Mtakatifu, mbwa-mwitu wakale na wenyi kushikwa na ugonjwa wa tauni ambao waliingiza katika ukamilifu wa Ekklezya ugonjwa kupona yenyi kuongoza kwa mauti; kwa hii, Wapadri Watakatifu walitenda kama watumishi watukufu wa Kristu wa waalimu wa utume takatifu.

Utukufu kwa Baba...*Sauti ya mnane.*

Wapadri watakatifu walipokuja toka mipaka ya dunia walitangaza asili moja na hali moja ya Baba, ya Mwana na ya Rohop Mtakaitfu na walitolea waziwazi Ekklezya fumbo ya mafundisho takatifu; ndio maana, tunapowatukuza kwa imani, tunawataja wenye heri na kuwaimbia: Enyi la ulinzi la Bwana, nyota za kuangaa za mbingu ya kiroho, minara ya sayuni ya siri, maua ya harufu, nzuri ya Paradizo, vinywa vyenye kupambwa vya Neno, ninyi mulio utukufu wa mji Nikea, nuru ya ulimwengu, muombeni Bwana kwa ajili ya roho zetu.

Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Mbarikiwa Ukupita, ewe Mzazi-Mungu Bikira; kwa kuwa naye aliye amepata mwili nawe, kuzimu imetekwa, Adamu amerejezwa, Laana imekufa, Eva amekombolewa, Mauti imewekwa kifoni, tena sisi tumeofikia uzima; kwa hiyo tukiimba na kupaza sauti umehimidiwa U Kristu Mungu wetu, liyependezwa hivi. Utukufu kwako.

### DOKSOLOGIA KUBWA.

## MU JUMA YA SABA YA WAPADRI WATAKATIFU KWA MANGARIBI

*Elezo: Kisha Bwana nimekuita tuinaimba wimbo tatu ya Wapadri Watakatifu toka Esperinos kubwa yao, mu posho mangaribi. Nikusema:*

Sauti ya sita. I apegnosmeni.

Baba alikuzaa tangu mwanzo wa nyakati bila mama hata kama Arius anakutukuza kama kiumbe, apana kama Mungu, akichanganya vibaya kiumbe na Muumba wake, na kwa hii anastahili moto ya milele, lakini Makutano ya Nikea inakutangaza kuwa Mwana wa Mungu, wewe Bwana mwenye kutawala pamoja na Baba na Roho Mtakatifu.

Ee Mwokozi, nani alipasua nguo yako? Na Arius mwenye kutenga na kugawanya utukufu na ufalme wa milele wa Utatu Mtakatifu; hakubali ya kama wewe ni Mumoja wa Utatu Mtakatifu, inamuwazisha Nestorius kukataa neno. «Mzazi-Mungu», lakini Makutano ya Nikea inakutangaza kuwa Mwana wa Mungu, wewe Bwana mwenye kutawala pamoja na Baba na Roho Mtakatifu.

Ameanguka katika zimu ya makafiri, huyu Arius ambaye kwa yeye nuru haiwezi kuonekana, na haki ya Mungu ilipasua tumbo lake, akafa vibaya kama Yudas kwa matendo na mawazo yake, lakini Makutano ya Nikea inakutangaza kuwa Mwana wa Mungu, wewe Bwana mwenye kutawala pamoja na Baba na Roho Mtakatifu.

***Tunaimba sasa tatu ya Mineon.***

Utukufu kwa Baba. *Sauti ya sita.*

Tutukuzeni leo Wapadri Wabebaji-Mungu, hawa waimbaji wa siri wa Roho Mtakatifu waliovumisha katika Eklezya umoja wa Mungu wakatangaza hali moja ya Utatu Mtakatifu; juu ya Arius wakashika imani ya kweli na wanamuomba daima Mungu kusudi ahurumie roho zetu.

Sasa na siku zote...sauti ya sita

Ee Kristu, mlimani takatifu tunapotazama utukufu wako, ee kianga ya utukufu wa Baba, tunaimbia nuru ya uso wako; tunaposujudia Mateso yako, tunatukuza Ufufuo wako takatifu na Kupanda kwako; utuhurumie.

## APOSTIKHA

*Elezo: Tunaimba Apostikha ya Wapadri Watakatifu toka Masifu ya Siku Kuu. Hivi:Sauti ya sita. Olin apothemeni.*

Walipokusanya maarifa yao yote ya kiroho kwa maongozi ya Roho Mtakatifu, Wapadri watakatifu wakandika Simvolo ya imani ambamo walitangaza waziwazi kabnisa ya kama Neno ni wa milele pamoja na Baba aliyemzaa na wa asili moja kweli kufwatana na mafundisho ya Mitume Watakatifu.*(mara mbili).*

Shairi: Utukufu kwako, ee Bwana, Mungu wa Baba zetu, sifa ni kwa jina lako, na utukufu milele.

Walipopokea nuru yote ya Roho Mtakatifu, Wapadri Watakatifu wakatangaza, kwa maombezi ya Mungu, fumbo ya imani iliyo fupi kwa maneno lakini tajiri kwa maana, na kama watangazaji wa Kristu wenye kuongozwa na mafundisho ya habari njema na ya mapokeo takatifu, walipokea juu mbinguni ufumbulio wa nuru, na walipoangazwa wote kwa nuru wakafasiria makanuni takatifu.

Shairi: Kusanyeni mbele yake Watakatifu wote ambao kwa sadaka yao walisabitisha agano pamoja naye.

Walipokusanya maarifa yao yote na walipochukizwa kwa chuki, Wachungaji Watakatifu wakafukuza, kwa kombeo ya Roho Mtakatifu, mbwa-mwitu wakale na wenyi kushikwa na ugonjwa wa tauni ambao waliingiza katika ukamilifu wa Ekklezya ugonjwa kupona yenyi kuongoza kwa mauti; kwa hii, Wapadri Watakatifu walitenda kama watumishi watukufu wa Kristu wa waalimu wa utume takatifu.

Utukufu kwa Baba...*Sauti ya tatu*

Enyi Wapadri Watakatifu, mulikuwa walinzi wa mafundisho ya Mitume; Waalimu wa imani ya kweli mulifundisha Utatu Mtakatifu wa asili moja, na mulikataa kufuru la Arius katika Makutano; mulimukataa pia Makedonius aliyekana Utatu Mtakatifu, mulimuhukumu Nestorius, Eftiki na Dioskori, Sabellius na Severi asiye na mkubwa, kwa maombezi yenu mutuokoe toka mafundisho ya uwongo na lindeni uzima yetu katika imani safi.

Sasa na siku zote...*Sauti ya sita.*

Mungu anapanda katika shangwe, Bwana, kwa sauti ya baragumu sababu ya kuinua sura iliyoanguka katika Adamu na toka mbingu mbinguni atatuma Roho Mfariji kusudi roho zetu zitakaswe.

**APOLITIKION** Ya Wapadri Watakatifu. *Sauti ya mnane.*

Utukuzwe, ee Kristu Mungu wetu, wewe uliyeweka duniani Wapadri wetu Watakatifu, kama taa na kwa ajili yao ulituongoza wote kwa imani ya kweli: Ee Mungu wa huruma Bwana, utukufu kwako.

Ya Kupanda Yesu Kristu Mbinguni. *Sauti ya ine.*

Unapanda katika utukufu, ee Kristu Mungu wetu, ukiwajaza wafwasi wako na furaha kwa ahadi ya Roho Mtakatifu, ukawapa nguvu na kuwabariki na mikono yako, kwani ndiwe Mwana wa Mungu, Mkombozi wa dunia.

# MU KAZI MOJA ASUBUI YA JUMA YA SABA

**KATHSIMA YA KWANZA.** *Sauti ya kwanza. Tu lithu sfragisthentos.*

Ee Mwokozi, Malaika waliposhangaa kupanda kwako na Wafwasi waliposangaza kwa kuchukuliwa kwako kwa ajabu, ulichukuliwa na utukufu kama Mungu, milango yalifunguliwa mbele yako; ndio maana majeshi ya mbinguni wakashangaa yakipaza sauti: Utukufu kwa mapendo yako, ee Mwokozi, utukufu kwa Ufalme wako, utukufu kwa kupanda kwako, ewe peke yako mpenda-wanadamu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*(mara ingine).*

**KATHISMA YA MBILI.** Sauti ya kwanza. Tu lithu sfragisthentos.

Ee chemchem ya uzima, uliponyanganya Hadeze na kwangazia ulimwengu, ulipanda na utukufu wewe mwenye kushika ulimwengu mkononi mwako; ndivyo maana tunakutukuza pamoja na Malaika, ee Bwana Mwenyezi. Utukufu kwa kupanda kwako, ee Kristu, utukufu kwa Ufalme wako, utukufu kwa rehema yako, peke yako mpenda-wanadamu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*(mara ingine).*

*Kisha tunaimba Kanuni, Kontakion, ikos, eksapostilarion na Masifu ya Siku Kuu na kisha:*

**APOSTIKHA** *Sauti ya mbili. Ikos tu efratha.*

Ninyi Waaminifu, pamoja na wafwasi wa Kristu, tupandeni mulima wa fazila ili tustahili kuona utukufu wa Bwana.

Shairi: Enyi mataifa yote, pigeni mikono shangilieni Mungu kwa furaha.

Roho za mbinguni zilinyamazisha uhalifu wa Wamanikea, wakawaonyesha ukweli wa kurudi kwa Kristu na mwili wake.

Shairi: Mungu anapanda katika shangwe, Bwana, kwa sauti ya baragumu.

Ee Daudi, imba na furaha kinubi kwani Kristu aliyepanda mbinguni kwa matendo anahakikisha unabii wako.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya mbili.*

Tangu mulima wa Mzeituni ulipanda katika utukufu mbele ya Wafwasi wako, ee Kristu Mungu wetu; unakaa kuume kwa Baba, wewe mwenyewe kujaza uliwemgu wote kwa umilele wa umungu wako, na uliwatumia Roho Mtakatifu kusudi roho zetu zipate katika yeye msaada, nuru na utakatifu.

# MU KAZI MOJA MANGARIBI YA JUMA YA SABA

*Kisha «Bwana nimekuita...» tunaimba wuimbo ya Siku Kuu tatu na tatu ya Mineon.*

***Wimbo ya Siku Kuu***.

*Sauti ya ine. Edokas simiosin.*

Kama mutu uliteswa, ee Mungu usiyeteseka, ulifufuka siku ya tatu mwenye kushinda mauti, ulifufua pamoja nawe wanadamu wote kaburini, ee Kristu, na ulipanda kwa Baba yako, ukaahidi Mitume wako Roho Mtakatifu, ee Bwana Mwenyezi na Mwokozi wa roho zetu.

Malaika waliyowatokea Wafwasi wakawauliza: Sababu gani munatazama mbinguni? Huyu muliona akipanda juu ya wingu la nuru atarudi sawasawa kuhukumu dunia kama alivyosema; kuendeni basi na fanyeni hii aliwaamuru ninyi.

Ee Bwana mwenyezi, kisha Ufufuo wako kaburini, ulichukua marafiki zako, ee Neno, ukawapeleka kule Bethania; na ukawabariki juu ya mlima wa Mzeituni mbele ya wewe kupanda mbinguni mwenye kuchukuliwa na malaika wa Mungu, ee Bwana Mwenyezi na Mwokozi wa Roho zetu.

***Wimbo tatu ya Mineon.***

Utukufu kwa Baba... Sasa na siku zote...*Sauti ya ine.*

Ee Bwana, wakati ulipofika juu ya milima wa Mzeituni kwa kutimiza nia ya wema ya Baba yako, malaika mbinguni walishangaa, na duniani mashetani walitetemeka; Mitume walijazwa na woga na furaha wakati ulizungumuza nao katikati yao; wingu liliongojea mbele yako kama kiti chenye kutayarishwa mbingu ilifungua milango yake ikiangaa na uzuri, incghi ilitambua mashimo yake sababu ya kuonyesha kuanguka kwa Adamu na kupanda kwake mpaka kwako; wakati nguvu isiyoonekana ilikunyanyua toka inchi ukasema maneno ya baraka kwa sauti kubwa sababu ya kusikilika; wingu likakuchukua na mbingu ikafungulika kwa kukupokea. Ee Bwana, hii ni tendo kubwa na la ajabu ulilotenda kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

**APOSTIKHA.** *Sauti ya mbili. Ikos tu efratha*

Ulipotimiza kwa kutaka kwako mapenzi ya Baba yako kisha kuunganisha inchi na mbingu, ulipanda kwa utukufu huko ulikuwa zamani.

Shairi: Enyi mataifa yote, pigeni mikono shangilieni Mungu kwa furaha.

Ulipanda kwa Baba yako bila kumuacha, ee Mungu wa mapendo, na uliinua, ee Bwana, mateso yetu ya hapa chini.

Shairi: Mungu anapanda katika shangwe, Bwana, kwa sauti ya baragumu.

Ee Bwana, wingu la nuru lilikuchukua mbinguni, na kwa mwito wako Malaika walikutumikia na woga wakitetemeka.

Utukufu kwa Baba... Sasa na siku zote...*Sauti ya ine.*

Ee Bwana, ubinadamu iliyoanguka katika Adamu mpaka chini kabisa ya udongo, uliitengeneza kuwa mpya katika wewe mwenyewe: Leo unaipandishja juu ya majeshi na ya matawala wa mbinguni; ulipopenda, unaipa kukaa pamoja nawe, kwa huruma uliiungamisha kwa hali yako, kwa hii ushirika,

unateswa pamoja nayo; kwa mateso yako, ee Mungu mvumilivu, uliitukuza; lakini majeshi ya Wabila-mwili wakaulizana: Huyu ni mutu gani mwenye kuvaa utukufu? Hayuko paka mutu, yeye ni Mutu-Mungu, kwani eko na hali zote mbili; na malaika wenye kuvaa mavazi ya kuangaa wakawazunguka pambeni wakawaambia: Enyi watu wa Galilea, huyu Yesu Mutu-Mungu aliyeondoka kwenu, kwa umungu-umutu wake atarudi tena kuhukumu wazima na wafu, kwa wenye kuamini atawapa maondoleo ya zam,bi na neema kubwa.

# MU KAZI MBILI ASUBUI YA JUMA YA SABA

**KATHISMA YA KWANZA** *Sauti ya mbili. Ta ano ziton*

Ee Kristu, uliposhuka duniani toka mbinguni, ulipanda mbinguni toka duniani kwa baba yako alikuzaa, na Wafwasi walikuona ukipanda, ewe Mungu Mwokozi; kwa hii Siku Kuu, pamoja nao tunaimbia Kupanda Kwako.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*(mara mbili).*

**KATHISMA YA MBILI.** *Sauti ya tatu. Tin oreotita.*

Mungu wa mbele ya milele alipogeuza kwa siri ubinadamu aliyochukua, leo amechukuliwa mbinguni, Malaika wanamutangulia na wanawaonyesha Wafwasi Bwana akichukuliwa na utukufu kubwa mpaka mbinguni, na wanaposujudu, wanasema: Utukufu kwa Mungu mwenye kupanda mbinguni.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*(mara mbili).*

*Kisha Zaburi 51, Kanuni ya Siku Kuu, ya Mineon. Kontakion, Eksapostilarion ya Siku Kuu.*

**APOSTIKHA.** *Sauti ya mbili. Ikos tu efratha***.**

Bwana aliwaambia marafiki zake: Sitawacha mayatima ninyi nilikusanya na kuchagua, lakini nitawatumia ninyi Roho Mtakatifu.

Shairi: Enyi mataifa yote, pigeni mikono shangilieni Mungu kwa furaha.

Malaika waliwaambia Mitume Watakatifu: Ninyi watu wa Galilaya, kama mulivyomuona akienda, Bwana atarudi vivyo hivyo.

Shairi: Mungu anapanda katika shangwe, Bwana, kwa sauti ya baragumu.

Ee Bwana, waliposhuka kwa furaha mlima wa Mzeituni, Wafwasi wako walitukuza na kuimbia Kupanda kwako takatifu.

Utukufu kwa Baba... Sasa na siku zote...*Sauti ya ine.*

Ee Kristu Mungu wetu, wakati ulinyanyuliwa katika utukufu, machobni mwa Wafwasi wako wawingu yakakuchukuwa na mwili wako? Milango yakafunguliwa mbinguni, Malaika wakafurahiwa, majeshi ya mbinguni-juu ya kapaza sauti ya kisema: Enyi milango, inueni kuta zenu ili Mfalme wa utukufu aingie; Wafwasi walioshikwa na woga wakasema: Usituache, ee Mchungaji mwema, lakini ututumie sisi Roho wako Mtakatifu kamili awe mwongozi na msaada wa roho zetu.

# MU KAZI MBILI MANGARIBI YA JUMA YA SABA

*Kisha: «Bwana nimekuita...» tunaimba wimbo tatu ya Siku Kuu na tatu ya Mineon.*

***Wimbo ya Siku Kuu.***

*Sauti ya ine. Os geneon en martisin.*

Mitume wako Watakatifu walikuona unapanda mbinguni na kukaa kuume kwa Baba aliyekuzaa ambaye haukuache, ee Mwana wa Mungu; na kwa ahadi yako uliwatumia Wahubiri hawa Mfariji ambaye alifanya dunia kuwa mbingu.

EeYesu, kwa wema wako ulijifanya mutu, ewe msiyekufa, uliteshwa na kufa Msalabani kwa kutaka kwako, lakini ulifufuka katika wafu siku ya tatu, na siku ya makumi ine ulipanda mbinguni huko ulishuka, kisha kuwapa wanadamu amani sababu yakuwaleta kwa Baba yako wa milele.

Ee Bwana, wakati Mitume wako walikuona umechukuliwa juu yawingu, wakalia na kujaa na sikitiko, kwa kulia kwao wakapaza sauti: Usituache mayatima wewe uliyetuonyesha mapendo mengi, lakini kwa ahadi yako ututumie sisi Roho wako Mtaaktifu kamili angazie roho zetu.

***Wimbo tatu ya Mineon***

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya tano.*

Kujeni, enyi Waaminifu wote, tulipofundishwa na Wafwasi wa Kristu tuimbe wimbo wa milele juu ya mlima wa Mzeituni kama Mitume Watakatifu; tupazeni sauti pamoja na Nabii Daudi: «Mungu anapanda kwa utukufu, Bwana, kwa sauti ya baragumu sababu ya kuokoa wanadamu toka mitego ya Adui» na kutuma nuru yake juu ya roho zetu.

**APOSTIKHA** *Sauti ya mbili. Ikos tu efratha.*

Hii ni mambo ya ajabu, mwili ya wanadamu inapanda mbinguni, inaungana na Neno la Mungu, Yeye Bwana mwenyezi.

Shairi: Enyi mataifa yote, pigeni mikono shangilieni Mungu kwa furaha.

Siku ya nuru ya kupanda kwa Bwana mbinguni inangaa na mwanga wake wote, inangaza dunia yote.

Shairi: Mungu anapanda katika shangwe, Bwana, kwa sauti ya baragumu.

Ee Kristu Mwokozi, kama ulivyowatumia toka mbinguni Wafwasi Roho Mtakatifu wa asili moja, tumia pia watu neema na nuru yako.

Utukufu kwa Baba... Sasa na siku zote...*Sauti ya tano.*

Ee Bwana, wakati ulichukulia mbinguni huko haukwacha, Malaika wakapaza sauti na furaha mumoja kwa mwingine: Ninyi Milango, inueni kuta zenu ili Mfalme wa utukufu aingie! Kwani kiti cha Wakheruvi ilikupokea na mwili wako, ee Bwana, matumaini yetu, utukufu kwako.

*Kisha tunaimba Apolitikion ya Siku Kuu na Kuaga.*

## MU KAZI TATU ASUBUI YA JUMA YA SABA

**KATHISMA YA KWANZA.** *Sauti ya ine. Epefanis simeron.*

Ee Bwana, walipokuona umepanda mbinguni, Mitume walipaza sauti wakisema: Unarudi kwa Baba yako, ee Mpenda-wanadamu na Muumba, bila kuwacha Wafwasi wako mayatima.

Utukufu kwa Baba... Sasa na siku zote..*(mara mbili).*

**KATHISMA YA MBILI.** *Umoja*

Majeshi tukufu ya Malaika wa Mungu walipoona Bwana wa utukufu amechukuliwa waziwazi na mwili wake, wakasemezana moja kwa mwingine: Ninyi milango, imeni kuta zenu.

Utukufu kwa Baba... Sasa na siku zote..*(mara mbili).*

*Kisha Zaburi 51, Kanuni ya Siku Kuu, ya Mineon. Kontakion, Eksapostilarion ya Siku Kuu.*

**APOSTIKHA** *Sauti ya sita. Triimeros anestis Hriste.*

Ee Kristu, kwa mapendo yako kubwa ulizaliwa mwilini kwa Bikira; uliteswa Msalabani kwa kutaka kwako, ulifufuka kaburini siku ya tatu, ee Mungu Mwema sababu ya kutupatia uzima na kutufufua.

Shairi: Enyi mataifa yote, pigeni mikono shangilieni Mungu kwa furaha.

Ee Kristu Mungu wetu, Mitume Watakatifu walikuona umechukuliwa toka duniani kwenda mbinguni, na ukawahidi, ee Chemchem ya uzima, kuwatumia Roho Mtakatifu toka Baba.

Shairi: Mungu anapanda katika shangwe, Bwana, kwa sauti ya baragumu.

Ee Bwana Yesu na Mfalme ulimwengu, Malaika wengi walishangaa kwa Kupanda kwako kwa sababu, na waliposhikwa kwa woga, majeshi, wakaambiana moja kwa mwingine: «Inueni milango ya mbingu.

Utukufu kwa Baba...sasa na siku zote...*Sauti ya Sita.*

Ee Yesu mupole kabisa, bila kuacha kifua cha Baba, duniani ulikua na ubinadamu wetu, unapanda leo mbinguni na utukufu tangu mulima wa Mzeituni, ukiinua kwa huruma yako hali yetu yenye kuanguka, sababu ya kuiweka karibu ya Baba pamoja na wewe; majeshi ya Wabila-mwili mbinguni wanaposhangaa na kuogopa, wanatukuza mapendo unapenda nayo wanadamu; na sisi duniani, pamoja nao tunatukuza mapendo yako kwa sisi na Kupanda kwako mbinguni tukisema: Ee Bwana uliyezaza na furaha kubwa siku ya Kupanda Kwako Wafuasi wako na Mzazi-Mungu aliyekuzaa, utupe na sisi pia, kwa maombezi yao, furaha ya mateule wako na neema ya wokovu.

## MU KAZI TATU MANGARIBI YA JUMA YA SABA

*Kisha: «Bwana nimekuita...» tunaimba wimbo tatu ya Siku Kuu na tatu ya Mineon.*

***Wimbo ya Siku Kuu.***

*Sauti ya ine. O eks ipristu klithis.*

Ee Kristu, ulipotimiza wokovu kwa ajili ya wote, ukapanda huu yamlima wa Mzeituni na kuloe ukapanda machoni mwa Mitume wako Watakatifu ukachukuliwa na utukufu mbinguni; waliposhangaa sababu ya hii fumbo majeshi ya juu-mbinguni wakapaza sauti moja kwa mwingine: Inueni milango kwa ajili yaMungu wetu mwenye kutawala ulimwengu wote kusudi ainjie mbinguni huko alitoka, kisha kutimiza wokovu wa dunia kwa kutaka kwake kwa namna ya ajabu.

Wafwasi walipokuona umepanda mbinguni wakakuuliza: «Ee Bwana, unaenda wapi unacha Watumishi wako? Unaenda wapi? Wewe mwenye kushika ulimwengu mkononi mwako? Sisi tuliacha vyote kwa ajili yako, tulikufwata na furaha kwa matumaini yakuwa daima pamoja na wewe; kwa ahadi yako, ee Baba Mwema kamili, usituache mayatima, lakini ututumie Roho Mtakatifu, ee Mwokozi wa roho zetu.

Ee Bwana, ulipowabariki marayako ya mwisho, ukawafunulia marafiki zako fumbo ya siri ukawambia: Ninyi marafiki, tazameni naenda kwa Baba, nitawatumia Mfariji mwingine, kwani siache kondoo nilikusanya, sasahau Wafwasi nilipenda; na wakati mutavaa nguvu yajuu mbinguni, kwendeni duniani kuwatangazia mataifa yote habari njema ya wokovu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya sita.*

Mungu anapanda katika shangwe, Bwana, kwa s auti ya baragumu sababu ya kuinua sura iliyoanguka katika Adamu na toka mbingu mbinguni atatuma Roho Mfariji kusudi roho zetu zitakaswe.

**APOSTIKHA.** *Sauti ya sita. E Agelike.*

Ulikuja duniani sababu ya kuinua mtumishi wako aliyeanguka katika Paradizo; ulipotwaa mwili wangu, ulinishukua pamoja nawe na kutukuzwa mpaka kunikalisha pamoja na Baba mbinguni, kisha kuharibu majivuno ya adui aliyeniangusa zamani duniani, naimbia, ee Bwana, mapendo yako mengi kwa ajili ya wanadamu.

Shairi: Enyi mataifa yote, pigeni mikono shangilieni Mungu kwa furaha.

Furahiwa Adamu, furahiwa Eva, ngozi mulivaa zamani katika Paradizo kwa mutumaini yauzima wa milele Muumba wetu aliivaa kwa namna ya ajabu na aliigeuza kuwa mwili wa milele ambao lao anainua kwa utukufu kuuma kwa Baba mbinguni.

Shairi: Mungu anapanda katika shangwe, Bwana, kwa sauti ya baragumu.

Kwa nguvu yake ya umungu alipoangushashetani huyu mzulumu muasi, huyu aliyetwaa hali yangu bila kugawanyika, bila kugeuka wa mchanganyiko, pamoja na hii alipanda kwa haraka kwa Baba mbinguni; sasa imalizike makelele ya wahalifu makafiri! Ssisi waaminifu tunamutukuza na imani.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya sita.*

Leo Majeshi ya juu wanapoona hali yetu mbinguni, wanashangaa kwa kupanda kwa ajabu na wanaulizana moja kwa mwingine wakisema: Huyu ni nani anakuja? Lakini wanapomutambua Bwana wao, wanaamuru milango ya mbinguni yafuanguliwe? Pamoja nao tunakuimbia daima wewe utakayerudi toka mbinguni na mwili wako kama Mwamzi wa ulimwengu tena Mungu mwenyezi.

# MU KAZI INE ASUBUI YA JUMA YA SABA

**KATHISMA YA KWANZA** *Sauti ya tano. Ton Sinanarkhon Logon.*

Ee Kristu, uliposhuka toka mbinguni mpaka duniani, sababu ya kuinua kwa umungu ukoo wa Adamu mwenye kulala chini ya kifungo cha Hadeze, kwa kupanda kwako ulipomupandisha mbinguni, pamoja nawe amekaa katika kiti cha ufalme cha Baba, kwa huruma na mapendo yako kwa wanadamu.

Utukufu kwa Baba... Sasa na siku zote..*(mara mbili).*

**KATHISMA YA MBILI.** *Sauti ya mnane. To prostakthen mistikos.*

Ee Mwokozi mwenye huruma, ulipopanda juu ya mlima wa Mzeituni, ukachukuliwa mbinguni; maana wingu la nuru likakuondoa duniani machoni mwa Wafwasi wako wenye kushangaa wakati mbinguni Malaika wakapaza sauti wakisema: Enyi Milango, kwa woga inueni kuta zenu! Pamoja na majeshi ya juu-mbinguni viumbe vyote vinakuimbia, ee Mfalme wa ulimwengu yote.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*(mara mbili).*

*Kisha Zaburi 51, Kanuni ya Siku Kuu, ya Mineon. Kontakion, Eksapostilarion ya Siku Kuu.*

**APOSTIKHA** *Sauti ya sita. E Agelike.*

Ee Kristu, ulipochukua ubinadamu wangu, uliiunganisha kwa hali yako ya umungu kwa namna ya ajabu, bila mchanganyo, bila kugeuka ao kugawanyika. Utukufu kwa mapendo yako ya ajabu, utukufu kwa mateso yako na Ufufuo wako, utukufu kwa Kupanda kwako, kwa ajili ya hii hali yetu ya dunia imechukuliwa mbinguni.

Shairi: Enyi mataifa yote, pigeni mikono shangilieni Mungu kwa furaha.

Ee Mwokozi, malaika wako waliwaambia Wafwasi: «sababu gani kumuona? Huyu aliyepanda kwa utukufu na mwili wake atarudi vivyo hivyo sababu ya kuhukumu yote ile yenyi uzima kwa hukumu ya kweli, kwani Yeye ni Mungu tena mutu.

Shairi: Mungu anapanda katika shangwe, Bwana, kwa sauti ya baragumu.

Ee Mwokozi, Wafwasi wako walipoona mlimani Kupanda kwako, wakalia na kufurahiwa, wakakulalamikia, ee Bwana: Usituache mayatima, lakini tuma Roho wako Mtakatifu angazie roho za watumishi wako.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya mnane.*

Ulipanda kwa utukufu toka dunia mpaka mbinguni, wewe ambaye umungu inajaa ulimwengu; unakaa kuuma kwa Baba wewe Neno uliyekuwa tangu mwanzo karibu ya Baba; walipoona hivi, malaika mbinguni wakashikwa kwa woga na wakawaambia Mitume: «Sababu gani munasimama mukitazama mbinguni? Huyu muliyeona akipanda atarudi na utukufu duniani kuhukumu wanadamu na kumulipa kila mumoja kadiri ya matendo yake «Tumwambieni: Wewe ambaye dunia haiwezi kuzunguka, ee Bwana mwenyezi, utukufu kwako.

*Mu kazi inne Mangaribi na kesho Mu kazi tano asubui tunafanya Sindikizo ya Siku Kuu ya Kupanda Yesu Kristu mbinguni. Hatusome Masomo ya Manabii, wimbo ya Litia na Polieleo.*

# MU KAZI INE MANGARIBI YA JUMA YA SABA NA MU KAZI TANO ASUBUI

**Elezo**: *Tunafanya Sindikizo ya Siku Kuu ya Kupanda Yesu Kristu mbinguni. Tunatosha paka ma Somo ya Manabii, Litia, Polieleo na Antifona ya ma Ibada yote*

# MU KAZI TANO MANGARIBI YA JUMA YA SABA

*Tunafanya makumbusho ya wafu wote wenye walipumuzika katika imani ya Kanisa Orthodokse na kitumaini ya ufufuo wao mu uzima ya milele.*

*Kisha* Bwana nimekuita...» *tunaimba wimbo tatu ya Paraklitiki na kisha wimbo tatu ya wafu.*

***Wimbo ya Paraklitiki*.**

*Sauti ya sita.*

Ee Bwana mashahidi wako hawakukukana, hawakujitenga ku mafundishoyako. kwa maombezi yao utuhurumie.

Ee Kristu, Mashahidi wako waliteswa mateso mengi, mwisho wakapokea utukufu mbinguni ili waombee roho zetu.

Mashahidi watukudu wakaaji wa inchi yambinguni, waliposhindana duniani wakateswa mateso mengi; kwa maombezi yao na kwa maombi yao, ee Bwana, utulinde.

***Wimbo ya wafu***

*Sauti wa mnane. O en Edem paradisos.*

Enyi waaminifu, leo tuwakumbukeni marehemu waaminifu wote waliolala na heri tangu milele; tumuimbie Bwana na Mwokozi wetu na kumuomba sana kusudi kwa wakati wa hukumu awahukumu na haki kwa baraza ya Mungu wetu atakayeketi kuhukumu dunia yote na wapate kusimama na furaha kuume kwake pamoja na wenye haki na Watakatifu kwa kuriti nuru na amani, na wawe wenye kustahili ufalme wake mbinguni.

Ee Mungu Mwokozi, kwa damu yako unakomboa wanadamu, kwa lufu yako unatuokoa toka uchungu wa mauti, kwa Ufufuo wako unatupatia uzima wa milele; ee Bwana, leta mapumziko kwa waaminifu wote waliolala na imani katika miji ao jangwa, inchini, baharini wala popote, wafalme ao

mapadri, maaskofu, watawa wa waaminifu, wa umri yote na wa daraja yote, uwastahilishe katika ufalme wako wa mbinguni.

Ee Kristu, kwa Ufufuo wako katika wafu, mauti haina na uwezo juu ya marehemu waaminifu; ndio maana tunakuomba sana uwape watumishi wako mapumziko katika uwanja wa Mungu na katika kifua cha Abraamu, kwa watumishi wako wote, tangu Adamu mpaka leo, waliokutumikia kwa kukuabudu na moyo safi, baba zetu na ndugu zetu, wazazi wetu, marafiki zetu, mutu wowote aliyetimiza na imani mapashwa yako; wote wale unaita kwako kwa namna mbalimbali: ee Bwana, uwastahilishe katika ufalme wako wa mbinguni.

Utukufu kwa Baba...*Sauti wa mnane.*

Ninalia na nalalamika wakati ninawaza mauti, wakati ninaona imelala kaburini bila hali, bila utukufu na bila uzuri, neema tuliyopewa kwa mfano wa Mungu: Ni fumbo ya ajabu kuliko bahari yetu! Namna gani unashuka kaburini? Namna gani tunafungwa kwa mauti? Kama ilivyo Maandiko, ni kwa amri ya Mungu anayewapa wafu mapumziko.

Sasa na siku zote...**THEOTOKION**. Sauti ya sita

Nani hatakuita wewe Mwenye heri, Bikira Mtakatifu kamili? Nani hataimba kuzaliwa kwa Mwana wako bila mume? Kwani Mwana wa pekee aliyeangaa mbele ya wakati kwa Baba, yeye vilevile alitokea kwa wewe uliyesafi, akitwaa mwili usiyosemwa; yeye ni Mungu sawasawa na hali yake, na akajifanya mtu kwa kadiri ya hali ya watu kwa ajili yetu; yeye hagawanyike kwa uso mbili, lakini anajulikana kwetu katika hali mbili bila muchanganyo. Umusihi, ee Bikira mutaratibu na heriu daima, kwa murehemu nafsi yetu.

*Kisha*: Mwangaza upole...

*Pahali pa fasi ya Prokimenon tunaimba na sauti ya tatu:*

Alliluia *(mara tatu).*

Shairi: Heri mutu wewe unayemuchagua na kumukaribisha ajaw viwanjani mwako.

Alliluia *(mara tatu).*

Shairi: Ukumbusho wako vizazi hata vizazi, ee Bwana.

Alliluia *(mara tatu).*

Kisha: Ee Bwana, utujalia mangaribi hii kutulinda na zambi...

## APOSTIKHA. *Wimbo ya Mashahidi. Sauti ya sita.*

Ee Bwana, kwa mashahidi Msalaba wako umekuwa utukufu usiyoweza kushindwa; walipoona mauti iliyowaongojea na walipotangulia kuona uzima gani unawaongojea, wakapata nguvu ku matumaini waliyokutumainia kwa maombezi yao, utukurumie.

Shairi: Roho zao zipumzike katika heri.

Ee Mwokozi, ulitengeneza kazi ya mikono yako kwa mfano wako, uligeuza umungu wako kuwa mwili ambako mimi nilisharikia, ee Neno, kwa uwezo wako kubwa ukaniweka duniani kama mfalme wa viumbe; ndio maana, ee Mungu Mwokozi, pumzisha watumishi wako katika makao ya wenye haki, katika inchi ya wazima.

Shairi:Heri wale ulichagua, wale ulichukua pamoja nawe, ee Bwana.

Kwa kutenganisha ukubwa wangu na viumbe vingine, uliweka, kwa ajili yangu, katika Deni shamba lenyi kupambwa na namna yote yamimea, hamuna sikitiko ao mateso, na duniani ulinisharikisha kwa uzima wa malaika na wa Mungu; ndio maana, ee Mungu Mwokozi, pumzisha watumishi wako katika makao ya inchi ya wazima.

Utukufu kwa Baba...*Sauti ya sita.*

Kwa neno lako la uumbaji uliniruhusu nizaliwe na niishi; kwa kunifanya mimi kuwa mutu mzima uliunganisha ndani yangu yenyi kuonekana na isiyoonekana; kwa udongo uliumba mwili wangu,

ulinipa roho kwa pumzi yako ya umungu na yenyi kuleta uzima; ee Mungu Mwokozi, uwape pia watumishi wako mapumziko katika makao ya wenye haki inchini mwa wazima.

Sasa na siku...**THEOTOKION**.

Ee Kristu, kwa maombezi ya huyu aliyekuzaa, ya Manabii, ya Mitume, ya Mashahidi, ya Maaskofu, ya wenye haki, ya wenye heri, na ya watakatifu wote, uwape marehemu watumishi wako mapumziko ya milele.

**Apolitikion.** *Sauti ya mnane.*

Ee zimu ya hekima yenyi kupenda wanadamu na kuongoza vitu vyote kwa ajili ya wokovu, peke yako Muumba ambaye kila mumoja anapokea ile yenye kumufaa, ee Bwana, leta mapumziko kwa roho za watumishi wako, kwa sababu matumaini yao ni kwako, ewe Fundi wetu, Muumba wetu tena Mungu wetu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...**THEOTOKION**.

Wewe ni boma na bandari yetu ya wokovu, muombezi wa kweli kwa Mungu uliyezaa, ee Bikira Mzazi-Mungu, ndiwe wokovu wa wakristu.

**KUAGA.**

*Kisha padri anafanya Ibada ya Wafu ao Panikhida. Tafuta mu kitabu Saa ukubwa.*

## MU POSHO ASUBUI YA JUMA YA SABA

*Kisha somo ya Eksapsalmos tunaimba mu sauti ya mnane*

Alliluia *(mara tatu).*

Shairi: Heri mutu wewe unayemuchagua na kumukaribisha ajabu viwanjani mwako.

*Alliluia (mara tatu).*

Shairi: Ukumbusho wako vizazi hata vizazi, ee Bwana.

*Alliluia (mara tatu).*

Apolitikion: Ee zimu ya hekima yenyi kupenda ...

Utukufu...Sasa... Wewe ni boma… *(ona yulu).*

**KATHISMA YA KWANZA.** *Sauti ya sita. Angelike dinamis.*

Kama Washindani katika uwanja, ndivyo walivyopigana wazulumu juu ya Mashahidi; makundi yamalaika waliwatayarishia taji la Washindaji; hekima yao iliwasangaza wazulumu na wafalme; walimushinda shetani walipomuungana Kristu. Wewe uliyewapa nguvu, ee Bwana, utukufu kwako.

Shairi: Mungu ni wa ajabu katika Watakatifu wake.

Watakatifu walishindana mashindano bora, wakapokea kwako tuzo la washindaji; na walipozarau hukumu ya makafiri, wakapokea sifa yamilele; kwa maombezi yao, ee Mungu wetu, utupe neema ya wokovu.

Shairi: Watakatifu walio duniani, wao ni wale wazuri sana ninaopendezwa nao.

Ee Bwana, makumbusho ya Mashahidi wako inatukumbusha Paradizo na shamba la Edeni; katika hii viumbe vyote vinafurahiwa, na kwa maombezi yao, ee Bwana, utupe amani na neema ya wokovu.

Utukufu kwa Baba. *Wimbo ya wafu. Sauti ya sita.*

Kweli ni ya bure! Uzima unapita kama ndoto, kama kivuli, wafu wanaogopa bure, kama yanavyosema Maandiko; wakati tutakapoondoka ulimwenguni, tutakaa lakini kaburini, maskini kama watajiri. Na tena ee Kristu Mungu wetu, kwa mapendo yako kwa wanadamu, uwape marehemu watumishi wako mapumziko.

Sasa na siku zote...**THEOTOKION**.

Wewe uliyemuita Mama yako Mwenyi heri na uliyeteswa kwa kutaka kwako, nuru yako iliangaa Msalabani, kwani ulitaka kwenda kumtafuta Adamu; ukawaambia Malaika: Furahini pamoja

nami, kwani imepatikana drakma iliyopotea. Wewe uliyefanya yote kwa hekima, utukufu kwako, ee Bwana Mungu wetu.

**MAHIMIDI YA WAFU.**

Ee Bwana, umehimidiwa U, unifundishe zilizo haki zako.

Kundi la Watakatifu, lilipata chemchem ya uzima na mulango wa Paradizo, na mimi nitapata njia kwa kutubu, mimi ni kondoo mupotevu, uniite tena, ee Mwokozi, na uniokoe.

Ee Bwana, umehimidiwa U. . .

We wa zamani, uliniumba toka si kitu, na ulinisifu kwa sura yako takatifu, lakini juu ya kuvunja amri, ulinirudisha tena ku udongo kule ulinitosha, kwa mufano wako sasa unirudishe, na ufanye mara ingine uzuri wangu wa kwanza.

Ee Bwana, umehimidiwa U. . .

Mimi ni sura, ya utukufu wako usiyonewa, hata niko na alama ya zambi, ee Rabi unirehemu kiumbe chako, na unisafishe kwa wema wako, tena unipatie inchi ninayotamania, unifanye mara ingine mwana inchi wa Paradizo.

Ee Bwana umehimidiwa U. . .

Ee Mungu, pumzisha mtumishi (wa) wako, na u(uwa)mupangishe katika Paradizo, fasi ya kundi la watakatifu, ee Bwana, na wenyi haki watangaa sawa nyota za mwangaza, u(uwa)mupumzishe mu(wa)tumishi wako huyu (hawa) anayelala(wanao), umusamehe (uwa) zambi zake (zao) zote.

Utukufu kwa Baba na kwa Bwana na kwa Roho Mtakatifu

Tuimbe na kupaza sauti, kwa uaminifu mianga tatu ya umungu moja, ewe Mtakatifu, Baba wasiyo mwanzo, Mwana aliye na Baba bila mwanzo na Roho Mtakatifu,; angaza sisi tuliokuabudu kwa imani, na utuopoe ku moto ya milele.

Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Salamu Muheshimiwa, uliyemzaa Mungu mwilini, juu ya wokovu wa wote, kwa ajili yako kabila la wanadamu ilipara wokovu, katika yako tutapata Paradizo, Mzazi-Mungu, safi mbarikiwa.

Alliluia, Alliluia, Alliluia, utukufu kwako, ee Mungu. *(Mara tatu).*

## Maombi ya wafu.

Shemasi*:* Utuhurumie, ee Mungu, mu huruma yako kubwa, tunakuomba sikiliza na hurumia.

Mwimbaji*:* Bwana hurumia *(mara tatu).*

Shemasi*:* Tena tunakuomba kwa ajili mapumziko ya roho za marehemu watumishi wa Mungu ili makosa yao ya kujua na yasiyokujua yasamehewe.

Mwimbaji*:* Bwana hurumia *(mara tatu).*

Shemasi*:* Ili Bwana Mungu aweke roho zao kule wamepumzika wenye haki.

Mwimbaji*:* Bwana hurumia *(mara tatu).*

Shemasi*:* Tumuombe Kristu Mungu wetu na Mfalme wetu wa milele awape rehema yake, maondoleo ya makosa ya ufalme wa mbinguni.

Waimbaji*:* Uwape, ee Bwana.

Shemasi*:* Tumuombe Bwana.

Waimbaji*:* Bwana hurumia.

Padri*:* Ee Mungu wa roho na wa mwili, uliyeshinda lufu na kumuharibu shetani, wewe uliyeleta uzima duniani, leta, ee Bwana, mapumuziko kwa roho ya m(wa)tumishi wako (jina lake), pahali pa mwangaza, pa majani mazuri, pa mapumziko, kule kunakimbia maumivu, sikitiko na masumbuko. Umusamehe zambi zake(zao) zote a(wa)litenda kwa sauti, kwa matendo na kwa mawazo, kwa sababu wewe ni Mungu mwema na mpenda-wanadamu, kwani hakuna mutu hata moja, anakaa mu uzima huu pasipo kufanya zambi, kwa sababu wewe peke yako msiye zambi, haki yako, ni haki ya milele, na amri yako ni ya kweli.

Kwa kuwa wewe ni ufufuo, uzima na mapumziko ya mu(wa)tumishi wako (jina lake) huyu (hawa) a(wa)melala, Kristu Mungu wetu, na kwako tunatoa utukufu pamoja na Baba wako wasipo

mwanzo na Roho Mtakatifu wako kamili. Mwema, Mpaaji wa uzima, sasa na siku zote, hata milele na milele.

Waimbaji*:* Amina.

**KATHISMA WA MBILI.**

*Sauti ya tano.*

Ee Mungu Mwokozi, kwa wema wako na kwa mapendo yako kwa wanadamu, pamoja na wenye haki pumzisha watumishi wako na uwaruhusu wakae katika uwanja wako, usihesabie makosa yao ya kujua na yasipokujua, ya kutaka na yasipo kutaka.

Utukufu. . . Sasa. . . **THEOTOKION**.

Ee Kristu Mungu wetu uliyezaliwa kwa Bikira sababu ya kuangazia ulimwengu, kwa maombezi yake utufanye sisi kuwa wana wa nuru, ee Bwana, utuhurumie.

## KANUNI YA WAFU.

### WIMBO YA KWANZA

**IRMOS:** Wakati Waisraeli waliposafiri kilindini kama pa inchi kavu, na walipoomuona Farao mzalimu ameangamizwa katika mawimbi, hapo wakapaza sauti: Tuimbeni wimbo wa ushindi kwa utukufu wa Mungu wetu.

Ee Rabi na Muumba, mwamzi na Bwana wa roho yangu yote, wewe mwenye kushika mkononi mipaka ya dunia yote, pumzisha waaminifu marehemu wote ndani yako.

Kwa ajili ya wanadamu waliyokufa wa kila umri, wa kila hali, wa kila daraja, wa kila cheo, tunakuomba sana kuleta wokovu kwa wale uliita kwako.

Ee Neno, wewe peke yako uliniumba kwa mkono wako takatifu, uliniumba kwa udongo, ukanipa roho kwa pumzi yako yenyi kuleta uzima : Wewe mwenyewe, ee Mungu mwenye huruma, okoa roho ulichukua pamoja nawe.

Ee Bikira Mtakatifu kamili, wewe kimbilio ya ulimwengu, ulinzi imara,maombezi yako yafanyike kwa ajili ya wote wale ambao katika hatari wal

### WIMBO YA TATU

**IRMOS:** Hakuna hata mmoja aliye Mtakatifu kama Wewe Bwana Mungu wangu; ulitukuza nguuuuvu ya Waaminifu katika wema wako, na ulitutia msingi pa mwamba imara wa maungamo ya jina Lako.

Wewe ambaye kwa sababu ya ufalme wako takatifu, toka mipaka ya dunia ulileta kwako kama juu ya mawingu roho za marehemu waaminifu, ee Kristu, pumzisha watumishi wako ulichukua pahali pote.

Ee Mwokozi, wewe peke yako uliweka watawala na wafalme, waamzi na mahakimu; ndio maana kama mungu wa wanadamu wote, wewe mwenyewe, kwa hukumu yako uwaokoe toka azabu.

EeMuumba wa ulimwengu, kwa wale ulichukua pamoja nawe, mabikira na wazee, wakubwa na vijana, uwape furaha ya milele, ee Kristu na raha kubwa ya paradizo.

Matumaini ya ulimwengu, ee Bikira Mzazi-Mungu, usiache wale wenye kukukimbilia wewe daima, lakini kwa maombezi yako ya heshima okoa toka hatari
wenye wanakusifu.

**KATHISMA** *Sauti ya mnane. Tin sofian ke Logon.*

Ee Bwana, wewe ambaye kwa uliumba ulimwengu, kwa wema wako pumzisha wakristu wote walikufa katika imani, babazetu, mababu zetu na wakambo yetu, nfugu zetu na marafiki zetu wote, watajiri na maskini, watawa, watawala ao wafalme, kule wanakaa wenye haki na Watakatifu wengi; ee Kristu Mungu wetu na Mfalme wetu, samehe zambi za Watumishi wako wote.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...**THEOTOKION**

Kama sadaka ndogo ya Mjane wa zamani, nakutolea, ee Bikira, utukufu yenye kukustahili na shukrani kwa mema wako: Kwani wewe ni msaada na ulinzi wangu, unaniopoa daima toka vishawishi na mateso yote; kama katikati ya tanuru ya moto unaniokoa kwa wazulumu wangu, na kwa moyo wangu wote nakulalamikia: Ee Mzazi-Mungu, kuja unisaidie na umuombe Kristu Mungu wetu anisamehe zambi zangu, kwani wewe ni matumaini ya mtumishi wako.

**KONTAKION**

Ee Mwokozi msiyekufa, wale waliondoka toka hii dunia yetu uwapumzishe pamoja na wenye haki katika makao ya Wateule; kwani kama walikosa katika maisha yao, wewe Bwana usiye na zambi uwasamehe makosa walikosa kwa kutaka wala bila kutaka, kwa maombezi ya Mzazi-Mungu aliyekuzaa, nakwa ajili yao tutalalamika kwa sauti moja: Alliluia.

**IKOS**

Ee Bwana, wewe peke yako ni msiyekufa, fundi na Muumba wa wanadamu; sisi wanadamu tuliyoumbwa kwa udongo tunarudi kwa udongo ileile kama alivyoamuru Muumba wangu wakati aliniambia: «Wewe ni udongo na utarudi kwa udongo», ni huko tunaenda sisi wote wanadamu, na kama ombolezo la kilio tunaimba: Alliluia.

**SINAKSARION YA SIKU YA LEO**

**KATAVASIA** Wimbo ya kwanza. *Sauti ya sita.*

Wakati Waisraeli waliposafiri kilindini kama pa inchi kavu, na walipoomuona Farao mzalimu ameangamizwa katika mawimbi, hapo wakapaza sauti: Tuimbeni wimbo wa ushindi kwa utukufu wa Mungu wetu.

Wimbo ya tatu.

Hakuna hata mmoja aliye Mtakatifu kama Wewe Bwana Mungu wangu; ulitukuza nguuuuvu ya Waaminifu katika wema wako, na ulitutia msingi pa mwamba imara wa maungamo ya jina Lako.

Wimbo ya ine.

Kristu ni nguvu yangu, Bwana wangu na Mungu wangu: huu ni wimbo kimungu Eklezia Takatifu inatangaza, na moyo wenye kutakasa inamuheshimu Bwana.

Wimbo ya tano.

Ewe Mungu mwema mno, nakuomba, angaza na nuru yako ya umungu roho za wapendwa wako wenye kukesha mbele yako ili wakujue, ewe Neno la Mungu, Wewe Mungu wa kweli mwenye kututosha ku giza ya zambi.

Wimbo ya sita.

Wakati ninapoona bahari ya hii uzima inanyanyuliwa kwa tufani ya vishawishi, nakimbilia ku bandari yako ya amani na napaza sauti, ee Mungu wa Wema: Komboa uzima wangu ku shimo.

Wimbo ya saba.

Katika tanuru ya moto Malaika akawamwangia Vijana washarifu umande, lakini moto ukawateketeza wakaldea kwa amri ya Mungu, na mzalima akalazimishwa kuimba: Umetukuzwa. Bwana Mungu wa Baba zetu.

Wimbo ya mnane.

Tunamsifu, tunamuhimidi na tunamusujudu Bwana.

Toka moto ukachirikiza umande kwa ajili ya Watakatifu Wako na kwa maji ukawakisha sadaka ya mwenyi haki, kwani ulitimiza vitu vyote paka kwa mapenzi yako: Ee Kristu, tunakutukuza milele.

**WIMBO YA TISA.**

**IRMOS*:*** Kwa wanadamu haiwezekane kumuona Mungu ambaye hata Malaika hawasubutu kutazama, lakini Neno aliyejifanya mtu kwako alionekana kwa wenye kufa, ewe Safi kamili, na wakati tunamutukuza pamoja na majeshi ya mbinguni tunakutangaza mwenye heri.

Ee Mungu wa mapendo, sasa majeshi ya malaika yanakuombawewe pamoja na Wakheruvi na Waserafi; Watawala, Wakubwa, Wenye mamlaka, Malaika wakuu na Wenye uwezo wanakuomba, ee Bwana mwenyezi, hurumia roho za marehemu.

Tazama andamano ya Manabii wenye kuongozwa, Mitume Watakatifu, Wapatriarki, Mashahidi, Wenye haki na Watakatifu wengi; wote pamoja wanakuomba: «Ee mpenda-wanadamu okoa roho zote za marehemu watumishi wako.

Utukufu kwa Baba…

Ee Bwana mwenyi kujua yote, unaona na kujua wanadamu wengi na mwisho wa kila uzima; leta maondoleo ya zambi na furaha ya Paradizo kwa kila mwaaminifu mtumihsi ulichagua kwa wema wako.

Sasa na siku zote…**THEOTOKION.**

Ee Bikira usiye na doa tena Malkia wa ulimwengu, wewe ni mlinzi wa wazima na wafu, mapumziko, utukufu na furaha yawale walio na heri ya kutumainia msaada wako: Kwa maombezi yako uwaokoe wote.

**Katavasia ya tisa.**

Kwa wanadamu haiwezekane kumuona Mungu ambaye hata Malaika hawasubutu kutazama, lakini Neno aliyejifanya mtu kwako alionekana kwa wenye kufa, ewe Safi kamili, na wakati tunamutukuza pamoja na majeshi ya mbinguni tunakutangaza mwenye heri.

**EKSAPOSTILARION** *Sauti ya tatu. O Uranon tis astris.*

Enyi waaminifu, tukiwakumbuka marehemu wote waliolala katika Kristu tukumbuke pia siku ya mwisho, tumwombe daima Kristu kwa ajili yasisi wenyewe na ya wafu wote.

**THEOTOKION. Umoja**

Ewe furaha yaMalaika, na watu wenye taabu, Mulinzi wa wakristu, Bikira Mama wa Bwana, unilinde na uponyeshe, toka mateso ya milele.

**MASIFU** *Sauti ya sita. I apegnosmeni.*

Ya woga ni hukumu ya Bwana kwa mwisho ya uzima: Kule juu mbinguni kunatayarishwa moto ya milele, nondo mwenyi kutafuta daima, kusaga meno, giza ya inje, azabu yamilele; ndio maana tumulalamikie Mwokozi: Kwa wema wako kubwa pumzisha wale uliita kwako toka hii dunia.

Ninyi wenyi kukamatwa kwa uzima, kujeni, inameni kaburini, tazameni namna dunia iliyo ya bure; wapi sasa uzuri wa mwili? Wapi nuru mingi? Wapi majivuno ya uzima? Kweli yote ni ya bure! Ndio maana tumulalamikie Mwokozi: Kwa wema wako kubwa pumzisha wale uliita kwako toka hii dunia.

Sasa eko kuzimuni huyu alikaa zamani juu ya kiti cha utawala, na huyu alivaa nguo nyekundu sasa anavaa uvumbi ya kaburi; ufalme imepotea, uzima ya watu inazimia kama ndoto; ndio maana tumulalamikie Mwokozi: Kwa wema wako kubwa pumzisha wale uliita kwako toka hii dunia.

Ee Mwokozi Mpenda-wanadamu, kwa rehema yako kubwa na kwa mapendo yako ya milele, waaminifu wote waliokufa kwa matumaini ya kupata uzima wa milele, wale waliokufa kwa namna mbalimbali, marehemu wa daraja yote, wa umri yote, wa hali yote, wanaume na wanawake, watoto wachanmga, uwaweke katika kifua cha Abrahamu pahali pa mapumziko.

Utukufu kwa Baba. *Sauti ya mbili*

Mutu wowote anafifia kama ndoto ao kama ua, lakini wakati baragumu itakayolia itatikisa wafu wote wataamuka juu ya kwenda kukutana na wewe, ee Kristu Mungu wetu; ee Rabi, weka wafu wetu katika makao yaWenye haki, na roho za watumishi wako katika uzima wa milele.

Sasa na siku zote...**THEOTOKION**. *Sauti ya sita.*

Wewe ni Mungu wetu, uliumba ulimwengu na hekima na kuijaza. ee Kristu, ulituma Manabii kutangaza kwako duniani na Mitume kutangaza matendo yako makuu: Wamoja walitabiri kuja kwako, wengine kwa Ubatizo waliangazia mataifa; kwa mateso yaoMashahidi walipata ile walitamaninia na wanakuomba pamoja na huyu alikuzaa: «Ee Mungu, pumzisha roho za wale uliochukua na utustahilishe ufalme wa mbinguni, wewe ambaye, kwa kuondoa hukumu yangu, uliteswa Msalabani, ee Mwokozi wangu na Mungu wangu».

**APOSTIKHA** *Sauti ya sita. Olin apothemeni.*

Ee Bwana kwa mapendo isiyokadirika unaye kwa ajili yetu na kwaChemchem isiyokwisha yawema wako, pokea wafu katika inchi ya wazima, uwaweke katika hema yamilele, ukiwawekea furaha ya mema waliyotamainia, kwani ulimwanga damu yako, ee Kristu, kwa kuikomboa dunia na bei ya uzima wako.

Shairi: Heriwale uliyochagua, wale uliyochukua pamoja, ee Bwana.

Kwa sisi kuishi uliitikia kufa, ulitirikisha Chemchem ya uzima kwa waaminifu unawapa heri yamilele: Uipane pia kwa wale waliyolala katika matumaini yaUfufuo, kwa wema wako zima zambi zao zote, kwani peke yako usiye na zambi; utuonyeshe mapendo yako ili litukuzwe jina lako, na tukiokolewa nawe, ee Kristu, tukutukuze milele.

Shairi: Na makumbusho yao ni milele na milele.

Ee Kristu, tunajuwa ubwana wako kimungu juu ya wazima na wafu; uwape watumishi waaminifu wako waliyomupatia mfazili wao pekee yake makao ya wateule wako, mahali pa baridi, katika utukufu wa Watakatifu wako, kwani ndiwe Mungu uliye na huruma na mwenyi kuokoa kwa wema wako wale uliyoumba kwa mfano wako.

Utukufu kwa Baba...*Sauti ya sita.*

Adamu alipata uchungu wakati alikula tunda lililokataziwa zamani katika shamba la Edeni, kwa sababu nyoka alimutumia sumu yake na katika yeye mauti yenyi kuangamiza wanadamu ikaingia duniani; lakini Bwana alikuja, aliua ule nyoka na alitupumzisha; ndio maana tunamulalamikia: ee Mungu Mwokozi, okoa wale ulichukua na uwapumzishe kati ya wateule wako.

Sasa na siku zote...**THEOTOKION.** *Olin apothemeni.*

Ee Bikira Mtakatifu kamili, ni wewe makao ya Mungu, ulimulinda tumboni mwako na bila ndoa ulizaa mtu mmoja mwenyi hali mbili; umuombe Mwana wa pekee namzaliwa wa kwanza aliyeacha salama ubikira wako hata kisha kuzaa awape waaminifu waliyolala na ibada mapumziko katika heri na nuru ya milele.

**Apolitikion.** *Sauti wa mnane.*

Ee zimu ya hekima yenyi kupenda wanadamu na kuongoza vitu vyote kwa ajili ya wokovu, peke yako Muumba ambaye kila mumoja anapokea ile yenye kumufaa, ee Bwana, leta mapumziko kwa roho za watumishi wako, kwa sababu matumaini yao ni kwako, ewe Fundi wetu, Muumba wetu tena Mungu wetu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...**THEOTOKION**.

Wewe ni boma na bandari yetu ya wokovu, muombezi wa kweli kwa Mungu uliyezaa, ee Bikira Mzazi-Mungu, ndiwe wokovu wa wakristu.

**KUAGA.**

# SIKU YA MUNGU YA PENTIKOSTI

## SIKU YA POSHO MANGARIBI KWA ESPERINOS KUBWA

Kisha : «Bwana nimekuita...» tunaimba wimbo kumi. Hivi: *Sauti ya kwanza*

Tushangilie Pentikosti na kushuka kwa Roho Mtakaitfu; katika hii ahadi imekamilika, matumaini imetimizika. Ni fumbo heshimiwa na yenyi kujaa na utukufu! Ndio maana tunakulalamikia: Ee Muumba wa ulimwengu na Bwana utukufu kwako *(mara mbili).*

Ee Bwana, uligeuza Wafwasi wako kusema luga za mataifa kusudi kwa hizi luga wakutangaze kama Mungu na Neno msiyekufa mwenye kuleta neema ya wokovu rohoni mwetu.

Neema yote inatoka kwa Roho Mtakatifu: Yeye ni Chemchem ya unabii, anafundisha mapadri na kuleta hekima kwa wasiyojua kusoma na kuandika, anageuza wavuvi kuwa wenyi kujua elimu yaMungu na anasabitisha Eklezya yote yenyi kukusanyika. Ee Roho Mtakatifu wa asili moja na Baba na Mwana na mwenyi kutambua pamoja nao, ee Bwana, utukufu kwako.

*Sauti ya mbili.*

Tumeona nuru ya kweli, tumepokea Roho wa mbinguni, tumepata imani ya kweli, tukiusujudu Utatu usiotengwa; kwani Huu umetuokoa. *(mara mbili).*

Ee Mwokozi, katika manabii ulitutangazia njia ya wokovu, ndani yaMitume wako muliangaa neema ya Roho wako Mtakatifu, kwa sababu mbele yanyakati ulikuwa Mungu, kisha wao ulikuwa Mungu, na uko Mungu milele.

Ee Mwokozi wa dunia, katika uwanja wako nitaimba na kupiga goti, mbele ya uwezo wako wa ushindi nitasujudu mangaribi, asubui na jua kati; na nitakutukuza daima, ee Bwana.

Ee Bwana, katika uwanja wako sisi waaminifu tunapopiga magoti ya roho zetu na ya miili yetu, tunakuimbia, ee Baba wa milele, pamoja na Mwana wako na Roho Mtakatifu kamili ambao unapotawala nao milele, angaza roho zetu na kuzitakasa.

Tumwimbie Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, Utatu wa asili moja, kwa sababu ni hivi walimutangaza Manabii wa wakati wote, Mitume na Mashahidi Watakatifu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote... *Sauti ya mnane.*

Kujeni, ninyi mataifa yote, tumwabudu Mungu mumoja katika watu tatu: Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu; kwani Baba alizaa Mwana inje ya wakati, anatawala naye milele na Roho Mtakatifu eko ndani ya Baba, anatukuzwa pamoja na Mwana: Uwezo mumoja, umungu mumoja, hali moja ambayo sisi waaminifu tunasujudia tukisema: «Ee Mungu Mtakatifu uliyeumba vyote katika Mwana kwa msalaba wa Utatu Mtakatifu, Mungu Mtakatifu na Mweza kwa ajili yake Baba alifunuliwa kwetu, na katika yeye Roho Mtakatifu alikuja duniani; Mungu Mtakatifu na msiyekufa, Roho mfariji anayetoka kwa Babana kukaa juu ya Mwana: Utatu Mtakatifu, utukufu kwako.

**KUINGIA Mwangaza upole...**

Prokimenon siku ya leo.

**Somo ya Hesabu tunasoma** *(Hesabu 11, 16-29).*

Bwana akamwambia Musa: Unikusanyie watu makumi saba wa wazeewa Israeli, watu unaojua kuwa wazee wa watu, na maakida juu yao; uwalete hata hema ya kusanyiko wasimame pale pamoja nawa. Nami nitashuka niseme nawe pale; na nitatwaa sehemu ya roho iliyo juu yako, na kuiweka juu yao; na watachukua mugizo wa watu pamoja nawe, usiuchukue peke yako. Na utawaambia watu: Mujitakase kwa kesho, nanyi mutakula nyama; kwa maana mumelia masikioni mwa Bwana mukisema: Nani atakayetupa sisi nyama tule? Maana kule katika Misri tulikuwa na heri; kwa hivi Bwana atawapa ninyi nyama na mutakula. Hamutakula siku moja, wala siku mbili, wala siku tano, wala sikukumi, wala siku makumi mbili; lakibni mwezi muzima hata nyama hii itakapotoka puani mwenu na mutaichukia; kwa sababu mumekataa Bwana aliye katikati yenu, na mumelia mbele yake mukisema: Kwa nini tumetoka Misri? Musa akasema: Watu hawa ninaokoa katikati yao ni watu elfu mia sita wanaokwenda na miguu; nawe umesema. Nitawapa nyama wapate kula mwezi muzima. Makundi ya kondoo na ngombe yatachinjwa kwa ajili yao kuwatosha? Ao samaki zote za bahari watakusanywa ili kuwatosha? Bwana akamwambia Musa: Mukono wa Bwana umepunguka kwa urefu? Utaona sasa kama neno langu litatimizwa kwako ama sivyo. Musa akatoka, akawaambia watu maneno ya Bwana; akakusanya watu makumi saba wa wazee wa watu, akawaweka kuzunguka Hema. Bwana akashuka katika wingu, akasema naye, akatwaa sahemu ya roho iliyokuwa juu yake na kuiweka juu yawale wazee makumi saba; na ilikuwa wakati roho ilipokaa juu yao, wakatabiri, lakini hawakufanya hivi tena. Lakini watu wawili walibaki katika kambi, jina la mumoja lilikuwa Eldadi, na jina la yule mwingine lilikuwa Medadi; roho ikakaa juu yao; nao waliokuwa wa wale walioandikwa, lakini hawakutoka kwenda Hemasi; wakatabiri kambini. Kijana mumoja akapiga mbio, akamwambia Musa, akasema: Eldadi na Medadi wanatabiri kambini. Na Yosua mwana wa Nuni, mutumishi wa Musa tangu ujana wake, akajibu na kusema: Bwana yangu Musa, uwakataze. Musa akamwambia: Una wivu kwa ajili yangu? Ingekuwa heri kama watu wote wa Bwana wangekuwa manabii na kama Bwana angewatia roho yake! Musa akakwenda, akaingia kambini, yeye na wazee wa Israeli.

**Somo ya Unabii ya Nabii Yoeli tunasoma**. *(2, 23-3,5).*

Furahini, basi ninyi watoto wa sayuni, na furahini katika Bwana, Mungu wenu, kwa sababu yeye anawapa ninyi mvua ya kwanza kwa kipimo cha haki, na anafanyiza mvua ya kwanza na mvua yasasa kuwaangukia ninyi, katika mwezi wa kwanza. Na sakafu zitajaa na ngano; na mashinikizo yatafurika kwa mvinyo na mafuta. Nami nitawarudishia ninyi miaka nzige ziliyokula, na funza, na wadudu wage, na mapanzi, jeshi langu kubwa nililotuma katikati yenu. Na mutakula tele na kushiba, na mutasifu jina la Bwana, Mungu wenu aliyewatendea ninyi kwa mushangao, na watu wangu hawatahayarishwa kamwe. Na mutajua ya kama mimi ni katikati ya Israeli, na ya kama mimi ni Bwana, Mungu wenu, wala hakuna mwigine; na watu wangu hawatahayarishwa kamwe. Na itakuwa nyuma yamaneno haya, nitamwanga Roho yangu juu ya watu wote; na wana wenu na binti zenu watabiri, wazee wenu wataota ndoto, vijana wenu wataona maono; na vilevile juu ya watumishi wangu, wanaume na wanawake, nitamwanga Roho yangu katika siku zile. Na nitaonyesha maajabu katika mbingu na katika dunia, damu na moto na nguzo za moshi. Jua litageuka kuwa giza, na mwezi kuwa damu mbele ya kutimia kwake ile siku kubwa ya Bwana, yenye kuogopesha. Na itakuwa kila mutuatakayeomba kwa jina la Bwana, ataokolewa. Kwani katika kilima Sayuni na katika Yerusalema watakuwa wenye kuokolewa, kama Bwana alivyosema, na katika baki wale Bwana anaowaita.

Kwa maana, tazameni, katika siku zile, na kwa wakati ule wakati nitakaporudisha tena wafungwa wa Yuda na wa Yerusalema, nitakusanya mataifa yote, na nitawashusha kwa bonde la

Yosafati, na nitawasihi pala kwa watu wangu na kwa uriti wangu Israeli, waliowasambaza katikati ya mataifa na kugawanya inchi yangu. Na wamepiga watu wangu kura; na wametoa kijana kwa kahaba, na wameuza musichana kwa mvinyo, wapate kunywa. Ndiyo, nanyi ni kitu gani kwangu, ee Tiro na Sidoni, na pande zote za Filistia? Mutanirudishia malipo? Na kama munanirudishia malipo, mbiombio na upesi nitageuza malipo yenu juu ya kichwa chenu wenyewe. Kwa sababu mumekamata feza yangu na zahabu yangu, na mulipeleka kwa mahekalu yenu vitu vyangu vyema na vya kupendeza.

**Somo ya Unabii ya Nabii Ezekieli, tunasoma.***(36,24)*

Kwa sababu nitawatwaa ninyi katika mataifa na kuwakusanya ninyi toka inchi zote, nami nitawaleta ninyi kwa inchi yenu wenyewe. Na nitawanyunyizia ninyi maji safi, na mutakuwa safi; nitawasafisha ninyi kwa uchafu wenu wote na sanamu zenu zote. Nitawapa ninyi moyo mupya vilevile, nami nitatia roho mpya ndani yenu, na nitaondosha moyo wa jiwe toka mwili wenu, na nitawapa ninyi moyo wa mwili. Na nitaweka rohjo yangu ndani yenu na kuwatembeza ninyi kwa sheria zangu, na mutachunga hukumu zangu na kuzifanya. Na mutakaa katika inchi niliyowapa baba zenu; na mutakuwa watu wangu, nami nitakuwa Mungu wenu.

**L I T I A.** *Sauti ya mbili.*

Ee Mwokozi, katika manabii ulitutangazia njia ya wokovu, ndani yaMitume wako muliangaa neema ya Roho wako Mtakatifu, kwa sababu mbele yanyakati ulikuwa Mungu, kisha wao ulikuwa Mungu, na uko Mungu milele. *(mara mbili).*

Ee Mwokozi wa dunia, katika uwanja wako nitaimba na kupiga goti, mbele yauwezo wako wa ushindi nitasujudu mangaribi, asubui na jua kati; na nitakutukuza daima, ee Bwana.

Ee Bwana, katika uwanja wako sisi waaminifu tunapopiga magoti ya roho zetu na ya miili yetu, tunakuimbia, ee Baba wa milele, pamoja na Mwana wako na Roho Mtakatifu kamili ambao unapotawala nao milele, angaza roho zetu na kuzitakasa.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya mnane.*

Ee Bwana, wakati uliwatumia Mitume wako Roho Mtakatifu, wana wa Israeli walipoona hii muujiza, wakashikwa na woga; wakawasikia wakisema luga zingine kadiri Roho Mtakatifu aliwapa kusema; walijazwa na hekima; katika nyavu zao wakavua mataifa, wakawaongoza kwa imani na kuwaonyesha mafumbo takatifu; ndio maana sisi pia tunakuimbia: «Wewe uliyeonekana duniani na kutuokoa toka udanganyifu, ee Bwana, utukufu kwako.

**APOSTIKHA** *Sauti ya sita.*

Ee Bwana, sawa vile hawakujua bado uwezo wa Roho Mtakatifu kamili uliwatumia Mitume wako, makutano wakawaona kuwa walevi sababu ya kusema luga zingine; lakini sisi wenye kuhakikishwa daima kwa neno lao, ee Mpenda-wanadamu, tunakuomba hivi: Usituondolee Roho wako Mtakatifu.

Shairi:Umba moyo safi ndani yangu, ee Mungu, na ufanye upya roho nzuri ndani yangu.

EeBwana, kumwanga kwa Roho Mtakatifu juu yakuwajaza Mitume wako iliwapa uwezo wa kusema luga za mataifa; na kwa ulevi hii muujiza ilionekana kwa wasioamini lakini kwa waaminifu inawapa wokovu; tunakuomba, ee mpenda-wanadamu, utustahilishe na sisi pia kupata nuru yake.

Shairi: Usinitenge na uso wako, wala usiondolee Roho yako mutakatifu.

Mfalme wa mbinguni, Wewe Mfariji. Roho ya ukweli, uliye pahali popote, na kuvijaza vitu vyote, Wewe hazina ya mambo mema, tena Mpaji wa uhai. Njoo kukaa kwetu na kutusafisha kila doa, hata kuziokoa roho zetu, Mwema We.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*Sauti ya mnane.*

Luga zilizochanganyika zamani sababu yaujasiri wa wajengaji sasa zimejaa na hekima kwa maarifa tukufu ya Mungu; zamani Bwana alihukumu makafiri sababu yazambi yao, sasa Kristu anangaza wavuvi katika Roho Mtakatifu; zamani mugawanyiko wa luga ilifanyika katika azabu: Sasa mapatano inafanyika kati yao kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

**Apolitikion.** *Sauti ya mnane.*

Uhimidiwe, ee Kristu Mungu wetu, wewe uliyewashushia Mitume wako Roho Mtakatifu, ukiwageuza kwa hekima yako wavuvi kuwa wavuvi wa watu ambao nyavu yatavua dunia yote. Bwana Mpenda-wanadamu, utukufu kwako. *(mara tatu).*

## SIKU YA MUNGU ASUBUI YA PENTIKOSTI

*Kisha Eksapsalmos tunaimba: «Bwanandiwe...» na Apolitikion mara tatu. Kisha:*

**KATHISMA YA KWANZA** *Sauti ya ine. Kateplagi Iosif.*

Ninyi waaminifu, kwa hii siku Kuu ya ukamilifu, tushangilie na furaha Pentikosti huko inatimizika ya Kristu: Kwani leo moto ya Roho Mtakatifu kwa mfano wa ndimi za moto inashuka duniani na Wafwasi wanapoangazwa wanafundishwa kwa mafumbo ya mbinguni: Tazama, nuru ya Roho Mtakatifu inangaa duniani.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*(mara mbili).*

**KATHISMA YA MBILI.**

Chemchem ya Roho Mtakatifu ilishukia wanadamu kwa ndimi za moto, juu ya Mitume waliangazwa kwa umande wa roho: Wingu iliwashukia ikawamwangia moto, moto yanuru na ya baridi nzuri; katika wao tumepewa neema kwa moto na kwa maji: Tazama, nuru ya Roho Mtakatifu inangaa ulimwangu duniani.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*(mara mbili).*

*Kisha Polieleo*

**KATHISMA YA TATU.** *Sauti ya mnane. To prostakthen.*

Ee Kristu, kisha Ufufuo wako kaburini na kupanda kwako juu mbinguni ulishusha utukufu wako juu ya Washuhuda wa umungu wako na uliweka Roho mpya wa haki ndani yamoyo wa Wafwasi wako; ndio maana, ee Mwokozi, walifundisha mafundisho yako na matendo yako ya wokovu kama kinubi chenyi masauti mazuri ya kimungu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*(mara mbili).*

**ANTIFONON YA SAUTI YA INE**

Toka ujana wangu, tamaa mbaya mingi inanigombanisha. Lakini Wewe Mwokozi wangu, unilinde na uniokoe *(Mara mbili)*

Enyi muliochukia Sayuni, mupate haya toka Bwana. Kwani kama majani mbele ya moto, mutakuwa wakikauka *(Mara mbili).*

Utukufu kwa Baba na kwa Mwana na Kwa Roho Mutakatifu.

Katika Roho Mutakatifu, kila nafsi inakuwa hai, na kwa usafisho inanyanyuliwa, inaangazwa, katika Utatu Umoja, kwa siri Takatifu.

Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Katika Roho Mutakatifu, maji ya neema inayotelemuka inatoka, ikinywesha kiumbe kiote, kusudi kiwe na uzima.

**PROKIMENON**

Roho yako ni mwema; uniongoze katika inchi ya haki. Shairi: Sikia maombi yangu, ee Bwana.

Mwimbaji: Kila mwenye pumuzi amsifu Bwana. *(mara tatu).*

**EYANGELION EOTHINON YA TISA**

ZABURI 50 (51) *Na kisha: Sauti ya pili.*

Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu.

Kwa ajili ya maombezi ya Mitume, ee Mrahimu, uufute wingi wa zambi zangu.

Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Kwa ajili ya maombezi ya Mzazi-Mungu, ee Mrahimu, uufute wingi wa zambi zangu.

Mrahimu, unihurumie, ee Mungu, sawasawa na huruma yako kubwa, kiasi cha wingi wa rehema zako, uyafute makosa yangu.

Mfalme wa mbinguni, Wewe Mfariji. Roho ya ukweli, uliye pahali popote, na kuvijaza vitu vyote, Wewe hazina ya mambo mema, tena Mpaji wa uhai. Njoo kukaa kwetu na kutusafisha kila doa, hata kuziokoa roho zetu, Mwema We.

## KANUNI

**WIMBO YA KWANZA**. *Sauti ya saba .*

**IRMOS:** Akamzika Farao na magari yake katika bahari Nyekundu huyu mwenye kuvunja vita kwa nguvu ya mkono wake: Tumwimbie, kwani amevaa Utukufu. *(mara mbili).*

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, Utukufu kwako.

Kristu mpenda-wanadamu, kama ulivyoahidi zamani Wafwasi wako kuja kwake ulipotuma Roho Mfariji uliangazia dunia kwa nuru.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, Utukufu kwako.

Ile iliyotangaziwa zamani kwa kinywa cha Manabii na Sheria leo imetimizika, kwa sababu neema ya Roho Mtakatifu inakaa juu ya mwaminifu wote.

*Sauti ya ine.*

**IRMOS:**Wingu wa kimungu ulifunika Musa mwenye-ulimi muzito, na Yeye alihubiri sheria iliyoandikwa na Mungu. Kwani akiondosha uchafu toka macho ya roho aliona Mungu Aliye, na aliingiza katika mafikili ya Roho, akimwimbia kwa wimbo kimungu. *(mara tatu).*

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, Utukufu kwako.

Neno takatifu na tukufu alisema: «Sitatengana na ninyi marafiki zangu; nitakapokaa pa kiti cha ufalme wa Baba mbinguni, nitamwanga neema ya Roho Mtakatifu sababu ya kwangazia wale wenyi kuitamainia na moyo mumoja.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, Utukufu kwako.

Anapopanda mlimani, Neno takatifu anatimiza hamu ya moyo wake safi; kwa maana lilipotimizika tendo lake, Kristu anawapata marafiki zake akiwapa Roho Mtakaitfu kwa mvumo wa upepo na kwa ndimi za moto kama alivyoahidi.

**WIMBO YA TATU.** *Sauti ya saba.*

**Irmos:** Uliwaambia Mitume: Musitoke Yerusalema lakini mungoje mpaka siku mutapokea nguvu toka juu mbinguni, nami nitawatumia Mfariji mwengine, Roho wa Baba na wangu, naye atawasabitisha ninyi. *(mara mbili).*

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, Utukufu kwako.

Kwa kushuka kwake nguvu yaRoho Mtakatifu ilikusanya zamani kwa umoja luga mbalimbali sababu ya mapatano ya katika uovu; kwa waaminifu wanawafunulia Utatu ambamo tumesabitisha.

*Sauti ya ine.*

**Irmos:** Minyororo la tumbo ya tasa ilikatika, na tena laumu isiyovumiliwa ya Muzazi, paka kwa maombi ya Hana nabii wakate, mwenye-kuwa moyo uliovunjika mbele ya Mufalme wa uwezo, na Mungu wa kujua yote. *(mara mbili).*

Utukufu kwa Baba….

Uwezo kubwa wa Mungu haitambulikane: Kwa hii watu wasiojua kusoma na kuandika wamekuwa waalimu, na kwa neno lao wananyamazisha waongo wa udanganyifu, wanaondoa mataifa yasiyojua kitu toka giza yao kubwa kwa nuru ya Roho Mtakatifu.

Sasa na siku zote…

Anatoka kwa nuru ya milele, nuru ya milele yenyi kuangaa na moto elfu, huyu ambaye neno la moto linafunuliwa mataifa katika Sayuni nuru ya asili moja toka Baba katika Mwana.

**KATHISMA.** *Sauti ya mnane. To prostakthen.*

Marafiki za Mwokozi walijazwa na furaha na wakapata moyo, wao ambao kwa mwanzo waliogopa, lakini leo ameshuka toka mbinguni Roho Mtakaitfu na anakaa juu ya Mitume; kila mutu aliwasikia wakisema kwa luga yake, kwa sababu amewagawanyia ndimi za moto ambazo haziwezi kuwateketeza, lakini kuwafunika umande.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*(mara mbili).*

**KONDAKION**. *Sauti ya Mnane.*

Alipochanganya lugha za ulimwengu, Bwana wa juu mbinguni akasambaza mataifa; lakini alipogawanya ndimi za moto, anawalika watu wote ku umoja na wote pamoja tunamutukuza Roho Mtakatifu kamili.

**IKOS**

Ee Yesu, tuliza imara sisi watumishi wako katika huzuni humo munapatikana akili yetu; usiache roho zetu katika sikitiko; usijitenge mbali ya mioyo yetu yenye kujaribiwa, lakini tangulia kutuonyesha. Kuja karibu yetu, ee Bwana, uliye popote; kwa wale wenye kukupenda ungana nao kwa wema wako kama ulivyowafanyia Mitume wako siku zote; kusudi tukiungana na Wewe tuweze kuimbia na kutukuza Roho wako Mtakatifu kamili.

**SINAKSARI**

Leo siku ya yengayaMunane ya Paska, tunashangilia Pentikosti Takatifu.

Shairi: Kwa upepo wenyi kuvuma Kristu anawapa Mitume Roho Mtakatifu kama ndimi za moto.

Kwa maombezi ya Mitume wako, ee Kristu Mungu wetu, utuhurumie. Amina.

**KATAVASIA**

Wimbo ya Kwanza. *Sauti ya Saba.*

Akamzika Farao na magari yake katika bahari Nyekundu huyu mwenye kuvunja vita kwa nguvu ya mkono wake: Tumwimbie, kwani amevaa Utukufu.

*Sauti ya Ine.*

Wingu wa kimungu ulifunika Musa mwenye-ulimi muzito, na Yeye alihubiri sheria iliyoandikwa na Mungu. Kwani akiondosha uchafu toka macho ya roho aliona Mungu Aliye, na aliingiza katika mafikili ya Roho, akimwimbia kwa wimbo kimungu.

Wimbo ya Tatu. *Sauti ya saba.*

Uliwaambia Mitume: Musitoke Yerusalema lakini mungoje mpaka siku mutakayoviiikwa nguvu ya Juu mbinguni, nami nitawatumia Mfariji mwengine, Roho ya Baba na yangu, naye atawasabitisha ninyi.

*Sauti ya ine.*

Minyororo la tumbo ya tasa ilikatika, na tena laumu isiyovumiliwa ya Muzazi, paka kwa maombi ya Hana nabii wakate, mwenye-kuwa moyo uliovunjika mbele ya Mufalme wa uwezo, na Mungu wa kujua yote.

Wimbo ya Ine. *Sauti ya saba.*

Alipofikiri pa majilio yako ya mwisho, ee Kristu. Nabii akapaza sauti: Niliona uwezo wako. Bwana, maana ulikuja kuokoa wale waliotolewa Kwako.

*Sauti ya ine.*

Mufalme wa wafalme. Mwana wa pekee na Neno, uliyezaliwa na Baba peke yake asiye mwanzo, ulituma Roho kweli sawa na wewe kwa mitume, kwa sababu wewe ni mwema, na wao waliimba: Utukufu kwa uwezo wako, ee Bwana.

Wimbo ya Tano. *Sauti ya saba.*

Bwana, Roho ya wokovu yako zamani Manabii walipokea na woga anafanya moyo safi ndani ya Mitume na anabadilisha katika mioyo yetu akili ya haki, kwani amri zake, ee Bwana, zinatuletea nuru na amani.

*Sauti ya ine.*

Mupokee usafisho unaozimisha zambi, mupokee upepo wa Roho ya umande na ya moto, enyi watoto wa Kanisa kwa uso ya nuru. Kwa maana sasa katika sayuni sheria ilitoka, neema ya Roho ilionekana ndini kama za moto.

Wimbo ya Sita. *Sauti ya saba.*

Ninaposafiri baharini mwenye kunyanyuliwa kwa Shurali za dunia, ninapoangamizwa katikati ya zambi zangu, na kutupwa kwa nyama mwenyi kurarua roho, kama Yona, ee Kristu, nakulalamikia: uniopoe kuzimuni kwa mauti.

*Sauti ya ine.*

Kristu Rabi, uko usamehe na wokovu, ukianga toka Bikira, ili utoshe toka uharibifu Adamu mwenye kuanguka na wote, kama ulitosha toka matumbo ya samaki nabii Yona.

Wimbo ya Saba. *Sauti ya saba.*

Katika tanuru ya moto Vijana wakageuza moto uliyowazunguuuka kuwa umande kwani walimutukuza Bwana wakiimba: Ee Mungu wa Baba zetu, umetukuzwa.

*Sauti ya ine.*

Upatanisho wa viombo vya musiki ilinguruma, kusudi mataifa waabudu sanamu isiyo na nafsi iliyofanywa kwa zahabu. Lakini neema ya Mufariji ilitayonuru iliwapatia moyo ya ukimya kwa waaminifu wapaze sauti: Utatu wa usawa pasipo mwanzo, uko peke yako mubarikiwa.

Wimbo ya Mnane. *Sauti ya saba.*

Tunasifu, tunamuhimidi na tunamusujudu Bwana.

Kichaka cha Sinai chenye kuwaka moto bila kuteketezwa kilifunua Mungu kwa Musa, kilipoeleeekea kwa huyu wasipo usemi wepesi; na katika moto Vijana watatu washujaa katika bidii yao kwa Mungu wakaimba wimbo wa Sifa: Mwimbieni Bwana, enyi wote viumbe vyake, mtukuzeni milele.

*Sauti ya ine.*

Mufano wa nuru tatu ya Umungu unafungula minyororo na unapoza moto. Watoto wanaimba na viumbe vyote vilivyoumbwa na Mungu, Mwokozi na Muumba peke yake, vinamubarikia, kwaq kuwa Yeye ni Mwema.

**WIMBO YA TISA** *Sauti ya saba.*

**Irmos:** Wewe uliyepata mimba katika usafi wote na kwako Neno muumba wa ulimwengu akajifanya mtu, ewe Mama usiyeolewa. Mzazi Bikira wa Mungu, Makao ya huyu mtu hata mmoja hawezi, kusonga, nyumba ya Wamilele, Muumba wako, tunakutukuza. *(mara mbili).*

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, Utukufu kwako.

Huyu alichukulia zamani na furaha juu ya gari yamoto, Nabii mwenyi kujaa na bidii na moyo, alitangulia kuonyesha kuja kwa Roho Mtakaitfu huyu anashukia leo Mitume toka mbinguni: Wanapoangaa na hii moto, wanaonyesha watu wote Utatu Mtakatifu.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, Utukufu kwako.

Sheria ya watu haisikie, kitu moja cha ajabu kinasikilika: Wakati, kwa neema ya Roho Mtakaitfu, sauti moja ya Mitume ilisikilika, watu, luga na mataifa walisikia mbalimbali maajabu ya Mungu, walifundishwa kwa maarifa ya Utatu Mtakatifu.

*Sauti ya ine*

**IRMOS:** Salamu, Malkia, utukufu kwa wazazi na wabikira. Katika kila kinywa kisemaji wepesi, wakati kinasema, hakitaweza kukusifu kwa kustahili. Tena kila akili kinapata kizunguzungu bila kuweza kusikia kulala kwako. Kwa hii sisi wote tunakusifu kwa sauti moja. *(mara mbili).*

Utukufu kwa Baba...

Nitaimbia Bikira Chemchem ya Uzima ambaye peke yake alificha tumboni mwake Neno mwenye kuponyesha wanadamu na toka kuume kwa Baba sasa anatutumia neema ya Roho Mtakatifu.

Sasa na siku zote...

Sisi wote tulipuliziwa na neema ya Mungu, tunapoangazwa kwa nuru na kubadilishwa, tunapotangulia kuona Hekima ya Utatu usiyotengana, tunatukuza nuru yake tatu.

**Katavasia ya tisa:** Wimbo ya Tisa. *Sauti ya saba.*

Wewe uliyepata mimba katika usafi wote na kwako Neno muumba wa ulimwengu akajifanya mtu, ewe Mama usiyeolewa. Mzazi Bikira wa Mungu, Makao ya huyu mtu hata mmoja hawezi, kusonga, nyumba ya Wamilele, Muumba wako, tunakutukuza.

*Sauti ya ine.*

Salamu, Malkia, utukufu kwa wazazi na wabikira. Katika kila kinywa kisemaji wepesi, wakati kinasema, hakitaweza kukusifu kwa kustahili. Tena kila akili kinapata kizunguzungu bila kuweza kusikia kulala kwako. Kwa hii sisi wote tunakusifu kwa sauti moja.

**EKSAPOSTILARION.** *Sauti ya tatu. O Uranon tis astris.*

Ee Roho Mtakatifu mwenyi kutoka kwa Baba na kuwashukia Wafwasi wasiojua kusoma na kuandika katika Mwana, okoa na takasa wote wale wenyi kukutambua kama Mungu.

**Ingine Umoja**

Nuru ni Baba, nuru ni Neno, nuru pia ni Roho Mtakatifu aliyetumwa juu ya Mitume kama ndimi za moto na katika Yeye dunia yote inapokea kwa ubatizo nuru sababu ya kuabudu Utatu Mtakatifu.

## MASIFU. *Sauti ya ine*

Leo mataifa yote wanaona maajabu katika muji wa Daudi wakati Roho Mtakatifu anashuka kama ndimi za moto kama alivyotuhadisia Mtakatifu Luka: Wafwasi wa Kristu walikusanyika, mara moja kelele ikasikilika toka mbinguni; ni upepo kali, na hii mvumo ikajaa nyumba yote humo walikaa; na wote wakaanza kusema kwa lugha zingine sababu ya kufundisha mafundisho mpya ya Utatu Mtakatifu.*(mara mbili).*

Roho Mtakatifu aliye, aliyekuwa, atakayekuako daima, wasipo mwanzo na mwisho, ni wa asili moja na Baba na Mwana; yeye ni Uzima, Bwana mletaji uzima, nuru na Chemchem ya uzima; yeye ni wema, hazina ya wema; katika yeye Baba amejulikana na Mwana ametukuzwa; anawafunulia wote uwezo moja, umoja, na ibada ileile ya Utatu Mtakatifu.*(mara mbili).*

Roho Mtakatifu, nuru, uzima, maji ya uzima yenye kutiririka kwa siri, Roho wa hekima, wa maarifa wa wema, uhaki, wa akili kubwa yenyi kutakasa zambi; yeye ni Mungu na anatufanya kuwa Mungu; moto yenyi kutirikiza moto, anasema, anatenda na kumwanga vipaji takatifu; katika yeye

Manabii wote na Mitume wa Mungu walipokea taji pamoja na Mashahidi: Ni maono ya ajabu, ni muujiza wa ajabu! Moto inawagawanyika sababu ya kugawanya zawadi. *(mara mbili).*

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*Sauti ya sita.*

Mfalme wa mbinguni, Wewe Mfariji. Roho ya ukweli, uliye pahali popote, na kuvijaza vitu vyote, Wewe hazina ya mambo mema, tena Mpaji wa uhai. Njoo kukaa kwetu na kutusafisha kila doa, hata kuziokoa roho zetu, Mwema We.

**DOKSOLOGIA KUBWA**

## LITURGIA TAKATIFU

### ANTIFONA YA SIKU KUU.

**Antifonon ya kwanza:**

Mbingu zinatangaza utukufu wa Mungu; na anga zinaonyesha kazi ya mikono yake.
Kwa maombi ya Mzazi-Mungu...
Muchana unasemezana na muchana, usiku unatolea usiku maarifa. Kwa maombi...
Sauti yao imeenea duniani mwote, na maneno yao hata miisho ya ulimwengu. Kwa maombi...
Utukufu... Sasa... Kwa maombi ya Mzazi-Mungu...

**Antifonon ya Mbili.**

Bwana akujibu siku ya taabu; jina la Mungu wa Yakobo likunyanyue.
Utuokoe, ee Mfariji Mwema Kamili, tunaokuimbia. Alliluia.
Akutumie kusaidia toka pahali patakatifu na kukupatisha nguvu toka Sayuni. Utuokoe...
Akumbuke zabihu zako zote, na kupokea sadaka yako ya kuteketezwa. Utuokoe...
Utukufu... Sasa... Uliye Mwana wa pekee...

**Antifonon ya Tatu.**

Mufalme atafurahi kwa nguvu yako, ee Bwana; na kwa wokovu wako ataona shangwe nyingi sana! Apolitikion ya Siku Kuu.
Umemupa hamu ya moyo wake, wala hukuzuiza maombi ya midomo yake. Apolitikion ya Siku Kuu.
Kwa sababu ulimutangulia na baraka ya vitu vizuri; unaweka taji ya zahabu safi juu ya kichwa chake. Apolitikion ya Siku Kuu.
Isodikon (Kuingia): Simama, ee Bwana, kwa enzi yako, nasi tutaimba na kusifu uwezo wako. Utuokoe...
Apolitikion *(mara tatu). Kontakion.*
*Pahali ya: Mungu Mutakaitfu leo tunaimba:* Ninyi wote muliobatiza.
*Apostolos na Evangelion ya Siku Kuu. Pahali ya fasi: Niwajibu kweli tunaimba Wimbo ya Katavasia ya Tisa. Kinonikoni:* Roho yako Mwema aniogoze kwenye inchi sawa. Alliluia. *Jina la Bwana,(mara tatu).*

**Kuaga**

Yeye aliyewatumia Wafwasi na Mitume wake Watakatifu Roho Mtakatifu kamili toka mbinguni kama ndimi za moto, Kristu Mungu wetu kweli...

# MU JUMA YA PENTIKOSTI MANGARIBI

### SIKU KUU YA ROHO MTAKATIFU

### IBADA YA KUPIGA MAGOTI

*Hii Ibadaiko namna yakuifanya mangaribi yamu Juma ya Pentikosti kwa sababu iko Esperinos yamu Kazi Moja, Siku Kuu yamakumbusho ya Roho Mtakatifu.*

*Kama padri anapenda kufanya hiyi sala asubui yamu Juma ya pentikosti kisha Kuaga ya Liturgia Takatifu ataanza hivi:*

Padri: Abarikiwe Mungu wetu daima...
*Msomaji atsasoma Zaburi 104 (Proimiakos) na  Padri atasoma ma sala saba.*
*Kisha Proimiakos Shemasi ao padri atasema Ektenia kubwa:*
Kwa amani, tumuombe Bwana. Waimbaji: Bwana hurumia
Kwa ajili ya amani inaotoka Juu na kwa ajili yawokovu wa roho zetu, tumuombe Bwana.

Kwa ajili ya amaniya dunia nzima, ustawi wa Eklezya Takatifu ya Mungu na ya umoja wa wote, tumuombe Bwana.
Kwa ajili ya hekalu hii takatifu na juu ya wale wanaingiamo na imani, heshima na oga ya Mungu, tumuombe Bwana.
Kwa ajili ya Askofu wetu *(jina lake)* ya wapadri weheshimiwa, Ushemasi katika Kristu, wateule wote na ya watu wote, tumuombe Bwana.
Kwa ajili ya Wakristiani waaminifu na Waorthodoksi tumuombe Bwana.
Kwa ajili ya muji hii na inchi hii, kila muji na inchi na ya Waaminifu wanaishi humo, tumuombe Bwana.
Kwa ajili ya taifa hili linaongojea neema ya Roho Mtakatifu, tumuombe Bwana.
Kwa ajili ya wale ambao mbele ya Bwana wanainamisha moyo wao na wanapiga magoti, tumuombe Bwana.
Kwa ajili tupate sisi nguvu juu yanamna ya kumupendeza kwa ukamilifu, tumuombe Bwana.
Kwa ajili ya kututumia tangu mbinguni rehema yake mingi, tumuombe Bwana.
Kwa ajili yakupokea ombi letu la magoti sawa ubani mbele yake, tumuombe Bwana.
Kwa ajili ya wale wote wanaotaka msaada wake, tumuombe Bwana.
Kwa ajili yakuokolewa ku uovu, hatari yoyote, masumbuko yoyote tumuombe Bwana.
Utulindie, utuokoe, utuhurumie, utuhifazie, ee Mungu, kwa neema yako.
PADRI: Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili, Asiye na doa, Mbarikiwa kushinda, Bibi wetu Mtukufu, Mzazi-Mungu na Bikira daima, pamoja na watakatifu wote, ili sisi kila mmoja mwenywe, na wenzetu wote, hata maisha yetu pia, tujiwekeye mikononi mwa Kristu Mungu.
MSOMAJI: Kwako, ee Bwana.
PADRI: Kwa kuwa utukufu wote, na heshima na usujudu ni haki yako, ya Baba, na ya Mwana na ya Roho Mtakatifu. Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.
*Kisha tunaimba:* «Bwana nimekuita...». *na wimbo sita, hii: Sauti ya ine*

Leo mataifa yote wanaona maajabu katika muji wa Daudi wakati Roho Mtakatifu anashuka kama ndimi za moto kama alivyotuhadisia Mtakatifu Luka: Wafwasi wa Kristu walikusanyika, mara moja kelele ikasikilika toka mbinguni; ni upepo kali, na hii mvumo ikajaa nyumba yote humo walikaa; na wote wakaanza kusema kwa lugha zingine sababu ya kufundisha mafundisho mpya ya Utatu Mtakatifu.*(mara mbili).*

Roho Mtakatifu aliye, aliyekuwa, atakayekuako daima, wasipo mwanzo na mwisho, ni wa asili moja na Baba na Mwana; yeye ni Uzima, Bwana mletaji uzima, nuru na Chemchem ya uzima; yeye ni wema, hazina ya wema; katika yeye Baba amejulikana na Mwana ametukuzwa; anawafunulia wote uwezo moja, umoja, na ibada ileile yaUtatu Mtakatifu.*(mara mbili).*

Roho Mtakatifu, nuru, uzima, maji ya uzima yenye kutiririka kwa siri, Roho wa hekima, wa maarifa wa wema, uhaki, wa akili kubwa yenyi kutakasa zambi; yeye ni Mungu na anatufanya kuwa Mungu; moto yenyi kutirikiza moto, anasema, anatenda na kumwanga vipaji takatifu; katika yeye Manabii wote na Mitume wa Mungu walipokea taji pamoja na Mashahidi: Ni maono ya ajabu, ni muujiza wa ajabu! Moto inawagawanyika sababu ya kugawanya zawadi.*(mara mbili).*

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*Sauti ya sita.*

Mfalme wa mbinguni, Wewe Mfariji. Roho ya ukweli, uliye pahali popote, na kuvijaza vitu vyote, Wewe hazina ya mambo mema, tena Mpaji wa uhai. Njoo kukaa kwetu na kutusafisha kila doa, hata kuziokoa roho zetu, Mwema We.

## MWANGAZA UPOLE (ILARON). . .

**PROKIMENON** *Sauti ya saba*

Ni nani aliye Mungu Mukubwa, kama Mungu wetu, Wewe ni Mungu wa pekee, aliyetenda matendo wa ajabu.
Shairi: Ee Mungu, ulionyesha mataifa yako nguvu yako.
Ni nani aliye Mungu Mkubwa. . .
Shairi: Na nikasema: Sasa mitaanza; Hii ni mageuzo ya Mukono wa Kuume wa Mwenyezi
Ni nani aliye Mungu Mkubwa. . .
Shairi: Nilikumbuka matendo ya Bwana na nilifurahi.

Ni nani aliye Mungu Mkubwa. . .
Shemasi: Tena na tena, tupige magoti, tumuombe Bwana.
*Hii saa waaminifu wote wanapigamagoti chini, padri atapiga magoti katikati yamilango bora, ataangalia kwa watu na ataanza kusoma sala hiyi ifwatayo kwa sauti kubwa na bora:*
PADRI: Bwana Mtakatifu, Msiyemuovu, wa milele, Msiye onekana, Msiye karibika, Mwenyi kusangaza, Imara, Msiye pitiliwa, Msiye kadirika, Mwenyi huruma, wewe peke msiye kufa na unaekaa ku nuru moja isiyokaribika; uliyefanya mbingu na dunia, bahari na vyorte vyenyi kuwamo, wewe unaetuliza ombi mbele yakulifasiria; tunakuomba na tunakusihi, Rabi rafiki yawanadamu, Baba wa Bwana wetu, Mungu na Mwokozi Yesu Kristu: Kwa ajili yasisi wanadamu na kwa ajili ya wokovu wetu alishuka ku mbinguni, alipata mwili kwa roho Mtakatifu na kwa maria, Bikira siku zote tena Mama Mtukufu wa Mungu; mbele alitufundisha kwa masauti zake, kisha alitupa mfano wa kazi: Wakati ilifika mateso yake ya wokovu, alionyesha kwa sisi watumishi wake wanyenyekevu wasiyostahili na wenyi zambi namna gani inafai kuomba pakuinamisha kichwa na pakupiga magoti juu ya zambi za pekee na juu ya zile za taifa. Wewe basi, Bwana wa huruma na rafiki yawanadamu, utusikilize kwa siku ile tunakuomba na hasa siku hiyi ya Pentikosti ambalo Bwana wetu Yesu Kristu, kisha pupanda mbinguni na kisha kukaa ku mukono wa kuume wa Mungu Baba yake, alituma Roho Mtakatifu juu yaWafwasi na Mitume wake; na Roho alikaa juu yakila mmoja wao, na wote walijazwa na neema yake isiyomalizika sababu yakusema maajabu zako mu luga zingine tena nakutoa unabii. Sasa basi, sikiliza uombi wetu na utukumbuke, sisi watumishi wanyenyekevu tunaostahili hukumu; rudisha roho zetu zenyi kufungwa, wewe ambaye mapendo inatuombea sisi, utupokee sisi tunasujudia mbele yako na tunaokulalamikia: Tulitenda zambi! Tuliaminisha kwako tangu kuzaliwa, tangu tumboni, ni wewe Mungu wetu. lakini sawa pumuzisiku zetu zilififia, tuliondolewa egemeo lako, tulitwaliwa kingo lolote. Tena pakuweka matumaini yetu mu wema wako tunalalamika: Usikumbuke zambi za ujana wetu ao za mapotevu zetu, ututakase ku makosa zetu za ficho, usitutupe ku wakati wa uzee, usitwache waakti nguvu yetu itapunguka; utugeuze mbele ya kurudi kwetu ku udongo, utuzungushe na neema na wema. Angalia zambi kadiri ya kipimo cha wema wako, kabilisha bahari ya rehema yakoku wingi wa makosa yetu. Tangu yulu ya makao yako takatifu, Bwana, angalia taifa lako linaloongojea kwako wingi wa huruma yako, utulinde mu wema wako, utuokoe ku nguvu ya uovu, sabitisha uzima wetu kwa sheria zako takatifu. Malaika moja mwaminifu awe mlinzi wa taifa lako; utukusanye sisi wote mu ufalme wako; leta huruma kwa wale wanakutumainia; kwao sawa kwa sisi usamehe zambi lolote; ututakase ku nguvu za Roho wako Mtakatifu, tengua kazi za Adui juu yetu.
*Padri atasoma na hii sala:*
Unatukuzwa, Bwana, Rabi mwenyezi, unayeangaza mchana na mwangaza wa jua tena unayeangaza usiku ku mwangaza wa moto; wewe ulituruhusa kwa kuishi muda wa siku yaleo na kufika ku mwanzo wa usiku sikiliza ombi letu na lile la taifa lako lote; utusamehe makosa yetu ya kutaka na yasiyo kutaka, pokea ombi letu la mangaribi na utume oa urizi wako wingi wa huruma yako na rehema yako. Utulinde na waMalaika wako Watakatifu kama boma, utufunike na ngao la uhaki wako, utuzungushe na ukweli wako; utukinge kwa uwezo wako, utuokoe ku mtego wowote wa fitina ya Adui; mangaribi hiyi na usiku ujayo ziwe kamilifu, takatifu, za furaha na bila zambi, zenyi kusahemewa na kosa na ndoto mbaya, kama masalia ya siku zote za maisha yetu. Tunakuombayo kwa maombezi ya Mama Mtakatifu wa Mungu na ya Watakatifu wote waliokupendeza tangu milele.
SHEMASI: Utulinde, utuokoe, utuhurumie, utuhifazie, ee Mungu kwa neema yako.
PADRI: Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili, Asiye na doa, Mbarikiwa kushinda, Bibi wetu Mtukufu, Mzazi-Mungu na Bikira daima, pamoja na watakatifu wote, ili sisi kila mmoja mwenywe, na wenzetu wote, hata maisha yetu pia, tujiwekeye mikononi mwa Kristu Mungu.
MSOMAJI: Kwako, ee Bwana.
PADRI: Kwani ni kwako kuturehemu na kutuokoeee Kristu Mungu wetu na tunakutukuza Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.
SHEMASI: Tuseme sisi wote, kwa moyo wetu na kwa roho yetu, tuseme.
Bwana Mwenyezi, Mungu wa Mababu, tunakuomba, utusikilize na utuhurumie.
Utuhurumie, ee Mungu, katika huruma yako kubwa, tunakuomba utusikilize na utuhurumie.
Tena tunakuomba kwa ajili ya Waaminifu waorthodoksi wote.

Tena tunakuomba kwa ajili ya Arkiaskofu wetu *(jina lake)*.
Tena tunakuomba kwa ajili ya ndugu zetu, mapadri, Washemasi, watawa na wandugu wote katika Kristu.
Tena tunakuomba kw ajili ya kupata rehema, uzima, amani, afya, wokovu, ulinz, usamehe na ondoleo ya zambi za watumishi wa Mungu, na Waaminifu waorthodoksi ambao wanakaamo na wanakutana katika muji huu (ao Monasteri, Kisanga), waparokia mawakili na wapotani wa hekalu hii takatifu.
Tena tunakuomba kwa ajili ya Watulivu na wenye heri, mashina wa hekalu hii takatifu, kwa ajili ya Baba na ndugu zetu wameofariki ambao wanaolala kwa madini na kwa ajili yawaorthodoksi wanaolala hapa na popote.
Tena tunakuomba kwa ajili ya Wafazili wa hekalu hii takatifu na heshimiwa, kwa ajili ya wapadri, kwa ajili ya wote wanaotumikamo na wanaoimbamo na kwa ajili ya watu wote wanapo hapa ambao wanakuongojea rehema kubwa na nyingi.
Kwa kuwa wewe ndiwe Mungu wa huruma na mpenda wanadamu na tunakutukuza Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.
SHEMASI: Tena na tena tupiga magoti, tumuombe Bwana.
Waimbaji: Bwana hurumia.
PADRI: Bwana Yesu Kristu Mungu wetu, wewe uliyeleta amani kwa wanadamu unasindikiza tena uzima wetu na siku zote unaleta kwa waaminifu zawadi ya Rohgo Mtakatifu juu ya urizi usiyowezwa kutuondolewa; kwa siku yaleo ulituma wazi neema hii kwa Wafwasi na Mitume wako, ukitakasa midomo yao kwa ulimi wa moto; kwa wao, sisi wote wanadamu tulipokea na tulisikia mu luga yetu maarifa ya Mungu, tuliangazwa mu nuru ya Roho na kukumbolewa kugiza za upotevu; bahati kumugawanyo wenyi kuonekana wa ulimi za moto na kwa nguvu ya ajabutulifunda kwa kukusadiki, kwa kukuungamia pamoja na Babana Roho Mtakatifu sawa Umungu moja, uwezo moja, ufalme moja. Wewe basi, kianga ya baba, alama isiyoweza kuharibika tena imara ya aina yake midomo yangu ya zambi, unifundishe namna gani na kwa nini napaswa kuomba. sababu wewe ni yule anaefahamia wingi wa zambi zangu, lakini huruma yako itapita ukubwa wao. Tazama ginsi nasimama mbele yako, mwenyi oga, natoa sikitiko ya roho yangu mu bahari ya mapendo yako. Ongoza uzima wangu, wewe ambaye neno na uwezo wa ajabu wa hekima yako zinaongoza kiumbe chote;kamata sukani ya uzima wangu, wewe badari yafuraha la wasafiri baharini muhatari; ongoza uzima wangu na unijulishe njia ambamo napaswa kutembelea. Leta ku mawazo yangu Roho ya hekima yako, ku ukosefu wangu wa akili Roho ya maarifa yako, ku vitendo vyangu vya bure Roho ya oga wako, badirisha mu moyo wangu Roho yauhaki. Roho bora linda roho yangu maskini! Ili kila siku, nikiongozwa mpaka ku mema kwa Roho wako wa wema, niweze kutimiza amri zako, tena nikumbuke bila kwacha majilio yako tukufu ambako utatezamia vitendo vyangu; usiruhusu niparuziwa ku tamaa za uovu za dunia hiyi, lakini unipe nguvu ya kukaza ku furaha za hazina zijao.

Wewe mwenyewe, ee Rabi, ulisema ya kama chochote kitaombwa mu jina lako kitapewa kwa haraka kuko Mungu na Baba ambaye munagawanya umilele; na mimi, mtenda zambi, kwa siku ya leo ambayo Roho Mtakatifu anashuka naomba wema wako: Unipe yote ninayoomba juu ya wokovu. Ndiyo, Bwana, msanifu wa fazili yote, mu wema wako na ukarimu wako ni wewe unaoleta kwa ziada ile tunaomba. Wewe Mungu wa huruma na unaejaa na mapendo ulipenda kuungana ku hali yetu ya mwili bila kujua zambi, uliinamisha roho yako kwa wale mbele yako wanapiga magoti, na juu ya zambi zetu ulijifanya majaliwa. Wewe basi, ee Rabi, uwape watu wako wingi wa mapendo yako, utusikilize tangu juu yambingu yako takatifu, ututakase kwa uwezo wa mkono wako wa wokovu, utuweke ku kivuli cha mabawa yako, usizarau kazi ya mikono yako. Tulitenda zambi mbele yako, lakini ni wewe peke tunatumikia, hatuweze kusujudia mbele ya mungu mwengine, ao kuinua mukonokwa mungu mwengine. Zima mahalifu zetu, na ukipokea ombi letu la shauri moja kama ubani wa harufu nzuri likipanda mbele ya kiti cha ufalme cha wingi wa wema.
*Kisha padri anaongeza na hii sala:*
Ee Bwana, Bwana, unatuokoa ku mushale unaoruka mchana, utuokoe tena ku tendo lolote linatendeka mu giza. Pokea sadaka ya jioni ya mikono yetu tunaoinua kwako. Tuwe kujaribiwa kwa maovu; utuokoe ku hofu yoyote na ku oga wowote zinazotoa kwa sisi kuiko shetani. Leta ku roho zetu majuto, ku mawazo yetu kumbusho ya majaribu ya amzi ya ajabu na ya haki. Toboa miili na misumari ya oga

wako tena regeza viungo vyetu vyenye kufungwa ku udongo ili mu ukimya wa usingizi tuangazwe kwa ndoto yaamzi zako. Tia mbali na sisi ndoto mbaya lolote na tamaa yote mbaya. Utuamushe saa ya maombi na nguvu mu imani na kuendelea mu njia yaamri zako.
SHEMASI: Utulinde, utuokoe, utuhurumie, utuhifazie, ee Mungu kwa neema yako.
PADRI: Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili, Asiye na doa, Mbarikiwa kushinda, Bibi wetu Mtukufu, Mzazi-Mungu na Bikira daima, pamoja na watakatifu wote, ili sisi kila mmoja mwenywe, na wenzetu wote, hata maisha yetu pia, tujiwekeye mikononi mwa Kristu Mungu.
MSOMAJI: Kwako, ee Bwana.
PADRI: Kwa mapenzi na wema wa Mwana wako wa pekee pamoja naye unatukuzwa tena na Roho Mtakatifu, Mwema na Mpaaji wa uhai, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.
MSOMAJI:

Ee Bwana, utujalie mangaribi hii kutulinda na zambi, umehimidiwa u, ee Mwana na Mungu wa Baba zetu, jina lako limehimidiwa na limetukuzwa milele. Amina. Ee Bwana, huruma yako iwe nasi tunavyokutumaini wewe, Ee Bwana umehimidiwa u, unifundishe zilizo haki zako. Ee Mtakatifu, umehimidiwa u, uniangaze kwa zilizo haki zako. Ee Bwana, huruma yako ni ya milele usitutoangalie sisi, viumbe vya mikono yako. Sifa zakulaiki kukuimbia ni kwako, utukuufu ni wako, wa Baba na Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.
SHEMASI: Tena na tena, tupige magoti, tumuombe Bwana.
WAIMBAJI: Bwana hurumia.
PADRI: Chemchem ya uzima na ya Mwangaza yenyi kuchuruzika bila kwacha, nguvu muumbaji na wa milele pamoja na Baba, wewe unayetimiza kwa ajabu taswira yoyote yaumungu juu ya wokovu wa wafu, ee Kristu Mungu wetu, ulivunja vifungo vya lufu na komeo ya Jehenama kisha kwangusha roho mbaya mingi; wewe ulijitolea kwa ajili yetu mu kafarabila doa, ulitoa mu sadaka mwili wako usiyo na zambi; ambao mu siri hiyi ya ajabu unatupatia uzima wa milele; wewe ambaye ulishuka kuzimuni, ulivunja komeo za milele na ulionyesha njia ya mbinguni kwa wale walikaa mu giza; wewe ambaye hekima ya umungu ilikamata ku ndoani nyama wa ajabu ku shimo, sultani wa uovu, na ulimufunga minyororo mu makao ya giza sana, moto yamilele isiyo zimika na giza za inje ambamo ulimufungia kwa uwezo wako wa milele; Hekima tukufu ya Baba, yegemeo sabiti ya wenyi kuelemea, nuru ya wao wanaokaa mu giza na kivuli cha lufu; wewe, Bwana wa utukufu usiyofifia, Mwana mpenzi wa baba wa Juu, Nuru ya milele yaNuru ya milele, Jua la haki, utusikilize sisi tunaokuomba; leta mapumziko kuroho za watumishi wako, mababu zetu na ndugu wafu, wazazi wetu wengine kadiri ya mwili na wandugu wote muimani ambao tunakumbuka sasa, sababu uko na uwezo pa vitu vyote na unashika mikononi mwako mipaka ya dunia.

Ee Rabi Mwenyezi, Mungu wa mababu zetu, tena bwana wa huruma, Muumba wa wenyi kufana wa wamilele, wa ubinadamu wote unaokuja duniani, kisha unajigawanya , wa uhai na wa lufu, wa makao hapa chini na wa mlango wa ngambo ingine; wewe unayepimiya viumbe wakati wao wa uzima tena unaesabitisha wakati wa lufu, unaeshusha kuzimu na kupandisha, unaefunga kwa uregevu na kufungua kwa nguvu, unaetengeneza kuwako juu yamema yetu na unaeongoza siku zijao kwa ajili yetu, unaefufua kwa matumaini ya ufufuo wale shindano yalufu iliumizwa, wewe mwenyewe, Bwana wa ulimwengu, Mungu na Mwokozi wetu, tumaini lamipaka yadunia na la visiwa vya mbali, wewe ambaye kwa siku hiyi ya mwisho, siku Kuu na mwema yaPentikosti ulitufumbulia siri ya Utatu Mtakatifu,wa aina moja, waumilele moja, usiyogawanyika tena uliyetayarisha kushuka na kuja kwa Roho wako Mtakatifu na Mpaaji wa uhai aliyeenezwa kwa wa Mitume wako mu namna ya ulimi wa moto, uliwafanya watangazaji wa imani yetu takatifu, waungamizi na minadiyamaarifa ya kweli ya Mungu;wewe ambaye kwa siku Kuu hii kubwa na bora ulipenda kupokea maiombi yetu juu yawale wanaozuia motoni, na ulitupatia matumaini kubwa yakuwakomboa wafu kumateso inayowaelemea na furaha yao: Sikiliza maombi yetu japo uregevu wetu na shidaletu; leta ku roho za watumishi wako waliofariki mapumzikomu makao ya nuru, ya ubaridi na ya amani. pa fasi ambapo hapana azabu, sikitiko na malalamiko; weka roho zao mu hema ya wenyi haki, wawe wastahilivu wa amani na wa faraja, kwani haina wafu watakutukuza, ee Bwana, ao wafungwa wa jehenama watakua na ukawa wa kuungama jina lako; lakini sisi wazima, tunakutukuza na tunakusihi, tunakutolea maombi yetu za usimamizi na sadaka za malipo juu ya roho zao.

*Kisha Padri ataongeza na hii sala:*

Mungu wa milele unaejaa na ufalme, Mtakatifu na rafiki yawanadamu, ambaye kwa saa hiyi anatuona tuko wastahilivu wa kuingia mu utukufu wako usiyokaribika juu yakuimba na kusifu maajabu yako, utupe mapenzi kama kwa watumishi wako wasiyostahili, utupe neema ya kukutolea bila mwisho, kwa moyo wa sikitiko, sifa yawimbo Mtakatifu mara tatu na ushukuru juu yamema zako mingi unazotimiza kila wakati kwa ajili yetu. Bwana kumbuka uregevu wetu, usitupoteze juu yazambi zetu, lakini wendeshe mapendo yako kubwa mpaka kushida letu, kusudi tukiacha giza za zambi, tutembee mchana kati wa haki, tena tukivaa silaha za nuru, tutaishi kumakimbilio ya udanganyifu wa Mwovu na mu vitu vyote tukutukuze na matumaini, wewe peke Mungu wa kweli na rafiki yawanadamu. Bwana na Muumba wa ulimwengu; sababu ni kweli siri kubwa ili ukombozi wa viumbe vyako ku wakati ulioainishwa, tena mkusanyo wao juu ya mapumziko ya milele. Juu ya vitu vyote tunakushukuru, juu yakuja kwetu umu duniani na juu ya kwenda kwetu ambako kwa sababu yamaagizo yako ya hakika inayozaa kwa sisi matumaini ya ufufuo na uzima usiyo changana ambao tunatamani kuwa nawp wakati wa kuja kwako kwa pili. Sababu ndiwe Mwongozi wa ufufuo wetru, mwamzi imara na mwema wa wote waliofariki. Rabi na Bwana wa matabisi; ni wewe ulipenda kusharikia kwa urafiki ku mwili wetu na damu yetu, kwa mambo moja ya upendeleo wako kubwa, kumasangao yetu isiyo na kilema mpaka kujitii mwenyewe ku kishawishi, ku alamayamapendo ambayo unatupenda; ambaye kisha kujaribiwa, unakua tegemeo yetu bora mu majaribu na unatukokota mpaka ku hali yako isiyoteseka. Pokea, basi, ee rabi, maombi yetu, leta mapumziko kwa wababa, wamama, ndugu zetu, watoto wetu, wazazi wetu na rafiki, kwa roho zote zilizofariki mbele yetu mu matumaini ya ufufuo na uzima wa milele; andika majina yao mu kitabu cha uhai, uwatie mu kifua cha Abrahamu, Isaaja na cha Yakobo, mu dunia ya wenyi uzima, mu ufalme wa mbingu, mu Paradizo ya furaha, uwapeleke wote mu makao matakatifu kwa msaada wa Wamalaika wa nuru, fufua miili yao ku siku uliyoaini kadiri ya maagano yako takatifu zisipoweza kukosa; sababu juu ya watumishi wako, ee Bwana, hakuna lufu hata kamwe; wakati tunachana na mwili wetu juu ya kukukutanisha, ee Mungu wetu, ni wakati kidogo wa uchungu ku furaha, ku mapumziko, ku raha. Kama tulitenda zambi juu yako, uwe mwema kwetu sawa kwao, sababu mbele yako hakuna wasipo aibu, lakini uzima wake ni wa muda wa siku moja tu, ila wewe peke ambaye duniani ulionekana bila zambi, ee Yesu Kristu Bwana wetu, wote tunatumainia kupokea kwako huruma na maondoleo ya zambi zetu. Joo maana, ee Mungu Mwema na rafiki ya wanadamu, samehe, ondolea, zima makosa yetu yakupenda na yasiyo kupenda, takuoonekana na ya ficho, ilitendewa kwa ufahamu ao kwa ujinga mu kitendo, mu wazo, mu neno, mu mwendo wetu wote na mu kazi zetu; kwa wale waliotutangulia uwape uhodari, maondoleo, kwa sisi wote tuko hapa baraka yako takatifu, kwa sisi na kwa taifa lako, mwisho wa ukimywa na wa furaha, utufungulie moyo wako unaojaa na mapendo kwa ajili yawanadamu ku siku ya kurudi kwako kwa ajabu na kwa oga tena tuwe wastahilivu wa ufalme wako.

*Kisha Padri ataongeza na hii sala:*

Mungu wa mbinguni unaejaa na ufalme, peke yako uko wa milele tena unaekaa mu nuru isiyokadirika, uiumba kiumbo chote na hekima, ulitenga nuru na giza, uliweka Jua juu ya kusimamia muchana, mwezi na nyote juu ya kusimamia usiku; na japo zambi zetu ulituruhusutusimame leo nbele ya sura yako juu ya kutangaza jina lako na kukutolea ibada yetu ya mangaribi. Bwana rafiki ya wanadamu, ongoza wewe peke ombi letu sawa ubani mbele yako na ulipokee sawa manukato ya harufu zuri. Utupe jioni moja na usiku moja wa ukimya; utuvike silaha za nuru; utukomboe ku oga wowote wa usiku na ku hila ya masumbuko mu giza; na usingizi uliyoleta kama mapumziko ku uregevu wetu uwe safi ku sura ya shetani. Ndivyo, ee Bwana na Rabi wa ulimwengu, mgawanyi wa mema yote fanya ili, katika usiku, tukienea na juto la zambi mu usingizi wetu, tukumbuke jina lako takatifu na roho yenyi kwangaza kwa ukumbusho wa amri zako, tuamuke mu furaha juu ya kutukuza wema wako na kutolea ku huruma wako maombi yetu juu ya zambi zetu wenyewe na juu yazile za taifa lako lote ambazo tunakuomba kuichunga mu mapendo yako kwa maombezi yaMama-Mzazi wa Mungu.

SHEMASI: Utulinde, utuokoe, utuhurumie, utuhifazie, ee Mungu kwa neema yako.

PADRI: Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili, Asiye na doa, Mbarikiwa kushinda, Bibi wetu Mtukufu, Mzazi-Mungu na Bikira daima, pamoja na watakatifu wote, ili sisi kila mmoja mwenywe, na wenzetu wote, hata maisha yetu pia, tujiwekeye mikononi mwa Kristu Mungu.
MSOMAJI: Kwako, ee Bwana.
PADRI: Kwa sababu wewe ni Mfalme wa amani na Mwokozi moyo wetu tena tunakutukuza we, Baba, mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.
SHEMASI: Tuumalize ombi wetu wa mangaribi kwa Bwana.
WAIMBAJI: Bwana, hurumia.
SHEMASI: Utulindie, utuokoe, utuhurumie, utuchunge, ee Mungu kwa neema yako.
WAIMBAJI: Bwana hurumia.
SHEMASI: Mangaribi hii kamili iwe timilifu, takatifu, tulivu, yasio zambi, tuombe kwa Bwana.
*Waimbaji wataimba kisha kila ombi:* Utupe, ee Bwana.
SHEMASI: Malaika wa amani, mlinzi wa roho na miili yetu, tuombe kwa Bwana.
SHEMASI: Usamehe na maondoleo ya zambi zetu na ya makosa yetu pia, tuombe kwa Bwana.
SHEMASI: Vilivyo vyema na vifaavyo kwa roho zetu, tena kuwe amani katika dunia, tuombe kwa Bwana.
SHEMASI: Kuyamaliza maisha yetu inabaki, katika amani na toba, tuombe kwa Bwana. .
SHEMASI: Tuombe ili mwisho wa maisha yetu uwe kiKristu, kwa amani, bila aibu, tena tuone mufano mzuri mbele ya kiti cha hukumu cha Kristu.
SHEMASI: Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili, asiye na doa, mbarikiwa kushinda Malkia wetu mtukufu. Mzazi-Mungu na Bikira daima, pamoja na watakatifu wote, ili sisi kila mmoja mwenyewe na wenzetu wote, hata maisha yetu pia, tujiweke mikononi mwa Kristu Mungu.
WAIMBAJI: Kwako, ee Bwana.
PADRI: Kwa kuwa u Mungu mwema na mpenda wanadamu, na kwako tunautoa utukufu kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.
PADRI: Amani kwa wote.
WAIMBAJI: Na kwa roho yako.
PADRI: Tuinamishe vichwa vyetu kwa Bwana.
WAIMBAJI: Kwako, ee Bwana.
*Sala ya kuinamisha nayo kichwa kwa sauti ya chini:*
PADRI: Ee Bwana Mungu wetu uliyeinamisha mbingu na ukashuka kwa ajili ya wokovu wa binadamu, uwatazamie watumishi wako na uriti wako kwa sababu wewe u Kuhani Mshindaji na rafiki wa watu. Usiyeongoja masaidio ya watu, kwa kuwa wao wamewazia huruma yako na kutumaini ukombozi wako, uwachunge mangaribi na usiku huu hata na wakati wowote kwa maadui, na kwa vitendo vidogo vya Shetani asiye na mafaa ya akili na mwenye mawazo mabaya.
*Padri anapaza sauti.*
PADRI: Kwa kuwa uwezo wa ufalme wako uhimidiwe na utukuzwe Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

**APOSTIKHA** *Sauti ya tatu. Idiomelon.*

Sasa luga zinakua sawa alama ya agizo yawote, sababu taifa ambako Kristu alitoka kadiri yamwili juu ya ukosefu wa imani linapoteza uhaki wa neema yaMungu, wakati sisi wenyi mapenzi, tunarizi mwangaza wa Mungu, tunahakikishwa kwa masauti yaMitume yaKristu tukitangaza utukufu wa Mungu na mfazili wa ulimwengu; tukiinamisha pamoja nao moyo wetu na tukipiga magoti, tunasabitishwa mu imani kwa Roho Mtakatifu, tunasujudia mbele ya Mwokozi wa roho zetu.

Shairi:Umba moyo safi ndani yangu, ee Mungu, na ufanye upya roho nzuri ndani yangu.

Sasa Roho Mfariji anaenea pa mwili wote; pakwanzia pa kundi la waimbaji la wa Mitume, anaeneza neema kwa mwaaminifu wote; anahakikisha ukweli wa kuja kwake kwa enzi pakuleta kwa Wanafunzi ulimi wa moto juu ya sifa na utukufu wa Mungu; na mu mwangaza wa kiroho unayoangazia mioyo yetu, tukipata nguvu mu imani kwa Roho Mtakatifu tunamuomba wokovu juu yaroho zetu.

Shairi: Usinitenge na uso wako, wala usiondolee Roho yako mutakatifu.

Sasa Mitume yaKristu wanavaa nguvu yaJuu, sababu Roho Mtakatifu anatolea hekalu la moyo wao, anafungua kuwako kwake kwa upya wa siri kwa maarifa ya luga za kigeni wataenda kutangaza juu ya kutufundisha namna ya kutukuza Utatu Mtakatifu, Mfazili wa milele wa ulimwengu; ku mwangaza wa mafundisho yao, tusujudie mbele ya Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, tukimuomba wokovuwa roho zetu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya mnane.*

Kujeni ninyi mataifa yote,tumushukuru Mungu moja mu Utatu Mtakatifu: Mwana kwa Baba pamoja na Roho Mtakatifu; sababu baba anazaa Mwana inje ya wakati, wanagawanya kiti moja na umilele moja,Roho Mtakatifu ni ndani mwa Baba, anatukuzwa pamoja na mwana: Uwezo moja, umungu moja, hali moja ambaye mbele yao sisi wote waaminifu tunasujudu tunasema: Mungu Mtakatifu aliyeumba vyote kwa Mwana pamoja na msaada wa Roho Mtaaktifu; Mweza Mtaaktifu na muhodari ambaye Baba alitufumbulia, na kwa ajili yake Roho Mtakatifu alikuja umu duniani; Msiye kufa Mtakatifu, Roho Mfariji anaetoka kwa Baba naanakaa muko Mwana: Utatu Mtakatifu, utukufu kwako.

PADRI: Sasa Bwana umuache mtumishi wako aende na amani, vile ulivyosema kwa maana macho yangu yameona wokovu wako uliyoutayarisha mbele ya makabila yote, mwanga wa kwangazia mataifa na sifa ya kundi lako Israeli.

MSOMAJI: Amina. Mungu Mtakatifu, Mweza Mtakatifu, Msiye kufa Mtakatifu, utuhurumie. *(mara tatu).* Utukufu Kwa Baba.… Sasa na siku.... Utatu Mtakatifu kamili utuhurumie, Bwana utusamehe zambi zetu, Rabi utuondolee makosa yetu, Mtakatifu utukaribie ukatuponye magonjwa yetu. Bwana hurumia, Bwana hurumia, Bwana hurumia.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku. . .

Baba yetu uliye mbinguni, jina lako litukuzwe, ufalme wako uje, mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama mbinguni, utupe leo chakula chetu cha kila siku, utusamehe makosa yetu kama sisi vilevile nasi tunawasamehe waliotukosea, tena tusishindwe na vishawishi, lakini utuokoe na yule mwovu.

PADRI: Kwa kuwa ufalme na uwezo, na utukufu ni wako, wa Baba, na wa Mwana na wa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote hata milele na milele. Amina.

**Apolitikion ya Siku Kuu** *(mara tatu.).*

PADRI: Hekima.

WAIMBAJI: Himidi.

PADRI: Aliye ahimidiwe, Kristu Mungu wetu daima, sasa na siku zote, hata milele na milele.

MSOMAJI: Amina. Bwana Mungu aimarishe imani takatifu, isiyo na lawama ya waKristu Watawa waorthodoksi katika mji na inchi hii milele na milele. Amina.

PADRI: Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe.

MSOMAJI: Uliye wa thamani kuwashinda wakheruvi, uliye na utukufu kuwapita bila kiasi Waserafi, uliye ukimzaa Mungu Neno umebaki bila kukuharibu, uliye Mzazi-Mungu kweli, tunakutukuza we.

PADRI: Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

MSOMAJI: Utukufu kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina. Bwana hurumia*(mara tatu).* Ee Rabi Mtakatifu bariki.

**Kuaga**

Padri: Yeye ambaye, katika kifua cha Mungu Baba, akajinyenyekeza, akashuka toka mbinguni hata duniani, akashuka hali yetu na akaifanya kuwa Mungu; yeye aliyepanda mbinguni na kukaa kuume kwa Mungu Baba aliyewatumia Wafwasi Mitume Wake Watakatifu Roho wa Mungu, Mtakatifu, wa asili moja na Baba, sawasawa naye kwa uwezo na utukufu na wa milele; yeye aliyewaangazia hivyo Nayo, na katika wao, ulimwengu wote, Kristu, Mungu wetu kweli, kwa maombi ya Mama yake asiye na doa, mtakatifu kamili, ya Mitume Watakatifu, watukufu na wasifiwa, wahubiri kimungu na wenye Roho Mtakatifu, na ya watakatifu wote, atuhurumie na atuokoe, kwani Yeye ni Mwema na Mpenda-Wanadamu.

# MU KAZI MOJA ASUBUI KISHA PENTIKOSTI

*Kisha Eksapsalmos, Bwana ndiwe...Apolitikion ya Siku kuu mara tatu, bila kusema katikati Utukufu kwa Baba...sasa na siku zote...*

**KATHISMA YA KWANZA** *Sauti ya ine. Kateplagi Iosif.*

Ninyi waaminifu, kwa hii siku Kuu ya ukamilifu, tushangilie na furaha Pentikosti huko inatimizika ya Kristu: Kwani leo moto ya Roho Mtakatifu kwa mfano wa ndimi za moto inashuka duniani na Wafwasi wanapoangazwa wanafundishwa kwa mafumbo ya mbinguni: Tazama, nuru ya Roho Mtakatifu inangaa duniani.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*(mara mbili).*

**KATHISMA YA MBILI. UMOJA.**

Chemchem ya Roho Mtakatifu ilishukia wanadamu kwa ndimi za moto, juu ya Mitume waliangazwa kwa umande wa roho: Wingu iliwashukia ikawamwangia moto, moto yanuru na ya baridi nzuri; katika wao tumepewa neema kwa moto na kwa maji: Tazama, nuru ya Roho Mtakatifu inangaa ulimwangu duniani.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*(mara mbili).*

*Zaburi 50 (51), Kanuni ya Siku Kuu. Kisha Wimbo ya tatu Kathisma.*

**KATHISMA** *Sauti ya mnane. Tin sofian ke Logon.*

Roho mtakatifu kamili anawashukia leo Mitume kama ndimi za moto, anashangaza mataifa yote: kama walivyosema lugha zao kila mutu aliwasikia wakisema lugha yake; hii muujiza ilioneka kwa wasioamini kuwa ulevi, lakini waaminifu walitambua wokovu; ndio maana tunatukuza uwezo wako, ee Kristu Mungu wetu, na tunakuomba, sisi watumishi wako, utuondolee zambi zetu nyingi.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*(mara mbili).*

**KONTAKION**

Alipochanganya lugha za ulimwengu, Bwana wa juu mbinguni akasambaza mataifa; lakini alipogawanya ndimi za moto, anawalika watu wote ku umoja na wote pamoja tunamutukuza Roho Mtakatifu kamili.

**IKOS**

Ee Yesu, tuliza imara sisi watumishi wako katika huzuni humo munapatikana akili yetu; usiache roho zetu katika sikitiko; usijitenge mbali ya mioyo yetu yenye kujaribiwa, lakini tangulia kutuonyesha. Kuja karibu yetu, ee Bwana, uliye popote; kwa wale wenye kukupenda ungana nao kwa wema wako kama ulivyowafanyia Mitume wako siku zote; kusudi tukiungana na Wewe tuweze kuimbia na kutukuza Roho wako Mtakatifu kamili.

**SINAKSARI YA WATAKATIFU WA LEO. Kisha:**

Leo, Siku ya kwanza ya Pentikosti, tunashangilia Roho Mtakatifu kamili, mwenyi kuleta uzima na mwenyezi, Mumoja wa Utatu Mtakatifu, Mungu mwenyi sifa sawa asili moja na utukufu sawa pamoja na Baba na Mwana.

Shairi: Kila mwenye pumzi amsifu Roho ya Bwana, ambaye katika Yeye pepo wachafu wote wamefukuzwa.

Kwa maombezi ya Mitume wako, ee Kristu Mungu wetu, utuhurumie. Amina.

**EKSAPOSTILARION.** *Sauti ya tatu. O Uranon tis astris.*

Ee Roho Mtakatifu mwenyi kutoka kwa Baba na kuwashukia Wafwasi wasiojua kusoma na kuandika katika Mwana, okoa na takasa wote wale wenyi kukutambua kama Mungu.

**Ingine Umoja**

Nuru ni Baba, nuru ni Neno, nuru pia ni Roho Mtakatifu aliyetumwa juu ya Mitume kama ndimi za moto na katika Yeye dunia yote inapokea kwa ubatizo nuru sababu ya kuabudu Utatu Mtakatifu.

## MASIFU *Sauti ya mbili.*

Ee Mwokozi, katika manabii ulitutangazia njia ya wokovu, ndani yaMitume wako muliangaa neema ya Roho wako Mtakatifu, kwa sababu mbele yanyakati ulikuwa Mungu, kisha wao ulikuwa Mungu, na uko Mungu milele. *(mara mbili).*

Ee Mwokozi wa dunia, katika uwanja wako nitaimba na kupiga goti, mbele yauwezo wako wa ushindi nitasujudu mangaribi, asubui na jua kati; na nitakutukuza daima, ee Bwana.

Ee Bwana, katika uwanja wako sisi waaminifu tunapopiga magoti ya roho zetu na ya miili yetu, tunakuimbia, ee Baba wa milele, pamoja na Mwana wako na Roho Mtakatifu kamili ambao unapotawala nao milele, angaza roho zetu na kuzitakasa.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*Sauti ya mnane.*

Luga zilizochanganyika zamani sababu yaujasiri wa wajengaji sasa zimejaa na hekima kwa maarifa tukufu ya Mungu; zamani Bwana alihukumu makafiri sababu yazambi yao, sasa Kristu anangaza wavuvi katika Roho Mtakatifu; zamani mugawanyiko wa luga ilifanyika katika azabu: Sasa mapatano inafanyika kati yao kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

**DOKSOLOGIA KUBWA**

***Mu Ibada ya Liturgia Kimungu tunaimba yoyote, sawa jana .***

# MU KAZI MOJA MANGARIBI KISHA PENTIKOSTI

*Kisha: «Bwana nimekuita...» tunaimba wimbo sita. tatu ya Siku Kuu na tatu ya Mineon.*

***Wimbo ya Siku Kuu:***

*Sauti ya kwanza. Ton uranion tagmaton.*

Sasa luga zinakuwa mupya sababu ya kusema waziwazi maajabu yaMungu kwa maneno yakugeni kama ndimi za moto ni sababu ya kusabitisha imani ulimwenduni kote, na kama alama imeonekana wokovu wa watu wote.

Ee Kristu, unapotimiza ahadi yako na kuwatumia Mitume wako nguvu yajuu mbinguni, unawatumia Roho Mtakatifu, ukituonyesha ya kama Wewe ni Ukweli, na wale wenye kutumainia wema wako hawatapata haya.

Ulipotimiza ahadi yako, ulituma Roho Mtakatifu duniani kama ndimi za moto sababu ya kuyeyusha kwa moto yaMungu zambi za ulimwengu na kuleta ushirika wa Roho Mtakatifu kwa waaminifu wenyi kumutambua kama Mungu.

***Wimbo tatu ya Mineon.***

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*Sauti ya kwanza.*

Tushangilie Pentikosti na kushuka kwa Roho Mtakaitfu; katika hii ahadi imekamilika, matumaini imetimizika. Ni fumbo heshimiwa na yenyi kujaa na utukufu! Ndio maana tunakulalamikia: Ee Muumba wa ulimwengu na Bwana utukufu kwako.

**APOSTIKHA** *Sauti ya mbili. Ikos tu Efratha.*

Ee Neno, kweli kwa ahadi yako uliwatumia Wafwasi Roho wako Mtakatifu, na uliwaangazia kwa nuru yake.

Shairi:Umba moyo safi ndani yangu, ee Mungu, na ufanye upya roho nzuri ndani yangu.

Kwa rafla nguvu ya Roho Mtakatifu tokas mbinguni ikawashukia Mitume ikawapa hekima na uwezo wa kufundisha maarifa yaMungu.

Shairi: Usinitenge na uso wako, wala usiondolee Roho yako mutakatifu.

wageni walishangaa wakati walisikia Mitume Watakatifu wakisema katika lugha zao sababu ya kutukuza Utatu Mtakatifu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*Sauti ya kwanza.*

Ee Bwana, uligeuza Wafwasi wako kusema luga za mataifa kusudi kwa hizi luga wakutangaze kama Mungu na Neno msiyekufa mwenye kuleta neema ya wokovu rohoni mwetu.

***Apolitikion ya Siku Kuu (mara tatu).***

# MU KAZI MBILI ASUBUI KISHA PENTIKOSTI

*Kisha Eksapsalmos, Bwana ndiwe...Apolitikion ya Siku kuu mara tatu, bila kusema katikati Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*

**KATHISMA YA KWANZA** *Sauti ya kwanza. Ton tafon su Sotir.*

Naimbia, natukuza Roho Mtakatifu kama Baba na mwana, umoja wa Mungu katika halizao; Roho Mtakatifu aliyewajaza Mitume wa Kristu aliwapa maarifa kufundisha dunia yote.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*(mara mbili).*

**KATHISMA YA MBILI.** *Umoja.*

Neema ya Roho Mtakatifu ilishuka kwa ajabu toka mbinguni kama ndimi za moto ikawangazia wafwasi wa kristu, ikawageuza kuwa nyote za nuru sababu ya kutangaza katika Utatu Mtakatifu uwezo moja na ubwana moja tunatukuza katika imani.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*(mara mbili).*

***Kanuni. Kontakion , Ikos, Eksapostilarion ya Siku Kuu.***

**APOSTIKHA.** *Sauti ya mbili. Ikos tu efratha*.

Ee Bwana, Wafwasi wako waliangazwa rohoni mwao kwa nuru taaktifu na walipokea chakula cha Roho Mtakatifu.

Shairi:Umba moyo safi ndani yangu, ee Mungu, na ufanye upya roho nzuri ndani yangu.

Toka mbingu ndimi kama moto zilionekana zimewashukia Mitume, zikagawanyika juu ya kila mumoja wao na kuwangazia bil;a kuteketezwa.

Shairi: Usinitenge na uso wako, wala usiondolee Roho yako mutakatifu.

Ee Mfariji, utushukia toka mbinguni kama ulivyowashukia Mitume zamani, takasa na okoa wale wenyi kukutangaza kama Mungu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*Sauti ya kwanza*.

Neema yote inatoka kwa Roho Mtakatifu: Yeye ni Chemchem ya unabii, anafundisha mapadri na kuleta hekima kwa wasiyojua kusoma na kuandika, anageuza wavuvi kuwa wenyi kujua elimu yaMungu na anasabitisha Eklezya yote yenyi kukusanyika. Ee Roho Mtakatifu wa asili moja na Baba na Mwana na mwenyi kutambua pamoja nao, ee Bwana, utukufu kwako.

# MU KAZI MBILI MANGARIBI KISHA PENTIKOSTI

*Kisha: «Bwana nimekuita...» tunaimba wimbo sita. tatu ya Siku Kuu na tatu ya Mineon.*

*Wimbo ya Siku Kuu:*

*Sauti ya kwanza. Ton uranion tagmaton.*

Ni desturi kwa mbingu kuwatangazia mataifa, katika ndimi za moto, utukufu wa Mungu uliyopamba mbingu kwa moto nyingi na kuangazia ulimwengu katika mwana na Roho!

Kwa ahadi, na kama ndimi za moto, Roho Mtakatifu alikaa juu ya Wafwasi wa kristu waliokusanyika katika Sayuni, akawageuza kuwa watangazaji wa nuru waliotangaza, kwa mafunuo ya siri, mafundisho ya Utatu Mtakatifu.

Panga zenye kufua kwa mbingu. Wafwasi wakawa hivi kwa kuja kwa Roho Mtakatifu sababu yakutolea inchi kwa Muumba, sababu ya kuangusha makafiri, sababu yakuharibu nguvu ya shetani na kuleta wokovu rohoni mwetu.

***Wimbo tatu ya Mineon.***

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*Sauti ya mbili.*

Tumeona nuru ya kweli, tumepokea Roho wa mbinguni, tumepata imani ya kweli, tukiusujudu Utatu usiotengwa; kwani Huu umetuokoa.

**APOSTIKHA.** *Sauti ya ine. Edokas simiosin.*

Leo nguvu ya Roho Mtakatifu anashukia Mitume wako, ee Bwana, na inawajaza ma mafundisho yako ya heri kwa kuwapa hekima kwa maarifa ya Mungu; ndio maana kwa shukrani tunatukuza tendo lako la wokovu, ee Bwana mwenyezi na Mwokozi wa roho zetu.

Shairi:Umba moyo safi ndani yangu, ee Mungu, na ufanye upya roho nzuri ndani yangu.

Leo Roho mwenyezi wa asili moja na wewe anashuka toka kwa Baba kama ndimi za moto na anatayarisha Mitume wako kutangza maajabu yako, ee Bwana; ndio maana kwa shukrani tunatukuza tendo lako la wokovu, ee Bwana mwenyezi na mwokozi wa roho zetu.

Shairi: Usinitenge na uso wako, wala usiondolee Roho yako mutakatifu.

Ee Mwokozi, leo unagawanyia mwanadamu wote vipaji vya Roho wako Mfariji, unamupa kuagua kama Wewe mwenyewe, ee Neno, ulivyosema na unamufundisha kuabudu Utatu usiyotengana; ndio maana kwa shukrani tunatukuza tendo lako la wokovu, ee Bwana mwenyezi na Mwokozi wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*Sauti ya mbili.*

Ee Mwokozi, katika manabii ulitutangazia njia ya wokovu, ndani yaMitume wako muliangaa neema ya Roho wako Mtakatifu, kwa sababu mbele yanyakati ulikuwa Mungu, kisha wao ulikuwa Mungu, na uko Mungu milele.

# MU KAZI TATU ASUBUI KISHA PENTIKOSTI

*Kisha Eksapsalmos, Bwana ndiwe...Apolitikion ya Siku kuu mara tatu, bila kusema katikati Utukufu kwa Baba...sasa na siku zote...*

**KATHISMA YA KWANZA**. *Sauti ya inne. Takhi prokataleve.*

Ee Kristu, kwa ahadi yako Roho Mtakatifu aliwashukia Mitume, alipatanisha lugha nyingi sababu ya kukiri imani moja katika Utatu wa milele; na kwa sisi pia, ee Bwana, tunakuomba kuja ukae kwetu, maana wewe ni Mwema tena Mpenda-wanadamu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*(mara mbili).*

**KATHISMA YA MBILI** *Sauti ya mnane. Tin sofian ke Logon.*

Roho mtakatifu kamili anawashukia leo Mitume kama ndimi za moto, anashangaza mataifa yote: kama walivyosema lugha zao kila mutu aliwasikia wakisema lugha yake; hii muujiza ilioneka kwa wasioamini kuwa ulevi, lakini waaminifu walitambua wokovu; ndio maana tunatukuza uwezo wako, ee Kristu Mungu wetu, na tunakuomba, sisi watumishi wako, utuondolee zambi zetu nyingi.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*(mara mbili).*

***Kanuni. Kontakion , Ikos, Eksapostilarion ya Siku Kuu.***

**APOSTIKHA.** *Sauti ya sita. Triimeros anestis.*

Roho Mtakatifu kamili nuru toka nuru alikuja duniani kama ndimi za moto sababu ya kuchoma zambi za wale wenyi kuabudu na imani Mungu mumoja katika watu tatu.

Shairi:Umba moyo safi ndani yangu, ee Mungu, na ufanye upya roho nzuri ndani yangu.

Ee Mungu, weka mioyoni mwetu Roho wako Mtakatifu kamili yule ulitumia Mitume wako zamani, ukawapa nguvu ya kutimiza duniani, ee Mungu wa mapendo, tendo lako la wokovu.

Shairi: Usinitenge na uso wako, wala usiondolee Roho yako mutakatifu.

Enyi Waaminifu, tutambueni Roho Mtakatifu kama Mungu tukisema: «usijitenge na sisi, ee Mfariji, wewe mwenye kuwapa watu wote wokovu na kutakasa wale wenye kukuimbia».

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*Sauti ya mbili.*

Ee Mwokozi wa dunia, katika uwanja wako nitaimba na kupiga goti, mbele ya uwezo wako wa ushindi nitasujudu mangaribi, asubui na jua kati; na nitakutukuza daima, ee Bwana.

*Apolitikion ya Siku Kuu (mara tatu).*

# MU KAZI TATU MANGARIBI KISHA PENTIKOSTI.

*Kisha: «Bwana nimekuita...» tunaimba wimbo sita. tatu ya Siku Kuu na tatu ya Mineon. Wimbo ya Siku Kuu:*

*Sauti ya kwanza. Ton uranion tagmaton.*

Mulimani Musa aliangalia katika moto Huyu aliye; sasa Roho Mtakatifu kama moto anashukia Mitume walioona Bwana sababu ya kuonyesha waziwazi ya kama niMungu Yule aliyesema zamani na leo.

Kwa ndimi za moto wale wanasema juu ya Mungu wakialika mataifa kwa Ubatizo takatifu wakateketeza kwa moto ya Roho Mtakatifu midomo ya makafiri; na wewe, Mfariji, angaza pia watumishi wako wenye kukutambua kama Mungu.

Ee Bwana, wale wenyi kukutumikia katika hii mwili ulitwaa, Roho wako Mtakatifu awafanya kuwa wapya kwa moto yake kama ulivyowafanyia malaika wako wabila-mwili; kwa matendo yako nyingi unastahili mastajabu!

***Kisha wimbo tatu ya Mineon.***

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*Sauti ya mbili.*

Ee Bwana, katika uwanja wako sisi waaminifu tunapopiga magoti ya roho zetu na ya miili yetu, tunakuimbia, ee Baba wa milele, pamoja na Mwana wako na Roho Mtakatifu kamili ambao unapotawala nao milele, angaza roho zetu na kuzitakasa.

**APOSTIKHA.** *Sauti ya ine. Os geneon en Martisin.*

Roho Mtakatifu anatawala pamoja na baba na Neno, hali moja na utawala moja milele, ukubwa moja, uwezo moja, na utukufu moja: Ni yeye mwenye kujaza Wafwasi wa kristu na hekima kusudi kwa lugha nyingi neno lao liweza kutangaza maajabu ya Mungu na mafundisho ya Utatu Mtakatifu.

Shairi:Umba moyo safi ndani yangu, ee Mungu, na ufanye upya roho nzuri ndani yangu.

Ee Bwana, watu wengi wenye kupofushwa kwa kutokuwa na elimu wakawastaki kuwa walevi wale ulifundisha waakti kwa lugha nyingi na kwa Roho walitukuza mafunuo mengi ya Mungu na kufukuza ulevi wa udanganyifu; lakini sisi tuliyokutambua katika wao tunakutangaza na furaha ya wokovu kama Mungu wetu.

Shairi: Usinitenge na uso wako, wala usiondolee Roho yako mutakatifu.

Ewe Chemchem yamilele isiyokauka ambako inatiririka mto yawema isiyokwisha, wewe mwenye kutirikiza daima maji ya uzima ya wokovu, osha roho yangu kwa maji yako, zimisha ndani yangu moto ya tamaa, makaa ya vishawishi kali na moto ya azabu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*Sauti ya mbili.*

Tuimbieni Baba. Mwana na Roho Mtakatifu, Utatu wa asili moja, kwani ni hivi waliitangaza manabii wa nyakati zote, Mitume na Mashahidi watakatifu.

*Apolitikion ya Siku Kuu (mara tatu).*

# MU KAZI INE ASUBUI KISHA PENTIKOSTI

*Kisha Eksapsalmos, Bwana ndiwe...Apolitikion ya Siku kuu mara tatu, bila kusema katikati Utukufu kwa Baba...sasa na siku zote...*

**KATHISMA YA KWANZA.** *Sauti ya kwanza. Ton tafon su Sotir.*

Tazama, maneno ya Manabii ya metimia, kwa sababu huyu alifunua kwa mifano siku za mbele anamwanga sasa, kama Mungu Roho Mtakatifu, nuru yake kamili juu ya Mitume na hata katika wao, juu ya wale wenyi kuabudu na imani Utatu Mtakatifu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*(mara mbili).*

**KATHISMA YA MBILI.** *Sauti ya tano. Ton Sinanarkhon Logon.*

Ee Mwokozi, Roho Mtakaitfu ambaye nuru iliyawajaza Mitume wako ikawafanya kuwa taa sababu ya kufukuza giza ya udanganyifu duniani na kuangazia roho za waaminifu kusudi wamuabudu baba na Roho Mtakatifu mwenyi kutakasa wote wale wenyi kusujudu yako.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*(mara mbili).*

***Kanuni. Kontakion , Ikos, Eksapostilarion ya Siku Kuu.***

**APOSTIKHA.** *Sauti ya ine. Os geneon en martisin.*

Kushuka kwa Roho Mtakatifu kulionekana katika ndimi za moto iliangaza Mitume na kuwafanya kuwa wasemaji wa kutangazia wote umoja wa kweli na usiyotengana wa Utatu Mtakatifu: Walipoona hivi, watu wa dunia wakashangaa mbele yaMitume ambao zamani hawakujua kusoma na kuandika walitangaza waziwazi mafumbo isiyokadirika.

Shairi:Umba moyo safi ndani yangu, ee Mungu, na ufanye upya roho nzuri ndani yangu.

Walipokaa katika chumba cha juu, Mitume walipokea nguvu ya Roho Mtakatifu aliyekuja kama upepo kali kwa mfano wa ndimi za moto na wakafundisha waziwazi mafundisho yao katika luga mbalimbali, wakahakikisha neno la ukweli: Kristu aliyeteswa kwa kutaka kwake yeye ni Mungu kweli.

Shairi: Usinitenge na uso wako, wala usiondolee Roho yako mutakatifu.

Ee Bwana, kama ulivyowatumia Mitume wako lao neema takatifu ya Roho Mtakatifu, utupe na sisi pia sasa ili nuru ya kuja kwake ingae daima moyoni mwetu, ili wote pamoja tuimbie kwa sauti moja Utatu usiyogawanyika.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*Sauti ya mbili.*

Ee Mwokozi, katika manabii ulitutangazia njia ya wokovu, ndani yaMitume wako muliangaa neema ya Roho wako Mtakatifu, kwa sababu mbele yanyakati ulikuwa Mungu, kisha wao ulikuwa Mungu, na uko Mungu milele.

# MU KAZI INE MANGARIBI KISHA PENTIKOSTI

*Kisha: «Bwana nimekuita...» tunaimba wimbo sita. tatu ya Siku Kuu na tatu ya Mineon.*
*Wimbo ya Siku Kuu:*

*Sauti ya ine. Edokas simiosin.*

Roho Mtakatifu kamili mwenyi kugawanya vipaji takatifu ameonekana duniani, lakini apana kama zamani alipoangaa ndani ya Manabii chini ya kivuli cha Sheria: Sasa tumepewa hali yake yote kwa msaada wa kristu; ndio maana tutakaseni mioyo yetu na tuipambe na fazila, tupokeeni kunakwake na nuru yake ya siri.

Ee Mpenda-wanadamu, usituondolee Roho Mtakatifu kamili, lakini leta neema yako ili roho zetu na mioyo yetu yakustahili na kwa uriti tupewe ushirika wako sababu yakuwa hekalu na makao ya Roho Mtakatifu, ee Yesu Mungu wetu naMwokozi wa roho zetu.

Tunaimbia na ibada Roho Mtakatifu kamili mwenyi kutakasa ulimwengu, na kwa imani tumulalamikia: Wewe ambaye kwa neema ya Baba ulikuja duniani humu, usijitenge mbali na sisi wenye kutukuza umungu wako, utufanye kuwa hekalu ya wema wako isiyokadirika na takasa waaminifu wote wenyi kukuimbia.

***Kisha wimbo tatu ya Mineon.***

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*Sauti ya saba.*

Kama tulivyokuwa na Kristu Mungu wetu sawa msimamizi wetu kwa Baba, alipokuja duniani, leo ametupa sisi Mfariji mwingine: Roho wa ukweli tunayeabudu katika imani.

**APOSTIKHA.** *Sauti ya kwanza. Panefimi martires.*

Roho Mtakatifu anayetoka kwa Baba nakutukuzwa katika Mwana, mwenyi kuchukua na kuongoza dunia yote kwa kuipatia uzima, maisha na wokovu, tumuimbieni kama Mungu wetu, enyi waaminifu: Ee Roho Mfariji, leta amani duniani.

Shairi:Umba moyo safi ndani yangu, ee Mungu, na ufanye upya roho nzuri ndani yangu.

Ee Chemchem yamema yote, Roho Mtakaitfu alikuja katika Mitume wa Kristu kujaza mipaka yote yadunia na nguvu yaMungu na wema wa mbinguni; ndio maana tumulalamikieni: EeRoho Mfariji, leta amani duniani.

Shairi: Usinitenge na uso wako, wala usiondolee Roho yako mutakatifu.

Roho Mtakatifu amejifunua kama Mungu wa asili moja na Baba na mwana na anatawala pamoja nao mbinguni, nuru kamili toka Nuru, anayetoka kwa baba katika Mwana bila mwanzo; ndio maana tunakulalamikia: ee Roho Mfariji, leta amani duniani.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya mnane*.

Ee Bwana, wakati uliwatumia Mitume wako Roho Mtakatifu, wana wa Israeli walipoona hii muujiza, wakashikwa na woga; wakawasikia wakisema luga zingine kadiri Roho Mtakatifu aliwapa kusema; walijazwa na hekima; katika nyavu zao wakavua mataifa, wakawaongoza kwa imani na kuwaonyesha mafumbo takatifu; ndio maana sisi pia tunakuimbia: «Wewe uliyeonekana duniani na kutuokoa toka udanganyifu, ee Bwana, utukufu kwako».

**Apolitikion ya Siku Kuu** *(mara tatu).*

## MU KAZI TANO ASUBUI KISHA PENTIKOSTI

*Kisha Eksapsalmos, Bwana ndiwe...Apolitikion ya Siku kuu mara tatu, bila kusema katikati Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*

**KATHISMA YA KWANZA** *Sauti ya mnane. To prostakthen.*

Ee Kristu, kisha Ufufuo wako kaburini na kupanda kwako juu mbinguni ulishusha utukufu wako juu ya Washuhuda wa umungu wako na uliweka Roho mpya wa haki ndani yamoyo wa Wafwasi wako; ndio maana, ee Mwokozi, walifundisha mafundisho yako na matendo yako ya wokovu kama kinubi chenyi masauti mazuri ya kimungu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*(mara mbili).*

**KATHISMA YA MBILI** *Sauti ya mnane. To prostakthen.*

Marafiki za Mwokozi walijazwa na furaha na wakapata moyo, wao ambao kwa mwanzo waliogopa, lakini leo ameshuka toka mbinguni Roho Mtakaitfu na anakaa juu ya Mitume; kila mutu aliwasikia wakisema kwa luga yake, kwa sababu amewagawanyia ndimi za moto ambazo haziwezi kuwateketeza, lakini kuwafunika umande.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote....*(mara mbili).*

Zaburi 50 (51).

Elezo*: Kanuni ya Siku Kuu na Mineon. Kontakion na Eksapostilarion ya Siku Kuu.*

**APOSTIKHA** *Sauti ya kwanza.Ton uranion tagmaton.*

Huyu aliyechukuliwa zamani na utukufu juu ya gari yamoto, Nabii mwenyi kujaa na bidii na moyo alitangulia kuonyesha kuja kwa Roho Mtakatifu anayewashukia Mitume lao toka mbinguni katika muji wa sayuni kusudi waangazie dunia yote.

Shairi:Umba moyo safi ndani yangu, ee Mungu, na ufanye upya roho nzuri ndani yangu.

Kwa ndimi za moto Mitume wote walipotangaza kiasi yakristu wakangazia kataifa kusudi wamuabudu na ibada Mungu mmoja katika watu tatu: Baba, Mwana, naRoho Mtakatifu.

Shairi: Usinitenge na uso wako, wala usiondolee Roho yako mutakatifu.

Salamu, ee Sayuni, Mama mtakatifu wa Maeklezya yote yaMungu, huko Roho Mfariji alishukia Mitume kama ndimi za moto; sasa cheza na furaha, ukitukuza Pentikosti pamoja na sisi, hii siku Kuu pendelevu duniani kote.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...*Sauti ya sita.*

Mfalme wa mbinguni, Wewe Mfariji. Roho ya ukweli, uliye pahali popote, na kuvijaza vitu vyote, Wewe hazina ya mambo mema, tena Mpaji wa uhai. Njoo kukaa kwetu na kutusafisha kila doa, hata kuziokoa roho zetu, Mwema We.

*Mukazi tano Mangaribi na mu Posho asubui tunafanya Sidikizo ya Siku Kuu ya Pentikosti. Hatusome Masomo ya Mangaribi, wimbo ya Litia na Polieleo.*

# MU JUMA YA WATAKATIFU WOTE

## MU POSHO MANGARIBI

*Zaburi ya Proimiakos. Kisha : «Bwana nimekuita...» tunaimba wimbo kumi; ya Ufufuo ya Kristu wimbo sita na ya Watakatifu ine.*

***Wimbo ya Ufufuo.***

*Sauti ya mnane.*

Tunakutolea, ee Kristu, wimbo wa mangaribi, na ibada yenye maana; kwani ulipendezwa kutuhurumia kwa ufufuo.

Ee, Bwana, Bwana, usitutupe mbali ya uso wako; lakini upendezwe kutuhurumia, kwa ufufuo.

Furahi, ee Sayuni takatifu, Mama wa Makanisa, nyumba ya Mungu; kwani wewe ulipokea kwanza usamehe wa zambi, kwa ufufuo.

Neno aliyezaliwa toka Mungu Baba, mbele ya milelena yeye mwenyewe aliyetwaa mwili kwa Bikira asiyeolewa, katika miaka ya mwisho, alivumilia usulubisho wa lufu kutaka kwake, na aliokoa mutu aliyekufa tangu zamani, kwa ufufuo wake.

Tunatukuza, ee Kristu, ufufuo wako katika wafu; kwa hii uliopoa uzao wa Adamu, toka uzulumu wa Hadeze; sawa na Mungu ulileta duniani, uzima wa milele na rehema kubwa.

Utukufu kwako, ee Kristu Mwokozi, Mwana wa pekee wa Mungu, uliyepigiliwa Msalabani, na uliyefufuka toka kaburi siku ya tatu.

***Wimbo ya Watakatifu.***

*Sauti ya sita. Olin apothemeni.*

Wasemaji wenye kuongozwa, kwa imani Wafwasi wa Mwokozi walipokuwa vyombo vya Roho Mtakatifu, wakatawanyika mpaka ku mipaka ya dunia sababu ya kutangaza neno takatifu na mafundisho ya ukweli; kwa msaada wa Bwana hii shamba takatifu likaota pa shina yao, ni kundi la Mashahidi wenye kufananisha Mateso takatifu ya Kristu na mateso yao mengi na ya moto; sasa wanaombea roho zetu.

Walipoungua na moto ya mapendo, walizarau moto ya kuni; walipowaka kama makaa ya chetezo, Mashahidi watakatifu wa Kristu waliteketeza nyasi ya majivuno ya udanganyifu; kwa maombi na sala walifunga kinywa cha simba na walipoonyesha kichwa yao kwa kukikata walikatakata adui na kwa uhodari wakamwanga damu yao, wakastawisha Kanisa na mbegu ya imani yao.

Waliposhindana na wanyama wakali wa pori, walipokatwa kwa upanga, walipokatwakatwa kwa misumeno, walipokatwa na kuteseka, walipotupwa motoni na kuungua wazima, walipokunyuwa, walipotobolea kwa mapigo, Mashahidi watakatifu walivumilia yote hii, walitangulia kuona bahati yao itakayokuja : taji takatifu na utukufu wa Kristu; sasa wanaombea roho zetu.

Kwa nyimbo takatifu tutukuzeni kama inavyofaa, duniani kote taifa takatifu la Mitume, la Mashahidi, la Maaskofu, la wanawake watakatifu, kwani wanadamu walipoungana na roho za mbinguni kwa msaada wa Kristu, kwa mateso yao walipokea uzima wa milele; wanatuangaza kama nyota, na sasa wanaombea roho zetu.

Utukufu kwa Baba… *Sauti ya sita.*

Enyi kundi takatifu la Mashahidi, ninyi msingi wa Kanisa na ukamilifu wa Habari Njema, mulitimiza maneno ya Mwokozi; ndani yenu milango ya Hadeze iliyofunguliwa juu ya Kanisa ilifungwa, damu yenu ilizima ibada ya mashetani; sadaka yenu ilisabitisha waaminifu wengi na ilishangaza Malaika wasiyo na mwili; mulipovaa taji, munasimama karibu ya Mungu na munaombea daima roho zetu.

Sasa na siku zote…**THEOTOKION.** *Sauti ya mnane.*

Mufalme wa mbinguni, kwa kupenda-wanadamu, alionekana juu ya inchi akazoea kati ya watu; kwani alipotwaa mwili kwa Bikira safi, na alipotokea kwa huyu, pamoja na hali ya umutu, huyu ni Mwana moja, kwa hali mbili, lakini hana uso mbili; kwa hii tukihubiri ya kama huyu kweli ni Mungu mkamilifu na Mtu mkamilifu, tunaungama Kristu Mungu wetu; umusihi ewe Mama usiyeolewa, kwa huruma wa nafsi yetu.

**KUINGIA.** Mwangaza upole (ilaron).

**MASOMO YA MANABII Unabii ya Isaya tutasoma (43,9-13)**

Bwana anasema hivi: Mataifa yote yakusanyike, na makabila ya watu wakutaniwe: Nani katikati yao anayeweza kutangaza neno hili, na kutuonyesha maneno ya zamani? Watoe washuhuda wao, wahesabiwe kuwa na haki; ao wasikie, na kusema: Ni kweli. Ninyi ni washuhuda wangu, Bwana anasema, mutumishi wangu niliyemuchagua; mupate kujua na kuniamini, na kufahamu ya kuwa mimi ndiye: mbele yangu hakuumbwa Mungu, wala nyuma yangu hatakuwa mwingine. Mimi, mimi ni Bwana; na pasipo mimi hapana mwokozi mwingine. Nimetangaza na nimeokoa, na nimeonyesha, wakati Mungu mugeni asipokuwa katikati yenu; kwa sababu hii ninyi ni washuhuda wangu, Bwana anasema, ya kama mimi ni Mungu. Ndiyo, tangu siku ya leo, mimi ndiye, wala hapana anayeweza kuokoa katika mukono wangu: nitafanya kazi, na nani ataizuiza?

**Hekima ya Solomono** (3,1-9)

Roho za watu wanyofu zimo mkononi mwa Mungu, wala masumbuko hayawashika. Machoni pa watu wapumbavu walionekana kwamba wamekufa, na kufariki kwao kulizaniwa kuwa msiba, na kutengwa kwao mbali nasi kulizaniwa kuwa upotevu; bali wao wakaa na amani. Watu wanawaza kwamba wanyofu hao wamepata azabu, bali wao wamepewa uzima wa milele sababu ya matumishi yao. Baada ya kupatilizwa kidogo, watapokea mema makubwa, kwa maana Mungu amewajaribu akawaona kuwa watu wema. Kama vile zahabu inavyogaribiwa katika moto, hivyo Mungu amewajaribu, amewapokea kama sadaka ya kuteketezwa. Wakati watakapoangaliwa na Mungu, wao watangara, watametameta kama ndimi za moto zenye kuchoma manyasi. Watawahukumu mataifa, watawatawala makabila, naye Bwana atakuwa mfalme wao milele. Wale wanaomtumainia Bwana watafahamu ukweli, nao walio waaminifu watakaa karibu naye katika mapendo maana Yeye waaminifu watakaa karibu naye katika mapendo.

**Hekima ya Solomono** (5, 16-23 )

Kwa hiyo watapokea ufalme wa utukufu na taji ya uzuri kwa mkono wa Bwana. Kwa maana atawalinda kwa mkono wake wa kuume na kuwakinga kwa ngao yake. Ataivalia bidii kama deraya, atavitumia viumbe kama silaha za kuwalipiza maadui kisasi. Badala ya valio la chuma atavalia haki, na badeala ya kofia ya chuma atajitia hukumu ya kweli. Atautwaa utakatifu kama ngao isiyoshindika ataifanyiza hasira kuwa upanga mkali. Pamoja naye ulimwengu wote utawapiga wapuzi. Mishale ya umeme iliyolingika sawa yaelekea shabaha ikitoka mawinguni kama ingerushwa kwa uta wa mviringano safi. Kwa hasira mvua ya mawe imetupwa na komeo. Mafuriko ya bahari yawafokea. Mito yagongana kwa nguvu juu yao. Pumzi yake Mweza yote yawapinga, kama chamchela yawatapanya. Hivyo ndivyo upotovu upotoavyo ulimwengu wote. Hivyo ndivyo uovu uangushwavyo viti vya utukufu vya watawala.

## LITIA Sauti ya kwanza

Kwa imani moja tushangilieni sikukuu kubwa ya wote wale tangu milele walipata neema kwa Mungu, tukikumbuka Watakatifu wote, Wapatriarche, Manabii, Mitume wa Kristu, Mashahidi na Watawa wa wakati wote, kwani wanaomba daima ili dunia ipewe amani na neema ya wokovu rohoni mwetu.

Muje, waaminifu wote, kwa zaburi na nyimbo za kiroho tutukuze makumbusho tukufu ya Watakatifu wote: Mbatizaji wa Mwokozi, Mitume, Manabii, Mashahidi, Maaskofu, Waalimu, Wenye heri, Watawa, Wenye haki na Wanawake watakatifu; tukitukuza makumbusho yao ya heri, wote pamoja tutaimba: Ee Kristu Mungu wetu na wema kubwa, kwa maombezi yao leta ku Kanisa yako amani, ushindi juu ya Adui na neema ya wokovu rohoni mwetu.

Utukufu kwa Baba… *Sauti ya tano.*

Enyi waaminifu, tuendeni wepesi ku sikukuu ya leo, kwani meza ya kiroho imetayarishwa, kikombe moja kimejaa kwa siri na vyakula vya furaha: ni fazila za Mashahidi ambao toka pande zote za dunia walitoa na ushujaa kwa Mungu majaribu mbalimbali walijaribiwa mwilini mwao, na kwa sadaka ya kiroho, maua ya miaka ya ujana wao, kichwa yao ilikatwa ao mikono yao yalikatwa, viungo vya miili yao vilikatwa; na wote pamoja, Watakatifu walisharikia mateso ya Kristu; lakini wewe Bwana uliyewarudishia taji za mbinguni juu ya mateso yao, kwa mapendo yako kwa ajili yetu, utupe sisi pia tufananishe fazila zao.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Bikira uheshimiwa kamili, uko hekalu na mulango, nyumba na kiti cha Mufalme; kwa wewe Kristu, Bwana na Mukombozi wangu, alifunuliwa kwa wale waliokaa katika giza; eko jua la haki, akitaka kwangaza wale walioumbwa kwa mufano wake kwa mikono yake; kwa hii, mwimbiwa kamili, kwa sababu uko na uhodari ya umama mbele yake, upatanishe bila kuacha, kwa kuokoa nafsi yetu.

## APOSTIKHA *Sauti ya mnane*

Ulipanda juu ya Msalaba, ee Yesu, uliyeshuka toka mbingu; ulikuja kwa lufu, ee Uzima usiyokufa. Wewe ni Nuru ya kweli kwa wale waliokaa gizani, ni ufufuo wa wote kwa wale walioanguka. Angazo na Mwokozi wetu, utukufu kwako.

Tutukuze Kristu, mwenye kufufuka katika wafu; kwani alipotwaa nafsi na mwili, kwa mateso alitenganisha yote mbili; nafsi yake isiyo na doa, ilishuka ku Hadeze, na ilimunyanganya; mwili wake takatifu haukujua uharibifu kaburini; yeye ni Mukombozi wa nafsi yetu.

Kwa zaburi na kwa nyimbo tutukuze, ewe Kristu, Ufufuo wako katika wafu; kwa hii ulituopoa sisi toka uzulumu wa Hadeze, na sawasawa na Mungu ulileta uzima wa milele na rehema kubwa.

Rabi wa wote, Muumba usiyosikilikwa wa mbingu na inchi, kwa mateso ya Musalaba, ulinichirizikia uzima usiyo na tamaa; ulipokubali maziko, na ulipofufuka na utukufu, ulifufua pamoja nawe Adamu, ku mkono wako wa uwezo. Utukufu kwa ufufuo wako wa siku tatu; kwa hii umetupatia uzima wa milele, na usamehe wa zambi, kwani wewe peke ni mwema.

Utukufu kwa Baba…*Sauti ya sita*

Muje, enyi waaminifu, tushangilie na furaha, leo tutukuze na ibada sikukuu ya Watakatifu wote na tutukuze makumbusho yao tukufu tukisema : " Salamu, Mitume, Manabii na Mashahidi, Maaskofu, Wenye haki, Wenye heri na Wanawake watakatifu pia; mumuombe Kristu alete amani duniani na neema ya wokovu rohoni mwetu.

Sasa na siku zote...**THEOTOKION** *Sauti ya ine.*

Muumba na Mukombozi wangu, Bwana Kristu, ewe Safi kamili, akitoka ku tumbo lako, na akinivaa, aliopoa Adamu toka apizo la kale; kwa hii tunakuita bila kuacha, ewe Safi kamili, kwani wewe wiko Mzazi-Mungu na Bikira kweli, na tunasema «Salamu» ya Malaika: salama, Bibi-Malkia, mulinzi na kivuli na wokovu wa nafsi yetu.

**APOLITIKION YA UFUFUO**

Toka juu ulishuka, ee Mwema, na ulikubali maziko ya siku tatu, kusudi utuokoe toka tamaa, Uzima na Ufufuo wetu, Bwana, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba…

**APOLITIKION YA WATAKATIFU WOTE** *Sauti ya ine*

Duniani kote Mashahidi wako walipamba Kanisa na damu yao. Unapovaa nguo nyekundu na kitani, kwa kinywa yao inakuimbia, ee Kristu Mungu wetu: Onyesha huruma yako kwa watu hawa walio wako, leta amani kwa watawala wetu wote na neema ya wokovu rohoni mwetu.

Sasa na siku zote...**THEOTOKION.** *Sauti ya ine.*

Siri ya kificho tangu milele iliyokuwa isijulikane na Malaika, imeonekana duniani katika wewe, ee Mzazi-Mungu; maana Mungu alitwaa mwili kwa ushirika, bila muchanganyo, na alikubali Msalaba kwa kutaka kwake kwa ajili yetu; juu ya hii akifufua Muumbwa wa kwanza, akaokoa toka lufu nafsi yetu.

## MU JUMA ASUBUI YA WATAKATIFU WOTE

**KATHISMA YA KWANZA.** *Sauti ya mnane.*

Ulifufuka katika wafu, ee Uzima wa milele, Malaika wa nuru akawaambia wanawake watakatifu: Musilie, nendeni mbio kuwapasha Mitume habari ya wokovu; imbeni mukipaza sauti, kwani Kristu Bwana amefufuka, kama Mungu alipenda kuokoa wanadamu wote.

Utukufu kwa Baba...

Ee Mwokozi, wenyi mauti walifunga kaburi yako, lakini Malaika akaondoa jiwe ku mulango wa kaburi; Wanawake walikuona ukifufuka katika wafu na wakapasha Wafuasi wako habari katika Siyoni: Tazama, amefufuka Uzima wa milele akivunja vifungo vya mauti. Ee Bwana, utukufu kwako.

Sasa na siku zote... **THEOTOKION**

Wewe uliyezaliwa kwa Bikira kwa ajili yetu, na uliyevumilia usulubisho, ee Mwema, uliyenyanganya mauti kwa lufu, na uliyeonyesha usimamao sawasawa na Mungu, usikengue walioumbwa kwa mukono wako; onyesha mapendo yako kwa wanadamu. Murehemu; pokea Mzazi Mungu aliyekuzaa, aliyepatanisha juu yetu, na okoa, ee Mwokozi wetu, taifa isiyotumainia.

**KATHISMA YA MBILI.** *Sauti ya mnane. To prostakthen.*

Alipovaa nguo mweupe na kuangaa kama umeme, Malaika Gabrieli alijongea ku kaburi ya Kristu na akasuma jiwe la mulango wa kaburi; walinzi wakashikwa na woga kubwa na wakawa kama wamekufa, kaburi ikawa wazi. Makafiri wapate haya, wakijuwa ya kwamba Kristu amefufuka!

Utukufu kwa Baba...*Tin sofian ke Logon.*

Ulipofufuka kweli kaburini, ukawaamuru wanawake watakatifu, kama inavyoandikwa, kuwapasha Mitume habari ya Ufufuo wako, na Petro akaenda mbio kaburini alipoona nuru kaburini akaogopa, kwani aliona paka sanda bila mwili takatifu; akasadiki na akalalamika: Utukufu kwako, ee Kristu, kwani unaokoa watu wote, ee Mungu Mwokozi, wewe uliye kweli Baba wa nuru.

Sasa na siku zote...**THEOTOKION.**

Ee Mjaliwa neema, katika wewe viumbe vyote vinafurahiwa: Malaika mbinguni na mataifa duniani; Ee Hekalu Takatifu la Bwana, shamba la ajabu la Paradizo tena utukufu wa ubikira, ambaye kwako Mungu mkuu alipata mwili na akawa mtoto mchanga, Yeye Mungu wa mbele ya nyakati Mungu wetu aliye juu mbinguni. Bwana aliweka kiti chake tumboni mwako, akalifanya kuwa pana kuliko mbingu. Ee Mjaliwa neema, katika wewe viumbe vyote vinafurahiwa: Utukufu kwako.

Elezo: *Tunaimba sasa mahimidi ya Ufufuo wa Kristu. Kisha tunasoma Ipakoi:*

**IPAKOI**

Mirofori walipokuja kaburini ya chemchem ya uzima wakatafuta katika wafu Rabi msiyekufa; lakini walipopokea kwa Malaika habari ya furaha, wakawaambia Mitume ya kama Bwana alifufuka kuleta duniani neema kubwa.

*Na tunaimba* **ANAVATHMI** *sauti ya mnane. (Tafuta mu Kitabu ya Paraklitiki).*

*Elezo: Tunaimba* **KANUNI YA UFUFUO YA PARAKLITIKI** *na Kanuni ya Watakatifu wote.*

**KANUNI YA WATAKATIFU WOTE**

**WIMBO WA KWANZA** *Sauti ya mnane.*

**IRMOS:** Zamani, farao alipotangulia jeshi lake akaangamizwa kwa fimbo ya Musa wakati, kwa alama ya Msalaba, akapiga juu ya bahari na kuigawanya, akaokoa Israeli aliyeweza kukimbia na kuvuka pakavu, akamwimbia Bwana wimbo.

Watakatifu wote wa Mungu mutuombee sisi.

Ee Bwana, ninapoimbia Watakatifu wako wote, kwa maombezi yao ninakuomba angaza roho yangu na nuru yako, kwani wewe ni Nuru isiyokaribika yenyi kufukuza na mianga yake giza za udanganyifu, ee Neno wa Mungu, wewe uliye Chemchem ya nuru.

Ee Bwana, ulipotukuzwa juu ya Msalaba, unaleta mataifa kwa kujuwa jina lako, unangazisha nuru ya Utatu Mtakatifu na kufukuzia udanganyifu mbali kwa utume wa Mitume wako, ee Mwokozi.

Ee Bwana,Walipotii amri yako, Mitume wako watakatifu waliacha na hekima mali yote ya hii uzima; kwa nuru ya neema waliangaza ulimwengu wote , walitangaza na utukufu habari njema ya wokovu wako.

Na furaha Mashahidi walipochukua msalaba wako na kukufwata sababu ya kufananisha Mateso yako takatifu walikataa na uhodari makamio ya wazulumu bila kutetemeka hata kidogo mbele ya upanga na moto, mbele ya njaa, mateso na lufu.

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe. **THEOTOKION**

Ee Bikira Mtakatifu kamili, Mabinti walionyesha nguvu ya kianamume,walivumilia majaribu ya mashahidi bila kuregea, na kwa neno la Daudi, kisha wewe walipelekwa kwa Mwana wako na furaha katika makao ya Mfalme mkubwa.

## WIMBO WA TATU

**IRMOS:** Ku mwanzo kwa akili yako, ulisabitisha mbingu na ukaumba inchi juu ya maji, ee Kristu, unisabitishe juu ya mwamba wa mari zako, kwani hakuna aliye Mtakatifu ila wewe peke yako Mpenda-wanadamu.

Maaskofu na Wachungaji walipovaa cheo cha mapadri kwa uongozi wao wa hekima wakaipamba na mafundisho takatifu Neno aliwapa.

Mulipoangaa na uzuri wa kwanza na kuangaa kama nyota, mulifanya Kanisa ya Kristu duniani kuwa mbingu yenyi nyota kwa wingi wa uzima wenu takatifu.

Utukufu kwa Baba…

Walipotii amri yako, watu wenye heri walipoangaa na fazila mingi wakajaza makao ya mbinguni : Katika nyumba ya Baba yako, ee Bwana, makao mengi yaliwapokea.

Sasa na siku zote…**THEOTOKION.**

Ee Mzazi-Mungu, kwa ajili yetu ulizaa tumboni mwako mwa bikira Neno Mtakatifu aliyezaliwa kwa Mungu, chombo cha mapendo takatifu ya mabikira wenye akili na safi ambao kisha wewe wamekuwa wenye kumusindikiza katika maandamano yake ya ufalme.

Elezo*: Sasa tunasoma Kontakion na Ikos ya Paraklitiki*

**KATHISMA** *Sauti ya mnane*

Tunaposhangilia makumbusho takatifu ya Watakatifu wote, Mababu, Mapadri, Wapatriarchi, Mitume na Mashahidi, Maaskofu, Manabii, Wenye haki, Watawa na Wenye heri na ya wote wale ambao jina limeandikwa katika kitabu cha uzima, tunapoomba ulinzi wao, ee Kristu Mungu wetu, tunakuomba: Kwa maombezi yao leta amani duniani ili wote pamoja tuweze kukuimbia tukisema: Ee Mpenda-wanadamu, uko kweli Bwana Mungu mwenye kutukuzwa katika baraza ya Watakatifu, wewe uliyetukuza makumbusho yao takatifu.

Utukufu kwa Baba… Sasa na siku zote...**THEOTOKION.**

Tuimbie Safina mpya tena mlanga wa mbinguni, mlima takatifu, wingu la nuru, mungaza wa mbingu, wokovu wa Eva, Paradizo ya siri tena hazina kubwa ya ulimwengu wote; kwani katika yeye wokovu umetimizika dunia imesamehewa deni yake ya zamani; ndio maana tunamulalamikia: Umsihi Kristu Mungu wetu awaondolee zambi zao wale wenyi kumuabudu Mwana wako na kusujudu mbele yake.

**KONDAKION YA WATAKATIFU** *Sauti ya mnane*

Ee Bwana, kama matunda ya inchi yanavyotolewa kwa Muumba, ulimwengu inakutolea mashahidi takatifu wabebaji-Mungu;kwa maombezi yao na kwa ile ya huyu alikuzaa linda Kanisa yako katika amani, ee Mungu mwenye rehema.

## IKOS

Wale ambao walishuhudia duniani wamekuwa raia wa mbinguni; walipofananisha Mateso ya Kristu, wanatukomboa toka mateso; wanapokusanyika leo kule mbinguni, wanaonyesha namuna gani Kanisa ya wazaliwa wa kwanza iko na alama ya baraza ya mbinguni; wanamwaambia Kristu

wakisema: Uko Mungu wangu; katika huyu alikuzaa, ee Bwana, unilinde, ee Mungu mwenye rehema.

**SINAKSARI**

Leo, Siku ya Yenga kisha Pentikosti, tunashangilia makumbusho ya Watakatifu wote walioishi duniani kote, katika Azia, Afrika, Ulaya, katika inchi za kaskazini na Australia.

Katika Bwana na Mungu wangu natukuza marafiki wote, natamainia kuwa siku moja katikati yao.

Kwa maombezi ya Mama yako Mtakatifu kamili na ya Watakatifu wote, ee Kristu Mungu wetu, utuhurumie na kutuokoa, kwa wema wako na mapendo yako kwa wanadamu. Amin.

**EKSAPOSTILARION YA UFUFUO YA PARAKLITIKI**
**YA WATATKATIFU WOTE** *Sauti ya mbili. Tis mathites*

. Kwa nyimbo zetu tumutukuze Mbatizaji na Mtangulizi, Mitume, Manabii na Mashahidi, Waierarkhi na Wenye heri, Watawa na Maaskofu mashahidi, Wanawake rafiki za Kristu na Wenye haki wa nyakati zote, pamoja na makundi ya Malaika kama inavyofaa : tuwaombe ili watupe tuufikie utukufu uleule karibu ya Kristu Mwokozi wetu.

**THEOTOKION**

Ee Bikira Mtakatifu kamili,Huyu mwenye kutukuzwa na Malaika kama Mungu, bila kwacha kifua cha Baba alishuka toka mbinguni sababu ya kuungana na wanadamu hapa chini, na wewe mwenyewe ulitupatia wokovu wakati, kupita akili yote ya wanadamu, ulimupa mwili tumboni mwako; utuombee kwake atupe maondoleo ya zambi zetu.

**MASIFU** *Sauti ya mnane*

Ee Bwana, japo ulisimama mbele ya baraza ya hukumu, ukihukumiwa kwa Pilato, lakini haukuache kiti cha ufalme pahali unapokaa pamoja na Baba; na ukifufuka katika wafu, uliopoa dunia toka utumwa wa adui, kama Mwema na Mpenda-wanadamu.

Ee Bwana, japo Wayuda walikuweka Kaburini kama mwenye kufa, lakini askari walikuchunga sawa Mfalme anayelala, na walikufunga kwa mhuri kama hazina ya uzima; lakini ulifufuka na ulileta uzima usiyoharibika kwa nafsi yetu.

Ee Bwana, ulitupatia Msalaba wako, kama silaha juu ya shetani; kwani yeye anaitetemekea na anaifazaikia kwa woga, bila kuweza kuona nguvu Yake; kwa kuwa Msalaba unafufua wafu, na uliharibu mauti; kwa hii tunaabudu, maziko na ufufuo wako.

Ee Bwana, Malaika wako, aliyehubiri ufufuko, aliogopesha wachungaji; tena aliita kwa wanawake, akiwaambia: Kwa nini munatafuta yeye aliye hai katika wafu? Alifufuka, kwa kuwa Yeye ni Mungu na alileta uzima kwa ulimwengu.

Uliteswa kwa Msalaba, ewe usiyeteswa katika umungu; ulikubali maziko ya siku tatu, kusudi utuopoe toka utumwa wa adui; na utufanye wasiokufa, na utupatiye uzima, ee Kristu Mungu mpenda-wanadamu, kwa Ufufuo wako.

***Wimbo ya Watakatifu*.**

*Sauti ya ine. Os geneon en martisin.*

Watakatifu waliokaa duniani Bwana aliwajaza na mema yake : mwilini mwao walipata alama ya mateso yake ambayo yalikuwa mapambo yao, wakaangaa na uzuri wa umungu; ndio maana kwa nyimbo zetu tunawatukuza kama maua isiyoweza kufifia, kama sadaka za kiroho, kama mbingu ya nyota ya Kanisa.

Shairi: Wenye haki wanapaza sauti : Bwana anawasikiliza na anawaokoa toka mateso yao yote.

Pamoja na Manabii, Mitume watakatifu, Wenye heri, Waalimu, Maaskofu, Wenye haki wa nyakati zote, Wanawake Mashahidi waliokombana katika uwanja na wale walioishi katika utawa, Wenye haki wengi na Watakatifu wengi wanapokea masifa yetu kwa nyimbo takatifu kama raia na wariti wa ufalme wa juu mbinguni, hii Paradizo mupya.

Shairi: Bwana ni wa ajabu katika Watakatifu, Yeye Mungu wa Israeli.

Mashahidi watakatifu ambao kwa nuru ya fazila zao waligeuza dunia kuwa mbingu mupya, walipofananisha lufu na mateso ya Kristu katika njia yenye kuleta uzima wa milele kwa tendo la

neema walitusafisha toka mateso yetu ya mauti, na duniani kote uhodari wao katika mashindano inastahili sifa ya nyimbo zetu.

Utukufu kwa Baba... **EOTHINON YA KWANZA.** *Sauti ya kwanza.*

Mlimani Bwana akaonekana kwa Wafuasi waliokuja mbio sababu ya kunyanyuliwa kwake hapa chini na wakasujudu mbele yake. Walipofundishwa juu ya uwezo wake wa milele, wakatumwa ku mataifa yote iliyo chini ya mbingu kutangaza ufufuo wake katika wafu na kurudi kwake mbinguni toka duniani.

Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Mbarikiwa Ukupita, ewe Mzazi-Mungu Bikira; kwa kuwa naye aliye amepata mwili nawe, kuzimu imetekwa, Adamu amerejezwa, laana imekufa, Eva amekombolewa, Mauti imewekwa kifoni, tena sisi tumeofikia uzima; kwa hiyo tukiimba na kupaza sauti umehimidiwa U Kristu Mungu wetu, liyependezwa hivi. Utukufu kwako.

**DOKSOLOGIA MKUBWA**

**Mwimbo kisha Doksologia:** *Sauti ya mnane*

Ee Bwana, ulipofufuka toka kaburini, ulivunja minyororo ya Hadeze, ulipasua hati iliyotuhukumu ku mauti; ulituokoa sisi wote toka mtego wa Adui na ulionekana katikati ya Mitume wako ambao ulituma duniani kuhubiri na katika wao ulileta amani yako duniani, wewe peke yako Bwana mwenye kutujaza na rehema yako.


## MONASTERI YA MTAKATIFU GRIGORIO

## KILIMA TAKATIFU

## GRECE-HELLAS

## 2002